RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI NA MASHIRIKA (P.A.C) YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR, 2013/2014.

SEHEMU YA KWANZA:

1.0 UTANGULIZI:

Katika kikao cha Bajeti ya mwaka 2013/2014, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia kwa Mhe. Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Utumishi wa Umma na Utala Bora, Mhe. Haji Omar Kheir, waliwasilisha ripoti mbili za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ambazo ni Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zote za mwaka 2011/2012.

Baraza la Wawakilishi kwa pamoja lilizipokea ripoti hizo na kuzikabidhi kwa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kuzifuatilia ripoti hizo ili kuja kutoa taarifa yake katika Baraza hili hili, na hivyo, Kamati hii imelazimika kuzifuatilia ripoti hizo kama ilivyotakiwa na kanuni ya 118(2) ya Kanuni za Baraza toleo la 2012.

1.1 WAJUMBE NA MAKATIBU WA KAMATI:

Kwa mwaka 2013/2014, Kamati inaundwa na Wajumbe 8 na Makatibu 2 kama ifuatavyo:

1. Mhe. Omar Ali Shehe - Mwenyekiti.
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Mjumbe
4. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Mjumbe
5. Mhe. Rufai Said Rufai - Mjumbe
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Mjumbe

Makatibu wa Kamati ni:-

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin; na
2. Ndg. Othman Ali Haji.

1.2 REJEA ZA KAMATI:

Kwa mwaka 2013/2014, Kamati ilifuatilia ripori mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo ndio rejea za Kamati. Ripoti zenyewe ni hizi zifuatazo:

- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2011/2012.
- Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ya mwaka 2011/2012.

Hata hivyo, kwa kutumia mamlaka iliyonayo, Kamati lifuatilia zaidi ya hoja zilizoelezwa na ripoti hizo na zaidi kupitia ripoti ya ukodishwaji wa ardhi kwa wawekezaji, taarifa ambayo inapatikana katika ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha haja hii imetokana na kupata taarifa mbali mbali kupitia vyanzo mbali mbali vya habari, ikiwa ni pamoja na majibu na mashirikiano ya pamoja na watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na watendaji wengine wa taasisi zilizohusika na kazi za Kamati.

1.3 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI:

Kamati imefanya kazi kwa utaratibu wa kawaida kama unavyoelekezwa na kanuni ya 108(7) ya kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2012, juu ya uwezo wa Kamati kujipangia kazi zake baada ya kushauriana na Spika. Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara ama Taasisi za Serikali zilizohusika na kazi, na hatimae Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kushuhudia uhalisia wa maelezo ya Wizara, Taasisi husika ama hoja ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Aidha, Kamati pia kwa kuzingatia haja iliyokuwepo, ilifanya ziara katika maeneo husika na baadae kufaya mjadala ama kuendelea na mjadala wa hoja mbali mbali.

Kamati pia iliwaita watu mbali mbali, ikiwa ni pamoja na viongozi wa taasisi za Serikali na binafsi na iliposhughulikia masuala ya ardhi iliziita Kampuni mbali mbali mbele ya Kamati na pia kufanya ziara katika maeneo yao ya uwekezaji.

1.4 UPEO WA RIPOTI:

Pamoja na kuzifanyia kazi ripoti mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kama tulivyoeleza awali, Kamati kwa mwaka 2013/2014 haikuweza kuzimaliza ripoti hizo kutokana na ufinyu wa muda uliopewa Kamati na Afisi ya Baraza la Wawakilishi, wakati huo huo ripoti hizo zimekusanya ukubwa wa kazi ambazo zinahitaji muda mwingi. Aidha, kwa mfano ndani ya ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2011/2012 imekusanya ripoti kuhusiana na hesabu hizo kwa Wizara zote 16, Mashirika na Serikali za Mitaa; ripoti ya ukaguzi maalum juu ya malipo ya wazee wasiojiweza, ukaguzi wa viinua Mgongo, ukaguzi maalum kwa hesabu namba 0211030005 ya Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Nyumba.

Aidha, ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ya mwaka 2011/2012, imekusanya Ukaguzi yakinifu kwa Miradi ya Wizara nne za Serikali na ukaguzi juu ya ukodishwaji wa ardhi kwa wawekezaji. Aidha, masuala ya ardhi kwa ukubwa na mchanganyiko wake, yangestahili kuundiwa Kamati maalum ya kudumu ya kufuatilia masuala yanayohusika na ardhi.

Kwa ujumla hali hiyo imeifanya Kamati kushindwa kuzifanyia kazi hoja zote za vitabu hivyo, ingawaje imejitahidi kwa kadiri ya uwezo wake kwa kuifanyia kazi Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi Maalum vya SMZ na Taasisi zake zote; na kuzifanyia kazi hoja zote za Pemba zilizoanishwa katika ripoti zote mbili (ingawaje kwa makosa ya Maofisa Wahasibu, Kamati haikuweza kufanya kazi baadhi ya taasisi zao, kama utakavyoona katika ripoti hii ya Ukaguzi wa Hesabu). Aidha, Kamati imeifanyia kazi Ripoti ya Ukaguzi yakinifu kwa Miradi kwa Baraza la Manispaa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Pemba na kumalizia kwa ripoti juu ya masuala ya ardhi. Kazi hii ni kubwa pamoja na uchache wa Taasisi zilizohusika, na imeifanya ripoti ya Kamati kuwa kubwa na kueleza masuala mengi.

1.5 KAMATI NA NAMNA INAVYOHUSIANA NA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR.

Kanuni ya 118(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2012 linaipa Kamati majukumu mazito na ya msingi yakiwa ni pamoja na Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Kuchambua na kutafakari ripoti yoyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale ambapo Rais aliagiza ukaguzi huo ufanywe.

Katika utekelezaji wa majukumu haya, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (P.A.C) na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hulazimika kushirikiana na kusiaidiana kwa karibu mno na kwa hali yoyote ile itakiwayo, ili malengo ya kuwepo kwao yaweze kufikiwa. Aidha, Katika Mabunge yote ya Jumuiya ya Madola, Kamati ya P.A.C na Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huwa ni ndugu wenye lengo moja la kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma. Hali hii huzifanya Kamati na Afisi za Wakaguzi Wakuu kushirikiana kwa namna moja ama nyengine, ili kufikia lengo la kujenga mataifa yao.

SEHEMU YA PILI (MAUDHUI YA RIPOTI):

UFAFANUZI WA HOJA MBALI MBALI ZILIZOFANYIWA KAZI NA KAMATI:

RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU KWA MAWIZARA, MASHIRIKA NA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012.

2.0 OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA VIKOSI MAALUM VYA SMZ.

2.1 KIKOSI CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM):

Hoja Nam. 19.1: Hesabu za Mwisho wa mwaka 2011/2012:

Taarifa za Matumizi ya kazi za Kawaida:

Kwa mwaka 2011/2012 Kikosi kiliidhinishiwa kutumia Tsh. 7,812,936,472 na ilipofikia Juni 2012 iliingiziwa Tsh. 7,812,936,472 (100%) ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi kwa kazi za Maendeleo:

Kikosi kiliidhinishiwa kutumia Tsh. 200,000,000 kwa kazi za maendeleo kwa kipindi cha 2011/2012, na ilipofikia Juni 2012, fedha zilizoingizwa na kutumika ni Tsh. 200,000,000 (100%) ya makadirio.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imehoji matumizi ya fedha za maendeleo na kuelezwa zimetumika kwa ujenzi wa hospitali ya Kikosi kwa ghorofa ya kwanza na fedha nyengine kwa ujenzi na vifaa vya theater. Pamoja na hivyo, Kamati haikupata muda wa kutosha wa kuangalia uchambuzi wa matumizi hayo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha kanuni za fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji muda wa ziada kufuatilia suala hili.

Hoja Nam. 19.2: Malipo yaliyofanywa kinyume cha kanuni na taratibu za manunuzi, Tsh. 195,957,100 NA Hoja Nam 19.3: Ununuzi wa Vifaa Hospitali, Tsh. 82,380,000 kupitia Hesabu ya Maendeleo (Development Account).

Tsh. 195,957,100 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali. Ukaguzi umebaini kwamba, manunuzi hayo yalizidi kiwango ambacho kinastahiki kuitishwa zabuni kwa mujibu wa sheria. Na Tsh. 82,380,000 zimenunuliwa vifaa vya hospitali bila ya kufuata utaratibu.

Majibu ya Kikosi:

Ni kweli hawakufanya utaratibu wa zabuni kutokana na matumuzi ya fedha hizo ni ya kitaalamu na hivyo, walilazimika kununua kupitia Kampuni ya Lab Equip Ltd iliyopo Kilimazi, Zanzibar. Aidha, Mganga wao Mkuu ndie aliyewaeleza na ndie waliemtuma, na hivyo walitumia 'single source' method of procurement.

Uchunguzi wa Kamati:

Uongozi wa Kikosi haukufuata taratibu za kufanya zabuni ya ununuzi wa vifaa vya hospitali wala vifaa vyengine vilivyohusika kwa kuelezwa kwamba, vifaa hivyo vinapatikana kwa Lab equip Ltd, kitu ambacho hakikukubaliwa na Kamati. Aidha, Uongozi huo umeshindwa pia kuthbitisha kupata ridhaa ya kikao cha Bodi ya Zabuni kuhusiana na kutumia 'single source' na kwa hali yoyote iwayo, Kikosi kimekiuka taratibu za sheria.

Aidha, Kikosi hakijapata ushauri wowote kupita Wizara ya Afya, ambapo inaaminika ndio wataalamu wa vifaa vya hospitali wanakopatikana, na ni Kamati iliyohusika na ujenzi wa hospitali hiyo ndiyo iliyoelekeza kununuliwa kwa vifaa hivyo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inapendekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa Afisa Mhasibu, kwa kukiuka matakwa ya sheria.

Hoja Nam. 19.4: Ununuzi wa vyakula kwa ajili ya askari wa KMKM Ths. 113,577,100.

Tsh. 113,577,100 zimetumika kwa kulipwa Canteen Akaunti, kwa ajili ya ununuzi wa chakula cha maaskari, kinyume na utaratibu.

Majibu ya Kikosi:

Uongozi wa Kikosi ulipata agizo kutoka Wizarani inayohusika na Vikosi kwamba, sio ruhusa kwa Kikosi kukata mishahara ya wafanyakazi wao kwa ajili ya chakula, hali iliyowapelekea kusumbuka na kwenda Wizara ya Fedha kuomba ingawa nako walikosa fedha, ingawaje walipata ushauri wa kutumia fedha zao za Canteen mpaka watakapoingiziwa fedha na Wizara ya Fedha na baada ya kuingiziwa fedha ndipo walipotafuta Mzabuni ambae anawapa huduma hiyo

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilihoji iwapo utaratibu wa kutumia fedha za Canteen ulifuata taratibu za uhaulishaji wa vifungu vyengine vya fedha, na kujibiwa kwamba wamefuata, ingawa majibu haya hayakuweza kuthibitishwa hata baada ya kuomba muda wa ziada na Kamati kuruhusu muda huo.

Canteen account haimo katika vifungu vyovyote vya matumizi ya Kikosi, uendeshaji wake ni kwa njia ya mkopo kwa wafanyakazi kukopa chakula na kutumia majumbani mwao, na wao hurejesha fedha za mkopo wao katika canteen hiyo na hatimae hupatikana fedha nyingi ambazo hutumiwa pia kwa matumizi na mahitaji mbali mbali ya Kikosi, kinyume na kufanya taratibu za

manunuzi zinazoelekeza kupata ushindani wa ‘suppliers’ wengine. Ofisi ikihitaji kufanya manunuzi hata kupitia ‘other charges’ na ‘capital expenditures’, basi ‘supplier’ huwa canteen.

Tatizo jengine ni kwamba, Canteen account haikuwa ikikaguliwa hapo kabla hata na Mkaguzi wa Ndani wa Wizara ama kikosi, lakini sasa kufuatia msisitizo wa Kamati, inatarajiwa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu pamoja na kusajiliwa Bodi ya Mapato kwa ajili ya ulipaji kodi.

Mapendekelezo ya Kamati:

Kamati inahimiza kukaguliwa kwa Canteen account kwani ni accounti rasmi na pia inapaswa kulipiwa kodi, kwani ni duka la biashara kama ilivyo kwa wafanya biashara wengine. Aidha, Kamati inakitaka Kikosi kuhakikisha kinafuata taratibu za sheria ya manunuzi na sio kufanya upendeleo wa kutumia canteen account katika matumizi ya fedha za Serikali kinyume na sheria.

Hoja Nam. 19.5: Malipo yasiyokuwa na vielelezo (Nyaraka pungufu), Tsh. 135,520,000.

Fedha hizo zimelipwa kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Kikosi:

Ni kweli wakati wa ukaguzi hawakuwa na vielelezo vyote, lakini Mkaguzi aliekagua aliwashauri wampelekee vielelezo hivyo Ofisini kutokana na uchache wa muda, jambo ambalo wamefanya, ingawa wamechelewa na dnio ripoti ilikuwa imeshatoka.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imeviangalia vielelezo hivyo na kugundua kwamba, havina uthibitisho wa Mkaguzi, yaani havina wino wa kijani kuonesha vimekaguliwa. Aidha, hakukuwa na wamasiliano yoyote rasmi kuhusiana na kuchelewa kuonekana kwa vielelezo hivyo.

Vile vile, Kamati ilivyovipitia vielelezo hivyo imejiridhisha kuwa na mapungufu kadhaa ikiwa ni pamoja na kukosa saini ya mpokeaji; kukosekana kwa baadhi ya risiti za mapokezi ya fedha; barua ya kuomba huduma ama haja ya matumizi yaliyofanyika pia zimekosekana kwa baadhi ya vielelezo, kwa ujumla Kamati imejiridhisha kwamba, vielelezo hivyo vimekosa sifa zilizoelezwa na kanuni ya 95 ya kanuni za fedha za mwaka 2005, na zaidi kifungu cha 95(4) cha kanuni hizo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kwamba, Kikosi kina mapungufu mengi ya kifedha, na hivyo inapendekeza kwamba, Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji wote waliohusika ikiwa ni pamoja na Kamanda Mkuu na Mhasibu wa Kikosi hicho.

2.2 KIKOSI CHA VALANTIA:

Kikosi cha Valantia kina hoja mbali mbali katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Hoja hizo ni:

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Kikosi cha Valantia kimechelewa kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa siku mbili, kwa kuwasilisha tarehe 2/10/2012 badala ya tarehe ya mwisho ya 30/09/2012 kinyume na Sheria namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2) kinachozitaka Taasisi zote za Serikali kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka si zaidi ya tarehe 30/09 ya kila mwaka.

Hoja Nam. 20.1: Hesabu za Mwisho wa mwaka.

Taarifa za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo.

Kikosi kiliidhinishiwa kutumia Tsh. 2,802,616,659 kwa kazi za kawaida na ilipofika Juni 2012 kiliingiziwa Tsh. 2,802,616,659 sawa na 100% ya makadirio. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo iliidhinishiwa kutumia Tsh. 100,000,000 na kuingiziwa Tsh. 90,000,000 na kutumika sawa na 90% ya makadirio.

Hoja Nam. 20.2: Akaunti ya Miradi (Development Account). Malipo yasiyokuwa na Vielelezo (nyaraka pungufu) Tsh. 90,000,000.

Fedha hizo zimelipwa kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo havikupatikana kwa ukaguzi. Kukosekana kwake ni kukiuka maelekezo ya kifungu cha 95(4) cha sheria ya fedha, namba 12 ya mwaka 2005.

Hoja Nam. 20.3: Malimbikizo ya madeni Tsh. 252,625,000

Fedha hizo zinadaiwa na wafanya biashara pamoja na taasisi mbali mbali kwa ajili ya utoaji wa huduma tofauti kwa Kikosi cha Valantia. Ukaguzi umebaini kwamba, madeni hayo ni ya muda mrefu na kuwepo kwake ni kinyume na mfumo sahihi wa kiuhasibu unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu ambao utatumika kwa Mawizara ya Serikali.

Hoja Nam. 20.4: Taarifa ya ukusanyaji wa mapato.

Ukaguzi uliofanyika kutokana na ukusanyaji wa mapato umegundua mambo yafuatayo:

Kikosi kinatoa huduma za ulinzi kwa taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi na kujipatia mapato na kuyatumia mapato hayo kwa shughuli zao mbali mbali. Mapato hayo yanapaswa kufuata taratibu za ukusanyaji wa mapato na kuwepo kwa stakabadhi za ukusanyaji pamoja na daftari la kumbu kumbu linaloonesha taarifa za mapato na matumizi kwa mujibu wa sheria. Ukaguzi umebaini dosari zifuatazo:

- Kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi za mapato.

- Kutotayarisha daftari la fedha taslimu (Cash Book).
- Kutokuwepo kwa hesabu ya mapato ya Kikosi.

Aidha, kutokana na dosari hizo, ukaguzi umegundua kuwa, Kikosi cha Valantia hakikufungua hesabu juu ya ukusanyaji wa mapato yake ya ndani na kupelekea kusababisha uvujaji wa mapato na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Aidha, ukaguzi umeshindwa kupata taarifa sahihi za mapato na matumizi kutokana na kutotayarishwa kwa daftari la mapato na matumizi, ambalo lingetoa taarifa za fedha zilizokusanywa na zilizotumiwa. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba, jumla ya Tsh. 64,674,000 zimekusanywa lakini taarifa ya fedha iliyowasilishwa kwa ukaguzi ilikuwa ni Tsh. 6,270,000 na kufanya tofauti ya Tsh. 58,404,000 ambazo taarifa zake hazijuulikani.

Hoja Nam. 20.5: Matumizi yaliyofanyika kiyume na vifungu, Tsh. 21,529,660.

Ukaguzi umebaini kwamba, kuna baadhi ya malipo yamefanyika kinyume na vifungu vilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Aidha, ukaguzi umebaini, taratibu za uhaulishwaji hazikufuatwa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya fedha, namba 12 ya mwaka 2005.

Kamati kufanyakazi na Kikosi cha Valantia:

Kamati haikufanyia kazi hoja zote za Kikosi kutokana na kutotoa mashirikiano kwa Kamati. Aidha, baada ya Kamati kutakiwa kufanya kazi zake mnamo mwezi wa Septemba 2013, iliandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ mnamo tarehe 02/09/2013 kupitia barua yenye kumbu kumbu namba BLW/K.10/2/VOL.IV/128 na nakla ikapelekwa kwa vikosi na Hamlashauri zote zilizohusika, ikiwa ni pamoja na kikosi cha Valantia.

Katibu Mkuu pamoja na Kamanda Mkuu wa Kikosi cha Valantia walihudhuria katika kikao cha kuthibitisha ratiba na walikubaliana na Kamati kwamba kazi ya kufuatilia hoja hizo zifanyike tarehe 12/09/2013, saa 3:00 asubuhi katika Afisi ya Kikosi.

Kwa masikitiko makubwa, Kamati ilipokea taarifa ya dharura ya Kamanda wa kikosi tarehe 11/09/2013 sa 6:48 mchana tena kwa njia ya simu kwamba, Kamanda wa Valantia, Mhasibu, Mkuu wa Utawala, watendaji wakuu wa Valantia pamoja wakuu wa vikosi vya SMZ wanaitwa na Mhe. Rais siku ya kazi ya Kamati (tarehe 12/09/2012) saa 3:00 asubuhi.

Aidha, Kamati ilimuandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, tarehe 12/09/2012 kueleza kusikitishwa kwake na utaratibu uliotumika kuzuia kufanya kazi za Kamati na nakla ya barua hiyo pamoja na watu wengine, pia ilinukuliwa kwa Kamanda wa Kikosi cha Valantia.

Mnamo tarehe 16/09/2013, Kamanda Mkuu wa Valantia alimjibu Mwenyekiti kwa barua yenye kumbu kumbu namba KV/M/112/VOL.41, akiomba radhi kwa Kamati kwa kutofanyika kikao

kama ilivyopangwa na mazingira ya ghafla ya wito wa Mhe, Rais. Aidha, akiishauri Kamati kufanya kazi siku nyengine kama itakavyopanga.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imepokea barua ya Kamanda Mkuu wa Kikosi cha Valantia kwa msisitizo wake, na inampongeza kwa uungwana aliouonesha baada ya kupewa barua na Kamati. Hata hivyo, kutokana na uchache wa muda, Kamati imeshindwa kupata muda wa ziada wa kufanya kazi hoja hizo na ni sawa na kusema kwamba, hoja hii bado haijapata majibu.

2.3 JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU):

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Sheria namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2) kinazitaka Taasisi zote za Serikali kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka si zaidi ya tarehe 30/09 ya kila mwaka, na JKU wamewasilisha hesabu zao kwa kuchelewa tarehe 18/10/2012.

Majibu ya JKU:

Ni kweli wamechelewa kuwasilisha hesabu hizo kwa wakati kutokana na Askari Tarishi kukosea kupeleka vitabu vyote viwili Wizara ya Fedha badala ya kuvipeleka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikukubaliana na hoja ya Afisi hii na kuona haina mashiko, ingawa viongozi walijaribu kuthibitisha kwa kutumia dispechi. Aidha, pamoja na Kamati kuelezwa kwamba barua ya awali ilipelekwa Wizara ya Fedha na nakla kwa Mdhibiti, barua hiyo ilipokaguliwa na Kamati imegundua kwamba, haina nakla yoyote.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inautaka Uongozi wa JKU kuwasilisha mapema hesabu zao za mwisho wa mwaka kama inavyoelekezwa na sheria.

Hoja Nam. 21.1.1: Kutopatikana kwa taarifa za fedha (mapato ya matumizi).

Ukaguzi umegundua JKU kikosi cha Bambi, kimefungua hesabu PBZ yenye namba 031206012147. Hadi ukaguzi unakamilika taarifa za hesabu hizo hazikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya JKU:

Uongozi umeikataa ‘account’ iliyoainishwa na Mdhibiti na kueleza kwamba, account yao ya Bambi Matora ni 02110800136 na ‘bank statement’ ndio ushahidi wao kwa account namba 021108001386. Aidha, kwa mwaka 2011/2012, JKU Bambi haikuwa na akaunti.

Uchunguzi wa Kamati:

Pamoja na maelezo hayo, Kamati imegundua kuwa account iliyoelezwa na Uongozi wa JKU ni tofauti na ile iliyomo katika 'bank statement', jambo linaloifanya Kamati kushidwa kuamini maelezo ya viongozi hao. Aidha, accounti iliyowasilishwa kwa Kamati ni ya mwaka 2013 badala ya 2011/2012 kama ilivyotipotiwa.

Aidha, pamoja na kasoro iliyojitokeza, Kamati ilihitaji ushahidi iwapo Uongozi wa JKU uliwasiliana na Mdhibiti kuhusiana na tofauti ya 'account', jambo ambalo Uongozi umekiri haukuandika barua yoyote.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati haikuridhika na majibu ya uongozi wa JKU na inauagiza uongozi huo kuwasilisha taarifa sahihi za account inayotakiwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ili ukaguzi wa account hiyo uweze kufanyika.

Hoja Nam. 21.1.2: Ulipaji wa Tsh. 50,000,000.

Fedha hizo amelipwa Ndg. Naushad M. Suleiman kutokana na wizi wa fedha na vyombo vya dhahabu uliotokea nyumbani kwake tarehe 13/6/2010 ambapo walinzi wa JKU ndio waliokuwa wakilinda nyumba hiyo. JKU ilifanya malipo hayo bila ya kuzingatia na kufuata taratibu za sheria kuhusiana na tukio hilo. Aidha, njia zilizotumika kumlipa mhusika zimekiuka utaratibu wa sheria ya fedha.

Vielelezo vya taarifa ya tukio la wizi; taarifa ya vyombo vya sheria (Polisi na Mahakama); taarifa ya madai ya mlipwaji na taarifa ya tathmini ya hasara na upotevu; taarifa ya vikao vya menejimenti vilivyojadili hasara na upotevu wa fedha hizo na taarifa za hatua zilizochukuliwa dhidi ya walinzi waliohusika zimekosekana kwa ukaguzi.

Majibu ya JKU:

Ni kweli wamelipa fedha hizo kutokana na kuwa wao ndio walinzi wa Ndg. Naushad baada ya kuarifiwa tukio hilo tarehe 15/06/2010. Baada ya kuripotiwa, waliwatuma Maofisa wao kuthibitisha tukio hilo na baada ya kujiridhsha kutokea kwa wizi huo, walifanya tathmini ya vitu vilivyoibiwa ambapo vilikuwa ni vitu na fedha tasli vyenye thamani ya Tsh. 50,000,000/-, na JKU waliwajibika moja kwa moja kufanya malipo hayo kutona na kifungu cha 5.3 cha Mkataba wa makubalino yao.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikuridhishwa na sababu za uongozi wa JKU kufanya malipo hayo, kutokana na mapungufu mengi yaliyojitikeza. Miongoni mwa mapungufu hayo ni kutoliripoti Pilisi suala hilo mara tu baada ya kutokea kabla ya wao wenyewe kujishuku na kujiingiza katika hatia.

Kwa kuzingatia barua ya Ndg. Noushad ya tarehe 15/06/2010, inayotoa taarifa ya tukio la wizi, tathmini yote ya Tsh. 50,000,000 imefanywa na Ndg. Noushad na sio JKU kama ilivyoelezwa. Jambo ambalo kwa namna yoyote ile, haikupaswa kuaminika usahihi wake.

Kamati haikupata ushahidi wa tathmini ya fedha zilizolipwa kama ndio halali ya upotevu ama wizi uliotokea, na hivyo imepata mashaka makubwa na usahihi wa malipo hayo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kwamba,Uongozi wa JKU uliohusika na malipo hayo, umefanya malipo kinyume na sheria na taratibu na hivyo, Kamati inapendekeza suala hili liangaliwe tena kisheria, lifanyiwe uchunguzi wake na Serikali ichukue hatua zinazofaa za kisheria na kinidhamu kwa watu wote waliohusika.

Hoja Nam. 21.2.1: Mapungufu yaliyojitokeza katika Uvunaji wa Mpunga.

Kikosi cha JKU-Upenja kimelima ekari 45 za mpunga kwa ajili ya matumizi ya kikosi, huku magunia (mapolo) 182 yamevunwa na kusambazwa katika vituo mbali mbali vya kikosi bila ya kufuata utaratibu wa uwekaji wa kumbu kumbu za uingizwaji na utoaji katika ghala. Kutokana na dosari hiyo, mpunga huo haukuweza kujuulikana jinsi ulivyotumika na ni nani waliofaidika.

Majibu ya JKU:

Mpunga huo ulitoka katika kambi ya JKU Upenja kuja Makao Makuu ya JKU na taratibu zore zimetekelezwa.

Uchunguzi wa Kamati:

Baada ya Kamati kutaka kupewa uthibitisho wa vipi magunia hayo yaligaiwa Upenja, ilielezwa kwamba, polo 27 walibadilisha mbegu Upenja na polo 155 ndizo zilizopelekwa Makao Makuu. Aidha, Kamati baada ya kuhitaji kupatiwa ‘Leger book’ na kulikagua, imegundua kuwa hisabu imerikodiwa, ingawa Kamati ilikuwa na wasi wasi kwamba, kurokodiwa huko ni baada ya taarifa ya Kamati kuifanya kazi hoja hii.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inautaka uongozi wa JKU kuwa makini katika kuvuna mpunga na kuweka vizuri taarifa za mavuno hayo.

Hoja Nam. 21.2.2: Malimbikizo ya Madeni:

Tsh. 149,115,200 zinadaiwa na wafanya biashara pamoja na taasisi mbali mbali kwa kutoa huduma kwa JKU. Madeni hayo ni ya muda mrefu na kuwepo kwake ni kinyume na mfumo sahihi wa kiuhasibu unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu ambao unatumika kwa Mawizara ya Serikali.

Majibu ya JKU:

JKU bado inakabiliwa na madeni na ni chamgamoto kubwa kwao, huku bado wakiendelea kuhitaji huduma za wafanya biashara hao. Hata hivyo, wanatumia kidogo walichonacho kupunguza madeni hayo, huku wakiishukuru Serikali kuwasaidia kulipa deni la Kampuni ya Regalia kwa kiasi kikubwa.

Uchunguzi wa Kamati:

Baada ya Kamati kuhitaji kuwasilishiwa barua na uthibitisho wa mawasiliano baina ya JKU na Wizara ya Fedha kwa ajili ya ulipaji wa madeni hayo, Kamati inaendelea na juhudi zake za kutaka suala la madeni ya muda mrefu yasiyolipika, liweze kutatuliwa.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inautaka uongozi wa JKU wakae pamoja na Wizara ya Fedha, ili kuangalia utaratibu wa kulipwa kwa madeni hayo, na taarifa ya hatua za kuchukuliwa iwasilishwe Barazani ili Wajumbe wafahamu hatua zilizochukuliwa.

2.4 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI:

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Sheria namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2) kinazitaka Taasisi zote za Serikali kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka si zaidi ya tarehe 30/09 ya kila mwaka, na Kikosi kimewasilisha hesabu zake kwa kuchelewa tarehe 2/10/2012.

Majibu ya Kikosi:

Wamechelewesha kuwasilisha hesabu kwa wakati kutokana na sababu za kibaadamu, kwamba wakati huo Kamishna wao alikuwa hayupo.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikubaliani na majibu mepesi ya kikosi hicho.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inautaka uongozi wa kikosi kurekebisha mara moja kasoro hiyo.

Hoja Nam. 22.2: Malipo yasiyokuwa na vielelezo (nyaraka pungufu) Tsh. 31,878,324.

Fedha hizo zimelipwa kwa matumiz mbali mbali lakini vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Kikosi:

Uongozi wa kikosi umekiri kukosekana kwa vielelezo hivyo wakati wa ukaguzi, ingawa wakati Kamati ilipofika walithibitisha kwamba wanavyo na kuitaka Kamati ivikague ili hoja ifutwe.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haioni haja ya kuvikagua na sio kazi yake, kwani kwa mujibu wa kifungu cha 70 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, vielelezo (ikiwa ni pamoja na risiti) vinatakiwa vipatikane mara tu fedha ya Serikali inapolipwa. Aidha, Kamati ilielezwa kwamba, uongozi wa kikosi ulielezwa kurudi tena kwa Mkaguzi na ndio maana hawakuvipeleka mapema, jambo ambalo limeshindwa kuthibitishwa kwa ushahidi wowote wa barua ama maandishi.

Mapendekezo ya Kamati:

Uongozi wa Kikosi umekiuka sheria na kanuni ya fedha, kwa kufanya matumizi ya fedha bila ya kuwa na vielelezo kamili, au kuchelewa kuvipata na hivyo, Kamati inapendekeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, kama anavyoteua Maofisa Wahasibu kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) cha sheria Namba 12 ya mwaka 2005, kumpa barua ya Onyo Afisa Mhasibu wa Kikosi hiki ili awe makini wakati anasimamia fedha za umma.

Hoja Nam. 22.3: Malimbikizo ya madeni, Tsh. 120,631,000.

Fedha hizo zinadaiwa na wafanya biashara na taasisi mbali mbali kwa kutoa huduma tofauti kwa Kikosi bila ya kulipwa tena kwa muda mrefu. Kuwepo kwa madeni hayo ni kwenda kinyume na mfumo sahihi wa kiuhasibu unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu ambao unatumika kwa Mawizara ya Serikali.

Majibu ya Kikosi:

Ni kweli kikosi kina madeni tena ya muda mrefu. Walilofanya ni kuiandikia Serikali na kwa bahati baadhi ya wafanya biashara, kwa mfano Regalia ameshalipwa, ingawa madeni yaliyobakia bado hayajalipwa, huku jukumu la malipo hayo likiwaelemea wao.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imegundua madeni hayo ni ya muda mrefu na hayana dalili za kulipwa, hivyo imemtaka Afisa Mhasibu na Mhasibu wa Kikosi kuyaorodhesha madeni yote na kukaa pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mhasibu Mkuu wa Serikali, ili kuyahakiki madeni yote na Serikali kupitia kikao hicho kuwa na kauli moja ya kuyalipa.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kusimamia kikao hicho kilichotajwa katika uchunguzi wa Kamati na hatimae taarifa yake iwasilishwe katika kikao cha kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Mambo mengine yaliyojitokeza kuhusiana na Kikosi:

Mnamo tarehe 8/3/2012, kikosi kimetoa risiti ya kikosi badala ya risiti ya Serikali, huku wakikusanya malipo kutoka Mkoa wa Kusini, Unguja. Kitendo hiki kinadhihirisha kupotea kwa fedha za malipo na kuingia mifukoni mwa wachache.

Majibu ya Kikosi:

Ni kweli huwa wanatoa risiti hizo kutokana na huduma mbali mbali wanazozitoa kwa taasisi za Serikali, na hili ni kwa sababu hawakuwa na account ila sasa wameshatakiwa kuwasilisha Serikalini.

Mapendekezo ya Kamati:

Katika kudhibiti mapato ya Serikali, Kamati inautaka Uongozi wa Kikosi kutumia risiti rasmi kwa kuwasiliana na Mhasibu Mkuu kwa kupewa risiti za Serikali na waache mara moja kutumia risiti binafsi.

2.5 CHUO CHA MAFUNZO:

Hoja Nam. 23.2: Malipo yasiyokuwa na vielelezo (nyaraka pungufu), Tsh. 120,033,000

Fedha hizo zimelipwa kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo havijapatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Chuo:

Ni kweli baadhi ya viambatanisho katika baadhi ya hati za malipo vilikosekana wakati wa ukaguzi, hali iliyosababishwa na baadhi ya wafanyabiashara kuchelewa kuleta risiti lakini sasa viambatanisho hivyo vipo kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imehoji sababu zilizowapelekea kushindwa kuviwasilisha wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti na kuelezwa kwamba, wakaguzi walipewa viambatanisho hivyo baada ya kuondoka na walikwenda kuvipitia, ingawa Chuo kinashangazwa kuona hoja hiyo katika ripoti ya Mkaguzi. Pamoja na majibu haya, Kamati ilihitaji kupewa mawasiliano hayo yaliyoelezwa kufanyika, jambo ambalo limeshindwa kuthibitika.

Kamati ilianza kupita hati za malipo zilizohusika na kwa hati namba 1/11 yenye thamani ya Tsh. 14,622,000 ilielezwa kuwa fedha hizo walizilipa kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe kama mshauri mwelekezi wa ujenzi wa gereza jipya la Hanyegwa Mchana. Aidha, Kamati imeshindwa kupatiwa Mkataba baina yao na kuelezwa kuwa suala hilo lipo Wizarani, vile vile Kamati

haikupata majibu muafaka wa sababu inayopelekea suala hilo kuwepo Wizarani wakati fungu la matumizi lipo chini ya Chuo cha Mafunzo.

Kimsingi, Kamati imegundua mbali na kukosekana kwa mkataba huo, lakini hakukuwa na taratibu za kisheria za kumtafuta na hatimae kumpata Mamlaka ya Mji Mkongwe kwama Mshauri mwelekezi. Suala hilo limefanywa kienyeji tu. Aidha, Kamati imeshtushwa na kupangwa kutumiwa Tsh. 175,000,000 kwa kuilipa Mamlaka ya Mji Mkongwe kama ada ya Ushauri welekezi pekee, huku Tsh. 70,000,000 zikiwa tayari zimeshalipwa.

Aidha, mbali na malipo hayo ya Tsh. 175,000,000, chuo cha Mafunzo kwa gharama zake kimegharamia gharama mbali mbali za kuwasafirisha Dar es Salaam maofisa ama wataalamu hao wa Mji Mkongwe pamoja na gharama nyengine za upimaji wa eneo husika.

Kuhusiana na hati namba 2/11 yenye thamani ya Tsh. 2,940,000 imelipiwa gharama za hoteli huku ikikosa barua ya maombi ya haja ya kukaa hotelini hapo Visitors Inn wala barua ya maombi ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha hati namba 4/11 ya Tsh. 3,200,000 haina barua ya maombi ya fedha zilizoidhinishwa wala hakuna barua ya kuonesha mawasiliano yao na Idara ya Upimaji na Ramani, kama vile pia ilivyokosa saini ya Afisa Mhasibu, Mhasibu wa Chuo na kukosa tarehe iliyoidhinishwa.

Kwa ufupi na kwa kuzingatia kanuni ya 95(4) ya kanuni ya fedha ya mwaka 2005, malipo hayo yamefanyika bila ya kuwa na vielelezo. Na kosa hilo pia kwa matumizi ya hesabu ya kawaida ya Tsh. 40,000,000 zilizolipwa kwa kugharamia timu ya mpira iliyoshiriki club bingwa Afrika, kwamba vielelezo vilivyomo katika hati hiyo ya malipo havijitoshelezi, huku risiti zilizowasilishwa kwa Kamati hazikuwa na Serikali.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imesikitishwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria katika Chuo cha Mafunzo, na kuitaka Serikali ichukue hatua za kuwachukulia za kinidhamu waliohusika.

Hoja Nam. 23.3: Malimbikizo ya madeni, Tsh. 215,800,973

Fedha hizo zinadaiwa na wafanyabiashara pamoja na taasisi mbali mbali kwa jili ya utowaji huduma tofauti kwa Chuo cha Mafunzo. Kuwepo kwa madeni hayo ni kinyume na mfumo sahihi wa kiuhasibu unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu ambao unatumika kwa Mawizara ya Serikali.

Majibu ya Chuo:

Ni kweli Chuo cha Mafunzo kina deni hilo lakini Idara imechukua hatua za kuhakikisha deni hilo inalipwa kwa kadiri fedha zinavyopatikana Serikalini. Hivi saa Tsh. 65,372,000 zimelipwa na Tsh. 150,428,973 bado zinadaiwa.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imehoji uhalali wa madeni hayo na kwa nini yawe kwa watoa huduma walioelezwa. Kwa mfano Sabah Store anahusika na manunuzi mengi, jambo ambalo iwapo Chuo kingelikuwa na Kitengo cha Manunuzi kingelifuatia kwa watoa huduma mbali mbali badala ya kila siku mfanyabishara mmoja. Aidha, Kamati imeelezwa kwamba Sabah Store alipatikana kupitia restricted tendering kwa sababu walitakiwa kumpata supplier huyo ndani ya mwezi mmoja.

Hata hivyo, Kamati haikubaliani na uharaka ulioelezwa kwani Chuo cha Mafunzo kilitakiwa kuwa na mpango wa manunuzi tokea awali na ununuzi wa vifaa hivyo usingekuwa wa haraka hivyo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inautaka uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwa wakati, ili kuepusha kasoro iliyopo.

Hoja Nam. 23.4: Matumizi yaliyofanyika kinyume na vifungu husika, Tsh. 59,869,500.

Fedha hizo zimetumika kinyume na vifungu vilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Aidha, ukaguzi umebaini taratibu za uhaulishaji hazikufuatwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya fedha namba 12 ya mwaka 2005.

Majibu ya Chuo:

Ni kweli Chuo cha Mafunzo kilifanya matumizi hayo kinyume na vifungu, hali iliyosababishwa na ufinyu wa bajeti ambayo haikukidhi huduma zilizohitajika kutokana na kifungu cha chakula cha wanafunzi kukosa fedha za mwezi June 2012.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikubaliani na hoja za Chuo aidha, uhaulishaji wa vifungu hivyo haukufuata taratibu za kisheria. Vile vile Kamati imejiridhisha kwamba, fedha hizo zimetumika kinyume na utaratibu na kukosekana ushahidi wa kutumika taratibu za manunuzi katika matumizi ya fedha hizo.

Fedha hizo zilizohaulishwa kinyume na sheria kutoka kifungu cha ununuzi wa gari na zeimetumika kwa ununuzi wa chakula.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inasikitishwa na uvunjaji wa sheria kwa uongozi wa Chuo na inapendekeza waliohusika wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kukiuka sheria. Aidha, Kamati inasisitiza ufuatwaji wa sheria za fedha na manunuzi.

Hoja Nam. 23.5: Malipo yaliyofanywa kinyume cha kanuni na taratibu za manunuzi, Tsh. 140,510,000

Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali huku manunuzi hayo yakizidi kiwango ambacho kinastahiki kuitishwa utaratibu wa zabuni kwa mujibu wa sheria ya manunuzi.

Majibu ya Chuo:

Ni kweli chuo kilinunua gari hiyo bila ya kufuata taratibu za zabuni. Walichofanya uongozi wa chuo ni kuandika barua kwa iliyokuwa Wizara ya nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuomba idhini ya kufanya hivyo kutokana na kutokuwepo kwa Kitengo cha Manunuzi kwa wakati huo, na ruhusa hiyo ilitolewa.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikuridhishwa na majibu hayo ambayo yanakiuka sheria na inashangazwa kwa Wizara hiyo kuruhusu kuvunjwa kwa Sheria, wakati ndio inayotakiwa kusimamia sheria.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuzisimamia sheria na ni kitendo kisichokubalika kwa Wizara kuruhusu kuvunjwa kwa sheria. Kamati inakitaka Chuo kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria.

Aidha, Kamati inakitaka Chuo kuajiri mtaalamu wa Ukaguzi wa ndani (internal auditor), kuunda 'Audit Committee' ili kuondosha kasoro za kifedha zilizopo.

2.6 MKOA WA MJINI MAGHARIBI:

Hoja Nam 14.1: Bakaa ya Tsh. 535,000 kwa malipo ya Msaada wa Wazee wasiojiweza.

Jumla ya Tsh. 31,705 huingizwa kila mwezi katika kila mkoa kwa mikoa mitatu Unguja kwa ajili ya ulipaji wa fedha za msaada kwa wazee. Ukaguzi umebaini fedha zilizotumika kwa kila mwezi ni Tsh. 26,350,000 kuwalipa wazee hao na kuacha bakaa ya Tsh. 5,355,000 kwa kila mwezi ambazo matumizi pamoja na vielelezo vyake au marejesho yake havikupatikana kwa ukaguzi. Hali hii imepelekea Tsh. 224,910,000 kwa kipindi kilichokaguliwa kutojuulikana matumizi yake au marejesho yake (na kwa upande wa Mkoa wa Mjini Magharib ni Tsh. 535,000).

Majibu ya Afisi ya Mkoa:

Kwa kawaida Wzee wanaohusika na Mkoa huu huja kuchukua fedha zao na Afisi ilikuwa inatangaza kwa uwazi na wanaolipa ni Maofisa Ustawi wa Jamii. Fedha zilizobakia na zinazohusika na hoja hii ni katika mwezi wa ukaguzi kufuatia zoezi la ukaguzi uliofanyika mwezi wa March, wazee hawakulipwa mwezi huo ila walilipwa mwezi uliofuata. Na fedha zilikuwa Tsh. 80,000 na sio 535, 000 kama ilivyoripotiwa.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imepatiwa orodha ya malipo na imejiridhisha usahihi wake, ingawa haikupata muda wa kuwapitia wazee wenyewe na kuwahoji, zaidi ya kuangalia saini za mapokezi ya fedha hizo.

Kuhusiana na tofauti ya idadi ya fedha baina ya Mdhibiti na Afisi ya Mkoa, Kamati ilimtaka Afisa Mdhibiti aliefuatana na Kamati kutoa ufafanuzi wa usahihi, ambapo ilielezwa taarifa za Mdhibiti ni sahihi kwani ndio zilivyoripotiwa na kama ingelikuwa si sahihi, basi Afisi ya Mkoa ingelishughulikia suala hilo mapema.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imeridhika na majibu ya Afisi ya Mkoa na kushauri hoja hii ifutwe, mpaka pale Afisi ya Mdhibiti itakavyoweza kuthibitisha vyenginevyo.

2.7 MKOA WA KUSINI UNGUJA.

Hoja Nam. 25.1: HESABU ZA MWISHO WA MWAKA 2011/2012.

Taarifa za Matumizi ya kazi za Kawaida:

Mkoa wa Kusini Unguja iliidhinishiwa kutumia Tsh. 886,300,000 kwa kazi za kawaida katika mwaka 2011/2012 na ilipofikia Juni 2012 iliingiziwa Tsh. 873,153,000 sawa na 98.5% ya makadirio ikiwa ni pungufu ya Tsh. 13,147,000 (1.48%) ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi kwa kazi za Maendeleo:

Afisi iliidhinishiwa kutumia Tsh. 20,000,000 kwa kazi za maendeleo kwa kipindi cha 2011/2012, na ilipofikia Juni 2012, fedha zilizoingizwa na kutumika ni Tsh. 20,000,000 (100%) ya makadirio.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imekagua matumizi ya fedha za maendeleo na kugundua kuzidi kwa Tsh. 138,000 na kufanya fedha zote kuwa Tsh. 20,138,000 (na sio tu 20,000,000 kama ilivyoelezwa). Wakati ilipofanya ukaguzi wa baadhi ya hati za malipo za fedha hizo, imejiridhisha kupitia Vocha Namba 1/2, cheque Namba 030139 kwamba haina barua ya maombi ya mahitaji ila vielelezo vilobakia vipo. Aidha, tatizo hili limejionesha katika vocha namba 7/2 ya tarehe 20/2/2012 kupitia cheque namba 030274 na pia takriban katika vocha zote zilohusika na matumizi hayo.

Vile vile vocha namba 6/2 ya tarehe 13/02/2012, cheque namba 030219 haina uthibitisho wa maombi ya mahitaji wala maombi ya matumizi fedha hizo kumuomba idhini Afisa Tawala (Afisa Mhasibu). Huku, vocha namba 3/2, cheque namba 030141 ya Tsh. 3,500,000, Tax invoice ya Alhakim General Traders, aliyelipwa fedha hizo, imetofautiana na risiti aliyoitoa katika namba ya invoice na tarehe iliyotolewa.

Vocha namba 3/3 ya tarehe 07 May 2012 haina sahihi ya 'Authorising Officer' wala vielelezo vya kuthibitisha malipo husika, huku kukiwa na barua moja tu ya tarehe 8/3/2012 inayoonesha maombi ya Tsh. 500,000 badala ya maombi ya fedha zote Tsh. 860,000 zilizohusika na vocha hii.

Kimsingi Kamati imejiridhisha kuwepo kwa kasoro nyingi zinazotokana na kutokuwepo kwa Afisa Manunuzi na Kitengo cha Manunuzi cha Afisi hii.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Afisi irekebishe mara moja kasoro zilizojitokeza, huku inaitaka Wizara ya Fedha kwa mashirikiano na Wizara husika, kupatika kwa maofisa Ununuzi na Afisi ya Mkoa inaagizwa kuunda Kitengo cha Manunuzi na Ugavi, mara moja.

Hoja Nam. 25.2.1: HESABU YA AMANA (DEPOSIT ACCOUNT); Bakaa la malipo ya msaada wa wazee Tsh. 43,119,150.

Ukaguzi umebaini kwamba, Tsh. 43,119,150 ikiwa ni bakaa ya fedha zilizokuwa zikiingizwa kwa ajili ya malipo ya wazee ya kila mwezi. Bakaa hiyo inatokana na kuingizwa fedha nyingi kwa ajili ya malipo ya wazee ambao idadi yao haikulingana na wazee halisi waliopo kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo kufariki, kuhama maeneo waliyokuweko awali na majina ya wazee wasiokuwepo. Aidha, vielelezo vya marejesho au matumizi ya fedha hizo havikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Afisi ya Mkoa:

Idadi ya fedha iliyotajwa na ripoti ya Mkaguzi ya Tsh. 43,119,150 haiko sahihi na badala yake fedha hizo ni Tsh. 30,125,000. Aidha, Afisi ya Mkoa wa Kusini inakiri kutoingizwa kwa malipo fedha walizozieleza kutokana na watendaji waliohusika na suala la malipo kwa wakati huo, hawakuwa waadilifu na badala yake fedha hizo zimeishia mikononi mwao.

Aidha, hatua walizozichukua ni kutoa taarifa Polisi na waliohusika taarifa zao ziko Polisi na wamesimamishwa kazi, huku Polisi wakikamilisha taratibu za kipelelezi na hatimae suala hilo lipelekwe Mahakamani. Aidha, taarifa zote zinazohusika na suala hili ziko Polisi na Afisi haina hata kopi ya taarifa hizo.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilihoji iwapo hatua za suala hili kupelekwa Polisi kama ni mara tu baada ya Mdhibiti hutoa ripoti yake au kabla, na ikajiridhisha kwamba, sula hilo limepelekwa Polisi baada ya taarifa zake kutoka kupitia ripoti, jambo ambalo halikuwa vyema na badala yake lilitakiwa lisubiri taarifa na mapendekezo ya Kamati.

Aidha, Kamati imekosa orodha ya wazee waliohusika na malipo kama pia ilivyokosa taarifa za upotevu wa fedha hizo, jambo ambalo limeizuia Kamati kulifuatilia kwa kina na kutoa taarifa zake sahihi suala hili.

Aidha, Kamati ilielezwa kwamba, fedha zinazodaiwa kupotea ambazo ni bakaa ya fedha zilizoingizwa kwa malipo ya wazee wasiojiweza (Tsh, 30,125,000 mara nyengine pia zinaelezwa kuwa Tsh. 10,000,000) bado zipo mikononi mwa Afisi, huku wakitakiwa kuzirejesha Hazina kupitia Akaunti ya 'Deposit' jambo ambalo halikufanyika kutokana na Afisi kueleza kwamba, wametakiwa na Polisi kukaa nazo kama ni sehemu ya ushahidi na kuweza kuthibitisha muda wowote wanaotakiwa kufanya hivyo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, na kwa kuzingatia kwamba, imekosa taarifa sahihi za kuthibitisha upotevu unaodaiwa kwa maelezo kuwa viko Polisi, Kamati inapendekeza kupatiwa muda wa ziada kulifanyia kazi suala hili ili iweze kutoa taarifa za kina na sahihi zaidi.

2.8 MKOA WA KASKAZINI - UNGUJA

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishwaji wa Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi.

Ukaguzi umebaini kuwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja haukuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya ukaguzi kama ilivyoelezwa na kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha Namba 12/2005 pamoja na kifungu cha 8 cha Sheria hiyo.

Majibu ya Mkoa:

Mkoa uliwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo badala ya kuziwasilisha hesabu hizo katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Baada ya kubaini kosa hilo Mkoa wa Kaskazini uliwasilisha taarifa hiyo kunakostahiki mnamo tarehe 21 Machi, 2013.

Uchunguzi wa Kamati:

Pamoja na maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, Kamati hii haikukubaliana na maelezo hayo. Hii ni kutokana na kuwa hakuna hata mwaka wa fedha mmoja ambao Mkoa wa Kaskazini uliwasilisha taarifa zake Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Aidha, Afisi ya Mkoa huu imeshindwa kuonesha kielelezo (i.e barua au 'dispatch') kinachothibitisha kauli

yao hiyo. Pia, imebainikia kuwa ripoti hiyo imeandaliwa baada ya kuteuliwa kwa Afisa Tawala aliyekuwepo hivi sasa.

Sambamba na hilo, Kamati imeoneshwa taarifa iliyowasilishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo, taarifa hiyo imeonekana kuwa na baadhi ya mapungufu, yakiwemo ya kutokuwekwa thamani ya samani zinazomilikiwa na Ofisi hiyo. Kitendo hiki kinaashiria kwamba ufungwaji wa hesabu hauko sahihi.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imeutaka Mkoa wa Kaskazini – Unguja kuwa na buku daftari litakaloandikwa kumbukumbu za mali 'Asset Register' badala la kutumika 'Vote book'. Vile vile, imemtaka Afisa Tawala, Mhasibu pamoja na watendaji wote wa Mkoa huo kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Kamati imeutaka Mkoa huo kufuatilia Wizara ya Fedha thamani halisi ya samani zilizopo Ofisini hapo kwa kuwa Ofisi hii ilipokea samani hizo kutoka Wizara ya Fedha ikiwa ni msaada kutoka kwa Mhe. Mohammed Raza mnamo miaka ya tisini.

2.9 BARAZA LA MANISPAA:

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu kwa ajili ya ukaguzi:

Pamoja na Sheria ya Fedha za Umma, namba 12 ya mwaka 2005, katika kifungu cha 24(2) kuelekeza na kuzitaka Taasisi zote za Serikali, ikiwa ni pamoja na Baraza la Manispaa, kufunga na kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar, Baraza la Manispaa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 halijawasilisha hesabu hizo.

Majibu ya Baraza:

Ni kweli hawajawasilisha kutokana na tatizo la kisheria. Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2) kweli kinawataka wawasilishe, lakini kifungu cha 47(2) cha Sheria Namba 3 ya mwaka 1995, kinawataka wafunge hesabu hizo kwa muongozo wa Wizara ya Fedha. Hivyo, wao wangelisubiri muongozo huo kutoka Wizara ya Fedha ambao bado hawajaupata.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikubaliani na maelezo ya Afisi ya Baraza kwani sheria zote mbili zinawataka wafunge hesabu zao na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Kifungu hicho cha 47(2) cha Sheria namba 3 ya mwaka 1995, kinawataka Baraza kuandaa hesabu za mwisho wa mwaka, ambazo pamoja na maelekezo mengine, taarifa zake nyengine zitakuwa zile zilizoelezwa na Wizara ya Fedha. Hapa Kamati haikatai kuwa kuna taarifa wanatakiwa waziandae kama inavyoelezwa na Wizara ya Fedha, lakini haikubaliani kwamba Baraza lisiandae na kuwasilisha hesabu hizo, kwani sheria iko wazi kuwataka wafanye hivyo.

Aidha, kufuatia mashauriano hayo ya kisheria, Baraza lilikubaliana na maelekezo ya Kamati na kueleza kwamba, wanakwanzwa kutokana na uwezo mdogo wa watendaji wao. Hata hivyo, wameahidi kurekebisha kasoro hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inamtaka Mkurugenzi wa Baraza hili kusimamia masharti na maelekezo ya sheria inavyostahiki na kuhakikisha wanafunga hesabu zao za mwisho wa mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti ndani ya muda ulioelezwa kisheria.

Hoja Nam. 38.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2011/2012. Taarifa za Mapato na Matumizi.

Baraza lilikadiriwa kukusanya Tsh. 2,135,872,200 kwa mwaka 2011/2012, na kufanikiwa kukusanya Tsh. 2,430,984,383, ikiwa ni ongezeko la wastani wa 14 ya makadirio.

Matumizi ya kawaida yalikuwa Tsh. 3,078,492,745 lakini hali halisi ya matumizi ilikuwa ni Tsh. 2,562,215,343.15 ikiwa ni 83.2 ya makadirio, na ni pungufu ya Tsh. 516,277,401.85 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Baraza lilikadiriwa kutumia Tsh. 146,600,000 kwa kazi za maendeleo na hatimae kuingizwa na kutumika Tsh. 61,339,400 sawa na 41.8 ya makadirio, ikiwa ni pungufu ya Tsh. 85,260,600, sawa na 58.2% ya makadirio.

Majibu ya Baraza:

Baraza linakubaliana na kuongezeka kwa makusanyo mbali mbali na hakukua na utaratibu maalum wa uhakika wa makusanyo (baseline), Baraza mara nyingi hufanya makisio kwa mnasaba wa bajeti ya mwaka iliyopita.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imehoji utaratibu unaotumiwa na Baraza hili katika kufanya makisio mbali mbali ya mapato na kuelezwa udhaifu huo wa makisio unatokana na kutokuwepo kwa watendaji wenye uwezo mkubwa wa masuala ya fedha hapo awali, ingawa sasa Baraza limeshapata wataalamu hao.

Aidha, Kamati imejiridhisha kwamba, nyongeza hiyo ya makusanyo na hata matumizi hayajapata idhini ya Baraza la Madiwani, na ni sawa na kusema fedha zimetumika kinyume na taratibu za kisheria.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imechukizwa kwa Baraza la Manispaa kukiuka sheria wakati linatakiwa kuwa kigezo kwa Mabaraza ya Miji na Halmashauri mbali mbali. Aidha, Kamati inautaka uongozi wa Baraza kurekebishe mara moja kasoro hizo.

Hoja Nam. 38.2: Malipo yasiyokuwa na vielelezo (Nyaraka pungufu), Tsh. 14,500,000

Fedha hizo zimelipwa kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Baraza:

Malipo hayo ni halali na walilipwa Madiwani kusaidia maendeleo ya wananchi katika wadi wanazoziwakilisha. Walipopokea fedha hizo Madiwani walitia saini katika hati za malipo ambayo ipo kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Vielelezo vilivyowasilishwa kwa Kamati sio sahihi kwa mnasaba wa hoja. Aidha, Kamati ilipovipitia imejiridhisha kwamba, risiti za malipo haziko sahihi, hazina VAT namba, vimekozeshwa na kufutwa futwa kama kwamba kuna ubabaifu unataka kufanyika. Aidha, vielelezo vyengine vimekosekana, aidha fedha zote zilizoonekana katika vielelezo vilivyowasilishwa kwa Kamati ni Tsh. 6,795,000 na sio Tsh. 14,500,000 kama ilivyoelezwa na Mdhibiti.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imechukizwa na upotevu wa vielelezo tena ikizingatiwa malipo hayo yamefanywa kwa Madiwani, viongozi wa Baraza hili. Kamati inautaka uongozi wa sasa wa Baraza la Manispaa kufanya juhudi za kufuata sheria ili makosa haya yasirejee tena.

Hoja Nam. 38.3: Mlimbikizo ya madeni wanayodai Baraza la Manispaa, Kitengo cha Mabango Tsh. 78,072,000

Baraza limebainika kuzidai baadhi ya taasisi fedha zilizoinishwa hapo juu kutokana na huduma zilizotolewa na Kitengo cha Mabango, hadi kufikia Juni 2012.

Majibu ya Baraza:

Ni kweli Baraza linazidai taasisi hizo kutokana na kuzipa fursa ya kuweka matangazo yao huku bado wakiwa wanadaiwa. Aidha, Airtel Zanzibar hawadaiwi kwa sababu huduma ya kuhaulisha malipo haikufanyika. Wao waliomba kuweka matangazo yao pamoja na kupatiwa gharama zake kabla ya Mkataba, ingawaje hadi leo hawajajitokeza, ingawaje kumbu kumbu ilisahauliwa kufutwa kabla ya kuja Mkaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imegundua kuwa kuna baadhi ya madeni yamelipwa ingawaje mengine bado hayajalipwa. Kwa mfano Tanadvert hajalipa bado deni lake la Tsh. 600,000; kuhusiana na Airtel Zanzibar, Kamati imeshindwa kujiridhisha na majibu ya Baraza kwa kushindwa kumuelekeza mapema Mdhibiti, huku Baraza likiwa limetoa tax invoice. Hata hivyo, Kamati inakubaliana kwamba, deni hilo limebaki Tsh. 31,594,000 badala ya Tsh. 78,072,000.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaelekeza kukamilishwa kulipwa kwa madeni hayo.

2.10 HAMLASHAURI YA WILAYA YA MAGHARIBI:

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Sheria namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2) kinazitaka Taasisi zote za Serikali kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka si zaidi ya tarehe 30/09 ya kila mwaka, huku Hamlashauri ya Wilaya ya Magharibi ikishindwa kuwasilisha kabisa hesabu zake kwa Mkaguzi.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli kwa mwaka 2011/2012 Halmashauri haikuwasilisha hesabu zake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwani walikuwa wanawasilisha hesabu zao kupitia Wizara inasimamia Halmashauri. Aidha, kutokana na hoja hii, Halmashauri zote zimekaa na Wizara yao na kukubaliana kuwasilisha hesabu hizo kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013, na kipindi hichi wanawasiliana na wataalamu wa kufunga hesabu.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imeshtushwa na kauli ya Halmashauri ya kutafuta wataalamu, wakati wameajiri Mhasibu na wasaidizi wake wa kazi, pamoja na kuelezwa uwezo mdogo wa wataalamu hawa. Aidha, baada ya kuelezwa kwamba, Mhasibu huyu ana elimu ya Post Graduate Diploma ya Uhasibu, ilishangaa sana kushindwa kufunga hesabu zake.

Vile vile Kamati iligundua kuwa, Halmashauri imepanga kutumia Tsh. 5,000,000 kwa ajili ya kuwalipa wataalamu wa nje, huku kazi yao kubwa ni kushauri na kazi ya vitendo ikifanywa na wataalamu wa Halmshauri hii, na zaidi Kamati imefahamu kwamba, Halmashauri haina kifungu cha bajeti cha malipo hayo ya fedha, na utaratibu wa kuwatafuta wataalamu hao wa kufunga hesabu haukufuata sheria za manunuzi na ugavi.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuangalia uwezo wa wataalamu wanaowapeleka katika Halmashauri uendane na kazi za Halmashauri na sio kuangalia kiwango kikubwa cha elimu, wakati uwezo wa wataalamu hao ni mdogo. Aidha, Kamati inaitaka Halmashauri izingatie na kufuata kikamilifu taratibu za kisheria katika kutafuta wataalamu wa kufunga hesabu na hata taratibu za malipo yao.

Hoja Nam. 29.2: Taarifa ya utekelezaji wa matumizi:

Taarifa ya utekelezaji wa matumizi kwa mwaka unaoishia tarehe 30/06/2012, umegundulika kuwa na tofauti kubwa katika vifungu vya matumizi kati ya makisio (budget) na matumizi halisi (actual), hali iliyopelekea kupindukia kwa matumizi ya baadhi ya vifungu. Aidha, ziada ya matumizi hayo haikuidhinishwa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri hii.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli Halmashauri imefanya hivyo, kutokana na kutokuwa na uhakika wa mapato ambayo huyatumia katika uendeshaji wa shughuli za miradi ya maendeleo na kazi za kawaida na hii ni miongozi mwa kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato ambavyo vingi vyao sasa vinakusanywa na ZRB, Bodi ya Madawa, Mifugo, Misitu n.k na kutokuwa na watendaji wa kutosha wenye ujuzi katika kitengo cha ukusanyaji wa mapato.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamatiilihitaji uthibitisho wa kikao cha Madiwani kilichokaa kuidhinisha matumizi hayo, kitu ambacho kilishindwa kuthibitishwa. Aidha, Uongozi wa Halmashauri ulikiri kukiuka sheria ya kufanya matumizi bila ya idhini ya Baraza la Madiwani.

Aidha, Kamati imepitia matumizi hayo yaliyofanywa kinyume na sheria, na kwa mfano, Vocha inahusika na ununuzi wa tela la kubebea wanyama, Tsh. 8,500,000 haikuwa na maombi ya ununuzi huo wala idhini ya Bodi ya Zabuni ya kuuhusu njia ya manunuzi iliyotumika.

Kuhusiana na matumizi ya Tsh. 23,010,000 yaliyofanywa kwa vocha tatu tofauti, hakuna barua ya maombi ya matumizi yake wala barua ya maombi ya fedha zilizotumika.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi iunde haraka iwezekanavyo Kamati ya Ukaguzi (Audit Committee), ili kupunguza kasoro nyingi za kihesabu.

Kamati inaitaka Halmashauri kurekebisha mara moja kasoro zilizojitokeza, huku ikiitaka Serikali kupeleka watendaji wenye uwezo katika Halmashauri hiyo.

Hoja Nam. 29.2.1: Vifungu vya malipo vilivyofanywa nje ya bajeti, Tsh. 20,100,000.

Kwa mwaka 2011/2012 Halmashauri iliidhinisha matumizi ya ununuzi wa vifaa mbali mbali, bila ya makisio ya bajeti. Hali hii hupelekea bajeti kutoonekana kama chombo cha udhibiti wa matumizi.

Majibu ya Halmashauri:

Halmshauri ilifanya matumizi hayo kwa kupata ridhaa ya kikao cha Baraza la Madiwani. Aidha, manunuzi ya projector, camera na vifaa vyengine vimepata Baraka hiyo kwa ajili ya kukiimarisha Kitengo cha Habari ambacho hakikuwa na vifaa hivyo.

Kuhusiana na ununuzi wa suti za Waheshimiwa Mdiwani, nao unatokana na maamuzi ya kikao cha Baraza ambapo Kamati ya Fedha ya tarehe 16/07/2011, kiliiagiza Ofisi ya Halmashauri kutekeleza suala hilo.

Uchunguzi wa Kamati:

Viongozi wa Halmashauri wanashindwa kufahamu majukumu ya Baraza la Madiwani, kama ilivyotajwa na kifungu cha 45(2) cha Sheria namba 4 ya 1995, hatimae kazi za Baraza hufanywa na Kamati ya Fedha ya Halmashauri kinyume na maelekezo ya sheria. Aidha, kamati imepatiwa kumbu kumbu mbili kuhusiana na majibu ya hoja hii, ambazo zote ni za Kamati ya fedha na sio Kikao cha Baraza la Madiwani.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imeridhika kwamba, sheria imekiukwa kwa kufanya matumizi nje ya bajeti na nje ya vikao halali vya Baraza la Madiwani na linawataka Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kufahamu wajibu wao ili kuleta ufanisi. Aidha, Serikali itoe mafunzo kwa watendaji na Waheshimiwa Madiwani na Wizara iwasimamie watendaji kutekeleza kazi za Halmashauri kwa mujibu wa sheria.

2.11 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI-UNGUJA:

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja, imeshindwa kabisa kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kinyume na Sheria namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2) kinachozitaka Taasisi zote za Serikali kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka si zaidi ya tarehe 30/09 ya kila mwaka.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli Halmashauri imekiuka sheria ya fedha Namba 12 ya mwaka 2005, pamoja na kukiuka masharti ya sheria namba 4 ya mwaka 1995 kwa kutowasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kutokana na mazoea ya hapo awali kuwasilisha taarifa zao za mapato na matumizi kwa Katibu Mkuu wa Wizara inayosimamia Halmashauri hizi.

Uchunguzi wa Kamati:

Mbali na uongozi wa Halmashauri kukiri kosa hilo, tatizo jengine ni kwamba, Madiwani wa Halmashauri hizi ambao ndio wasimamizi wa shughuli za Halmashauri, hawajui wajibu huu wa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa sheria.

Hoja Nam. 30.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka:

Taarifa ya mapato na matumizi:

Halmashauri ilikadiriwa kukusanya Tsh. 94,676,000 kwa mwaka 2011/2012 na ilipofika June 2012, ilikusanya Tsh. 131,249,193 sawa na 138.6 ya makadirio.

Aidha, iliidhinishiwa kutumia Tsh. 60,536,000 kwa kazi za kawaida na kwa kazi za maendeleo ni Tsh. 35,000,000. Hata hivyo, hadi kufikia Juni 2012 ilitumia Tsh. 139,425,875 kwa kazi za kawaida na maendeleo huku kukiwa na ongezeko la Tsh. 43,889,875 (46% ya makadirio).

Majibu ya Halmashauri:

Kuhusiana na kukusanya fedha nyingi kuliko walivyokadiria, ofisi ilieleza kwamba, kumetokana na Ofisi kukaza kamba na kuwa makini katika ukusanyaji.

Uchunguzi wa Kamati:

Pamoja na Ofisi ya Halmashauri ikiwa chini ya Katibu wake kujibu hoja hii, Kamati ilihoji iwapo makusanyo hayo yaliyoongezeka yalipata idhini ya Baraza la Madiwani, lakini kutokana na kuwa Katibu wa Halmashauri alikuja ikiwa tayari bajeti imeshapitishwa, Kamati haikupata majibu muafaka wa suala hili.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kufanya makisio halisi ya uwezo wao wa juu katika makusanyo na isiwe katika kiwango cha chini. Aidha, makusanyo yote pamoja na nyongeza yake yapate idhini ya Baraza la Madiwani kama sheria namba 4 ya mwaka 1995 inavyoelekeza.

Hoja Nam. 30.2: Taarifa ya utekelezaji wa matumizi:

Taarifa ya utekelezaji wa matumizi kwa mwaka unaoishia tarehe 30/06/2012, umegundulika kuwa na tofauti kubwa katika vifungu vya matumizi kati ya makisio (budget) na matumizi halisi (actual), hali iliyopelekea kupindukia kwa matumizi ya baadhi ya vifungu. Aidha, ziada ya matumizi hayo haikuidhinishwa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri hii.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli Halmashauri imefanya matumizi ya ziada kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya uendeshaji wa shughuli za kila siku.

Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa zao, ongezeko hilo ni Tsh. 28,170,750 sawa na 20% na sio Tsh. 33,425,350 sawa na 24% kama ilivyoelezwa na Mdhibiti. Pia ongezeko hilo limepata idhini ya Baraza la Madiwani.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilihitaji kupatiwa uthibitisho wa kikao cha Baraza la Madiwani lililoidhinisha matumizi hayo, na kupewa kumbu kumbu ambazo zinathibitisha kwamba, kikao hicho kimekaa baada ya matumiz hayo kufanyika. Aidha, Kamati ilifanya mahojiano kuhusiana na tofauti ya hesabu iliyoelezwa na Halmashauri kwa kutakiwa kuleta uthibitisho wa matumizi yote waliyofanya, walikiri hatimae kwamba, hesabu iliyoelezwa na Mdhibiti kuwa ni sahihi.

Kuruatia hali hii na kwa kuzingatia hesabu waliyoiwasilisha kwa Kamati kuwepo na tofauti ya Tsh. 5,254,600 ambazo Kamati imehitaji kupewa ushahidi wa matumizi yake, jambo ambalo lilipelekea Kamati kutaka muda wa ziada kwa ajili ya kufuatilia hoja hii, bila ya mafanikio.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kufamya matumizi yote na makusanyo yake, kwa kupata idhini ya Baraza la Madiwani kama inavyoelekezwa na sheria namba 4 ya mwaka 1995. Aidha, kuhusiana na tofauti ya hesabu hiyo, Kamati inahitaji muda wa ziada ili ifuatilia hesabu hiyo na kutoa maoni yake yanayofaa.

2.12 HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI:

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Halmashauri haikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kinyume na Sheria namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2) kinachozitaka Taasisi zote za Serikali kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka si zaidi ya tarehe 30/09 ya kila mwaka.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli Halmashauri imeshindwa kuwasilisha taarifa ya mwaka kwani haijapata mfumo rasmi wa utaoji wa taarifa za kila mwaka. Hivyo, wanawasiliana na Wizara ya Fedha ili waweze kupata muongozo wa kutumia kutayarisha na kuwasilisha taarifa ya mwaka ili kosa la aina hiyo lisitokee tena.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imehoji uwezo wa Mhasibu wa Halmashauri hii na kuelezwa kuwa ana Post Graduate Diploma ya Uhasibu, lakini kilichoishangaza Kamati ni kushindwa kwake kufunga hesabu na kuziwasilisha kwa Mkaguzi, wakati muongozo tayari umeshatolewa katika sheria namba 12 ya mwaka 2005, sheria ya fedha za Umma ambayo kila Mhasibu huifanyia kazi. Aidha, kufuatia udhaifu huo, Kamati ilihoji iwapo Halmashauri ina Daftari la kuhifadhia mali za kudumu na kugundua kuwa haina wala haijaweka taarifa za mali zake katika muongozo uliotolewa na Wizara ya Fedha.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kufunga na kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa sheria.

Hoja Nam. 33.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka:

Taarifa ya mapato na matumizi:

Halmashauri ilikadiriwa kukusanya Tsh. 175,000,000 kwa mwaka 2011/2012 na ilipofika June 2012, ilikusanya Tsh. 174,250,151 sawa na 99.6 ya makadirio.

Aidha, ilikadiriwa kutumia Tsh. 174,000,000 kwa kazi za kawaida katika kipindi kinachoishia Juni 2012.

Uchunguzi wa Kamati:

Pamoja na kwamba, Mdhibiti hakuonesha matumizi ya kawaida, Kamati ilihitaji kupatiwa ufafanuzi huo na kuelezwa kwamba, walitumia Tsh. 158,246,030 kukiwa na upungufu wa Tsh. 15,753,970 ya makadirio.

Kufuatia mahojiano, Kamati ilielezwa kwamba, Halmashauri ilipanga kujenga soko la Chwaka kwa mwaka huo, lakini kutokana na kukosa kiwanja, walishindwa kujenga. hata hivyo, Kamati iligundua kuwa, mradi huo ulitokana na Halmashauri na sio wananchi, kiasi ambacho haukuweza kupata mashirikiano ya wananchi hao.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kufanya makisio na matumizi ya fedha za kawaida na maendeleo kwa kuangalia vipaumbele na mahitaji yatokanayo ya wananchi.

Hoja Nam. 33.2: Kukosekana kwa kumbu kumbu za vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya wananchi, Tsh. 35,000,000.

Fedha hizo zimetumika kwa ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya wananchi wa Wilayah ii, lakini wakaguzi wameshindwa kupatiwa kumbu kumbu za upekeaji wake, utoaji na utumiaji wa vifaa hivyo.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli fedha hizo zimetumika kwa matumizi yaliyotajwa, ingawaje wakaguzi hawakuwahi kulifanyia ukaguzi buku la stoo (store ledger) la miradi husika, wakati vitu hivyo vilikuwa vimesharikodiwa tokea awali na kuwasilishwa kwa wananchi na kutumika katika miradi kama ilivyokusudiwa.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imehoji juu ya vifaa hivyo kutoonekana na wakaguzi jambo ambalo halikuweza kuthibitishwa na majibu ya Halmashauri zaidi ya kueleza kwamba, alipokuja mkaguzi, afisa wao wa stoo alikuwa anafanya mtihani. Aidha, pamoja na Kamati kushuhudia kurikodiwa kwa vifaa hivyo, Kamati haikutaka kuthibitisha uingizwaji huo, kwani hiyo ni kazi ya Mdhibiti.

Vile vile Kamati ilipitia baadhi ya matumizi yalihohusika, na kwa mfano Hundi namba 977620 ya tarehe 8/3/2012 haina barua yoyote ya maombi ya haja ya kufanywa manunuzi wala barua ya kuomba fedha hizo, wala haijaidhinishwa matumizi yake na Afisa Mhasibu, wala saini ya mpokeaji wa fedha hizo, aidha vocha nyingi zilizoshuhudiwa na Kamati zimeonekana kufutwa kwa wino, jambo linaloashiria ubabaifu wa matumizi yake.

Mapendekezo ya Kamati:

Pamoja na juhudi za Serikali kufanya marekebisho ya Serikali za Mitaa, ikiwa ni pamoja na Halmashauri, Kamati inapendekeza marekebisho hayo yaelekezwe zaidi kwa Halmashauri hii, ambayo bado ina mapungufu makubwa ya matumizi ya fedha za umma.

2.13 HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI 'A':

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Kwa mwaka 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A, haikuwasilisisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kinyume na maelekezo ya kifungu cha 24(2) cha sheria namba 12 ya mwaka 2005. Aidha kufanya hivyo ni kukiuka sheria inayoanzisha Halmashauri hizi, namba 4 ya mwaka 1995, kifungu cha 43.

Majibu ya Halmashauri:

Kwa kipindi hicho hakukuwa na muongozo wa kutayarisha na kuwasilisha hesabu hizo za Halmashauri na badala yake walikuwa wanawasilisha taarifa zao za mapato na matumizi kwa Wizara ya Fedha. Aidha, Halmashauri imejipanga kutekeleza maelekezo ya sheria .

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikubaliani na maelezo ya Halmashauri kuhusiana na muongozo wa kufunga na kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa sababu sheria ya Fedha za Umma, ya mwaka 2005 tayari imeshatoa muongozo huo na ni wajibu wa Halmashauri kupitia wataalamu wake wa fedha, kuufuata na kutekeleza kisheria.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kufunga na kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa sheria.

Hoja Nam. 31.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka:

Taarifa ya mapato na matumizi:

Kwa mwaka 2011/2012, makadirio ya makusanyo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' ilikua ni kukusanya Tsh. 33,000,000 na ilipofika June 2012, iliweza kukusanya Tsh. 199,730,000 zikiwa ni sawa na asilimia 605.2 ya makadirio.

Kwa matumizi ya kawaida, Halmashauri ilikadiriwa kutumia Tsh. 20,460,000 na ilipofika Juni 2012, iliweza kutumia Tsh. 103,768,500, sawa na 507% ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri:

Hesabu za mapato wanazozifahamu wao ni Tsh. 189,730, 000 na sio 33,000,000 kama ilivyoripotiwa na Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati:

Pamoja na majibu ya Halmashauri, Kamati ilihitaji ushahidi wa majibu yao kupitia kumbu kumbu za kikao cha Baraza la Madiwani walioidhinisha fedha hizo na majibu waliyompelekea Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, baada ya kufahamu tofauti ya hesabu hiyo. Hata hivyo, hakuna ushahidi wowote ulioletwa mbele ya Kamati hali inayoifanya Kamati kuamini usahihi wa maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kukusanya mapato na kufanya matumizi kwa kuzingatia sheria na sio vyenginevyo.

Hoja Nam. 31.2: Makusanyo yasiyopelekwa Benki. Tsh. 14,200,00.

Fedha hizo zilikusanywa mwaka 2011/2012 ikiwa ni mapato ya lesenu za vileo, lakini ukaguzi umebaini fedha hizo hazikupelekwa benki ambapo ni kinyume na sheria za fedha za mwaka 2005.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli Halmashauri walifanya kosa kwa mwaka huo kwa kutopeleka Benki mapato yao kama yalivyoripotiwa na Mdhibiti, ingawa sasa tayari kosa hilo wamelirekebisha na mapato yote yanapelekwa Benki kama ilivyo sheria.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imefurahishwa kwa Halmashauri kujibu ukweli wa hoja hii. Aidha, baada ya kuelezwa kurekebishwa kwa kasoro hiyo, Kamati ilijiridhisha.

Mapendekezo ya Kamati:

Halmashauri iwe makini katika kutekeleza majukumu ya sheria, huku ikimtaka Katibu wa Halmashauri hii kuhakikisha fedha zote zinapelekwa Benki kama inavyoelekezwa na sheria.

Hoja Nam. 31.2.1: Upotevu wa Risiti za kukusanyia mapato:

Imebainika kwamba, baadhi ya risiti katika Halmashauri hii zimechanwa nakala zake zote, hali iliyopelekea wakaguzi kushindwa kujua kiwango halisi cha mapato kilichokusanywa kupitia risiti hizo. Aidha, taarifa za mapato kupitia risiti hizo hazikuonekana popote katika kumbu kumbu za Halmashauri.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli tatizo hilo lilijitokeza na Katibu wa Halmashauri alichukua hatua zinazostahiki, huku akiimarisha eneo la ukusanyaji wa mapato ndani ya Ofisi hiyo.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilipohitaji ni hatua zipi zilizochukuliwa, ilielezwa kuwa ni kubadilisha maofisa wote wa mapato isipokuwa mtu mmoja tu, ili kusaidia wengine wapya na hatua nyengine ni kuimaisha mfumo wao wa uhifadhi na kununua self ya fedha.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imesikitishwa na kitendo kilichotokea Halmashauri hiyo na kuitaka Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa, kulifanyia uchunguzi suala hili na hatimae kuwachukulia hatua za kisheria kwa wote waliohusika.

Hoja Nam. 31.3: Taarifa ya utekelezaji wa matumizi:

Taarifa ya utekelezaji wa matumizi kwa mwaka unaoishia tarehe 30/06/2012, umegundulika kuwa na tofauti kubwa katika vifungu vya matumizi kati ya makisio (budget) na matumizi halisi (actual), hali iliyopelekea kupindukia kwa matumizi ya baadhi ya vifungu. Aidha, ziada ya matumizi hayo haikuidhinishwa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri hii.

Majibu ya Halmashauri:

Pamoja na maelezo ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu, baadhi ya hesabu zilizoelezwa katika ripoti hiyo zimekosewa katika mapato na hata matumizi. Kwa ujumla badala ya tofauti ya Tsh. 46,748,500 kama ilivyoelezwa na Mdhibiti, usahihi ni Tsh. 17,281,850.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilipoelezwa tofauti iliyopo baina ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ilihitaji kufahamu iwapo fedha hizo zilizozidi zimetokana na makusanyo yepi na kuelezwa kwamba, hakukuwa na makusanyo mapya isipokuwa Halmashauri imefanya uhaulishaji wa baadhi ya vifungu kwenda kwenye vifungu vyengine.

Kamati ilipohitaji kupatiwa uthibitisho wa uhaulishaji huo, kama ulipata idhini ya Baraza la Madiwani, kwa bahati viongozi wa Halmashauri walikiri kutopata idhini hiyo na hivyo ni kusema kwamba, wamefanya matumizi kinyume na taratibu.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inasikitishwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria katika Halmashauri, na inaitaka Wizara kusimamia utekelezwaji wa sheria ili kuondosha kasoro zilizopo.

Hoja Nam. 31.4: Vifungu vya malipo vilivyofanywa nje ya bajeti, Tsh. 36,200,000

Katika mwaka 2011/2012 Halmashauri iliidhinisha matumizi ya ununuzi wa vifaa mbali mbali bila ya makisio ya bajeti. Hali inayoepeleka bajeti ktuoonekana kama chombo cha udhibiti wa matumizi. Malipo hayo ni msaada wa mazishi Tsh. 1,200,00; ununuzi wa gari Tsh. 10,000,000; posho la wadhifa (Madiwani) Tsh. 21,000,000 na msaada kwa ujumla Tsh. 4,000,000.

Majibu ya Halmashauri:

Mkaguzi alikosea kuisoma vizuri bajeti ya Halmashauri, kwa mfano table ya Mkaguzi kwenye No. 1,3,4 hivi vyote vimo ndani ya bajeti ya Halmashauri. Aidha, kuhusiana na kifungu cha

ununuzi wa gari ni muendelezo wa ulipaji wa deni la ununuzi huo uliofanyika miaka ya nyuma, aidha, kifungu hicho hakikutumika.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imegundua kuwa malipo hayo pamoja na hoja iliyotolewa na Halmashauri, yamefanywa kwa kuhaulisha vifungu mbali mbali vya matumizi. Aidha, Kamati ilipohoji kuhusiana na uhalili wa uhaulishaji huo, Halmashauri ilikiri kwamba, hakukua na idhini yoyote ya Baraza la Madiwani na hivyo, matumizi hayo yamefanywa kinyume na sheria.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inanamtaka Katibu wa Halmashauri kusimamia sheria na kuwataka Madiwani kuzifahamu sheria na majukumu yao kisheria, ili watekeleze maelekezo ya sheria hizo.

Hoja Nam. 31.5: Utaratibu usioridhisha wa upokeaji na utoaji wa mafuta, Tsh. 14,134,150.

Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya petrol huku ikibainika kuwa hakuna utaratibu mzuri wa uwekaji wa kumbu kumbu za utoaji wa mafuta aina ya petrol katika Halmashauri hii. Hali hii imepeleka ukaguzi kushindwa kuthibitisha utokaji na utumiaji wa mafuta. Aidha baadhi ya kasoro hizo ni kutokuwa na orodha ya majina na sahihi kwa wanaopewa mafuta; kukosekana kwa baadhi ya namba za vyombo na kutooneshwa kwa bakaa ya mafuta yanayobakia.

Majibu ya Halmashauri:

Taarifa hizo zipo. Mfano orodha ya majina na sahihi zimo kwenye ‘stores ledger’, namba za magari zimo kwenye kitabu (customer order) na bakaa ya mafuta zimo ndani ya kitabu cha stores ledger.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imekosa taarifa za ushahidi kama zilivyoelezwa na Halmashauri. Aidha, kuhusiana na ununuzi wa mafuta, kufuatia uchunguzi wa Kamati, viongozi wa Halmashauri ilikiri kwamba, hapo awali mafuta yalikuwa yananunuliwa kupitia utaratibu wa ‘cash’ na utaratibu wa kuyaingiza katika daftari la stoo, umeanza hivi karibuni, yaani 1/10/2012 baada ya kuajiriwa mtu was too.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inasikitishwa na majibu ya Halmashauri ya kutoangalia uwezo na uzito wa majibu yao mbele ya Kamati. Aidha, Serikali inapaswa kuchukua hatua zaidi za kufanya marekebisho makubwa kwa Halmashauri hizi, ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini ‘A’.

2.14 HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI ‘B’:

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Hesabu za mwaka za Halmashauri hazikuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kinyume na Sheria namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2).

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli Halmashauri haijawasilisha hesabu za mwisho wa mwaka 2011/2012 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ingawaje ilikuwa inawasilisha taarifa zake za mapato na matumizi kwa Katibu Mkuu wa Wizara inayoisimamia. Aidha, Halmashauri imezimia kuondoa kasoro hiyo.

Uchunguzi wa Kamati:

Mhasibu wa Halmashauri hii alieeleza kwamba, hakuweza kufunga hesabu hizo kwa kukosa muongozo wake, ameeleza kwamba, alifuatilia Wizara ya Fedha lakini haikuweza kumsaidia. Mhasibu huyu mwenye elimu ya post graduates ya Uhasibu, ameshindwa hata kutumia muongozo na maelekezo ya kuandaa hesabu hizo kupitia sheria ya Fedha za Umma, namba 12 ya mwaka 2005.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kufunga na kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa sheria.

Hoja Nam. 32.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka:

Taarifa ya mapato na matumizi:

Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' ilikadiriwa kukusanya Tsh. 65,000,000 kwa mwaka 2011/2012 na ilipofika June 2012, jumla ya Tsh. 100,000,000 zilikusanywa, sawa na 153.8% ikiwa ni ongezeko la Tsh. 35,000,000 sawa na 53.8% ya makadirio.

Aidha, ilikadiriwa kukusanya Tsh. 114,000,000 kwa mchango wa maendeleo na ilipofika Juni 2012, Tsh. 40,000,000 zilikusanywa ikiwa ni pungufu la Tsh. 74,000,000 ya makadirio.

Kwa kazi za kawaida ilikadiriwa kutumia Tsh. 55,720,000 na ilipofika Juni 2012, Halmashauri ilitumia Tsh. 93,910,000 sawa na 168.5% ya makadirio, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 38,190,000 sawa na 68.5 ya makadirio.

Vile vile kwa kazi za maendeleo, Halmashauri ilikadiria kutumia Tsh. 40,000,000 na ilipofika Juni 2012, ilitumia Tsh. 100,000,000 sawa na 250% ya makadirio, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 60,000,000 sawa na 150% ya makadirio.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilihitaji kupatiwa idhini ya Baraza la Madiwani kuruhusu nyongeza ya makusanyo na matumizi, na kukabidhiwa kumbu kumbu ya tarehe 29/05/2012, ambayo inaelekeza majukumu ya Baraza la Madiwani kukaimishwa kwa Kamati ya Fedha. Aidha, tarehe 31/5/2012 Kamati ya Fedha ilikaa na kufanya kazi iliyokaimishwa kwake, ila hakuna kumbu kumbu nyengine ya mkutano inayothibitisha maamuzi ya Kamati juu ya suala hili la kupatikana ridhaa ya Baraza la Madiwani katika makusanyo na matumizi ya nyongeza. Aidha, hakuna taarifa za kuthibitisha kukaa kwa Baraza la Madiwani na kupitisha maamuzi ya nyongeza hiyo ya makusanyo na matumizi.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Halmashauri kufanya makisio ya matumizi ikiwa ni pamoja na nyongeza zake kwa kufuata sheria, huku Madiwani wakitakiwa kuyafahamu majukumu yao ya kisheria.

TAARIFA ZA MIKOA, HALMASHAURI NA MABARAZA YA MIJI-PEMBA:

2.15 MKOA WA KASKAZINI - PEMBA

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi:

Ukaguzi umebaini kuwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja haukuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya ukaguzi kama ilivyoelezwa na kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha Namba 12/2005 pamoja na kifungu cha 8 cha Sheria hiyo.

Majibu ya Mkoa:

Mkoa wa Kaskazini uliieleza Kamati kwamba iliwasilisha kitabu cha hesabu za mwisho wa mwaka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tarehe 28/09/2012, kwa barua yenye kumbukumbu Namba MKP/F.10/VOL.III/192 badala ya kukiwasilisha kitabu hicho katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar. Hata hivyo, mnamo tarehe 7/10/2012 waliwasilisha tena nakala ya kitabu hicho kwa barua yenye kumbukumbu Namba MKP/F.10/VOL.III/192 baada ya kujulishwa kwamba kitabu hicho hakijaonekana.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iliitaka Ofisi hiyo kuonesha barua zilizotumwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na ‘dispatch’ iliyotumika. Baada ya majadiliano marefu Kamati ilibaini kuwa barua hizo zilikuwa na kumbukumbu inayofanana ingawa zilitumwa tarehe tofauti. Pia, ilibainika kuwa barua hizo hazikutumwa kwa ‘dispatch’ isipokuwa zilipelekwa kienyeji kitendo ambacho ni kinyume na utaratibu.

Vile vile, Kamati ilibaini kuwa barua hizo zimefanyiwa marekebisho kwa mkono katika eneo moja. Jambo hili limeitia mashaka Kamati na kuhisi kwamba barua hizo zimeandaliwa kwa makusudi ili kuficha kasoro hiyo.

Kutokana na kasoro hizo, Kamati imebaini kuwa baadhi ya Wahasibu hawajui utaratibu wa shughuli zao. Hii ni kutokana na kuwa kitabu hiki cha hesabu kilipaswa kuwasilishwa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali – Pemba, kwa kuwa Ofisi hii ndiyo yenye dhamana kwa upande wa Taasisi na Mashirika yaliyopo huko.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inamtaka Afisa Tawala, Mhasibu pamoja na Watendaji wote wa Ofisi hii kuwa makini katika kutekeleza majukumu yao.

Hoja Nam. 28.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2011/2012

Taarifa ya Matumizi ya Kawaida

Kwa mwaka 2011/2012 Mkoa uliidhinishiwa kutumia Tsh. 950,000,000 ingawaje fedha zilizoingizwa na kutumika ni Tsh. 1,038,578,000 ikiwa ni ongezeko la Tsh. 88,578,000/- sawa na asilimia 9.3 ya makadirio

Majibu ya Mkoa:

Afisi hii imetumia ongezeko hilo baada ya Serikali kuongeza mishahara ya watumishi pamoja na maposho. Ongezeko hilo liliombwa kwa Waziri wa Wizara hii na hatimae Wizara kuiomba Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tarehe 25 Januari, 2012, isipokuwa, kwamba fedha zilizoombwa ni Tsh. 126,315,193 na kufanya jumla ya fedha zilizoombwa kuwa Tsh. 1,076,315,193 kati ya fedha hizo zilizotumika mpaka tarehe 30/6/2012 ni Tsh. 1,031,879,237 (na sio 1,038,578,000 kama zilivyoripotiwa na Mdhibiti) na kuacha bakaa ya bajeti (fedha ambazo hazikutumika Tsh. 44,435,956).

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imebaini kuwa kuna mgongano wa taarifa juu ya ongezeko la matumizi ya fedha baina ya Ripoti ya Mdhibiti na barua ya maombi iliyotumwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kamati pamoja na mgongano huo, imeridhishwa na usahihi wa taarifa zilizowasilishwa na Mkoa kwani zimewasilishwa kwa ushahidi.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inazitaka Taasisi za Serikali kutoa mashirikiano mazuri na taarifa sahihi kwa wakaguzi, ili kuepusha usumbufu wa taarifa moja ya Taasisi kutofautiana na inayowasilishwa kwa Mkaguzi.

Hoja Nam. 28.2.1: Hesabu ya Amana (DEPOSIT ACCOUNT) 041101000047: Kukosekana kwa mapato ya kodi ya Kituo cha Mafuta Tsh. 5,300,000/-

Ukaguzi umebaini kuwa Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini – Pemba inamiliki na imekodisha kituo kimoja cha mafuta kilichopo Wete – Sokoni ambacho mwanzo kilijulikana kama Northern Esso Service kwa sasa kinaitwa Wete Star General Supply kilichokodishwa kwa Ndg. Moh'd Salim Said kuanzia tarehe 16/01/1994. Mapungufu yafuatayo yameonekana;-

- Kutokuwepo kwa ushindani katika ukodishwaji wa kituo hicho kwa kutotangazwa zabuni.
- Kutokuwepo kwa rejea ya mkataba.
- Kutotajwa kwa muda wa kipindi cha mkataba.
- Kutokuwepo maelezo ya wazi yenye kutaja njia za malipo (Method of payment) kama ni kwa njia ya hundi au ya T.T n.k
- Kutotajwa Kiwango halisi cha malipo bali mkataba umetaja asilimia 10% ya faida ghafi wakati mfanyabiashara huyo hatayarishi hesabu za kila mwaka.
- Kituo kubadilishwa jina Northern Esso Service na kuitwa Wete Star General Supply bila ya makubaliano katika mkataba.
- Hakuna kumbu kumbu za makusanyo ya mapato yatokanayo na kituo hicho na malipo hufanywa kwa njia ya fedha taslimu ambapo ni kinyume na sheria za fedha.

Majibu ya Mkoa:

Ofisi hii inakiri kuwepo kwa kasoro hizo, isipokuwa kwamba kasoro hizi zimetokea kwa kuwa Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini – Pemba kwa wakati ule haikuwa na Mwanasheria. Hata hivyo, baada ya kuupitia Mkataba huo na kubaini kasoro hizo, mnamo tarehe 16 Januari, 1994 Ofisi hii iliamua kuusitisha mkataba huo kwa barua ya tarehe 18 Oktoba, 2012 yenye kumbu kumbu Namba MKP/M.6/1/4/VOL.II/207 iliyotumwa kwa Mkodishwaji (Ndg. Moh'd Salum Said) na hatua za taratibu za manunuzi na kufunga mkataba mpya zimechukuliwa ili uendane na Sheria ya Manunuzi ya 2005. Kilichokwamisha hivi sasa ni kuwa Mkodishwaji amefungua kesi ya madai Mahkamani na Mahkama imezuia hatua ya kubadilisha mkataba huo mpaka maamuzi ya kisheria yatakapotolewa.

Kuhusu Kituo cha Mafuta kubadilishwa jina kutoka Northern Esso Service na kuitwa Wete Star General Supply kitendo hicho kilifanywa na Mkodishwaji bila ya idhini ya Mkodishaji na suala hili limebainika baada ya mapitio ya mkataba wa ukodishwaji.

Kwa upande wa kumbu kumbu za makusanyo ya mapato yatokanayo na kituo hicho, Ofisi hii imekiri kupokea Tsh. 5,300,000/- ambapo fedha hizi zilitumika kuendeshea ofisi kwa yale mambo ya dharua kwa kuwa bajeti yake ilikuwa haikidhi haja.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ya PAC haikukubaliana na maelezo yaliyotolewa hasa ikizingatiwa kuwa Ofisi ya Mkoa tokea awali ilipaswa kupata ushauri wa kisheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa Mkoa haukuwa na Mwanasheria.

Hata hivyo, kamati ilifanya majadiliano na Watendaji wa Mkoa huu na katika kuchunguza hili Kamati ilibaini kuwa Mkondishwaji alikuwa analipa Tsh. 200,000/- kwa mwezi, kiwango kilichowekwa maalum (fixed), ingawaje hakikuweza kuthibitishwa katika kifungu chochote cha Mkataba, kwani Mkataba ulilazimisha kulipwa kwa 10% ya faida ghafi. Hali hii inathibitisha udhaifu wa Mikataba na utaratibu wa malipo kwa Taasisi nyingi za Serikali.

Vile vile, Kamati imebaini kuwa hadi inafuatilia hoja hii Mkodishwaji alikuwa anaendelea kutumia kituo hicho cha mafuta. Sambamba na hilo, cha kusikitisha zaidi imebainika kuwa Mkondishwaji anaidai Ofisi ya Mkoa jumla ya Tsh. 23,000,000/- ikiwa ni deni la mafuta ambalo Ofisi hii ilikuwa inachukua kituoni hapo. Kutokana na deni hilo uchunguzi umebaini kuwa kiasi hicho cha fedha kiliifanya Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini – Pemba kumuomba na kumueleza Mkodishwaji, Ndg. Moh'd Salim Said, kwa barua ya tarehe 2/04/2013 yenye kumbu kumbu namba MKP/M.6/1/4/VOL.III/16 kuwa Afisi ya Mkoa iko tayari kulipa deni hilo kwa kila mwezi Tsh. 500,000 hadi deni hilo litakapomalizika.

Aidha, imebainika kuwa mapato yaliyokuwa yanakusanywa kutokana na kituo hicho yalipofikia Tsh. 5,300,000, fedha hizo zilitumika kuendeshea Ofisi kwa baadhi ya shughuli za dharura, bila ya fedha hizo kupelekwa benki na kuingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Matumizi hayo yameisikitisha Kamati na zaidi kwa kuwa yalifanywa bila ya kuandikwa barua ya maombi, wala vielelezo vyovyote vya kuthibitisha matumizi yake, kitendo ambacho ni kinyume na Sheria za fedha.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria watendaji wote wa Mkoa, waliohusika na ubadhirifu wa fedha za kituo na zaidi kwa kuwa wazembe katika kusimamia mali ya Serikali. Aidha, Kamati ilihitaji zaidi kulifuatilia suala hili, ikiwa ni pamoja na kukaa na Mkodishwaji, lakini imezuilika kutokana na suala hili kuwepo Mahkamani.

Hoja Nam. 28.2.2: Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye Daftari la Ghalani Tsh. 7,355,000/-

Jumla ya Tsh.7,355,000/- zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali lakini vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la vifaa ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake. Kutokuwepo kwa kumbu kumbu za vifaa ni kwenda kinyume na kanuni ya 198 ya kanuni ya fedha ya 2005.

Majibu ya Mkoa:

Kamati ilielezwa kwamba tatizo hilo limejitokeza kwa kuwa Ofisi hii haina Mtunza ghala mwenye taaluma ya fani hiyo. Aidha, Mkoa wa Kaskazini Pemba haukuwa na Afisa anayehusika na manunuzi kwa wakati huo, Afisa huyu ni kiungo kikubwa kati yake na Mtunza ghala.

Kwa upande wa manunuzi ya kompyuta aina ya Laptop, kompyuta hii haikuingizwa kwenye daftari kwa kuwa Ofisi hii ilimuagiza msambazaji kompyuta kabila la Toshiba na badala yake aliipatia kabila la HP.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kupata uhalali wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini - Pemba, Kamati ilitaka kujua elimu na uzoefu wa kazi wa Mtendaji anayehusika na shughuli hii. Kwa kuwa Mtendaji huyu ana uzoefu wa kazi wa mwaka mmoja, ingawa hana taaluma ya fani hiyo, Kamati haikushawishika kuikubali taarifa iliyotolewa na Ofisi hii na iliamini kuwa makosa haya yalifanywa kwa kuwa fedha hizo zilitumika kinyume na utaratibu.

Mapendekezo ya Kamati:

Afisa Tawala achukue juhudi za makusudi katika kufuatilia utendaji wa taasisi yake na Watendaji wa Serikali wawe makini katika kutekeleza majukumu yao.

2.16 MKOA WA KUSINI – PEMBA

2.16.1 TAARIFA ZA UKAGUZI MAALUM:

2.16.2 MALIPO YA MSAADA KWA WAZEE WASIOJIWEZA:

Ukaguzi umebaini kuwa fedha za misaada ya wazee wasiojiweza kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kilichoanzia Juni, 2008 hadi Machi, 2012, ulifanyika kwa kupitia Mikoa yote mitano (5) ya Zanzibar ambapo mapungufu mbali mbali yaligundulika. Baadhi ya mapungufu hayo ni kama yafuatayo;-

- Kuendelea kulipwa wazee ambao wameshafariki dunia.
- Kulipwa watu wasiostahiki kupata msaada.
- Kulipwa kwa wazee ambao majina yao hayamo katika orodha ya malipo.
- Kutokufuata sheria za fedha wakati wa ulipaji na upokeaji wa fedha.

2.16.3 KWA UPANDE WA PEMBA

Jumla ya Tsh. 23,705,000/- huingizwa kila mwezi katika Mkoa kwa ajili ya ulipaji wa feha za msaada kwa wazee wasiojiweza. Ukaguzi umebaini kwamba fedha zilizotumika kwa kila mwezi ni Tsh. 21, 695,000/- kwa kuwalipa wazee hao na kuacha bakaa ya Tsh. 2,010,000/- kwa kila mwezi ambapo matumizi pamoja na vielelezo vyake au marejesho yake havikupatikana kwa ukaguzi, hali hii imepelekea jumla ya Tsh. 26,130,000/- kwa kipindi kilichokaguliwa kutokujulikana matumizi yake.

Hali halisi ni kama ifuatavyo;-

MKOA	FEDHA ZILIZOINGIZWA	FEDHA ZILIZOLIPWA	BAKAA
KUSINI – PEMBA	12,385,000/-	10,375,000/-	2,010,000/-
KASKAZINI - PEMBA	11,320,000/-	11,320,000/-	-
JUMLA	23,705,000/-	21,695,000/-	2,010,000/-

Majibu ya Mkoa wa Kusini – Pemba

Mkoa wa Kusini – Pemba haukukubaliana na hoja iliyotolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kuingiziwa jumla ya Tsh.12,385,000/- kwa ajili ya malipo ya wazee wasiojiweza.

Katika mwaka 2008 Ofisi ya Mkoa wa Kusini – Pemba ililipa fedha za Wazee hao kama inavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo;-

MAELEZO	WILAYA YA CHAKE CHAKE	WILAYA YA MKOANI	JUMLA
Makisio kwa mwaka	Tsh. 86,640,000/-	Tsh. 49,200,000/-	Tsh. 135,840,000/-
Matumizi kwa mwezi	Tsh. 7,220,000/-	Tsh. 4,100,000/-	Tsh. 11,320,000/-

Uchunguzi wa Kamati

Kabla ya Kamati kuifuatilia hoja hiyo katika Mkoa huu, ilianza na Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambao haukuwa na hoja ya bakaa lolote. Kutokana na Mkoa wa Kusini kueleza kwamba hoja hiyo sio yao kwani hawakuwa na bakaa lolote, Kamati ilihitaji uthibitisho wa Afisa Mkaguzi aliefuatana na Kamati ambae kwa juhudi alizozifanya na kuwasiliana na Mkaguzi aliefanya kazi ya ukaguzi wa Mkoa huo, aliieleza Kamati kuwa, maelezo ya afisi ya Mkoa wa Kusini ni kweli na hivyo, Kamati ikajiridhisha kuwa ama hoja hiyo imeingia kimakosa ama ni ya Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kufuatia Mafunzo maalum yaliyoandaliwa kwa Kamati moja kati ya michango ya wajumbe wa Kamati kupitia Makatibu wao, ilikuwa ni hoja hiyo na kwa kuwa miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo ni pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mdhibiti aliipata taarifa ya hoja hiyo na baadae aliifuatilia na kuwasiliana na Katibu Kamati kuwa, hoja hiyo iko sawa kama ilivyoelezwa katika ripoti yake.

Aidha, Kamati ilitaka kuifanyia kazi tena hoja hiyo kwa kuikutanisha pamoja Mikoa yote miwili ya Pemba, lakini kutokana na busara za Kamati ilihitaji kuwepo na ufafanuzi wa ziada (wa maandishi) ili Kamati iweze kuwa na mwega wa kushika, kwa kuzingatia hapo awali Mikoa yote

ilikataa kuhusishwa na hoja hii. Hata hivyo, ufafanuzi huo wa ziada kutoka Afisi ya Mdhibiti haukuweza kupatikana kwa Kamati zaidi ya kutegemea ripoti hii ya Mkaguzi ambayo tokea awali ilifuatiliwa na Kamati na hivyo Kamati haikufuatilia tena hoja hii.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuifanyia kazi tena hoja hii na kuiarifu Kamati ili iweze kuifuatilia zaidi.

Hoja Nam 12.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2011/2012

Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Kawaida

Ukaguzi umebaini kuwa Mkoa wa Kusini Pemba ilitumia ongezeko la Tsh. 106,977,917/- sawa na asilimia 16 ya makadirio kwa kazi za kawaida, kufuatia kuidhinishiwa kutumia Tsh. 644,000,000 na hatimae kuingiziwa na kutumia Tsh. 750,977,917.

Majibu ya Mkoa:

Mkoa wa Kusini – Pemba ulikubaliana na hoja ya ongezeko la fedha kwa matumizi ya kazi za kawaida. Ongezeko hili limetokea baada ya kupandishwa viwango vya mishahara ya Watumishi wa Umma kuanzia mwezi wa Oktoba, 2011. Kutokana na kadhia hiyo Taasisi hii ilibaini kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya zake zitakuwa na upungufu wa fedha za kulipa mishahara kuanzia mwezi wa Machi, 2012 hadi Juni, 2012 na ndipo ilipolazimika kuomba fedha ya nyongeza kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Zanzibar.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia suala hili Kamati ya P.A.C iliomba kupatiwa barua inayothibitisha maombi hayo ya fedha, ambapo ilithibitisha kuwa maombi hayo yalifanywa tarehe 14 Februari, 2012 kwa barua yenye kumbukumbu Namba MKUP.1/2.VOL.VII/61. Isipokuwa kwamba, Kamati ilibaini kuwa fedha za nyongeza zilizoombwa ni Tsh.121,865,331/- wakati fedha zilizotumika ni Tsh.106,977,917/- tu.

Kamati ilitaka kujua kwa nini Ofisi hii ikaomba fedha za ziada ambazo ni Tsh. 14,887,414/- wakati nyongeza halisi ya mishahara inajulikana?. Katika kulipatia jibu suala hili Watendaji wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa waliieleza Kamati kuwa baadhi ya watendaji walistaafu na wengine walifariki, hivyo, fedha zilizobaki zilirejeshwa Wizara ya Fedha.

Kamati haikuridhika na majibu hayo na kwa bahati uongozi wa Mkoa uliomba kupewa muda wa ziada ili kuwasilisha taarifa sahihi, huku Kamati pia ikiwataka wawasilishe orodha ya matumizi ya Tsh. 106,977,917 na majina ya watendaji waliofariki na waliostaafu.

Aidha, kabla ya Kamati kuondoka Pemba iliwasilishiwa majibu hayo kupitia barua ya tarehe 30/09/2013 yenye kumbu kumbu namba MKUP.1/25.VOL.II/51 ikikubaliana na sababu ya kuongezeka kwa mahitaji ya fedha hizo na utaratibu walioutumia kuomba Wizara ya Fedha. Aidha, barua ilieleza kuwa baada ya ongezeko la Tsh. 133,167,331 bajeti ya Mkoa wa Kusini Pemba ilifikia Tsh. 777,167,331 na fedha walizoziomba ambazo ni nyongeza ya bajeti ya mishahara ni Tsh. 133,167,331 na sio Tsh. 121,865,331 kama ilivyodaiwa.

Vile vile, matumizi halisi ya fedha walizoziomba ni Tsh. 129,564,395, bakaa ni Tsh. 3,602,936 kwa mishahara na posho. Na hivyo bakaa ya jumla ni Tsh. 26,189,414/-.

Hata hivyo, Kamati haijakaa kupata ufafanuzi huo na Mkoa wa Kusini Pemba, na hivyo, pamoja na taarifa hiyo kufika kwa Kamati, haiwezi kutegemewa usahihi wake bila ya kikao cha pamoja.

Mapendekezo ya Kamati:

Kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha, Kamati inahitaji muda zaidi wa kufikia maamuzi juu ya usahihi wa hoja hii.

2.16.4 HESABU YA AMANA (DEPOSIT ACCOUNT)

Hoja Nam. 27.2.1: Kukosekana kwa Mapato ya Kodi ya Vituo vya Mafuta Tsh. 7,200,000/-

Ukaguzi umebaini kuwa Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini – Pemba inamiliki na kukodisha vituo viwili vya mafuta vya Chake Chake Petrol Station na Misufini Petrol Station kwa Ndg. Fatma Karume na Ndg. Khalid Idd Mabruki wa Zanzibar mnamo tarehe 14/8/2008 kwa makubaliano ya Tsh. 150,000/- kwa kila kituo kwa mwezi ambapo ni sawa na Tsh. 1,800,000/- kwa mwaka.

Mapungufu yafuatayo yamejitokeza katika ukaguzi;-

- Kukosekana kwa ushindani kwa kutotangazwa kwa zabuni.
- Mkataba wa ukodishaji kutokuwa na Namba ya rejea (Refrence Number).
- Baadhi ya stakabadhi zilizotumika kwa kupokelea malipo hayo hazikubaliki kisheria.
- Hakuna kumbu kumbu za makusanyo ya mapato yatokanayo na vituo hivyo na malipo hayo hufanywa kwa njia ya fedha taslimu ambapo ni kinyume na sheria za fedha. Malipo yenyewe ni kama ifuatavyo;-

STAKABADHI NAMBA	TAREHE YA MALIPO	FEDHA ZILIZOPOKELEWA	MAELEZO
01333	1/2/2010	3,600,000/-	Malipo ya kodi ya vituo vya mafuta
51	18/1/2012	3,600,000/-	Malipo ya kodi ya vituo vya mafuta

JUMLA		**7,200,000/-**	

Majibu ya Mkoa:

Hoja hizi zilipatiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

- ***Kukosekana kwa ushindani kwa kutotangazwa kwa zabuni***

Ofisi ya Mkoa ilikubaliana na hoja hiyo na kueleza kuwa wakati vituo hivyo vinakodishwa Mkoa wa Kusini – Pemba haukuwa na Bodi ya Zabuni. Aidha, vituo hivyo ni Misufini Petroli Station na Chake Chake Petroli Station ambavyo vimekodishwa kwa Mama Fatma Karume na Ndg. Khalid Iddi Mabrouk. Hata hivyo, kwa hivi sasa Mkoa una Bodi ya Zabuni na taratibu zote za kutangazwa zabuni zinafuatwa kama sheria inavyoelekeza.

Uchunguzi wa Kamati:

Baada ya kuelekezwa kwa kina historia ya vituo hivyo vya mafuta, ilifahamika hatimae kuwa, vituo hivyo kabla ya Mkuu wa Mkoa na Afisa Tawala waliopo sasa, vilikuwa havijuulikani kabisa kuwa chini ya Mkoa huu na kama sio juhudi yao, visingelifahamika hadi leo. Aidha, baada ya kuvifahamu Afisa Tawala alipokea amri kutoka Wizara ya Fedha ya kuvikodisha kwa Mama Fatma Karume na hakukuwa na njia nyengine zaidi ya kujaza mkataba haraka haraka na hatimae fedha zikawa zinalipwa kwa Mkoa.

Aidha, vituo hivyo baadae kufuatana na mabadiliko ya Wakuu wa Mikoa vilikodishwa kwa Ndg. Abdalla Khalfan Thiney, tarehe 26/10/2000 kwa malipo ya Tsh. 75,000 kwa mwezi, kwa muda usiozidi miaka mitano ambapo pia baadae vilikodishwa tena kwa Mama Fatma Karume na Ndg. Khalid Iddi Mabrouk, tarehe 1/1/2009 kwa Tsh. 150,000 kwa mwezi kwa kila kituo, huku kima hicho kikibaki kama kilivyo (fixed) bila ya kubadilishwa na ni mkataba wa miaka 10. Katika hatua zote hizo za kukodishwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwengine, hakukuwa na taratibu za kisheria zinazoelekezwa na sheria ya manunuzi zilizofuatwa.

- ***Mkataba kutokuwa na namba rejea (Reference Number)***

Ofisi ya Mkoa iliieleza Kamati kuwa mkataba ulikosa nambari rejea kutokana na watayarishaji wa mkataba huo kutoelewa kwamba mikataba nayo huekwa kitu hicho. Aidha, kukosekana kwa Mwanasheria kwa wakati huo katika Taasisi hii kulichangia kuwepo kwa mapungufu hayo.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikuridhika na majibu ya Mkoa kwamba, hawakuwa wakijua maelekezo hayo. Aidha, Kamati inaamini suala hili limechangiwa zaidi na kutofuata sheria ya manunuzi katika kutafuta mkodishwaji wa vituo hivyo, lakini pia katika kuingia nae mkataba wa ukodishwaji huo.

- ***Baadhi ya stakabadhi zilizotumika kwa kupokelea malipo hayo hazikubaliki kisheria***

Hoja hii ni ya kweli, isipokuwa kwamba stakabadhi iliyotumika kwa makosa ni moja tu baada ya stakabadhi za Serikali kumalizika Ofisini hapo. Kwa kuwa mhusika alipofika alidai kupatiwa risiti yoyote ile kama ni uthibitisho wa malipo aliyofanya, Ofisi hii ililazimika kumpatia risiti ambayo haikubaliki kisheria.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kujiridhisha na hoja hii Kamati ilitaka kuona nakala ya risiti hiyo, hata hivyo, Ofisi hii ilishindwa kutoa risiti hiyo kwa kisingizio kuwa haionekani. Aidha, Ofisi ilikiri kwamba, risiti walizokuwa wakitoa ni pamoja na risiti za mchango wa mwenge, ambazo kweli sio za Serikali. Hali hii inaashiria kupotea kwa fedha zilizokodishwa vituo hivyo na kwa bahati Kamati ilielezwa kwamba, makusanyo hayo yaliishia mikononi mwa baadhi ya Wakuu wa Mikoa wa Mkoa huo (ukiachia Mkuu wa Mkoa aliepo sasa) na kutumika kwa matumizi madogo madogo ya ofisi, ikiwa ni pamoja na kulipwa kwa njia ya kupewa mafuta ya magari ya Mkoa.

- ***Kukosekana kwa kumbukumbu za makusanyo ya mapato yatokanayo na vituo vya mafuta***

Ukaguzi umebaini kuwa makusanyo ya mapato yatokanayo na vituo vya mafuta hufanywa kwa njia ya fedha taslimu ambapo ni kinyume na sheria za fedha. Malipo yenyewe ni kama ifuatavyo;-

STAKABADHI NAMBA	**TAREHE YA MALIPO**	**FEDHA ZILIZOPOKELEWA**	**MAELEZO**
013338	1/2/2010	3,600,000/-	Malipo ya kodi ya vituo vya mafuta
51	18/1/2012	3,600,000/-	Malipo ya kodi ya vituo viwili vya mafuta
JUMLA		**7,200,000/-**	

Majibu ya Mkoa:

Ofisi ya Mkoa ilikiri mbele ya Kamati hii kuwa taratibu za makusanyo ya fedha hizo hazikufanywa. Aidha, kufuatia mapungufu hayo, Mkoa umeshafanya marekebisho na utaendelea kupokea maelekezo yenye lengo la kudizi kuleta ufanisi kazini sio tu katika utendaji hadi katika usimamizi na udhibiti wa fedha au mali za Serikali kwa maslahi ya Taifa.

Aidha, ilielezwa zaidi na Afisa Tawala wa Mkoa wa Kusini – Pemba, Ndugu Hanuna I. Massoud kuwa, wakati anakabidhiwa Ofisi hii hakukabidhiwa Vituo hivyo. Isipokuwa kwamba, alipata taarifa kutoka kwa watendaji wa Ofisi ya Mkoa huu kuwa miongoni mwa mali za Mkoa wa Kusini – Pemba ni pamoja na vituo vya mafuta pamoja na gari la kubebea mafuta. Suala hili

aliliripoti kwa Mkuu wa Mkoa wa wakati ule Mheshimiwa Msham Abdalla Khamis ambaye na yeye hakukabidhiwa mali hizo. Katika kufuatilia hili waligundua mali hizo.

Alizidi kueleza kuwa kabla ya kuteuliwa kushika wadhifa huo, fedha za kodi ya vituo alikuwa akilipwa Mwangalizi wa Ofisi aliyekuwepo wakati ule. Isipokuwa kwamba, baada ya kufuatiliwa suala hili mkodishaji aliwaomba wakodishwaji kuwapatia mafuta badala ya kulipa fedha ingawa Ofisi ya Mkoa na Ofisi hii ilikuwa inatumia fedha kwa shughuli zake mbali mbali. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2013 wametakiwa kuziwasilisha fedha za kodi za vituo vya mafuta huko Wizara ya Fedha na Mipango ya Maendeleo (barua zenye kumbukumbu Namba MKUP.1/2 VOL.111/110 na MKUP.1/2 VOL.VIII/4) zinathibitisha hili.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilipohoji zaidi kuhusiana na matumizi ya fedha za vituo hivyo, ilibaini kuwa mbali na fedha hizo kutumika kwa matumizi ya ofisi, lakini ilifika wakati ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilikuwa inavuja, wakatumia fedha za mapato ya vituo vya mafuta kumtafutia nyumba nyengine. Aidha, kuhusiana na Mkataba wa sasa baina ya ofisi ya Mkoa na Mama Fatma Karume na Ndg. Khalid Iddi Mabrouk, ilifahamika kwamba, wakodishwaji hao hufanya malipo baada ya kufuatiliwa sana na mkodishaji jambo ambalo ni kinyume na kifungu No.11 paragrafu ya iii ya mkataba. Pia, mkodishwaji hulipa fedha za kodi hiyo kwa awamu (pay slip za tarehe 16/04/2013 na tarehe 04/07/2013) zinathibitisha hili.

Aidha, Kamati imebaini kuwa kabla ya mwaka 2013, takriban katika kipindi kisichopungua miaka minne fedha za kodi ya vituo vya mafuta zimetumika kinyume na utaratibu, na kama ilivyoelezwa awali, ziliishia katika matumizi binafsi zaidi kuliko huduma ya Ofisi ya Mkoa wala Serikali.

Vile vile kuhusiana na makusanyo hayo yanayoelezwa kukusanywa vyema kuanzia mwaka 2013, Kamati ya P.A.C ilishangazwa na kitendo cha Mkoa wa Kusini – Pemba cha kuwasilisha fedha za kodi ya vituo hivyo katika Wizara ya Fedha na Mipango ya Maendeleo. Hii ni kutokana na kuwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza la Wawakilishi la Zanzibar halijaidhinishia Afisi ya Mkoa wa Kusini Pemba, kukusanya mapato hayo. Hivyo, inajiuliza ni Taasisi gani yenye mamlaka ya kuidhinisha kukusanya mapato ukiachia mbali Baraza la Wawakilishi?.

Mapendekezo ya Kamati:

Taasisi za Serikali zifuatilie na zitambue mali zilizochini yake pamoja na kuwa na hati miliki ya mali hiyo na kuingia mikataba yenye tija na manufaa kwa Taifa. Aidha, Kamati imesikitishwa na usimamizi mbaya wa vituo vya mafuta vya Mkoa, na kuitaka Ofisi isimamie vituo hivyo kwa kufuata ipasavyo sheria ya Manunuzi, ili viweze kuleta tija kwa taifa.

2.17 HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAKE CHAKE

Hoja Namba 13.1 Kuhusiana na Uwasilishaji wa Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake haikuwasilisha hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na Matumizi kama vifungu vya 24(2) na 8 vya Sheria ya Fedha Namba 12/2005 vinavyoelekeza.

Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake

Katibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake alikiri kosa hilo kwa misingi kuwa utaratibu wa kuwasilisha hesabu za mwaka haukuwepo na haukufahamika umuhimu wake. aidha, alizidi kueleza kuwa, Taasisi zinazohusiana na masuala ya fedha hazikutoa muongozo hapo kabla. Kwa kuwa Taasisi zinazohusiana na masuala ya fedha tayari sasa zimeshatoa muongozo, aliahidi mbele ya Kamati kuwa tatizo hilo halitojitokeza tena.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati haikukubaliana na maelezo hayo kutokana na kuwa Sheria ya Fedha imeanza kufanya kazi tangu mwaka 2005. Vile vile, kushindwa kwa Taasisi za fedha kutoa muongozo sio kigezo cha kuifanya Halmashauri hii isifunge hesabu zake. Hii ni kutokana na kuwa Sheria ya fedha ya mwaka 2005 tayari imeshatoa muongozo wa kufunga na kuwasilisha hesabu hizo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake imeshawasilisha hesabu za mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Kamati imetoa msamaha kwa taasisi hii kwa kosa walilofanya katika mwaka wa fedha ulopita na kuitaka kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Hoja namba 34.1 Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2011/2012

Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa Kazi za Kawaida na Maendeleo

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake ilikusanya mapato yake kwa ongezeko la Tsh. 9,132,488/- sawa na asilimia 26 ya makadirio. Aidha, imetumia kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa ongezeko la Tsh. 7,132,300/- sawa na asilimia 20.4 ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake

Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake iliieleza Kamati kwamba kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikisia kukusanya jumla ya Tsh. 35,200,000/- na hadi kufikia Juni, 2012 ilifanikiwa kukusanya Tsh. 37,461,038/- kinyume na ilivyoripotiwa na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2011/2012. Hii ni kutokana na kuwa Katibu aliyekuwepo wakati ule Ndugu Mgeni Othman Juma aliipotosha Ofisi hiyo pamoja na Kamati ya PAC ilivyoitembelea Halmashauri hii mnamo tarehe 27 Novemba, 2012 kwa kutoa taarifa za uongo.

Walizidi kueleza kuwa fedha zilizoripitiwa kuwa zimekusanywa ambazo ni Tsh 44,132,488/- zilijumuisha pia na fedha zilizotumika kutoka katika Mfuko wa Maendeleo Jimbo la Wawi.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na maelezo yaliyotolewa na Watendaji na Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri hii, Kamati ya P.A.C haikukubaliana na kauli hiyo. Hii ni kutokana na kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliwasilisha taarifa ya Hoja hiyo tarehe 21 Disemba, 2012 kwa barua yenye kumbukumbu Namba AUD/D.35/2/VOL.II/6 na Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake haikuchukua hatua yoyote kuhusiana na Hoja hiyo.

Sambamba na hilo, Watendaji wa Halmashauri hii walishindwa kuionesha Kamati hii kumbukumbu ya Kikao cha Baraza la Madiwani kilichopitisha ongezeko la makusanyo hayo.

Kwa mnasaba huo, Kamati inakubaliana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa kwa mwaka fedha 2011/2012 Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake ilikusanya jumla ya Tsh. 44,132,488/-. Kutokana na kuwa Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huandaa ripoti kwa mujibu wa taarifa na vielelezo anavyopatiwa na Watendaji wa Taasisi husika.

Mengineyo

Waheshimiwa Madiwani kwa pamoja waliieleza Kamati kuwa Katibu aliyekuwepo wakati ule alikuwa anatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa utashi wake. Hii ni kutokana na kuwa hutekeleza shughuli zake kinyume na maamuzi ya Baraza la Madiwani.

Mapendekezo ya Kamati:

Kwa kuwa Baraza la Madiwani ndio lenye dhamana na utendaji wa Halmashauri kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria Namba 4/1995, Kamati imewataka Waheshimiwa Madiwani kuyajua majukumu yao ili waweze kuyasimamia vyema.

Kamati ilishauri pia, kuwe na mashirikiano na mawasiliano mazuri baina ya Watendaji wa Halmashauri na Waheshimiwa Madiwani.

Kwa kuwa Katibu aliyekuwepo hivi sasa ni mpya, Kamati imemtaka Katibu huyo kutekeleza majukumu yake kama sheria na kanuni zinavyoelekeza, pamoja na kuhakikisha kuwa kasoro zote zilizotokea nyuma hazitokei tena.

2.18 HALMASHAURI YA WILAYA YA WETE:

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.

Halmashauri ya Wilaya ya Wete imeshindwa kuwasilisha hesabu za mwihso wa mwaka 2011/2012, kinyume na maelekezo ya kifungu cha 24(2) cha sheria namba 12 ya mwaka 2005. Na kifungu cha 43 cha sheria namba 4 ya mwaka 1995.

Majibu ya Halmashauri:

Wanakiri kushindwa kufunga hesabu za mwaka kutokana na uelewa mdogo wa kazi hiyo na kukosa taaluma ya uhasibu. Aidha, wamechukua hatua za kujielimisha na tayari kuanzia mwaka 2012/2013 wameshatayarisha ripoti ili kuiwasilisha kunakohusika.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati haikubaliani na sababu za kushindwa kufunga hesabu, kwani kifungu cha 8 cha sheria namba 12 ya mwaka 2005, kinamtaka Katibu wa Halmashauri hii kutekeleza majukumu hayo. Aidha, baada ya Kamati kupitia hesabu zao walizozifunga na kusema wameziwasilisha kwa Mdhibiti, imegundua mapungufu mengi ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa Daftari la kuhifadhia mali lenye mfumo uliotolewa na Wizara ya Fedha lakini pia limekosa taarifa muhimu.

Hali hii ilitokana na kiwango kidogo cha elimu ya Mhasibu wa Halmashauri hii mwenye cheti tu cha elimu hiyo tena ameajiriwa na Halmashauri yenyewe badala ya Wizara ya Fedha.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inamtaka Mhasibu Mkuu wa Serikali kufanya marekebisho makubwa katika kitengo kinachohusika na fedha kwa kuanza kumpeleka Mhasibu awe na angalau kiwango cha elimu cha ‘Post Graduate Diploma’ ya uhasibu na uzoefu wa kutosha wa kazi zake, badala huyo aliepo sasa.

Hoja Nam. 35.1: Hesabu za mwisho wa mwaka, 2011/2012:

Taarifa za mapato na matumizi:

Kwa mwaka 2011/2012, makadirio ya makusanyo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Wete ilikua ni kukusanya Tsh. 40,000,000 na ilipofika Juni 2012, iliweza kukusanya Tsh. 71,766,000 zikiwa ni sawa na asilimia 179.42 ya makadirio, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 31,766,000 sawa na 79.42% ya makadirio.

Kwa matumizi ya kawaida, Halmashauri ilikadiriwa kutumia Tsh. 20,000,000 na ilipofika Juni 2012, ilitumia Tsh. 42,690,448 sawa na 213.45% ya makadirio, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 22,690,448 sawa na 113.45% ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, ilikidiriwa kutumika Tsh. 20,000,000 lakini hadi kufikia Juni 2012, Tsh. 28,527,900 zilitumika sawa na 142.64% ya makadirio ikiwa ni ongezeko la Tsh. 8,527,900 sawa na 42.64% ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri:

Kuongezeka kwa mapato hayo kunatokana na zao la karafuu kuongezeka na kufikia Tsh. 18,000,000 kutoka msimu wa kawaida Tsh. 300,000 hadi 400,000. Aidha, ongezeko hilo lilifanyiwa marekebisho kwenye kikao cha Baraza cha tarehe 31/12/2011 kwa kufanyiwa bajeti ya ziada ya Tsh. 22,190,000.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilihitaji kuangalia makisio ya miaka ya nyuma na kugundua kuwa, mwaka 2010/2011 walikisia kukusanya Tsh. 24,000,000 na hali halisi ikawa makusanyo ya Tsh. 25,862,090; mwaka 2011/2012 walifanya makisio ya makusanyo Tsh. 40,000,000 na wakakusanya Tsh. 71,766,000 na mwaka 2012/2013 walifanya makisio ya Tsh. 61,000,000 na kukusanya Tsh. 53,000,000.

Aidha, Kamati ilipohitaji taarifa za kushuka kwa makisio ya makusanyo baina ya mwaka mmoja na mwengine ilielezwa kwamba, inatokana na miaka baada ya 2011/2012 kushuka kwa makusanyo kutokana na kushuka kwa karafuu.

Hali hii iliipelekea Kamati kuhitaji kuangalia vitabu vya mauzo ya karafuu hizo, jambo ambalo Halmashauri imeshindwa kuikabidhi Kamati.

Aidha, Kuhusiana na iwapo idhini ya Baraza la Madiwani ilipatikana wakati wa kukusanya mapato zaidi ya makisio pamoja na kufanya matumizi, Uongozi wa Halmashauri pamoja na Waheshimiwa Madiwani waliohudhuria kikao hicho walikiri kwamba hakuna kikao cha Baraza kilichokaa. Aidha Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani nae alikiri kwamba, hawakukaa wala kuidhinisha na wala hawajui wanatakiwa kisheria kufanya kazi hiyo.

Hata hivyo, katika hali ya kusikitisha, uongozi wa Halmashauri hii ulitoa kumbu kumbu za mkutano zilizokunjana sana na zenye taarifa za uongo zilizowasilishwa kwa Kamati, kwa lengo la kuidanganya Kamati. Kumbu kumbu hiyo yenye namba 6 kama ‘reference’ ya faili huku barua zisizopungua mbili za nyuma ya kumbukumbu hii zikiwa na nambari 8 (ya usajili wa upokelewaji na ushughulikiwaji wa barua katika mafaili).

Aidha, kumbukumbu hizo zilizotobolewa zimeithibitishia Kamati kwamba, zimefanywa kwa udanganyifu. Na kwa bahati Uongozi huo baada ya mjadala mkali na Kamati, ulikubali kufanya makosa hayo na kuomba msamaha kwa Kamati.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati imesikitishwa na vitendo vya kuidanganya Kamati vinavyofanywa na uongozi wa Halmashauri. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kutoa elimu na semina kwa Waheshimiwa Madiwani ili wafahamu majukumu yao.

2.19 HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

Hoja Nam. 13.1 Kuhusiana na Uwasilishaji wa Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni haikuwasilisha hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na Matumizi kama vifungu vya 24(2) na 8 vya Sheria ya Fedha Namba 12/2005 vinavyoelekeza.

Majibu ya Halmashauri:

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni iliieleza Kamati kuwa ni kweli haikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi kutokana na kutokuwepo utaratibu na mwongozo ulioelekeza kufanya hivyo.

Hata hivyo, waliiomba radhi Kamati na walizidi kueleza kuwa, kwa kuwa suala hili limeshatolewa muongozo na taasisi husika pamoja na Kamati hii ilivyoitembelea mnamo tarehe 28 Novemba, 2012, Halmashauri hii imeshawasilisha hesabu zake za mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - Pemba tarehe 23 Septemba, 2013. Waliahidi mbele ya Kamati kuwa kosa hilo halitorejewa tena na taasisi hii.

Uchunguzi wa Kamati

Ingawa Sheria inayohusiana na Baraza la Mji na Halmashauri ya Wilaya, Namba 4/1995, sambamba na Sheria ya Fedha, Namba 12/2005 zinazungumzia suala hili muhimu kwa maendeleo ya nchi. Kamati hii imetoa msamaha kwa taasisi hiyo kwa kosa hilo kutokana na hatua walizozichukua.

Mapendekezo ya Kamati:

- Kwa kuwa Mhasibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni alifunga hesabu zao baada ya kupata msaada kutoka kwa watendaji wengine, Kamati ya P.A.C inamtaka Mhasibu huyo kuchukua juhudi za makusudi na hatimae aweze kufunga hesabu bila ya kutegemea msaada wowote.

- Serikali iwe karibu na Waheshimiwa Madiwani na watendaji wa Halmashauri hii ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na kukuza mashirikiano, ili kuleta maendeleo yaliyokusudiwa.

Hoja Nam. 36.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2011/2012

Taarifa Ya Mapato:

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilikusanya mapato yake kwa ongezeko la Tsh. 42,552,737/- sawa na asilimia 141.8 ya makadirio. Hali hii imetokana na Halmashauri kukadiriwa kukusanya Tsh. 30,000,000 na kufanikiwa kukusanya Tsh. 72,552,737 kwa mwaka 2011/2012.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilivuka malengo yake ya kukusanya mapato kutokana na sababu zifuatazo;-

i. Mashirikiano makubwa baina ya Madiwani na Watendaji wa Halmashauri.
ii. Kuvitambua na kuvisimamia ipasavyo vianzio vya mapato vya Halmashauri
iii. Kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa kulipa kodi.

Sambamba na hilo waliieleza Kamati kuwa ongezeko la makusanyo hayo yalipata ridhaa ya Kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 8 Februari, 2012.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ya P.A.C haikuwa na pingamizi na ongezeko hilo kwa kuwa lilifuata taratibu zote kama Sheria Namba 4/1995 inavyoelekeza. Aidha, Kamati ilibaini kuwa Halmashauri hii haina msingi mbaya wa kukadiria ukusanyaji wa mapato. Hii ni kutokana na kuwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 walikadiria kukusanya Tsh. 20,000,000/- na walifanikiwa kukusanya Tsh. 40,000,000/-, kwa mwaka 2011/2012 walikadiria kukusanya Tsh. 30,000,000/- na walifanikiwa kukusanya Tsh. 72,000,000/- na kwa mwaka wa fedha 2012/2013 walikadiria kukusanya Tsh.77,000,000/- na walifanikiwa kukusanya Tsh. 80,000,000/-.

Taarifa ya Kazi za Kawaida

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri hii ilitumia kwa kazi za kawaida ongezeko la Tsh. 34,330,000/- sawa na asilimia 286 ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri:

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilikiri kufanya matumizi ya ziada kwa kazi za kawaida baada ya kupata ridhaa kutoka kwa Baraza la Madiwani na muongozo wa Wizara. Miongoni mwa sababu zilizopelekea kufanya hivyo ni pamoja na;-

i. Kuongezeka ufuatiliaji wa kazi, ikiwemo kuvifufua, kuvikagua na kufanya operesheni mbali mbali kwenye vianzio vya mapato.
ii. Kuajiri mfanyakazi mwenye ujuzi wa kisheria (mwanasheria), isipokuwa kwamba hivi sasa yupo aliyeajiriwa na Serikali.
iii. Kuongeza ari kwa wafanyakazi na viongozi.
iv. Kupunguza malimbikizo ya madeni.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilikubaliana na matumizi yaliyofanywa kwa maendeleo ya wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa ujumla.

Taarifa ya Kazi za Maendeleo

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri hii ilitumia kwa kazi za kawaida ongezeko la Tsh. 7,090,400/- sawa na asilimia 39.4 ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri:

Ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilitumia fedha za ziada katika kazi za maendeleo. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni;-

i. Ujenzi wa Skuli ya Msingi Mawe Matatu
ii. Kusaidia ujenzi wa Skuli ya Micheweni Sekondari
iii. Ununuzi wa vespa mbili
iv. Ujenzi wa choo Konde
v. Kusaidia Wajasiriamali
vi. Kusaidia kilimo na mazingira
vii. Kusaidia wanafunzi na majanga
viii. Kusaidia ujenzi wa karo Konde Polisi
ix. Kusaidia ujenzi wa choo Wingwi Kitaalani
x. Ujenzi wa uzio na kibanda cha Walinzi

Uchunguzi wa Kamati

Kamati haina pingamizi na matumizi haya.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaipongeza Halmashauri hii kwa juhudi zao wanazozichukua katika kuongeza mapato, lakini imefurahishwa zaidi na namna inavyofuata matakwa ya sheria ya kulishirikisha Baraza la Madiwani katika maamuzi na uendeshaji wa Halmashauri. Aidha, Kamati iliishauri Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuendelea kushikamana kwa lengo la kuleta tija iliyokusudiwa.

2.20 HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani haikuwasilisha hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na Matumizi kama vifungu vya 24(2) na 8 vya Sheria ya Fedha Namba 12/2005 vinavyoelekeza.

Majibu ya Halmashauri:

Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani ilikiri kosa la kutowasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi kama sheria hiyo inavyoelekeza, sanjari na kuomba radhi. Hii ni kutokana na kutokuwa na watendaji wenye sifa ya ufungaji wa hesabu kama vile Mhasibu kwa muda mrefu. Sambamba na

ukosefu wa muongozo wa kutekeleza hayo kutoka katika Taasisi zinazohusiana na masuala ya fedha.

Kutokana na hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuwapatia watendaji wenye sifa, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imeiahidi Kamati kuwa tatizo hilo halitojitokeza tena. Katika kuhalalisha kauli yao hiyo waliieleza Kamati kuwa wameshawasilisha hesabu za mwaka wa fedha 2012/2013 katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali – Pemba kwa ajili ya ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa kuwa Sheria inayohusiana na Baraza na Halmashauri ipo tokea mwaka 1995, sambamba na kuwepo kwa Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, Kamati ya P.A.C haikukubaliana na maelezo yaliyotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani.

Hata hivyo, Kamati imetoa msamaha kwa taasisi hiyo kwa kosa hilo baada ya kuomba radhi na kuieleza Kamati kuwa imeshawasilisha hesabu za mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa hatua zinazohusika.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imewashauri Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani kuzitii sheria za nchi na kanuni zake na waache utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea.

Hoja Nam. 37.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2011/2012

Taarifa ya Mapato na Matumizi:

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani ilikusanya ongezeko la Tsh. 20,822,442/- sawa na asilimia 69.4 ya makadirio, kutokana na makisio ya makusanyo kuwa Tsh. 30,000,000 lakini mapato halisi kuwa Tsh. 50,822,442. Aidha, kwa upande wa matumizi, Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri hii ilitumia kwa kazi za kawaida ongezeko la Tsh. 16,799,661 sawa na asilimia 105 ya makadirio. Aidha, ilitumia ongezeko la Tsh. 3,765,000/- sawa na asilimia 27 ya makadirio kwa kazi za maendeleo.

Majibu ya Halmashauri:

Ongezeko la ukusanyaji wa mapato kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani limetokana na uuzaji wa vyeti vya mazao kwa wingi, ada, faini, marejesho ya madeni, leseni za biashara, mauzaji ya huduma na makusanyo.

Vile vile, waliieleza Kamati kuwa hawakuwa na akaunti ya mapato kwa wakati ule, jambo ambalo lilipelekea kushindwa kubaini kuwa wameshazidi kiwango walichotakiwa kukusanya na waliendelea kukusanya mapato bila ya kupata ridhaa ya Baraza la Madiwani.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufanya uchunguzi wa suala hili, Kamati ilitaka kujua kigezo kinachotumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani wakati wa kukisia mapato ya mwaka husika. Kamati ilielezwa kuwa kigezo kinachotumiwa na Halmashauri hii, ni kuangalia mapato yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha uliopita. Hali hii inatakiwa kuangaliwa kwa makini ili iweze kutoa uhalisia wa mapato ya Halmashauri ama Taasisi nyengine yoyote ya Serikali.

Aidha, Halmashauri baada ya mjadala na Kamati, ilikiri kutumia fedha kinyume na ilivyotakiwa baada ya kuongezeka kwa mapato. Matumizi hayo ya ziada yalitokana na semina na mikutano, gharama za petroli, safari kikazi na matumizi ya mengine ya ofisi.

Pia, waliieleza Kamati kuwa matumizi hayo hayakupata ridhaa ya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kwa kuwa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani ndilo lenye dhamana ya kusimamia mapato ya Halmashauri hii kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria Namba 4/1995, Kamati inawataka Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wa Halmashauri watekeleze majukumu yao kama sheria inavyoelekeza ili kuepusha kasoro zisizokuwa za lazima.

2.21 BARAZA LA MJI MKOANI

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani haikuwasilisha hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na Matumizi kama vifungu vya 24(2) na 8 vya Sheria ya Fedha Namba 12/2005 vinavyoelekeza.

Majibu ya Baraza la Mji:

Baraza la Mji Mkoani lilikiri kosa la kutowasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi kutokana na sababu zifuatazo;-

i. Uelewa mdogo wa kazi hiyo ya ufungaji wa hesabu; na
ii. Hakukuwa na muongozo kutoka katika taasisi husika.

Hata hivyo, waliiomba radhi Kamati na walizidi kueleza kuwa, kwa kuwa suala hili limeshatolewa muongozo na taasisi husika, Baraza la Mji Mkoani limeshawasilisha hesabu zake za mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - Pemba tarehe 23 Septemba, 2013. Waliahidi mbele ya Kamati kuwa hatua hii inaonesha dhahiri kuwa kosa hilo halitorejewa tena na taasisi hii.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ya P.A.C haikukubaliana na maelezo yaliyotolewa na Baraza la Mji Mkoani. Hii ni kutokana na kuwa Sheria inayohusiana na Baraza la Mji, Namba 4/1995, sambamba na Sheria ya Fedha, Namba 12/2005 zinazungumzia kwa kina suala hili muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Hata hivyo, Kamati imetoa msamaha kwa taasisi hiyo kwa kosa hilo kutokana na hatua walizozichukua.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imewashauri Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wa Baraza la Mji Mkoani kutekeleza majukumu kama sheria zinavyoelekeza.

Hoja Nam.39.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2011/2012

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani lilikusanya mapato yake kwa ongezeko la Tsh. 25,508,500/- sawa na asilimia 134 ya makadirio, hali inayotokana na kukadiriwa kukusanya Tsh. 19,000,000 na kufanikiwa kukusanya 44,508,500 kwa mwaka 2011/2012.

Majibu ya Baraza la Mji:

Baraza la Mji Mkoani limeliarifu Kamati kuwa limekusanya mapato kinyume na lilivyoidhinishiwa na Baraza la Madiwani kutokana na kuongezeka kwa mambo yafuatayo;-

i. Ada ya usafi katika mji
ii. Vyeti vya mazao
iii. Ada ya maegesho ya gari
iv. Ada ya ukumbi wa mikutano
v. Kuongeza juhudi katika ufuatiliaji wa makusanyo kwenye vianzio vya mapato na kuchukua hatua za kisheria kwa wale ambao wanakwenda kinyume na matakwa ya Baraza.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati haikukubaliana na ongezeko hilo kutokana na kuwa Baraza la Mji Mkoani halina msingi ‘baseline’ mzuri wa kupanga mapato yake. Kwa mfano; katika mwaka wa fedha 2010/2011 lilikisia kukusanya Tsh. 17,000,000/- na lilifanikiwa kukusanya Tsh.28,031,450/-, mwaka wa fedha 2011/2012 lilikadiria kukusanya Tsh.19,000,000/- na lilifanikiwa kukusanya Tsh. 44,508,500/- na mwaka wa fedha 2012/2013 lilikadiria kukusanya Tsh. 35,000,000/- na lilifanikiwa kukusanya Tsh.47,000,000/-.

Kwa kuwa Baraza la Madiwani ndilo lenye dhamana ya kusimamia mapato na matumizi ya Baraza la Mji Mkoani, Kamati ilitaka kujua kama ongezeko la kukusanya mapato hayo lilipata

ridhaa ya Baraza. Katika kufuatilia hili, Kamati imebaini kuwa ongezeko hilo halikupata ridhaa ya Baraza la Madiwani kufuatia kumbukumbu za Kikao kilichowasilishwa mbele ya Kamati.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati ililishauri Baraza la Mji Mkoani kuitisha Kikao cha Baraza la Madiwani cha kupitisha maamuzi ya mambo yake kabla jambo husika halijachukuliwa hatua za utekelezwaji na Watendaji.

Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Kawaida

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani lilitumia kwa kazi za kawaida ongezeko la Tsh. 27,290,100/- sawa na asilimia 303 ya makadirio, kutokana na kukadiriwa kutumia Tsh. 9,000,000 na hatimae ilipofikia Juni 2012, lilitumia Tsh. 36,290,100.

Majibu ya Baraza:

Baraza hili limeongeza matumizi ya ziada kwa kazi za kawaida kutokana na sababu zifuatazo;-

i. Kuongezeka kwa gharama za kuimarisha usafi wa Mji na
ii. Kuongezeka kwa gharama za shughuli za Ofisi ikiwemo gharama za safari kikazi.

Walizidi kuieleza Kamati kuwa matumizi hayo yaliridhiwa na Baraza la Madiwani.

Uchunguzi wa Kamati:

Ili kuthibitisha uhalali wa kauli iliyotolewa na Baraza la Mji Mkoani, Kamati iliomba kupatiwa kumbukumbu za kikao cha Baraza kilichoridhia matumizi hayo. Katika kuipitia kumbukumbu hiyo Kamati ilibaini kuwa kikao kilifanyika wakati shughuli zimeanza kutekelezwa. Vile vile, Kamati ilibaini kuwa tarehe iliyoandikwa kumbukumbu ndio tarehe ambayo kumbukumbu hizo zimeridhiwa na Waheshimiwa Madiwani kitu ambacho ni kinyume na utaratibu.

Mapendekezo ya Kamati:

Kutokana na makosa yaliyojitokeza, Kamati imeshindwa kuzikubali kumbukumbu hizo na kulitaka Baraza la Mji Mkoani kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa sheria.

Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Maendeleo

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani lilitumia kwa kazi za maendeleo mapungufu ya Tsh. 1,781,600/- sawa na asilimia 18 ya makadirio, kutokana na kukadiriwa kutumia Tsh. 10,000,000 na kuingiziwa Tsh. 8,218,400 kwa kazi za maendeleo ya mwaka 2011/2012.

Majibu ya Baraza la Mji:

Baraza la Mji Mkoani limeiarifu Kamati kuwa limeshindwa kutumia fedha ililoidhinishiwa na Baraza la Madiwani kutokana na kukosa eneo la kujenga slabi moja huko Uweleni na kufanikiwa kujenga slabi nne badala ya tano. Pia, walishindwa kuweka kifusi katika Barabara ya Makadara baada ya kufikiria kuwa Mradi wa ZUSP utaanza karibuni na endapo wataijenga barabara hiyo watapoteza fedha za walipa kodi wa Mkoani.

Kwa hiyo, fedha zilizopangwa kutumika kwa shughuli hizo zilitumika kwa kazi nyengine ambazo ziliridhiwa na Baraza la Madiwani.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imehoji fedha zilizobakia katika ujenzi wa silabi moja iliyobakia ambayo haikujengwa huku ikiwa imeidhinishwa na Baraza la Madiwani. Hata hivyo, fedha hizo zimeelezwa zipo katika Mfuko wa Baraza, ingawaje Kamati imeshindwa kuzithibitisha.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inalitaka Baraza kutumia fedha za maendeleo kwa mnasaba wa maelekezo ya Baraza la Madiwani na sio vyenginevyo.

2.22 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Chake Chake haikuwasilisha hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na Matumizi kama vifungu vya 24(2) na 8 vya Sheria ya Fedha Namba 12/2005 vinavyoelekeza.

Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake

Baraza la Mji Chake Chake lilikiri kosa la kutowasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi kama sheria inavyoelekeza. Hii ni kutokana na uzoefu mdogo wa kazi hiyo kwa watendaji wake. Hata hivyo, baada ya kupata muongozo na maelekezo kutoka katika Taasisi zinazohusiana na masuala ya fedha, Baraza la Mji Chake Chake limeiahidi Kamati kuwa tatizo hilo halitojitokeza tena.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa kuwa Sheria inayohusiana na Baraza la Mji ipo tokea mwaka 1995, sambamba na kuwepo kwa Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, Kamati ya P.A.C haikukubaliana na maelezo yaliyotolewa na Baraza la Mji Chake Chake. Hata hivyo, Kamati imetoa msamaha kwa taasisi hiyo kwa kosa hilo baada ya kuieleza Kamati kuwa imeshawasilisha hesabu za mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imewashauri Watendaji wa Baraza la Mji Chake Chake kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na waache kufanya kazi kwa mazoea.

Hoja Nam. 40.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2011/2012

Taarifa ya Mapato

Kutokana na kukadiriwa mapato ya Tsh. 64,000,000 kwa Baraza la Mji Chake Chake mwaka 2011/2012 na kufanikiwa kukusanya Tsh. 85,735,954, ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Chake Chake lilikusanya mapato yake kwa ongezeko la Tsh. 21,735,954/- sawa na asilimia 34 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Mji:

Baraza la Mji Chake Chake limeiarifu Kamati kuwa limekusanya mapato ya ziada kutokana na juhudi kubwa walizochukua za kufuatilia vyanzo vyao vya mapato. Walizidi kueleza kwamba ongezeko la mapato hayo yaliridhiwa na Kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 17 Aprili, 2012.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imeridhika na majibu yaliyotolewa na Baraza la Mji Chake Chake ya ongezeko la mapato hayo. Pia, Baraza hili lina msingi ‘baseline’ mzuri wa kupanga mapato yake. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza lilikisia kukusanya Tsh. 50,000,000/- na lilifanikiwa kukusanya Tsh. 65,000,000/-, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 lilikadiria kukusanya Tsh. 64,000,000/- na lilifanikiwa kukusanya Tsh. 85,000,000/- na mwaka wa fedha 2012/2013 lilikadiria kukusanya Tsh.83,000,000/- na lilifanikiwa kukusanya Tsh. 100,000,000/-.

Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Chake Chake lilitumia kwa kazi za kawaida kwa ongezeko la Tsh. 31,297,255/- sawa na asilimia 98 ya makadirio**.** Aidha, lilitumia kwa kazi za maendeleo mapungufu ya Tsh. 9,576,200/- sawa na asilimia 30 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake

Baraza la Mji Chake Chake lilikiri kuongeza matumizi hayo kufuatia Kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 17 Aprili, 2012.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya P.A.C haikuwa na pingamizi na matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo yaliyofanywa na Baraza la Mji Chake Chake na hasa ikizingatia kuwa matumizi hayo yaliridhiwa na Baraza la Madiwani ambalo ndilo lenye dhamana ya kuridhia matumizi ya ziada kwa mujibu wa kifungu cha 41 cha Sheria ya Baraza la Mji Namba 4/1995.

Mengineyo

- Waheshimiwa Madiwani kwa pamoja walimuomba Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kumkumbusha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kutekeleza ahadi alizozitoa kwa Waheshimiwa Madiwani wa Baraza la Mji Chake Chake. Miongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na kuwaandalia mafunzo, semina, ziara za kimafunzo nakadhalika.

- Baraza la Mji Chake Chake linakabiliwa na upungufu wa watendaji hususan katika eneo la usafi, eneo ambalo ni moja kati ya kianzio chake cha mapato.

Mapendekezo ya Kamati:

- Kamati hii inalikumbusha Baraza la Mji Chake Chake kuitisha Kikao cha Baraza la Madiwani cha kupitisha maamuzi ya mambo yake kabla jambo husika halijachukuliwa hatua na Watendaji.

- Kwa kuwa baadhi ya Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya zimepiga hatua ukilinganisha na nyengine, Kamati inalishauri Baraza hili kuwa na utamaduni wa kuwaalika wengine ili wabadilishane mawazo kuhusiana na uendeshaji wa Taasisi hizi.

- Ingawa Baraza lina upungufu na watendaji wa aina hii, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa watendaji waliopo huondoka katika sehemu zao za kazi mapema. Hivyo, inashauri Baraza la Mji la Chake Chake kuwafuatilia kwa karibu watendaji wake ili wawajibike ipasavyo.

- Kwa kuwa baadhi ya Waheshimiwa Madiwani wa Baraza la Mji Chake Chake walishindwa kukunua suti kama walivyotakiwa, Kamati hii imeshauri wakabidhiwe suti kamili ili kuepusha kasoro iliyojitokeza hapo awali.

2.23 BARAZA LA MJI WETE

Hoja Nam. 13.1: Uwasilishaji wa Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Wete haikuwasilisha hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na Matumizi kama vifungu vya 24(2) na 8 vya Sheria ya Fedha Namba 12/2005 vinavyoelekeza.

Majibu ya Baraza la Mji Wete

Baraza la Mji Wete lilikubaliana na hoja ya kutowasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kutokana na kukosekana kwa miongozo na Wataalamu wenye ujuzi wa kufunga hesabu.

Hata hivyo, waliiomba radhi Kamati hii na walieleza kuwa kosa hilo halitarejewa tena kwa kuwa suala hili limeshatolewa muongozo na taasisi husika pamoja na kupatiwa wataalamu wenye ujuzi wa kufanya hivyo. Katika kuthibitisha hilo walieleza kuwa wameshawasilisha hesabu zao za mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - Pemba tarehe 23 Septemba, 2013 kwa barua yenye kumbukumbu Namba BLMW/OR/TMV/1.M/P/M.60/VOL.1/75.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imetoa msamaha kwa taasisi hiyo baada ya kuridhika na hatua zilizochukuliwa.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inawashauri Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wa Baraza la Mji Wete kutekeleza majukumu kama sheria zinavyoelekeza. Hii ni kutokana na kuwa Sheria zinazozitaka Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwasilisha hesabu zao kwa ajili ya ukaguzi katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zipo siku nyingi.

Hoja Nam. 41.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2011/2012

Taarifa ya Mapato:

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Wete lilikusanya mapato yake kwa ongezeko la Tsh. 10,200,000/- sawa na asilimia 22 ya makadirio.

Majibu ya Baraza:

Ongezeko la ukusanyaji wa mapato kwa Baraza la Mji Wete limetokana na kuongezeka kwa vianzio vya mapato pamoja na kuvisimamia vyema vianzio vilivyopo.

Vile vile, waliieleza Kamati kuwa ongezeko la mapato hayo hayakupata ridhaa ya Baraza la Madiwani.

Uchunguzi wa Kamati:

Wakati wa majadiliano na Watendaji wa Taasisi hii Kamati ilibaini kuwa Baraza la Mji Wete lilikusanya mapato hayo bila ya ridhaa ya Baraza la Waheshimiwa Madiwani kwani ilielezwa kuwa, Kamati ya Fedha ya Baraza la Mji Wete ndio iliyokuwa inaidhinisha mapato na matumizi huku ikikutana kila baada ya miezi mitatu. Kutokana na kasoro hiyo Kamati ililitaka Kamati hiyo kutokufanya kazi ya Baraza la Madiwani tena bila ya idhini na kuitaka Afisi ya Baraza kuitisha Vikao vya Baraza la Madiwani kwa kutekeleza majukumu yaliyopewa kwake kisheria.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inawataka Watendaji wa Baraza hili wahakikishe kuwa, sheria ya kuanzishwa kwa Mabaraza ya Miji na Sheria nyengine za Fedha zainatekelezwa na kusimamiwa ipasavyo.

Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Wete lilitumia kwa kazi za kawaida ongezeko la Tsh. 8,000,000/- sawa na asilimia 39 ya makadirio. Aidha, lilitumia mapungufu ya Tsh. 2,200,000/- sawa na asilimia 9 ya makadirio.

Majibu ya Baraza:

Baraza la Mji Wete lilikiri kutumia fedha za ziada kinyume na lilivyotakiwa baada ya kupindukia malengo ya ukusanyaji. Vile vile, waliieleza Kamati hii kuwa matumizi hayo yaliyofanywa hayakupata ridhaa ya Baraza la Madiwani la Baraza la Mji Wete.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imethibitisha kwamba, afisi ya Baraza imefanya matumizi bila ya idhini ya Baraza la Madiwani kutokana na hata Madiwani waliofika katika kikao hicho walikubali kosa hilo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inalitaka Baraza kufahamu majukumu yao kisheria na kuzitekeleza sheria kwa vitendo.

Mengineyo

- Kamati ililitaka Baraza la Mji Wete kukamilisha kulijaza Daftari la Mali zake ili kuwa na kumbukumbu sahihi.
- Ili kukomesha vitendo viovu katika Taasisi mbali mbali za Serikali, Waheshimiwa Madiwani wameishauri Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu Watendaji wote wanaotekeleza majukumu yao kinyume na misingi ya kiutendaji na sio kubadilishwa Taasisi.

2.24 OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBILISHO:

Hoja Nam. 42.2: Malipo yasiyokuwa na vielelezo (nyaraka pungufu), Tsh. 219,390,619.

Fedha hizo zimelipwa kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Ofisi:

Ofisi imekiri kutokea kwa kasoro hiyo wakati wa ukaguzi, ingawa wakati wa Kamati vilikuwa vimeshapatikana na kuitaka Kamati ivikague.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati inafahamu kuwa, kifungu cha 70(1) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, kinaelekeza kuwa risiti za kuthibitisha ama kuwa kielelezo cha ushahidi wa matumizi ya fedha za umma ni

lazima zipokelewe na kupatikana mara tu fedha za umma zinapolipwa. Aidha, kama yangelifuatwa maelekezo ya kanuni hii na kanuni nyengine zinazohusika, basi kusingelikuwa na haja yoyote ya vielelezo hivyo kukosekana wakati wa ukaguzi na ni jambo la kustaajabisha kuwa vielelezo hivyo vinapatikana wakati wa ukaguzi wa kazi za Kamati. Hivyo basi, Kamati inaelekeza kwamba, haina jukumu la kuvikagua vielelezo hivyo ambavyo vimekosekana wakati wa ukaguzi.

Mapendekezo ya Kamati:

Ofisi hii iwe makini wakati wa kufanya matumizi ya fedha za umma, kwani kutokuwa na vielelezo au kuwa na vielelezo pungufu ni kwenda kinyume na sheria ya Fedha ya mwaka 2005, kama pia ilivyoelezwa na kifungu cha 95(4) cha sheria hiyo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kumuonya kwa maandishi, Afisa Mhasibu wa Afisi hii kwa kutokuwa muangalifu wakati wa matumizi ya fedha za Serikali.

3.0 WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI:

Hoja Nam. 58.1: Hesabu za Mwisho wa Mwaka.

Taarifa ya Mapato:

Wizara ilikadiriwa kukusanya Tsh. 2,198,343,000 katika kipindi cha mwaka 2011/2012, lakini hadi kufikia Juni 2012 ilikusanya Tsh. 2,447,200,002 sawa na 111.3%, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 248,857,002 (11.3%) ya makadirio.

Matumizi ya Kawaida:

Wizara iliidhinishiwa kutumia Tsh. 5,714,468,388 na kuingiziwa na kutumia Tsh. 5,533,323,016 sawa na 96.83% ya makadirio, ikiwa ni pungufu ya Tsh. 181,145,372 (3.17%) ya makadirio.

Matumizi ya Maendeleo:

Wizara ilikadiriwa kutumia Tsh. 4,996,902,000 kwa kazi za maendeleo kwa kipindi cha 2011/2012 na kuingiziwa na kutumia Tsh. 4,903,254,000 sawa na 98.1% ya makadirio, ikiwa ni pungufu ya Tsh. 93,648,000 (1.9%) ya makadirio.

Majibu ya Wizara:

Kuhusu kuongezeka kwa mapato kunatokana na kuongezeka kwa malipo ya madeni ya miaka ya nyuma ambayo hawakuyatarajia kulipwa kwa kiwango kilicholipwa na wadaiwa.

Kuhusiana na matumizi kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo, suala hilo halimo mikononi mwao, bali ni jukumu la Wizara ya Fedha.

Uchunguzi wa Kamati:

Kuhusiana na mapato, Kamati imetaka kupewa namna ya malipo hayo ya madeni yalivyolipwa kwa mwaka husika, ili kujiridhisha. Kuhusiana na suala la matumizi, Kamati italifuatia suala hilo Wizara ya Fedha. Aidha, kwa upande wa Matumizi ya kazi za Maendeleo, Kamati pia imehitaji kupatiwa mnyambuliko wa matumizi hayo kifungu kwa kifungu, jambo lililoahidiwa kukabidhiwa.

Mapendekezo ya Kamati:

Mpaka Kamati inaandika ripoti hii, haijapatiwa taarifa za ulipwaji wa madeni hayo ili ikajiridhisha kama ilivyoahidiwa. Na hivyo, imeshindwa kutoa maoni yake kuhusiana na suala hilo.

Hoja. Nam. 58.2: Malipo yasiyokuwa na Vielelezo (Nyaraka Pungufu) Tsh. 26,559,500

Jumla ya Tsh. 26,559,500 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi. Kukosekana kwa vielelezo ni kwenda kinyume na kanuni ya 95(4) ya kanuni za fedha za Zanzibar ya mwaka 2005. Kwa hali hiyo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa.

Majibu ya Wizara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi stakabadhi za ununuzi wa mbao zilikosekana. Kukosekana stakabadhi hizo kumesababishwa na aliekabidhiwa fedha hizo kutokuwasilisha kwa wakati na tayari hivi sasa zimeshawasilishwa kwa kukaguliwa.

Uchunguzi wa Kamati:

Pamoja na Wizara kukiri kwamba wakati wa ukaguzi vielelezo hivyo vilikosekana na sasa vipo tayari kwa ukaguzi, maelezo haya yanapingana na maelekezo ya kifungu cha 70 cha kanuni za Fedha za mwaka 2005, kinachoelekeza kuwa vielelezo (risiti) vipatikane mara tu malipo ya fedha yanapofanyika.

Aidha, Kamati ilipopitia vocha zilizohusika, imebaini makosa kadhaa ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:

- Hati Namba C7/01/2012 ya Tsh. 6,750,000 hakuna maombi ya fedha kwa ‘Accounting Officer’.
- Hati Namba R84/10/11 ya Tsh. 5,547,500 inahusiana na posho na nauli ya kwenda na kurudi Sychelles, lakini hamna maombi ya malipo ya fedha hizo wala dokezo lolote.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 95(4) cha Kanuni za fedha za mwaka 2005, kukosekana kwa kielelezo kimoja tu kati ya vielelezo muhimu katika hati ya malipo, ni sawa na kukosekana vielelezo vyote, na kwa hali hii, uhalali wa malipo hayo hauwezi kuthibitishwa na Kamati.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati haikuridhishwa na udhaifu uliooneshwa na Wizara hii jinsi ya kuzisimamia Idara zake na inapendekeza kurekebishwa kwa kasoro hizo.

Hoja Namba 58. 3; Kukosekana kwa marejesho ya masurufu (Imprest) Tsh. 15,450,000.

Fedha hizo zimelipwa ikiwa ni masurufu lakini marejesho ya matumizi hayo hayakupatikana kwa ukaguzi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 102(1)(2) ya kanuni ya Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2005.

Majibu ya Wizara:

Wizara imesahihisha matumizi ya fedha hizo kwamba sio 'imprest' bali Tsh. 10,000,000 kupitia Hati Namba C6/10/2011 ni ya 'Ukaguzi Maalum' na Tsh 450,000 kupitia Hati Namba R51/03/2012 ni malipo ya 'overtime', huku Tsh. 5,000,000 zimeripotiwa kimakosa.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imejiridhisha kwamba, malipo ya Tsh. 450,000 ni 'overtime' kama walivyoeleza Wizara. Hata hivyo, Kamati inasimamia hoja ya kutorejeshwa kwa marejesho ya fedha hizo, huku ikijiridhisha kwamba, kwa matumizi ya overtime, barua ya maombi ya fedha hizo haikuonesha idadi halisi ya fedha zilizoombwa, jambo ambalo linaonesha udhaifu wa utaratibu mzima wa maombi na uidhinishaji wa fedha za umma. Aidha, vielelezo vya malipo yaliyohusika havikuweza kupatikana na kuthibitishwa na Kamati.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kurekebisha mara moja ili kasoro za aina hii, zisijitokeze tena.

Hoja Namba 58. 4: Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye Daftari la Ghalani, Tsh. 29,812,000

Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali lakini havikuingizwa kwenye daftari la vifaa ili kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake. Kutokuwepo kwa kumbu kumbu za vifaa ni kwenda kinyume na kanuni ya 198 ya kanuni za fedha za 2005.

Majibu ya Wizara:

Wanakiri kufanya kosa hilo kwa vifaa vya Mahakama ya Ardhi pamoja na manunuzi ya mafuta. Aidha, kwa Idara ya Ujenzi kuhusiana na Hati Namba R47/10/11 ya malipo ya ununuzi wa vespa, wanasema vespa hiyo wameipeleka Pemba, na hivyo ingelirikodiwa katika daftari la huko. Kuhusiana na Hati Namba C5/12/11 kuhusiana na ununuzi wa saruji, wameingiza katika daftari.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imethibitisha kwamba, Wizara haikuingiza katika daftari la ghalani kwa vifaa vya Mahakama ya Ardhi ikiwa ni pamoja na mafuta. Kuhusiana na ununuzi wa vespa, Kamati haikubaliani na hoja ya Wizara. Pamoja na kusafirishwa Pemba, kwa kuwa vespa hiyo imenunuliwa Unguja, walitakiwa warikodi katika daftari la vifaa vya Unguja. Aidha, kuhusiana na manunuzi ya saruji, Kamati imepitia na imethibitisha upokewaji wa mifuko 500 ambayo haijapelekwa Bambi kama ilivyoombwa na badala yake imepelekwa Bungi, kinyume na matumizi yaliyoombwa.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati hairidhishwi na maelezo pamoja na utendaji wa Wizara na inapendekeza kasoro hizo zirekebishwe mara moja na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watendaji wote waliohusika wachukuliwe hatua za kinidhamu.

3.1 IDARA YA MAJENZI NA UTUNZAJI WA NYUMBA:

Hoja Namba 58.5.1: Kukosekana kwa Marejesho ya Masurufu (imprest) Tsh. 79,750,000

Fedha hizo zimelipwa kama masurufu lakini marejesho ya matumizi hayo hayakupatikana kwa ukaguzi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 102(1)(2) cha Kanuni za fedha za mwaka 2005.

Majibu ya Wizara/Idara:

Tsh. 60,600,000 ndizo marejesho yake hayakupatikana kwa ukaguzi. Tsh. 19,150,000 marejesho yake yalikuwepo na yaliwekwa kwenye jalada maalum ambalo alikabidhiwa Mkurugenzi wa Ujenzi kwa ajili ya kusubiri kufanyiwa ‘verification’ na Mkaguzi. Kwa bahati mbaya, jalada hilo lilipotakiwa kuwasilishwa kwenye Kamati iliyoundwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu halikupatikana hata wakati wa kazi za Kamati.

Suala hilo limepelekwa Polisi tokea mwaka 2012 kwa uchunguzi zaidi kulingana na kanuni za Fedha za Zanzibar na bado Polisi haijakamilisha taratibu zao na kufungua mashtaka dhidi ya waliohusika.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwamba, hakukuwa na vielelezo vya kuthibitisha marejesho hayo. Aidha, kitendo cha Mkurugenzi kupoteza faili, hakivumiliki na ni kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

Kuhusiana na upotevu wa fedha hizo, Kamati imepatiwa barua ya tarehe 07/08/2012 yenye kumbu kumbu namba AD.3/172/01/3 na barua ya tarehe 22/08/2012 yenye kumbu kumbu namba AD.3/172/01/8 zinayohusiana na upotevu wa fedha za matumizi kwenye hesabu ya ‘Deposit’ ya

Idara ya Ujenzi, Tsh. 57,000,000. Aidha, Kamati imethibitishiwa kwamba, watendaji waliohusika ambao ni Ndg. Ali Hassan Rajab (Mhasibu); Ndg. Mrisho Kassim Ali (Mshika Fedha), wamesimamishwa kazi na suala lao limeripotiwa Polisi kwa barua namba AD.3/172/01/12 ya tarehe 30/08/2012.

Kamati imeshangazwa kwa nini kadhia hiyo isimhusishe pia Ndg. Saada Abdalla (Msaidizi Mhasibu) ambae alikiri pamoja na wenzake waliotajwa hapo juu kuhusika na upotevu huo kupitia barua ya tarehe 19/07/2012 yenye kumbu kumbu namba IU/AMMN/. Aidha, Kamati pia inaamini Mkurugenzi wa Idara hii anahusika kwa namna moja ama nyengine katika kadhia hii, na zaidi kwa kitendo chake cha kuharibu ushahidi husika kwa kupoteza faili lenye kumbu kumbu zote muhimu.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali imchukulie hatua za kinidhamu na kijinai Mkurugenzi kwa kupoteza faili na kumbu kumbu za Idara zinazohusiana na matumizi ya fedha hizo.

Kuhusiana na washtakiwa waliopelekwa Polisi, Kamati inaitaka Polisi ikamilishe uchunguzi wake, ili watuhumiwa hao wapelekwe Mahakamani na Sheria ichukue mkondo wake. Aidha, katika kadhia hiyo, Msaidizi Mhasibu, Ndg. Saada Abdalla ahusishwe sambamba na watuhumiwa waliobakia, ili haki iweze kutendeka.

Hoja Namba 58.5.2: Malipo yasiyokuwa na Vielelezo (Nyaraka Pungufu) Tsh. 17,137,000

Fedha hizo zimelipwa kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi. Kukosekana kwa vielelezo ni kwenda kinyume na kanuni ya 95(4) ya kanuni za fedha za Zanzibar za mwaka 2005. Kwa hali hiyo, uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa.

Majibu ya Wizara/Idara:

Wizara imekiri kwamba, hawakuwa na vielelezo vyote vilivyohitajika kwa ajili ya kuthibitisha matumizi ya fedha zilizoripotiwa. Kwa mfano, katika:

- Hati namba D13B/10 yenye thamani ya Tsh. 525,000 kwa ajili ya malipo ya ‘Concrete mixer’ Mkataba wa ukodishwaji wa mashine husika umekosekana.
- Hati namba 18B/11/2011 yenye thamani ya Tsh. 150,000 kwa ajili ya malipo ya ushonaji wa sare, risiti za uhalali wa malipo hayo hazikupatikana.
- Hati namba D18A/11/2011 yenye thamani ya Tsh. 1,230,000 aliyolipwa Mkurugenzi wa Idara hii (Ndg. Ramadhan M. Bakar, kwa ajili ya safari ya kikazi, haina vielelezo (tiketi).

Uchunguzi wa Kamati.

Kamati imejiridhisha udhaifu wa Idara hii katika matumizi ya fedha za Serikali, na inasikitishwa kwa kitendo cha Mkurugenzi wa Idara hii kushindwa kusimamia matumizi ya fedha hizo na hata

yeye mwenyewe anapolipwa fedha kwa ajili ya matumizi ya safari, anashindwa kufanya marejesho yanayotakiwa kisheria.

Mapendekezo ya Kamati:

Serikali ichukue hatua za kuisimamia Idara hii iweze kutumia fedha za umma kwa mujibu wa sheria. Kwa udhaifu uliojitokeza, Kamati inapendekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa waliohusika.

Hoja Namba 58.5.3: Malipo yaliyotofauatiana na 'Bank Statement', Tsh. 163,580,000/

Ukaguzi umebaini kwamba kuna idadi kubwa ya fedha zimelipwa kwa shughuli mbali mbali lakini malipo hayo yanatofautiana kati ya hati ya malipo na fedha halisi zilizotoka Benki.

Majibu ya Wizara/Idara.

Inakubaliana na hoja ya Mdhibiti kuhusiana na tofauti iliyopo baina ya 'Bank Statement' na hati za malipo. Hali hiyo kwa kiasi kikubwa ndio iliyowafanya wagundue upotevu wa Tsh. 57,000,000 kwenye hesabu hiyo. Waliieleza Kamati kwamba wamechukua hatua zifuatazo:

- Kuifunga hesabu hiyo na kuhamishia shughuli zake katika hesabu ya Deposit ya Wizara (badala ya Idara ya Ujenzi), yaani 'Central Payment Deposit Account'
- Suala la upotevu huo kuliripoti katika vyombo husika kama Kanuni za Fedha zinavyoelekeza kupitia kifungu cha 22(a) hadi (o).
- Wahusika wa upotevu huo ambao ni Mhasibu na Mshika Fedha wake, wamesimamishwa kazi kwa mujibu wa sheria namba 2 ya mwaka 2011 na wanalipwa nusu mshahara hadi pale suala hilo litakapopatiwa ufumbuzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imejiridhisha kuwepo kwa udhaifu mkubwa wa fedha uliopelekea wizi wa zaidi ya Tsh. 57,000,000. Aidha, Kamati imegundua udhaifu wa Mkaguzi wa Ndani, ambae hakuliripoti tatizo hilo katika ripoti ya mwaka, huku ukaguzi pekee uliopelekea kuwepo wazi kwa taarifa hizo ni ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu.

Mapendekezo ya Kamati:

Serikali ichukue hatua za kinidhamu na kijinai kwa waliohusika. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa ndani ili kiweze kutoa taarifa sahihi zinazohitajika.

Hoja namba 58.5.4: Hati zilizokosekana kwa ukaguzi (missing vouchers) Tsh. 340,450,600

Fedha hizo zimetumika kwa malipo mbali mbali lakini hati za malipo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni ya 95(4) ya kanuni ya fedha ya mwaka 2005.

Majibu ya Wizara/Idara:

Baadhi ya hati za malipo zilizoripotiwa na Mkaguzi zilikuwepo lakini kutokana na utaratibu mbovu wa utunzaji wa kumbu kumbu Idarani hapo, hazikuweza kupatikana pale zilipohitajika. Aidha, kwa upande mwengine, ongezeko la vocha zilizokosekana kwa mwaka huo, limechangiwa na kuingizwa kwa vocha za miezi kumi na kumi na moja ya mwaka 2012 ambazo hazikupaswa kuwemo katika hesabu za mwaka 2011/2012. Thamani ya vocha hizo ni Tsh. 70,513,500 na zile zilizokosekana kutokana na utaratibu mbaya wa utunzaji, thamani yake ni Tsh. 52,459,500 ambazo kwa pamoja zingeweza kupunguza idadi iliyopo juu kufikia Tsh. 217,477,600.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati inaendelea kusikitishwa na udhaifu mkubwa wa matumizi ya fedha za umma kwa Idara hii. Aidha, pamoja na maelezo ya tofauti ya fedha zilizoripotiwa na Mdhibiti pamoja na hesabu za Idara, viongozi wa Wizara na Idara wameshindwa kuthibitisha usahihi wa maelezo hayo na hivyo Kamati haiwezi kukubaliana na maelezo yao.

Mapendekezo ya Kamati:

Serikali iwachukulie hatua kali za kisheria na kinidhamu wahusika wote waliotajwa ndani ya ripoti hii, kuhusiana na Idara hii.

Hoja namba 58.5.5: Kuhusina na matumizi ya fedha yaliyokosa maelezo, Tsh. 65,164,212.41, Hesabu namba 9928161504:

Kutokana na barua yenye kumbu kumbu namba OR/FUMM/B10/7/VOL.V/ ya tarehe 18/6/2012, barua hiyo iliitaka Idara ya Ujenzi na Utunzaji Nyumba kuhamisha salio la fedha kwenda kwenye hesabu 9928161504 ‘central payment deposit account’. Katika ukaguzi uliofanyika umebainika, hadi kufungwa kwa hesabu namba 021103000519 ya Idara ya Ujenzi, ilitakiwa kuwa na bakaa ya Tsh. 57,000,000 kupitia barua ya 31/07/2012 iliyomtaka Mhasibu Mkuu wa Idara kutoa statement ya mwisho hadi kufikia tarehe ya ukaguzi huu.

Jumla ya Tsh. 1,212,687.59 ndizo zilizohaulishwa kwenda ‘central payment deposit account’, kupitia ‘bank statement’ ya 19/6/2012. Na jumla ya Tsh. 55,787,312.41/- hazikupatika kwa ukaguzi.

Aidha, ukaguzi umebaini jumla ya Tsh. 9,376,900/- zilizolipwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kazi za studio Bungi kupitia hundi namba 112309 ya tarehe 22/6/2012 hazikuwekwa kwenye hesabu namba 9928161504 central payment deposit account, hadi kukamilika kwa ukaguzi huu.

Majibu ya Wizara/Idara:

Kwa mujibu wa kumbu kumbu za Wizara, hesabu hiyo ipo katika taratibu za kufungwa kulikuwa na salio la Tsh. 57,000,000 ambazo ndizo zilizopaswa kuhamishiwa kwenye hesabu namba 9928161504 'Central payment Deposit Account' wakati taarifa za benki zinaonesha ni Tsh. 1,212,687.59 ndizo zilizokuwepo wakati huo. Katika kufuatilia suala hilo waligundua kuwa, Tsh. 55,787,312.41 zimetolewa kwa njia ya udanganyifu na kutumika nje ya lengo lililokusudiwa. Vile vile Tsh. 9,376,900 ni kweli hazikuingizwa kwenye hesabu husika. Suala hilo wameshaliripoti Polisi kwa hatua za kisheria.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imesikitishwa na taarifa za viongozi wa Wizara pamoja na Idara kuhusiana na suala hilo. Kamati pia imefahamishwa kwamba, katika njia za upotevu wa fedha hizo, hata 'Bank Statement' zilizotumiwa na watuhumiwa wa upotevu wa fedha za account hiyo, ni za udanganyifu na hata mihuri iliyotumika ni ya kufoji.

Aidha, pamoja na Idara kukamilisha ujenzi wa studio za ZBC, Bungi. Mradi ambao umepelekea Idara kupata fedha na nyengine kumalizia mikononi mwa watendaji wachache, Kamati imejuilishwa kwamba, bado Idara imebakia na madeni mengi kutoka kwa 'suppliers' tofauti huku fedha ambazo ndio zingelitumika kulipa madeni hayo, zimeishia mifukoni mwa watendaji.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaendelea kusisitiza kuchukuliwa kwa hatua za kisheria na hatua za kinidhamu kwa watendaji wote waliohusika, bila ya kumsahau Mkurugenzi wa Idara hii na msaidizi mhasibu, Ndg. Saada Abdalla.

Hoja Namba 58.5.6: Malipo yaliyofanyika kinyume na taratibu kwa kukosa hati za malipo. Tsh. 33,182,100

Jumla ya fedha hizo zimetumika kwa malipo ambayo yalilipwa moja kwa moja kupitia hundi bila ya kuwepo hati ya malipo pamoja na vielelezo vyenye kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Majibu ya Wizara/Idara:

Wizara imekiri kutokuwepo kwa vielelezo vilivyohitajika, ikiwa ni pamoja na hati namba 994859 yenye thamani ya Tsh. 2,400,000 na hati namba 9944867 ya thamani ya Tsh. 13,150,000. Aidha, hati nyengine zilobakia, Watendaji wa Wizara wanasema zilikuwepo, ingawaje zimepotea pamoja na nyengine kupitia faili alokabidhiwa Mkurugenzi wa Idara.

Uchunguzi wa Kamati:

Pamoja na maelezo kwamba, baadhi ya vielelezo vilikuwepo hapo awali, Kamati haikuweza kukubaliana na hoja hizo kwa sababu havikuweza kuthibitishwa mbele ya Kamati. Aidha, kuendelea kuelezwa kupotea kwa vielelezo hivyo na mahusiano yake na upotevu wa faili, kunaifanya Kamati kusikitishwa zaidi na usimamizi wa fedha za umma katika Idara hii.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaendelea kusisitiza kuchukuliwa hatua za kisheria na kinidhamu kwa Mkurugenzi wa Idara hii pamoja na waliohusika.

Hoja Namba 58.5.7: Kuvunjwa kwa hundi Tsh. 127,128,848

Fedha hizo zimelipwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa ujenzi wa studio katika eneo la Bungi, ambayo ilikuwa kwa Idara ya Ujenzi, imefunguliwa na haikuweza kuingizwa Benki na pia haikupatikana kwa ukaguzi. Ukaguzi umebaini kwamba, hundi hiyo haikuingizwa benki na badala yake imevunjwa na kupatikana fedha taslim.

Hadi ukaguzi unakamilika, fedha hizo hazikujuulikana zimepelekwa wapi na kumbu kumbu za matumizi yake hazikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Wizara/ Idara:

Ni kweli hundi hiyo imevunjwa kwa makusudi na kutolewa Tsh. 2,000,000 kinyume na taratibu, na salio la Tsh. 125,128,848 zimewekwa benki kwenye hesabu namba 021103000519 (hesabu ya Amana ya Idara ya Ujenzi). Fedha hizi zililipwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za matangazo ya redio Bungi. Wizara ya Ardhi imefanya utafiti wa matumizi yaliyokusidiwa na kubaini kwamba, ujenzi uliokusudiwa umefanyika lakini haukuweza kukamilika ipasavyo.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imejiridhisha juu ya ukweli wa maelezo ya Wizara na usahihi wa hoja ya Mdhibiti na imefuatiali hadi eneo la Bungi kwenye ujenzi husika na kushuhudia hali halisi. Aidha, fedha zilizotumika katika ujenzi huo ni nyingi huku hakuna uthibitisho wa matumizi ya fedha hizo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inapendekeza kuchukuliwa kwa hatua za kisheria na kinidhamu kwa waliohusika.

Hoja namba 58.5.8: malipo yaliyofanyika bila ya kuidhinishwa na Mkurugenzi, Tsh. 3,400,000

Fedha hizo zimebainika kulipwa bila ya idhini ya Mkurugenzi, lakini malipo hayo hayakuwa halali kutokana na kubuniwa kwa saini ya Mkurugenzi wa Idara.

Majibu ya Wizara/Idara:

Kukosekana kwa hati za malipo, Wizara imeshindwa kuifanyia kazi hoja hii.

Uchunguzi wa Kamati:

Hoja hii inahusika pamoja na hoja zilizoripotiwa kuhusiana na wizi ama upotevu wa fedha katika Idara hii. Kamati pia inasikitishwa na maelezo kwamba faili husika limepotea, ikiwa ni pamoja na hati za malipo za hoja hii, mikononi mwa Mkurugenzi wa Idara.

Mapendekezo ya Kamati:

Mkurugenzi na watendaji wa hesabu waliohusika wachukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu ili kukomesha mapungufu hayo.

Hoja namba 58.5.9: malipo yaliyofanywa kinyume cha kanuni na taratibu za manunuzi, Tsh. 25,000,000/-

Fedha hizo zimetumika kwa gharama za ununuzi wa gari aina ya RV4 yenye chasis namba: ZCA 26-00 8051, yenye rangi Golden, Moden 2001, Engine namba ZZ/FE,CC:1794. Ununuzi huo umezidi kiwango ambacho kinastahiki kuitishwa utaratibu wa zabuni. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni ya 73.

Majibu ya Wizara/Idara:

Wanakiri kuwepo kwa ukiukwaji huo wa taratibu za manunuzi, ambapo ndio chanzo kikuu kilichochangia kuifunga hesabu namba 021103000519 ya Idara ya Ujenzi, baada ya kugundua kwamba, Idara hiyo ilifanya manunuzi hayo bila ya kuomba idhini au kupitia kwa Katibu Mkuu na bila ya kufuata taratibu wa zabuni kama sheria za manunuzi zinavyoelekeza. Katibu Mkuu alimuandikia Mkurugenzi wa Idara ya Ujenzi kutaka kupata ufafanuzi wa suala hilo na akachukua hatua za kuizuia gari hiyo kutumika mpaka pale atakapopata maelezo ya msingi kuhusiana na ukiukwaji wa taratibu hizo.

Uchunguzi wa Kamati:

Kwa kuzingatia maelezo ya kweli ya Wizara juu ya kukiukwa kwa sheria kwa Wizara hiyo chini ya Idara yake ya Ujenzi, Kamati hairidhiki tu kwa Katibu Mkuu kupata ufafanuzi kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara, alistahiki kwa kuzingatia sheria kuchukua hatua zaidi kama zilivyoelezwa na sheria hizo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria kwa watendaji waliohusika na ununuzi wagari kinyume na utaratibu.

3.2 WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI-PEMBA:

Hoja Nam. 58.6.1: Kukosekana kwa vielelezo vya ukodishaji wa matangi ya kuhifadhia mafuta yaliyoko Wesha-Chake Chake.

Ukaguzi umebaini Wizara kupitia Idara ya Nishati, Pemba, inamiliki matangi matano (5) ambayo yanakodishwa kwa kampuni ya GAPCO. Matangi haya yameanza kukodishwa tarehe 11/7/2005 kwa Tsh. 288,000,000 kwa mwaka. Utaratibu wa ukodishwaji wa matangi hayo haukufuatwa, aidha, kumbu kumbu zinazohusiana na ukodishwaji wa matangi hayo hazikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Wizara:

Depot ya Wesha ilijengwa mwaka 1985 na kuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Maji na Umeme. Mwaka 1993 hadi 1994 ilikodishwa kwa Kampuni ya Bulk Oil; 1994 hadi 2001 ilikodishwa kwa kampuni ya Zanzibar Petroleum; mwaka 2001 hadi 2003 ilikodishwa kwa kampuni ya Ecco Teck; 2003 hadi 2005 ilikodishwa kwa kampuni ya Zanzibar Petroleum na 11 Julai 2005 hadi hivi sasa yamekodishwa kwa kampuni ya GAPCO.

Aidha, Kampuni ya GAPCO imekodishwa matangi hayo na Wizara ya Fedha kwa Tsh. 2,000,000 kwa mwezi na kufanya jumla ya Tsh. 24,000,000 kwa mwaka. Vile vile kuanzia mwaka 2005 hadi 2012, kampuni ya GAPCO imeshalipa Tsh. 192,000,00 ikiwa ni malipo ya miaka minane.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imeupitia Mkataba ulioingiwa baina ya Wizara ya Fedha na GAPCO Zanzibar Litd, ulioingiwa tarehe 9/03/2005 na ni wa miaka 10 kwa thamani ya Tsh 24,000,000 kwa mwaka. Hata hivyo, Kamati imehoji hesabu mbili zinazotofautiana baina ya Mkaguzi na Wizara, na ilipouliza kwani taasisi hizi mbili zisikae mapema kufahamiana usahihi wa bei ya kodi, Wizara ilieleza kwamba, kwa wakati alipokuja Mdhibiti hawakua na kopi ya Mkataba kwa vile uko chini ya Wizara ya Fedha.

Kutokana na hali hiyo, Kamati imekubaliana na taarifa za Mkataba, ingawaje ilihitaji kupata mkataba wa asili (original) na sio kopi kama ilivyowasilishwa kwake. Hata hivyo, hadi tunaandika ripoti hii Kamati haikupatiwa Mkataba huo wa asili.

Mapendekezo ya Kamati:

Kwa kuzingatia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji mkataba ‘original’ na hivyo inahitaji muda wa ziada kufuatilia hoja hiyo.

3.3 MAMLAKA YA MAJI (ZAWA) – PEMBA

Hoja Nam. 74.2.1: Malipo yaliyokosa idhini ya mhusika Tsh. 57,583,555.

Ukaguzi umebaini kuwa kuna hati za malipo za matumizi mbali mbali yaliyofanywa bila ya kuwepo idhini (Saini) ya Afisa muidhinishaji, ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 87(1) cha kanuni za fedha za 2005.

Majibu ya Mamlaka:

Ni kweli kwamba wakati wa ukaguzi ilionekana malipo ambayo hayana saini ya Afisa muidhinishaji. Hata hivyo, hati hizo baadae zilisawazishwa na kuwasilishwa kwa Wakaguzi kwa uhakiki na uthibitisho wa uhalali wa matumizi hayo na kuridhiwa na Wakaguzi. Kasoro hii imetokea kwa kuwa Waidhinishaji wa hati hizi wanatumikia Zanzibar yote, hivyo kutokana na wingi wa hati hizo baadhi yake hazikupata saini hiyo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iliomba kuoneshwa hati hizo ili kujiridhisha, hata hivyo, haikukubaliana na maelezo yaliyotolewa. Hii ni kutokana na kuwa hakukuwa na alama yoyote inayoonesha kuwa hati hizo zimepitiwa na Wakaguzi hao.

Aidha, katika kuthibitisha hilo Kamati iliwaeleza Watendaji hao kuwa kwa kawaida kama Wakaguzi wameridhia hoja fulani, basi hoja hiyo huwa haiingizwi kwenye Ripoti ya Ukaguzi. Kwa msingi huo, Kamati ya PAC inahisi kuwa hoja hii ipo sahihi isipokuwa kwamba Watendaji wa Mamlaka ya Maji wameshindwa kuipatia majibu.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati haiwezi kupita vocha hiyo kwani kazi hiyo hufanywa na Mkaguzi. Kamati inaitaka Mamlaka ya Maji kuwa makini katika kufanya matumizi kwa kupata idhini halali ya Afisa Mhasibu.

Hoja Nam. 74.2.2: Vifaa ambavyo havikuingizwa katika Daftari la Ghalani Tsh. 8,820,000/-

Jumla ya Tsh. 8,820,000/- zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali lakini vifaa hivyo havukuingizwa kwenye daftari la vifaa ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake. Kutokuwepo kwa kumbu kumbu za vifaa ni kwenda kinyume na kanuni ya 198 ya kanuni za fedha ya 2005.

Majibu ya Mamlaka:

Hali hii ilionekana wakati wa ukaguzi, hata hivyo, baadae vielelezo husika viliwasilishwa kwa Wakaguzi kwa uhakiki pamoja na kuingizwa katika daftari la vifaa Namba 5 katika ukurasa wa 47 na daftari namba 1 katika ukurasa wa 73. Vifaa hivi vilitumika katika ujenzi wa uzio tangi la Ziwani – Wilaya ya Chake chake na Mota ilitumika kwenye chem. Chem. Ya Gawani – Wilaya ya Wete.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati hii ilibahatika kuviona baadhi ya vifaa ambavyo vimeorodheshwa katika madaftari hayo. Hata hivyo, imegundua kuwa kuna mapungufu ya uingizwaji wa vifaa katika madaftari hayo.

Aidha, Kamati ilizidi kusisitiza kuwa ingawa baadae Wakaguzi walipatiwa taarifa hizi lakini inadhihirisha wazi kuwa hawakuridhika na taarifa hizo kwa kuwa hoja hii imeingizwa kwenye Ripoti ya Ukaguzi. Hivyo, Kamati ya PAC inahisi kuwa pia hoja hii ipo sahihi, isipokuwa kwamba Watendaji wa Mamlaka ya Maji wameshindwa kuipatia majibu.

Aidha, katika kuthibitisha hilo Kamati iliwaeleza Watendaji hao kuwa kwa kawaida kama Wakaguzi wameridhia hoja fulani, basi hoja hiyo huwa haiingizwi kwenye Ripoti ya Ukaguzi. Kwa msingi huo, Kamati ya PAC inahisi kuwa hoja hii ipo sahihi isipokuwa kwamba Watendaji wa Mamlaka ya Maji wameshindwa kuipatia majibu.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati ya PAC imewataka Watendaji wa Mamlaka ya Maji (ZAWA) kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Hoja Namba 74.2.3 Kukosekana kwa Marejesho ya Masurufu (Imprest) Tsh. 1,100,000/-

Jumla ya Tsh. 1,100,000/- ikiwa ni masurufu, lakini marejesho ya matumizi hayo hayakupatikana kwa ukaguzi. Kutokuambatanisha marejesho ya masurufu ni kwenda kinyume na kifungu cha 102(1)(2) cha kanuni za fedha ya 2005.

Majibu wa Mamlaka:

Ni kweli kwamba vielelezo hivyo havikupatikana wakati wa ukaguzi, hata hivyo, Mamlaka ya Maji ililazimika kupata vielelezo hivyo na kuviwasilisha kwa Wakaguzi kwa uthibitisho na uhalali wa matumizi hayo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilizidi kusisitiza kuwa kwa kuwa taarifa hazikukamilika wakati wa ukaguzi ingawa baadae Wakaguzi walipatiwa taarifa hizi na bado hoja hii imeingizwa kwenye Ripoti ya Ukaguzi. Hivyo, Kamati ya PAC inahisi kuwa bado hoja hii ipo sahihi.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Mamlaka kuhakikisha inatekeleza ipasavyo sheria za fedha na kutoa mashirikiano mazuri kwa wakaguzi.

4.0 WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO – PEMBA

Hoja Nam. 59.5.1: Malimbikizo ya Madeni Tsh. 266,814,550/-

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya Tsh. 266,814,550/- zinadaiwa na wafanya biashara pamoja na taasisi mbali mbali kwa ajili ya utowaji huduma tofauti kwa Wizara ya Miundo Mbinu na Mawasiliano. Deni hilo ni la muda mrefu.

Majibu ya Wizara:

Wizara imekubaliana na hoja hiyo, hata hivyo, imeeleza kuwa deni hilo ni kwa ajili ya vipando vilivyoathirika katika ujenzi wa barabara hizo na sio deni la wafanyabiashara pamoja na taasisi mbali mbali kama ilivyodaiwa na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Aidha, wameeleza kuwa deni hilo litalipwa baada ya kumaliza kulipa deni la fidia za nyumba.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imesikitishwa na muda mrefu wa madeni hayo, huku ikiwa ni moja kati ya sababu inayokwamisha kuendelea kwa kazi za ujenzi wa barabara. Aidha, kitendo cha Serikali kutolipa kwa wakati kwa wakandarasi wa ujenzi, wakati mikataba inaelekeza kulipwa mapema, kunachangia sana wakandarasi hawa kupata kisingizio cha kutofanya kazi kwa wakati, na mara nyingi hupelekea hasara kwa Serikali. Vile vile Kamati imesikitishwa sana na tabia ya Serikali kuchelewa kuwalipa fidia wananchi, wakati wanakuwa tayari wameshakabidhiana na kuingia mikataba ya ujenzi na wakandarasi mbali mbali, hali inayopelekea kula hasara kila siku.

Mapendekezo ya Kamati:

- Kwa kuwa deni hili ni la muda mrefu, Kamati inaishauri Wizara kuchukua juhudi za makusudi za kuwalipa wananchi hawa, ili waendelee kuwa na imani na Serikali yao.
- Kwa kuwa Wakandarasi wanaidai pia Serikali fedha za faini kama ni adhabu kwa kwenda kinyume na matakwa ya mikataba (kwa mfano; kulipa fedha kwa wakati), Kamati inaishauri Serikali kutokuingia katika mikataba mipya hadi pale itakapomaliza madeni hayo. Aidha, baada ya kumaliza kulipa madeni hayo ingiie kwenye mikataba kutokana na uwezo wake wa fedha na sio vyenginevyo.
- Serikali iepuke kuwaridhia sana wajenzi wa barabara zetu ili tuwe na barabara zenye kiwango kinachotakiwa.
- Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inashauriwa kufanya ukaguzi kwa barabara mbali mbali zinazojengwa ili kuhakikisha kuwa thamani ya fedha (value for money) inafikiwa.

Mengineyo

- Kamati haikurishwa na upana wa barabara za Pemba, huku ikiwa na mashaka mengi juu ya ubora wa barabara nyingi za hapa Zanzibar. Aidha, pamoja na kukosa wakati, Kamati inahitaji kupata muda muafaka wa kufuatilia ujenzi wa barabara, lakini kwa ufanisi wa suala hili, Kamati inaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuanza kufanya ukaguzi maalum wa viwango vya barabara zetu.

5.0 WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

5.1 MAHKAMA KUU

5.1.1 OFISI YA MRAJIS WA JIMBO (MAHKAMA KUU) – PEMBA

Hoja Nam. 45.2.1: Kulipwa Mshahara Ndg. Khamis Hamad Abdalla Baada ya Kustaafu Tsh. 2,275,200/-

Ukaguzi umebaini kuwa Ndg. Khamis Hamad Abdalla ambaye alikuwa mfanyakazi wa Mrajis wa Jimbo Mahkama Kuu Pemba kama Kadhi wa Rufaa ambaye alikuwa analipwa Tsh. 1,137,600/- kwa mwezi alistaafu kazi mwezi wa Novemba, 2011 lakini mara baada ya kustaafu kwake mshahara wake ulihamishiwa katika hesabu (Account) iliyoko Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) yenye namba 041206009170 ambayo ni hesabu ya Ndg. Suleiman Omar Suleiman. Mshahara huo uliendelea kuingia katika hesabu hiyo kila mwezi kuanzia mwezi wa Novemba, 2011 hadi Disemba, 2011 kitendo kilichopelekea upotevu wa fedha za Serikali Tsh. 2,275,200/-. Hadi ukaguzi unafanyika fedha hizo bado hazijarejeshwa Serikalini.

Majibu wa Ofisi ya Mrajis:

Baada ya upotevu huu na kabla hoja hii haijaripotiwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Mrajis wa Jimbo – Pemba na Mahkama kiujumla imechukua hatua zifuatazo;-

- Kumsimamisha kazi mfanyakazi husika kwa barua ya tarehe 26 Januari, 2012 yenye kumbu kumbu namba MK/CH.P/MJP/21/VOL.VIII/33/12 kama kifungu cha 84(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma 2/2011 inavyoelekeza.
- Mhusika alirudishwa kazini kwa barua ya tarehe 25 Septemba, 2012 yenye kumbu kumbu namba MMK/408/2012 baada ya miezi sita (6) iliyowekwa kisheria katika kifungu kilichotajwa hapo juu kutokana na kutokukamilika kwa uchunguzi wa kadhia hii.
- Mnamo tarehe 19 Disemba, 2012 Ofisi ya Mrajis wa Jimbo – Pemba iliripoti kadhia hii katika Kituo cha Polisi Madungu, kwa hatua za kijinai na hatimae kulipeleka shauri hili Mahkamani. Baada ya uchunguzi wao wa kitaalamu Polisi waliijulisha Ofisi ya Mrajis wa Jimbo – Pemba kwa nakala ya barua ya tarehe 04 Februari, 2013 kuwa uchunguzi umekamilika na ni kweli kwamba mhusika kwa makusudi alitenda kosa la wizi wa Tsh. 2,275,200/- na kwa maoni yao mhusika afikishwe Mahkamani kujibu shutuma za wizi wa mali ya Serikali.
- Kwa mujibu wa kifungu cha 82(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Mhusika alishushwa cheo kutoka Afisa Utumishi Mahkama – Pemba na kuwa Karani wa Mahkama, pamoja na kutakiwa kulipa fedha taslim alizoiba barua ya tarehe 09 Septemba, 2013 yenye kumbu kumbu namba MMK/278/2013 inathibitisha hilo.
- Hadi tarehe 04 Oktoba, 2013, Ofisi ya Mrajis wa Jimbo – Pemba ilikuwa inasubiri shauri hili lifikishwe Mahkamani, kama Mkurugenzi wa Mashtaka atakavyoona inafaa.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilibaini kuwa jina halisi la aliyekuwa Kadhi wa Rufaa ni Sheikh Khamis Hamad Abdalla badala ya Sheikh Khamis Hamad Ali kama ilivyoripotiwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Baada ya majadiliano na Watendaji wa Ofisi ya Mrajis wa Jimbo – Pemba na Watendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria wakiongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Ndg. Mdungi Makame pamoja na kuyapitia majibu ya Mtuhumiwa (Ndg. Suleiman Omar Suleiman), Kamati hii haikuwa na pingamizi na shutuma hiyo.

Hata hivyo, Kamati inaiomba Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kushirikiana na vyombo vyengine vinavyohusika ikiwemo Serikali kufuatilia kwa kina suala hili ili kuwachukulia hatua wale wote waliohusika kwa namna moja au nyengine, hasa ikizingatiwa kuwa suala la utayarishaji wa mshahara lina mchakato kubwa (yaani linajumuisha zaidi ya mtu mmoja). Vile vile, suala la kuingizwa mshahara kwenye hesabu (Account) linahitaji pia mashirikiano na Wizara inayohusika na mambo ya Fedha.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kulichukulia hatua suala hili, kwani hivi sasa Mtuhumiwa ameshapelekwa Mahkamani kwa hatua zaidi.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuendelea kufanya ukaguzi katika eneo hili la mishahara kwani bado kuna udanganyifu mkubwa unaofanywa na baadhi ya watumishi wa Serikali wasio waaaminifu. Aidha, Kamati inawataka Watumishi wa Umma watekeleze majukumu yao kwa kufuata misingi na maadili ya kazi zao na waachane na mambo ya tamaa.

5.2 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA-PEMBA.

Hoja Nam. 44.2.1: Kiwango kidogo cha fedha za kodi za milango mbali mbali ya Wakfu.

Ukaguzi umebaini kwamba, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inakodisha milango ya biashara kwa wafanyabiashara mbali mbali lakini kiwango cha kodi kinachotozwa ni kidogo kulinganisha na hali halisi ya thamani ya milango hiyo katika maeneo hayo, hali inayopelekea Kamisheni kukosa mapato yanayostahiki.

Ufanyaji wa kazi wa hoja hii:

Kamati imeshindwa kuifanyia kazi hoja hii kwa kutokuhudhuria kwa Katibu Mkuu (Naibu Katibu Mkuu), ambae kwa mujibu wa kanuni ya Fedha ya mwaka 2005, kifungu cha 52(2) kinamtaka afike mbele ya Kamati na kujibu masuala atakayoulizwa. Aidha, ikielezwa mbele ya Kamati sababu iliyomfanya ashindwe kuhudhuria ni kuwa alikusudia ahudhurie lakini alipata agizo la shughuli muhimu za sherehe ya Mapinduzi, hivyo alilazimika abakie Zanzibar, huku akimtaka Afisa Mdhamini wa Wizara hii amuagie.

Aidha, sababu nyengine iliyoifanya Kamati ishindwe kuifanyia kazi hoja hii ni kutokamilika kwa majibu ya maandishi yaliyowasilishwa kwa Kamati. Majibu hayo yameandikwa na Ndg. Abdulla Kh. Juma, Afisa Msaidizi Mkuu wa Katibu Mtendaji-Pemba, ambae hakuyatia saini ili kuthibitisha kuwa ni majibu yake, lakini pia yametayarishwa tarehe 20/9/2013, wakati Kamati ilifika Afisini kwa ajili ya kazi tarehe 08/01/2014. Kamati ilielezwa kuwa Afisa huyo ameshafariki ndio maana hakuna saini yake na aliyatayarisha mapema kabla ya kufariki kwake.

Mapendekezo ya Kamati:

Kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji muda zaidi kufikia maamuzi ya hoja hii.

6.0 WIZARA YA AFYA - PEMBA

Hoja Nam. 56.1: Malipo yasiyokuwa na vielelezo Tsh. 3,090,000/-

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya Tsh. 3,090,000/- zimelipwa kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi. Kukosekana kwa vielelezo ni kwenda kinyume na kanuni ya 95(4) ya kanuni ya fedha. Kwa hali hiyo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa.

Majibu ya Wizara:

Watendaji wa Wizara hii Pemba waliwataka Watendaji wa Hospitali ya Chake Chake ambao ndio waliofanya ununuzi wa mashine ya X-ray yenye thamani ya Tsh. 2,000,000/- kupitia kwa Ndg. Masoud Hassan Juma kuwasilisha stakabadhi halisi ya malipo hayo na badala yake waliwasilisha kivuli cha stakabadhi hiyo. Hadi tarehe 30 Septemba, 2013 stakabadhi halisi haijawasilishwa Wizarani kwa kuwa Mtendaji huyo hivi sasa amechukua likizo bila ya malipo, hivyo Wizara imeshindwa kumpata.

Kwa upande wa Tsh. 1,090,000/- ambazo ni gharama za masomo kwa Ndg. Khatib Shaame Khatib aliyelipwa Tsh. 800,000/- na Ndg. Seif Nassor Seif aliyelipwa Tsh. 290,000/-, malipo haya yalifuata taratibu zote za malipo. Stakabadhi ya malipo ya Ndg. Khatib Shaame tayari imepatikana ingawa imechelewa na kwa upande wa stakabadhi ya malipo ya Ndg. Seif Nassor Seif bado haijapatikana.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati haikuridhika na majibu hayo, hivyo haikuipokea stakabadhi hiyo kama ni uthibitisho wa manunuzi hayo hasa ikizingatiwa kuwa kivuli cha nyaraka yoyote ni rahisi kughushiwa.

Ama kuhusu malipo yaliyofanyika kwa ajili ya gharama za masomo Kamati hii imebaini kuwa Wizara ya Afya – Pemba husomesha vijana hata wasiokuwa wafanyakazi wa Wizara hii ingawa karatasi ya malipo namba 483278 ya tarehe 27 Aprili, 2012 inaonesha kuwa wasomi hawa ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya.

Sanjari na hilo, Kamati ilishindwa kupata barua za maombi za Wahusika juu ya malipo hayo na badala yake ilifanikiwa kupata barua zilizoandikwa tarehe 17 Aprili, 2012 na Ndg. Othman b. Moh'd ambaye ni Afisa Mafunzo isipokuwa kwamba barua hizo zimeonesha kuwa zimeandikwa kwa niaba ya Afisa Mafunzo wa Wizara hii ingawa aliyesaini ni Ndg. Othman b. Moh'd (afisa mafunzo mwenyewe).

Kamati ya PAC ilitaka kufanya mahojiano na Ndg. Othman b. Moh'd ili kujiridhisha na kile ilichokibaini, hata hivyo, Ndg. Othman hakuweza kupatikana kwa kuwa alikuwa ni mgonjwa.

Aidha, kuhusiana na nakala ya stakabadhi ya malipo iliyowasilishwa kwa Kamati, yenye namba 16705 inaonesha malipo yaliyohusika yalikuwa ni Tsh. 1,500,000 wakati Ndg. Khatib Shaame Khatib aliyehusika na malipo hayo, amelipwa Tsh. 800,000 huku Kamati ikielezwa kuwa muombaji alikubaliana na Wizara kwamba, atalipwa fedha hizo, ingawaje hakukuwa na maandishi yoyote hata ya dokezo yaliyothibitisha kauli hiyo. Hali hii inaashiria kuwepo kwa udanganyifu mkubwa katika Wizara hii.

Maoni ya Kamati

Kamati inamtaka Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya kulifuatilia kwa kina suala hilo na kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji wote waliohusika na ubadhirifu huo.

RIPOTI YA UKAGUZI YAKINIFU KWA MIRADI YA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWKA WA FEDHA 2011/2012, PAMOJA NA RIPOTI YA UKODISHWAJI WA ARDHI KWA WAWEKEZAJI.

1.0 BARAZA LA MANISPAA:

Hoja Nam. 9.1: Soko la Mbogamboga - Mombasa.

Soko hilo lililojengwa kwa ajili ya kuwapatia wananchi mahitaji yao muhimu, limekuwa halitumiki kwa muda mrefu na limekuwa na matatizo yafuatayo:

- Mazingira yasiyoridhisha hali inayowafanya wafanya biashara wengi kushindwa kutumia eneo la ndani ya soko na kupelekea kujenga vibanda pembezoni mwa soko hilo bila ya ridhaa ya Baraza la Manispaa.
- Uchafuzi wa mazingira ikiwa ni pamoja na jaa la taka, vyoo visivyosafishwa kwa muda mrefu na kukosekana maji ya uhakika.
- Hali ya ukusanyaji wa mapato usioridhisha ukilinganisha na matarajio na shughuli zilizopangwa kufanyika katika soko. Uchache wa ukusanyaji wa mapato unasababishwa zaidi na kuwepo kwa idadi ndogo ya wafanya biashara, hali inayopelekea baadhi yao kutumia eneo zaidi ya moja bila ya malipo ya ziada.
- Suala la uungaji wa umeme kinyume na taratibu, kutokana na sababu za kushindwa kujiendesha na hivyo kupelekea baadhi ya wafanyabiashara kuunga umeme kibinafsi na kwa kuathiri mandhari ya soko na eneo hilo.

Majibu ya Baraza:

Baraza linakiri udhaifu mbali mbali uliojitokeza katika soko la Mombasa, ingawaje sasa tayari uongozi wa Baraza umesharekebisha kasoro hizo.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imehoji sababu zilizopelekea kuwepo kwa udhaifu huo na kuelezwa umetokana na uongozi mbaya wa Baraza la Manispaa kwa wakati huo. Kamati ilielezwa kuwa matatizo hayo yamerekebishwa na suala la umeme kwa mfano, sasa unalipiwa kila mwezi, huku mazingira yakiwa safi na soko hilo linatumika kama kawaida.

Aidha, wakati Kamati ilipofanya matembezi ya eneo hilo haikuridhishwa na ujenzi wa vibanda kujengwa nje ya utaratibu. Aidha, wapangaji wa biashara eneo la nje ni tatizo na hawalipii kodi, wakati wafanya biashara wa ndani ndio wanaolipia kodi, huku wananchi wengi humalizia mahitaji yao nje ya soko.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati imeutaka uongozi wa Baraza kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wa nje katika soko hilo wanaingizwa ndani, ili kudumisha usafi na kuwafanya wafanyabiashara hao walipie kodi kama inavyotakiwa.

Aidha, Kamati inautaka uongozi wa sasa wa Baraza kuhakikisha makosa hayo hayatokezei tena na wazirekebishe kasoro zote zilizojitokeza ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kuwasilishwa ripoti hii mbele ya Baraza.

2.0 CHUO CHA MAFUNZO:

Hoja Nam. 11.4: Mradi wa Ujenzi wa Gereza jipya Hanyegwa Mchana, Tsh. 399,638,000.

Fedha hizo zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa gereza jipya Hanyegwa Mchana kwa mwaka 2011/2012. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa mwenendo wa ujenzi huo hauridhishi kwa sababu muda uliotakiwa uanze tayari umeshapita na hakuna hatua yoyote ya ujenzi iliyoanza zaidi ya usafishaji wa eneo, uchoraji ramani na ufyatuaji wa matofali.

Aidha, wakaguzi hawakupatiwa sababu za kuridhisha kutokana na kuchelewa kuanza ujenzi huo na inaashiria kwamba, shughuli zilizopangwa katika ujenzi wa gereza hilo hazitotekelezeka ipasavyo kutokana na kuwepo uwezekano wa kupanda kwa gharama za ujenzi na kupelekea kuathiri bajeti ya miaka inayofuata.

Majibu ya Chuo:

Ni kweli kuwa Chuo cha Mafunzo kimeanzisha mradi wa gereza jipya, eneo la Hanyegwa Mchana lakini tayari ujenzi huo umeshaanza, isipokuwa kwamba ujenzi huo hivi sasa umesita kutokana na uhaba wa fedha.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imekagua eneo husika na kwa bahati kabla ya kufanya ziara ya eneo hilo, Kamati ilipatiwa maelezo juu ya ujenzi wenyewe. Tatizo kubwa ambalo Kamati imeliona ni uhalisia wa jengo lenyewe kuwa kubwa na gharama kubwa, wakati uwezo wa serikali yetu ni mdogo sana.

Aidha, ujenzi huo una sua sua na kama Serikali haitalishughulikia suala hili kwa udhati, basi ujenzi huo hautamalizika ama utachukua muda mrefu sana hadi kukamilika kwake.

Mapendekezo ya Kamati:

- Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutafuta wafadhali au Mifuko ya Kijamii kwa lengo la kujenga jengo hilo badala ya kuwaachia Chuo cha Mafunzo peke yao kwani gharama za ujenzi huo ni kubwa na Chuo cha Mafunzo hakina uwezo wa kugharamia.

- Kwa kuwa michoro ya jengo hilo yamekopia zaidi magereza ya Ulaya, nchi zilizoendelea, Kamati inaitaka Serikali kuangalia uwezekano wa ujenzi wa jengo hilo kuwa na mazingira yetu na na uwezo wetu, na isibaki kuwa nadharia isiyoweza kutekelezwa.

- Kamati inautaka uongozi wa Chuo cha Mafunzo kutumia fedha za ujenzi wa gereza hilo kwa kuzingatia sheria kwani kinyume na kufanya hivyo, malengo yaliyokusudiwa hayatafikiwa.

3.0 WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI-PEMBA.

Hoja Nam. 2: Ukarabati wa nyumba za Maendeleo-Wete.

Tsh. 110,080,000 zilitengwa na kuingizwa kwa ajili ya ukarabati wa jumba namba 4 lilioko Wete Mtemani,Pemba. Ukaguzi umebaini kwamba, fedha hizo zilizoingizwa, hazikutumika kwa ukarabati wa jumba hilo, na badala yake fedha hizo zilitumika kwa shughuli nyenginezo zikiwemo safari za kikazi, ununuzi wa mafuta, stationary, matengenezo ya magari pamoja na gharama za mafunzo.

Hadi ukaguzi unakamilika, ujenzi huo haujaendelea na hali ya jengo hairidhishi kutokana na uchakavu, ubovu wa makaro na kuzagaa kwa uchafu hali ambayo inanyima haiba ya majengo hayo.

Aidha, hakukuwa na maelezo yanayoridhisha juu ya kutotumika fedha hizo kwa lengo lililopangwa na hasa kwa kuzingatia ukarabati huo ulitakiwa ufanyike kwa haraka. Kufeli kwa utekelezaji wa ujenzi wa jengo hilo ambalo linatishia maisha ya wananchi na mali zao, hali hii inapelekea kuathiri mipango ya Serikali zaidi ya wananchi wake.

Majibu ya Wizara:

Fedha hizo Tsh. 110,080,000/- zilitengwa kwa ajili ya shughuli zote za Idara ya Nyumba Pemba ikiwa ni pamoja na matengenezo ya nyumba zote za Serikali (Nyumba za maendeleo, za vijiji na za kutaifishwa) kwa Pemba nzima. Aidha, fedha zilizopatikana ni Tsh. 62,881,644 na zimetumika kwa ukarabati wa nyumba za maendeleo Block No.5 iliyoko Mtemani Wete, nyumba Namba T. 17B iliyoko Kilimatinde Chake, matengenezo ya makaro na mitandao ya maji machafu katika nyumba za maendeleo Micheweni, Machomanne Chake na Mkoani na matengenezo ya nyumba Namba T.67 iliyopo Tibirinzi Chake Chake.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilipofanya ziara katika eneo hilo la Mtemani, imeshuhudia hali mbaya ya uchakavu wa majengo hayo, huku uchafu ukikithiri na kuhatarisha maisha ya wananchi wanaoishi katika

majumba hayo ya maendeleo na waliokaribu. Tatizo pia ‘system’ ya kupeleka uchafu pwani imeharibika na ni gharama kubwa kuitengeneza.

Kamati ilielezwa kwamba, ugumu wa kupata magari ya kunyonyea uchafu na sehemu zilizotarajiwa kupita maji machafu na kumwagia baharini imejengwa sana na wananchi, ndio sababu iliyoepelekea uchafu wa kukithiri eneo hilo. Aidha, mashirikiano ya wananchi katika maeno hayo pia ni madogo ukilinganisha na haja inavyotakiwa.

Kamati pia ilihitaji kupata ufafanuzi wa matumizi halisi ya fedha hizo kama ilivyoripotiwa na Mdhibiti na kwa kuzingatia muda, ilihitaji kufahamu baadhi ya matumizi ya fedha zilizopatikana kama kweli zote zimetumika kama walivyoeleza Wizara na sio kama alivyoeleza Mkaguzi. Hivyo, Kamati ilielezwa kuwa, kati ya fedha hizo zipo zilizotumika kwa kulipia gharama za maji ZAWA. Aidha, Tsh. 35,000/- zilitumika kuwalipa posho maofisa wa Wizara kutoka Micheweni kuja Chake Chake. Maofisa hao wawili walikuwa wanakwenda Chake Chake mara moja kwa wiki. Hata hivyo, Kamati imeshuhudia kutofautiana kwa majibu hayo, kwa maana Mhasibu wa Wizara hii alieleza Kamati kwamba, fedha hizo zimetumika kwa matengenezo ya uzibuaji wa maji machafu. Hata hivyo, Kamati kutokana na tofauti hizo, ilitaka kupitia hati za malipo za fedha hizo na ikathibitisha kwamba fedha hizo zimetumika kwa malipo ya safari ya kikazi kwa Ndg. Hamad H. Juma ambae ni Karani wa Mapato na Nyumba Micheweni, kibaya zaidi hakuna vielelezo vya risiti za marejesho ya nauli hizo.

Aidha, Kamati imethibitisha kwamba, Tsh. 6,454,344/- zimetumika kulipwa posho; Tsh. 7,716,800 zimetumika kwa ununuzi wa mafuta; Tsh. 5,872,500 zimetumika kwa safari; Tsh. 3,580,000 zimetumika kwa ununuzi wa stationary; Tsh. 4,767,000 zimetumika kwa gharama za mafunzo; Tsh. 12,746,000/- zimetumika Chake; Tsh. 35,000 zimetumika kwa safari kutoka Micheweni na Tsh. 970,000/- zimetumika kwa malipo ya maji ZAWA.

Aidha, Kamati imejiridhisha kwamba, Tsh. 1,696,000/- zimetumika kwa kugharamia matengenezo ya nyumba ya Wizara ambayo imepangishwa kutokana na mpangaji huyo kuwaomba kufanyiwa matengenezo katika Boma lake, sehemu ya uwani kuanguka. Hivyo, Wizara imetumia fedha hizo kumjengea mpangaji huyo.

Kamati imehoji iwapo mpangaji huyo aliomba kufanyiwa ujenzi huo kwa barua yoyote na Wizara bila ya kusita sita ilieleza kwamba, wao hawana barua hiyo kwani mpangaji huyo alifika Wizarani akalalamika na wao walipojiridisha ndipo walipoamua kumjengea. Aidha, Kamati imehitaji kupatiwa namna Wizara ilivyofanya ukaguzi wa boma hilo kabla ya kutengenezwa na taarifa ya ukaguzi wa Wizara kabla ya kufanya ujenzi au angalau baada ya ujenzi huo. Hata hivyo, Wizara pia imejibu kuwa hakuna taarifa yoyote zaidi ya kuangalia vocha za malipo ya gharama za ujenzi husika, huku Kamati ikihakikishiwa kuwa kama hilo ni kosa, basi pia hufanyika kwa majengo ya Wizara yaliyopo Wete, Chake Chake na sehemu nyengine.

Mapendekezo ya Kamati:

- Kamati inaitaka Serikali kutilia nguvu matengenezo ya nyumba hizo za maendeleo kwani hali yake ni mbaya sana.

- Kamati inaitaka Wizara kuzitumia vizuri, kwa malengo yaliyokusudiwa na kwa kufuata sheria zinazohusika, fedha zote zinazohusika na ukarabati wa majengo hayo, ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

- Serikali iharakishe kuunda Shirika la nyumba ambalo litakuwa na uwezo mzuri zaidi katika kukusanya kodi na kuzifanyia matengenezo nyumba zitakazokuwa chini ya Shirika hilo.

4.0 WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

Hoja Nam. 11.1: Mradi wa Ofisi ya Uvuvi, Pemba.

Mradi wa ujenzi wa Afisi ya Uvuvi Pemba, umefadhiliwa na MACEMP na kuanza tarehe 25/01/2010 huku Serikali ikitiliana Mkataba na DB SHAPRIYA Co.Ltd ya Dar es Salaam, mkataba namba DFMRZ/MACEMP/CW/DPT.1/09 kwa thamani ya USD 1,614,504.64.

Jumla ya USD 732,100.8 zimetumika katika mwaka huu wa fedha, huku ukaguzi haukuridhishwa na hali halisi ya ubora wa ujenzi ukilinganisha na fedha zilizotumika. Aidha, mapungufu yaliyobainika ni Mkataba wa mradi kutoonesha tarehe ya uanzaji wala umalizikaji wa mradi huo; kufanyika kwa nyufa katika madirisha ya vigae, chumba namba 21; kupasuka kwa baadhi ya kuta za jengo hilo; kutokamilika kwa baadhi ya kazi kama vile ujenzi wa tangi la maji na kuharibika kwa baadhi ya sehemu za jengo kama vile sehemu ya dari, chumba cha mkutano na sehemu ya mapokezi.

Majibu ya Wizara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi ulipofanyika, Mkandarasi alikuwa yumo katika kipindi cha kurekebisha kasoro mbali mbali zilizojitokeza (defect liability period). Kwa muda huu marekebisho yote hayo yameshafanyika na kukamilika.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati kwa kuzingatia uhaba wa muda, ililazimika zaidi kuangalia marekebisho yaliyojitokeza ambayo Wizara iliahidi kuyasawazishwa. Aidha, Kamati imetembelea eneo la ofisi hiyo na kujiridhisha kwamba, marekebisho kweli yalifanyika.

Hata hivyo, Kamati ilihitaji kuthibitishiwa iwapo marekebisho hayo yalifanywa na Mkandarasi pamoja na kuangalia mkataba wa ujenzi na BOQ ili kujiridhisha zaidi. Uthibitisho huo ulielezwa upo makao makuu, Unguja, ingawaje Kamati kutokana na ufinyu wa muda, haikupata nafasi ya kuangalia kwa makini vitu hivyo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inahitaji kupata muda wa ziada wa kujiridhisha juu ya suala hili ili iweze kutoa mapendekezo yanayofaa.

Hoja Nam. 11.3: Mradi wa Ujenzi wa sehemu ya kuuzia samaki, Tumbe Pemba, Tsh. 263,824,666.87

Mradi wa ujenzi wa sehemu ya kuuzia samaki Tumbe, Pemba uliofadhiliwa na MACEMP kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Zanzibar, umeanza 27/01/2011 ambapo Serikali imetiliana mkataba na Ngogo Engineering Ltd, P.O.Box 552 Tanzania, mkataba namba DFMRZ/MACEMP/CW/F.L.SITE/1/2011 thamani ya mradi hadi kukamilika kwake ni Tsh. 1,074,808,177 (bila ya VAT).

Ukaguzi umebaini Tsh. 263,824,666.87 zililipwa kwa Mkandarasi kupitia Transfer Order GEF Local Account. Aidha, Mshauri Mwelekezi MEKON ARCH CONSULTANT LTD, P.O Box 31924 Mlimani City Dar es Salaam amelipwa Tsh. 13,621,220 kupitia hati namba 1/6 ya 15/6/2012 ikiwa ni malipo ya ushauri elekezi na usimamizi. Aidha, jumla Tsh. 18,815,836.58 zimelipwa kama ni malipo ya VAT kupitia hati namba 1/5 ambapo ni kwenda kinyume na Miradi ya Washirika wa Maendeleo. Ukaguzi haukuridhishwa na ujenzi huo ukilinganisha na fedha zilizotolewa na kutumika. Hadi ukaguzi unamalizika, ujenzi huo ulikuwa haujakamilika.

Majibu ya Wizara:

Ni kweli maelezo ya Mdhibiti kuhusiana na Mkataba wa ujenzi na ujenzi ulisita kwa muda mrefu sasa, ingawaje kosa hasa lipo kwa Mjenzi. Wizara imetumia utaratibu unaofaa katika kumpata Mshauri Mwelekezi na hata Mjenzi wa soko hilo. Aidha, kuchelewa kwa ujenzi wa soko hilo na kutumika kwake kunatokana na sababu nyingi ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa eneo la kujengea soko hilo kwa muda mrefu, hali iliyomchelewesha Mjenzi. Aidha, Mradi huo hapo mwanzo haukuwa soko bali ni ujenzi wa Diko, hivyo kubadilisha na kuwa soko umekumbana na mazingira mengi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kitu cha mwanzo ilichofanya Kamati ni kutembelea eneo la soko na kushuhudia kuwa ujenzi wa soko hilo hauridhishi, limejengwa chini ya kiwango. Aidha, soko hilo lilitarajiwa kukabidhiwa na kutumika mnamo Agosti - Septemba 2011, lakini mpaka Kamati inafika katika eneo la soko, bado halijakamilika na bado halijakabidhiwa kwa wananchi.

Vile vile miongoni mwa mambo yaliyoishangaza Kamati ni kununuliwa kwa majokofu mapema kabla ya soko hilo kukamilika. Huku majokofu hayo yakinunuliwa 2012 wakati ujenzi haujakamilika na hivyo ni kusema hayafanyi kazi iliyokusudiwa wala hayapo katika eneo la soko kama ilivyotazamiwa.

Hali hii ya ujenzi isiyoridhisha, iliilazimu Kamati kuhoji juu ya taratibu zilizotumika kumpata Mshauri Mwelekezi na hata Mjenzi wa soko hilo na kugundua kuwa, taratibu hizo zimefuatwa

ipasavyo kwa mnasaba wa majadiliano na hata taarifa zilizomo katika nyaraka, ila ukweli ni kwamba taratibu zilizotumika kumpata mjenzi hazikufuatwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na kutozitembelea na kuzikagua kazi zake mapema jambo ambalo kabla ya Wizara kuamua kuingia nae mkataba walitakiwa kwa mujibu wa sheria wajiridhishe uwezo wake kupitia kazi zake mbali mbali alizozifanya, aidha ni lazima wajiridhishe uwezo wake kupitia kazi mbali mbali alizozifanya.

Aidha, Kamati ya Tathmini ambayo ndio chanzo kikuu cha kuteuliwa kwa Mjenzi ama Mshauri Mwelekezi, haikuandaa kanuni za maadili na kuzisaini ili kuthibitisha kwamba wajumbe wa Kamati hiyo hawana maslahi binafsi na Mjenzi ama Mshauri Mwelekezi. Kufanya hivyo ni kukiuka maelekezo ya kifungu cha 48(6) cha sheria ya manunuzi, jambo ambalo linaweza kuleta tafsiri nyingi ikiwa ni pamoja na wajumbe wa Kamati hiyo ya Tathmini kutokuwa waadilifu walipokuwa wanatekeleza kazi zao na usahihi huo unapatikana kwa kasoro zilizojitokeza za ujenzi wa soko hilo.

Aidha, pamoja na Mshauri Mwelekezi kushiriki katika kupatikana kwa Mjenzi, tatizo jengine ni kukosekana kwa tathmini ya kimazingira kabla ya ujenzi huo kuanza. Kama hiyo haitoshi, Mshauri huyu mwelekezi aliefika mbele ya kikao cha Kamati aliithibitishia Kamati kwamba, Mjenzi aliepewa kazi hiyo hakuwa na hana uwezo wa kifedha, jambo linalomkwamisha kukamilisha kazi alizopewa, yeye anategemea alipwe na Wizara ndio aweze kufanya kazi jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Kamati pia imesikitishwa na hali ya Mjenzi huyo kwa Wizara kutolishughulikia suala hilo mapema kwani waliandikiwa ripoti ya Mshauri Mwelekezi kuelezea ujenzi unavyoendelea na uwezo mdogo wa Mjenzi. Aidha, Kamati imeelezwa pamoja na kasoro zote hizo, Mjenzi huyo ameshalipwa fedha za kazi yake, ingawaje Wizara imesema kuna fedha za dhamana Tsh. 50,000,000/- ndio Wizara itazitumia kurekebisha kasoro za umaliziaji wa jengo zinazohitajika.

Mbali na kasoro hizo, kuna madeni makubwa kwa wananchi mbali mbali walioshiriki katika ujenzi huo na hata walinzi ambao hawana matumaini ya kulipwa fedha zao na Mjenzi wa soko hilo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inasikitishwa na usimamizi mbaya na uteuzi wa Wajenzi wa miradi mbali mbali ya Serikali. Kitendo cha soko hilo kutokamilika hadi leo, kinaisikitisha Kamati na inaitaka Serikali kuwachukuliwa hatua za kinidhamu waliohusika na usimamizi wa ujenzi wa soko hilo. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha wananchi wanalipwa fedha zao na kuhakikisha soko hilo linakamilika na kukabidhiwa kwa wananchi haraka iwezekanavyo sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kuwasilishwa kwa ripoti hii mbele ya Baraza.

5.0 IDARA YA ARDHI NA USAJILI, KITENGO CHA UKODISHAJI ARDHI KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012.

Hoja Namba 13.1: malipo ya kodi ya ardhi yaliyolipwa pungufu, USD 98,209.50 sawa na Tsh. 152,224,725 kwa miaka mitatu.

Ukaguzi umebaini kwamba, kwa mujibu wa mikataba iliyotiwa saini baina ya miradi mbali mbali na Serikali inaonesha kwamba, kuna upungufu mkubwa wa malipo ya kodi ya ardhi iliyolipwa na wawekezaji ambayo ni kinyume na malipo yaliyoainishwa kwenye mkataba husika. Kufanya hivyo ni kuipunguzia Serikali mapato yake na ni kwenda kinyume na mikataba husika.

Aidha, hakuna maelezo wala vielelezo vinavyohusiana na upungufu huo uliojitokeza katika malipo hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 47(5) cha sheria namba 12 ya mwaka 1992.

Aidha, miradi iliyolipa kodi pungufu ni Zanzibar Crown Hotel and Resort, iliyopo Mazizini Unguja, iliyosajiliwa kwa namba DP/ 790/2006, Kodi ya mwaka kwa mujibu wa Mkataba ni USD 9,000, kwa miaka mitatu amelipa kodi ya USD 5000 kwa kila mwaka, hivyo pungufu kwa USD 12,000 kwa miaka mitatu.

Mradi mwengine ni Bell Rosa Zanzibar Limited, uliosajiliwa kwa namba DP/965/2009, kodi kwa mujibu wa mkataba ni USD 25,800 kwa mwaka, lakini analipa USD 10,000 na hivyo kwa mwaka mmoja, Serikali imekosa USD 10,000. Aidha, Mradi mwengine ni Hotel and Property Development uliosajiliwa kwa namba DP/809/2007, kwa mujibu wa mkataba mmiliki anatakiwa kulipa USD 80,000 kwa mwaka, lakini analipa USD 48,190.50 kwa mwaka, na hivyo Serikali imekosa USD 31,809.50 kwa mwaka mmoja.

Ngalawa Beach Village ni mradi mwengine unaohusika, uliotakiwa kulipia USD 12,500 kwa mwaka lakini mmiliki wake analipa USD 6,300 na hivyo, kuna upungufu wa USD 6,200 kwa mwaka.

Aidha, Fishing Zanzibar Company Limited yenye usajili wa DP/ 909/2008 unaotakiwa kulipa USD 2,060, kwa mwaka hulipiwa USD 1,860 na hivyo kuna bakaa ya USD 200 kwa mwaka. Na mradi wa mwisho ulioorodheshwa katika hoja hii ni Residence Hotel (Mchanga Mle-Kizimkazi) inayopaswa kulipa kwa mwaka USD 80,000, lakini hulipia USD 42,000 na hivyo kuwa na deni la USD 38,000 kwa mwaka.

Majibu ya Wizara/ Idara:

Zanzibar Crown Hotel and Resort:

Katika hoja hii kuna kasoro ya kimahesabu. Deni halisi ni USD 4,000 na sio USD 12,000. Uthibitisho uko tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kufuatia maelezo ya Wizara, Kamati ilihitaji kupata Mkataba wa ukodishwaji kwa Kampuni hii na kupatiwa, na Kamati ikajiridhisha kwamba, kodi inayotakiwa kulipwa kwa mwaka ni USD 9,000 kama ilivyoelezwa na Mdhibiti. Ni kweli kwamba mwekezaji huyu aliomba kupewa punguzo la kulipia kodi hiyo, ili iwe USD 5000 kwa mwaka badala ya 9,000 lakini maombi hayo ni kwa mwaka 2011, na hivyo Kamati ilifanya rejea ya mkataba husika, ilikubaliana na watendaji wa Idara kwamba muekezaji huyu kulipa kuanzia Novemba 2009, kwani mkataba wake ni wa tarehe 11/4/2007, huku akiwa na 'grace period' ya miezi 30, sawa na miaka miwili na nusu.

Hata hivyo, Kamati imethibitishiwa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) kwamba, Mwekezaji huyo hajapunguziwa kodi hiyo na anatakiwa alipe USD 9,000 kama Mkataba wake unavyoelekeza. Kwa msingi huo mwekezaji huyu alitakiwa na ZRB kulipa deni la USD 4,000 kwa kuwa awali alikuwa analipa USD 5,000. Mwekezaji huyu alilipa kama alivyotakiwa na Kamati imethibitishiwa na ZRB kwamba, fedha hizo ameshalipa na hivi sasa hana deni.

Mapendekezo ya Kamati:

Kwa kutumia kanuni ya 52(5)(c) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

Bell Rossa Zanzibar Limited:

Mwekezaji huyu alilipa tarehe 7/11/2011 jumla ya USD 25,800 kwa risiti namba 044881 na sio USD 15,800 kama ilivyoelezwa. Vielelezo hivyo vipo tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imejiridhisha kwamba, mwekezaji huyu amelipa USD 25,800 kama mkataba wa ukodishwaji unavyojieleza. Mkataba ulianza tarehe 6/3/2009 lakini una kipindi cha 'grace period' ya miaka miwili na nusu. Hivyo, alitakiwa kulipa Oktoba 2011 na imeelezwa kwamba amelipa hizo USD 25,800 na vielelezo vya malipo vimethibitishwa na Kamati.

Isipokuwa kwamba, muekezaji huyu aliomba grace period ambayo inaishia Disemba 2013 na kutakiwa kuanza kulipa kodi mwezi huu wa Januari 2014, lakini Kamati imethibitishiwa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) kwamba, muekezaji huyu ameomba kupewa 'grace period' kwa kipindi cha miaka mitatu mengine kwa barua aliyoituma kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na nakala ya barua hiyo (pamoja na watendaji wakuu wengine) imenakiliwa kwa Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar na kupokelewa tarehe 29 Novemba, 2013, ingawaje hakuna uthibitisho wa kukubaliwa kwa ombi hilo kwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ambae ndie mwenye mamlaka ya maombi hayo.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati imeridhika na majibu ya ZRB, ingawaje imesikitishwa na maombi ya kila siku ya kuongezewa muda wa ujenzi (grace period) ambayo yanasikilizwa na kukubaliwa na Waziri.

Aidha, pamoja na kwamba Mhe. Waziri wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ndie mwenye mamlaka ya kukubali maombi ya 'grace period' kwa mnasaba wa sheria ya Ardhi, Namba 12 ya mwaka 1992, Kamati ina wasi wasi mkubwa na matumizi ya mamlaka hayo na athari zake hupunguza mapato kwa Serikali na huwapa kiburi na jeuri baadhi ya wawekezaji ambao wana uhusiano wa karibu na Waziri huyo.

Hotel and Property Development:

Tofauti hiyo ya malipo ilitokana na punguzo la kodi ya ardhi alilopewa na Mhe. Waziri kisheria. Kielelezo hicho cha punguzo hilo kipo tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Mkataba wa ukodishwaji umeanza tarehe 15/2/2007 na mmiliki wa kampuni hiyo baada ya kupita miezi 30 ya 'grace period' alitakiwa aanze kulipa kodi hiyo Septemba 2009. Kamati ilielezwa kwamba, mwekezaji huyu baada ya kumalizika kwa 'grace period' ya miezi 30, alipewa tena 'grace period' na Mhe. Waziri wa Ardhi.

Kamati ilitaka kujiridhisha iwapo kampuni hiyo iliomba 'grace period' hiyo lakini kwa bahati mbaya hakuna ushahidi wa maombi hayo uliowasilishwa kwa Kamati kwa mwaka 2009 mara tu walipotakiwa kulipa kodi, na ushahidi wa maombi uliowasilishwa ni wa tarehe 22/09/2011 na kujibiwa tarehe 30/09/2011 na walichoomba ni kuongezwa muda wa 'grace period' ya mwaka mmoja na kuomba kulipa USD 1,000 kwa kila hekta badala ya kulipia USD 2,500 kwa hekta kama Mkataba wa awali unavyoelekeza.

Aidha, maombi yao yalizingatiwa kwa kupewa miezi 6 tu ya 'grace period' badala ya mwaka mmoja walioomba na kutakiwa kulipa USD 1,500 kwa hekta na sio USD 1000 kama walivyoomba. Mhe. Waziri ametumia kifungu cha 47(5) cha Sheria Namba 12 ya mwaka 1992, kifungu kinachotoa maelekezo kama yafuatayo:

> "Waziri kwa kuzingatia ushahidi wa wazi na unaomshawishi, anaweza kutoa punguzo la kodi iwapo (kutoa punguzo hilo) lina maslahi ya umma".

Pamoja na ufafanuzi huo, Kamati inasisitiza kwamba, mwekezaji huyo alitakiwa kulipa tokea 2009 na kwa kuwa hajalipa kwa miaka miwili, basi deni lake ni USD 160,000. Aidha, kwa mwaka 2011 baada ya kupunguziwa na kuomba 'grace period' na kupewa ya miezi 6, anatakiwa kulipa kuanzia Aprili, 2012, lakini kwa bahati njema Kamati kwa mwaka 2012 ilithibitishiwa kwamba, mwekezaji huyo alilipa USD 48,190.5 ambazo ni sawa na anazotakiwa kulipa baada ya punguzo.

Hata hivyo, Kamati ilipofuatilia suala hili ZRB, ilielezwa kwamba, kwa mujibu wa kumbu kumbu zao, mwekezaji huyu ameshalipa deni lote kwa mnasaba wa alivyopungumziwa na hivyo kwao wao hana deni lolote.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inasikitishwa na kitendo cha Viongozi wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuyatumia vibaya majukumu yao kwa kuwasaidia zaidi wawekezaji badala ya kuisaidia nchi na wananchi.

Ngalawa Beach Villge:

Deni kwa mwaka ni USD 12,600 na sio USD 12,500. Mwekezaji huyu alilipa kwa awamu mbili. Tarehe 30/04/2012 risiti namba 16785 USD 6,300 na tarehe 27/11/2012 risiti namba 387870 USD 6,300 na kufanya jumla ya malipo kwa mwaka 2012 kuwa USD 12,600. Vielelezo hivyo vipo tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Mkataba wa Ngalawa Beach Village ni wa tarehe 27/8/2007 na mmiliki wake alitakiwa alipe kodi kuanzia February 2010 na kwa mujibu wa mkataba kodi yake ni USD 12,600. Pamoja na watendaji wa Wizara/ Idara kusema kwamba mwekezaji huyu amelipa, Kamati imeshindwa kupatiwa ushahidi wa malipo hayo, na ushaidi uliotolewa ni wa malipo ya tarehe 30/4/2012 na 27/11/2012, miaka ambayo haihusiki na ripoti inayofanyiwa kazi na Kamati.

Kamati imethibitishiwa na watendaji wa ZRB kwamba, muwekezaji huyu ameshalipa kodi kama inavyotakiwa. Eneo hili hapo awali lilikuwa chini ya muwekezaji mwengine. Hivyo, muwekezaji huyu hivi sasa hana deni.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe. Aidha, kuhusiana na mwekezaji wa nyuma (kabla ya Ngalawa Beach Village) ambaye Kamati imeelezwa ndie aliekuwa na deni, Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ndani ya miezi mitatu baada ya kuwasilishwa kwa ripoti hii iwe imeshafuatilia suala hili kwa kumtambua mwekezaji huyo na taarifa ya deni alilokuwa nalo na hatimae wawasiliane na Bodi ya Mapato ya Zanzibar, kwa hatua za kufuatiliwa kulipa deni linalomkabili na akishindwa kulipa, Kamati inapendekeza hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Fishing Zanzibar Company Limited:

Mwekezaji huyu amelipa USD 2,060 kwa risiti namba 15287 ya tarehe 12/04/2012 na sio USD 1,860 kama ilivyoelezwa katika ripoti ya ukaguzi. Vielelezo vya malipo vipo tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kwa Kampuni hii ni wa tarehe 22/4/2008 na mwekezaji alitakiwa alipe kuanzia November 2010. Kamati imeelezwa kwamba fedha hizo zimelipwa na imejiridhisha baada ya kuangalia hati za malipo.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inashauri hoja ya deni la kodi ya ardhi kwa kampuni hii kwa mwaka 2011/2012 ifutwe.

Residence Hotel (Mchangamle-Kizimkazi):

Residence Hotel Mchangamle Kizimkazi ni 'trading name' ya 'Hotel and Property Development Ltd' iliyotajwa hapo juu yenye namba DP namba 809/2007 ambayo maelezo yake yapo kwenye Hotel and Propert Development. Uthibitisho huo upo tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imejiridhisha na kukubaliana na maelezo ya Wizara kwamba, hoteli hii ni sawa na Hotel and Property Development na hivyo maelezo yaliyotolewa kwa hoteli hiyo ni sawa sawa na hoteli hii.

Hoja Namba 13.2: malipo ya kodi ya ardhi baada ya kufanya utanuzi (extension) wa eneo la ardhi lenye urefu wa hekta '0.705' ambapo hekta moja ni sawa na USD 15,000.

Ukaguzi umebaini kwamba, Kampuni ya Zanzibar Fishing Club, P.O Box 2698, Zanzibar yenye namba ya usajili DP 779/2007 ya tarehe 14/6/2007 imefanya utanuzi wa eneo lake la hoteli kutoka hekta 0.1836 (Plot 'A') ambalo lilikuwa likilipiwa USD 326 kwa mwaka hadi kufikia hekta 0.705 (Plot 'B' = 0.36 hekta na Plot 'C' = 0.182 hekta) ambalo linaendelea kulipiwa USD 7,000 kila mwaka katika mwezi wa Mei.

Kwa mujibu wa makisio yaliyoambatanishwa katika faili hilo, kampuni ilitakiwa kulipa USD 10,575 kwa mwaka (USD 15,000 x 0.705 hekta = USD 10,575) , lakini hadi sasa kampuni inaendelea kulipa USD 7,000 kwa mwaka ambapo ni sawa na hekta 0.47 x 15,000 na hakuna maelezo wala vielelezo juu ya malipo hayo pungufu ya USD 3,575 kwa mwaka.

Majibu ya Wizara/Idara:

Kwa mujibu wa viwango vyao vya kodi ya ardhi, inazingatiwa aina ya mwekezaji, aina ya uwekezaji, ukubwa wa eneo na mahala lilipo eneo husika la mradi. Mabadiliko ya mapitio ya viwango kwa wakati huo yalikuwa yakifanyiwa kazi na Wizara kupitia Idara ya Ardhi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imepatiwa viwango vilivyoelezwa na watendaji wa Idara ambavyo vimependekezwa kuanzia mwaka 2013. Viwango vyenyewe ni hivi vifuatavyo:

AINA YA KODI (MRADI)	**MMILIKI**	**KIWANGO KWA HEKTA KWA MWAKA-USD**					
		ARDHI YA MIJINI			**ARDHI YA VIJIJINI**		
		Viwango	Mapendekezo	Asilimia	Viwango	Mapendekezo	Asilimia

		vya zamani (2003)	ya viwango vipya 2013	ya ongezeko au punguzo	vya zamani (2003)	ya viwango vipya 2013	ya ongezeko au punguzo
KIWANDA	MGENI	U$ 3.200	U$ 3.500	9.37%	U$ 1,285	U$ 1,500	16.7%
	MENYEJI	U$ 300	U$ 300	-	U$ 200	U$ 200	-
HOTELI	MGENI	U$ 4,500	U$ 7,000	U$ 55.5%	U$ 4,000	U$ 5,000	25%
	MENYEJI	U$ 1,500	U$ 2,319	U$ 54.6%	U$ 1,000	U$ 2,000	100%
KILIMO	MGENI	U$ 642	U$ 500	- 22%	U$ 385	U$ 300	-22%
	MENYEJI	U$ 200	U$ 100	- 50%	U$ 100	U$ 50	-50%
HUDUMA	MGENI	U$ 1,785	U$ 2,500	39.6%	U$ 1,285	U$ 2,000	55.6%
	MENYEJI	U$ 600	U$ 1,500	150%	U$ 400	U$ 1,000	150%
MAKAAZI	MGENI	U$ 2,570	U$ 3.500	34.6%	U$ 2,570	U$ 3000	16.7%
	MENYEJI	TITLE/ OFFER	TITLE/OFFER	-	TITLE/ OFFER	TITLE/OFFER	-
MAKAAZI YA UKANDA WA UTALII	MGENI	U$ 4,500	U$ 7,000	55.5%	U$ 4,000	U$ 5,000	25%
	MENYEJI	U$ 2,570	U$ 3,500	34.6%	U$ 2,570	U$ 3,000	16.7%

Pamoja na Kamati kupatiwa viwango hivyo, imehitaji kujua iwapo viwango hivyo vinatolewa kwa mujibu wa sheria ama kanuni ya ardhi na kuelezwa kwamba, imetolewa na Idara ya Ardhi, ikajadiliwa katika Kamati Tendaji ya Wizara na hatimae kukabidhiwa Waziri na kuithibitisha. Kwa hali hii, Kamati imeelezwa kwamba, kifungu cha 12 cha sheria namba 12 ya mwaka 1992, ndicho kilichompa Mhe. Waziri wa masuala ya ardhi, kuandaa viwango hivyo.

Hata hivyo, Kamati imekipitia kifungu hicho cha sheria chenye vifungu vidogo viwili kama ifuatavyo:

Kifungu cha 12(1)

> "Taasisi za ukopeshaji (kifedha) zilizoelezwa katika jadueli liliomo katika sheria hii, zitatoza gharama za ardhi kama ilivyoelezwa chini ya sheria ya usajili wa ardhi"

Kifungu kidogo cha (2) kinaeleza:

> "Waziri atafanya mapitio na kurekebisha, penye umuhimu, jadueli inayoonesha taasisi za ukopeshaji, zilizopewa mamlaka ya kutoza gharama za ardhi, kwa kila baada ya miaka mitatu"

Kamati inaeleza kwamba, kifungu hicho cha sheria hakijafuatwa ipasavyo na Wizara ama Waziri wa Wizara hii katika kuandaa orodha hiyo, na inaitaka Wizara kuangalia upya matumizi ya viwango hivyo kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Kuhusiana na hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Wizara iliieleza Kamati kwamba, mwekezaji huyo alijumuishiwa Plot 'A' ; Plot 'B' na Plot 'C' na kuwa kiwanja kimoja na hivyo kumtoza kwa mujibu wa viwango vyao vya bei (USD 7000).

Hata hivyo, majibu haya hayakuwa ya msingi kwa Kamati, ambayo inakubaliana na hoja ya Mdhibiti.

Mapendekezo ya Kamati:

- Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ahakikishe jumla ya USD 10,575 zinalipwa na Mwekezaji wa Kampuni ya Zanzibar Fishing Club, kwani ndio inayostahiki na sio USD 7000 kama anavyolipa sasa. Fedha zote zilizolipwa pungufu tokea utanuzi huo zilipwe na Mwekezaji, na Katibu Mkuu ahakikishe kwamba fedha hizo zinalipwa si zaidi ya mwezi March 2014, pamoja na asilimia kumi (10%) ya adhabu.

- Kwa kipindi cha miaka 10 (tokea mwaka 2003 hadi 2013), Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ilishindwa kufanya mapitio ya viwango vya kodi, na hata marekebisho yaliyofanywa, hayazingatii hali halisi.

- Kuhusiana na mabadiliko ya viwango vya kodi ya ardhi, Kamati inaitaka Serikali kufanya mabadiliko hayo kwa mujibu wa sheria lakini pia kwa viwango hivyo viwe halisi kwa mnasaba wa mabadiliko ya wakati, si viwango hivyo vilivyopendekezwa.

Hoja Namba 13.3: Upungufu wa kodi baada ya uhaulishaji wa ardhi kwa Kampuni ya Grand Properties Limited, USD 16,410 ni sawa na Tsh. 25,435,500.

Ukaguzi umebaini kwamba, kabla ya uhaulishaji Kampuni ya Reem Beach Resort, yenye anuani P.O Box 4229 ambayo ilisajiliwa kwa namba DP 806/05 ya tarehe 25/4/2005 na kujuulikana tena kwa jina la Reem Beach Resort, P O Box 4525 iliyosajiliwa tarehe 1/1/2007 ambayo ikilipia kodi ya ardhi ya USD 6,600 kwa mwaka. Baada ya kufanyiwa uhaulishaji kutoka majina hayo na kuitwa kwa jina la Kampuni ya 'Grand Properties Limited' P.O Box 4525 iliyosajiliwa tarehe 13/3/2007, kampuni hii iliendelea kulipia kodi ya ardhi ya USD 3,318 kwa mwaka badala ya kodi ya awali ya USD 6,600 kwa mwaka.

Ukaguzi umebaini kwamba, hakuna maelezo wala vielelezo kuhusiana na ushukaji wa kodi hiyo kutoka USD 6,600 hadi USD 3,318.

Majibu ya Wizara/Idara:

Uwekezaji wa mwanzo ulifanywa kwa mwekezaji mzalendo ambae ni 'Sunrise Resort Limited' kwa kodi ya ardhi ya USD 3,318 kwa mwaka. Baadae ukahaulishwa kwa mwekezaji mgeni ambae ni Reem Beach Resort kwa kodi ya ardhi USD 6,600 kwa mwaka. Na baadae mradi ukarudi tena kwa Grand Properties Ltd, wazalendo kwa kodi ya USD 3,318 kwa mara nyengine. Kumbu kumbu za uhaulishaji huo zipo kwa ukaguzi zaidi.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilihitaji kufahamu kwa hatua moja baada ya nyengine juu ya uwekezaji huo na kuelezwa kwamba, mwekezaji wa kwanza Sun rise Resort, aliomba kwa kupitia barua ya tarehe 29/12/2006 iliyotoka kwa Ndg. Hashim J. Siddique, Hussein J. Siddique, Ndg. Abdullatif J. Siddique na Muhammad J. Siddique ambao ndio waliokuwa wamiliki wa kampuni hiyo na baada ya kupewa kibali cha kujenga hoteli ya kitalii, walihaulisha ardhi hiyo kwenda kwa Reem Beach Resort.

Kamati ilipotaka ushahidi wa uhaulishaji wa ardhi hiyo kisheria, ilielezwa kwamba, kwa mwaka 2006 ilipohaulishwa ardhi hiyo masuala ya uhaulishaji wa ardhi yalikuwa chini ya Msajili wa Serikali, ambapo Idara ya ardhi hivi sasa haina kumbu kumbu hizo.

Aidha, Idara ya ardhi pia haina kumbu kumbu za 'Memorandum of Association' za kampuni ya Reem Beach Resort wala Grand Properties Limited, kumbu kumbu ambazo zingeliweza kuithibitisha Kamati wamiliki halisi wa kampuni hiyo na uwiyano wao na waliohusika na uhaulishaji wa ardhi hiyo.

Pamoja na majibu ya watendaji, Kamati haikukubaliana kwa Kampuni ya Grand Properties Ltd, kulipa kodi pungufu na kuitaka Wizara hii ifanye marekebisho hayo. Hata hivyo, Kamati ilihitaji kukutana na wamiliki wa kampuni hii ili kuwasilikiliza na maoni yao, lakini kutokana na uchache wa muda wa kazi za Kamati, imeshindikana kufanya hivyo.

Mapendekezo ya Kamati:

Katibu Mkuu wa Wizara ahakikishe kwamba Kampuni ya Grand Properties Ltd, inalipa tofauti ya USD 6,600 kuanzia tarehe 13/3/2005, na deni hilo lilipwe si zaidi ya mwezi June 2014.

Hoja Namba 13.4: Deni la kodi ya ardhi ambalo halijalipwa na wawekeaji wa hoteli, USD 902,370.

Ukaguzi umebaini kwamba, wawekezaji wa hoteli ya Venta Club, Kiwengwa yenye usajili wa ardhi DP 98/1992 ya mwaka 1992 na Mawimbini Hotel Village Limited iliyopo Chuini yenye namba DP 2/87 ya tarehe 23/8/1988 ni wawekezaji waliokodishwa ardhi kwa mujibu wa sheria, kwa ajili ya kuendesha biashara ya hoteli za kitalii.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba, hoteli hizo zimetelekezwa na kukimbiwa na wawekezaji hao bila ya kutoa taarifa Serikalini na kuisababishia Serikali hasara ya USD 902,370 zikiwa ni kodi na adhabu (penalts) ambazo hazijalipwa hadi sasa.

Kutokulipwa kwa deni hilo ni kwenda kinyume na mkataba wa ukodishwaji wa ardhi namba DP 98/1992 ya mwaka 1992 na namba DP 2/1987 ya tarehe 23/8/1988.

Majibu ya Wizara/Idara:

Wizara baada ya kufanya uchunguzi wa awali, imegundua kwamba, miradi hiyo ni miongoni mwa makampuni yaliyopata misukosuko ya kifedha (economic crisis) kwa muda mrefu na inaonekana imeshindwa kurudi katika hali yake ya kiuchumi ya awali.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imefuatilia hoja hii ikiwa ni pamoja na kutembelea maeneo husika yaliyokuwa yamejengwa hoteli hizo na kujiridhisha kwamba jeti hizo zimejengwa kama ilivyoelezwa na Mdhibiti.

Kuhusiana na Hoteli ya Venta Club, Kamati imeshuhudia wizi mkubwa uliotokea wa majengo ya hoteli hiyo baada ya kutelekezwa, huku wananchi ndio waliohusika. Aidha, Kamati imeshangazwa kufika katika eneo la hoteli na kushuhudia wananchi wakiendelea kuiba na kuvunja taizi katika bwawa la kuogelea huku kila kitu kikiwa kimeibwa.

Kamati inailaumu Serikali kwa kushindwa kuilinda mali ya hoteli hiyo, na huku ikiwaacha wananchi wakifanya hujuma bila ya kuingilia kati. Kamati inaamini Serikali ilipaswa kuyalinda majengo ya hoteli hiyo bila ya kujali kama wamiliki wake wamekimbia, kwani ilikuwa rahisi kuwakodisha wawekezaji wengine, lakini kwa hali ilivyo sasa, Serikali itakodisha ardhi pekee.

Aidha, kwa upande wa Mawimbini Hotel Village, Kamati pia ilishuhudia kutelekezwa kwa hoteli hiyo ambayo yamebakia magofu, lakini angalau bado pana walinzi huku milango na vifaa mbali mbali vimetolewa na kuhifadhiwa katika vyumba kadhaa vya majengo ya hoteli hiyo.

Wakati Kamati ilipokuwa inafanya mahojiano na watendaji wa Idara na Wizara ya Ardhi, ilielezwa kwamba, suala la Hoteli hizi lipo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambae analitizama suala hilo kisheria, huku kukiwa na kesi baina ya Serikali na wamiliki wa kampuni hizo, bila ya kusahau kuwepo kwa madai kadhaa ya wananchi wanaowadai wamiliki wa hoteli hiyo.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ilihitaji kujua kuhusiana na deni lililoripotiwa na Mdhibiti kama litalipwa na vipi Wizara inalifuatilia, na Wizara kueleza kwamba, huu ni mradi uliokuwa ‘declared bankrupt’ na kulishghulikia suala hilo katika ngazi ya Idara ama Wizara, ni sawa na kupoteza muda bila ya mafanikio yoyote.

Aidha, kuhusiana na malipo, Kamati ilielezwa kwamba Hoteli hizo hapo awali zilikuwa zinalipia vizuri tu, lakini mambo yalikuja badilika baadae. Kwa mfano, Hoteli ya Mawimbini tokea mwaka 2005 hadi 2009 walikuwa wanalipa vizuri ila kuanzia hapo wameshindwa kulipa hadi sasa. Kamati ilipotaka kuthibitishiwa iwapo Bodi ya Mapato waliwataarifu wadaiwa hao, ilielezwa kwamba, walipelekewa barua na invoice mbali mbali za kutakiwa kulipa deni lakini hawakufanya malipo yoyote.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati aliahidi mbele ya Kamati kulifuatilia suala hili kwa undani na kuitaarifu Kamati, kutokana na Kamati kutaka kujua hatua ambazo Serikali imejipanga kuzichukua dhidi ya deni linalodaiwa kwa kampuni hizo.

Mapendekezo ya Kamati:

Bila ya kuathiri hatua zilizopo, Kamati inaitaka Serikali kurejesha ardhi hizo mikononi mwake, ili kutafutwe wawekezaji wengine wawekeze katika maeneo hayo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali isimamie ipasavyo ulipwaji wa deni hilo dhidi ya wawekezaji hao, na kutoa taarifa ya utekelezaji wa suala hili si zaidi ya June 2014.

Hoja Namba 13.5: Mapungufu yaliyojitokeza katika Ujenzi wa 'Jet' unaofanywa na baadhi ya hoteli:

Ukaguzi umebaini kwamba, baadhi ya hoteli zinajengwa 'Jet' ambazo huchukua sehemu ya bahari kwa ajili ya kutoa huduma za mapumziko na kuzamia kwa watalii. Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Ardhi na Usajili haifaidiki na malipo ya kodi ya ardhi hiyo (land lease rent) vile vile ni kwenda kinyume na sheria na kanuni za uhifadhi wa mazingira.

Majibu ya Wizara/Idara:

Idaraya Ardhi na Usajili imeshayaona mapungufu hayo na kwa sasa imo kwenye hatua ya kuzitafutia ufumbuzi wa kuliwekea utaratibu wa kisheria katika marekebisho ya sheria za ardhi ambayo rasimu yake inaandikwa. Hivyo baada ya sheria kuruhusu ndipo utafuata utaratibu na muda wa kupima maeneo ya 'jetty' zote zilizokwishajengwa kwa kukodishwa ardhi hizo na kutoza kodi kwa mujibu wa ukubwa wa eneo husika.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati imegundua kuwa suala la ujenzi wa jeti, bado halijashuhgulikiwa ipasavyo na Idara ya Ardhi na Usajili. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati haijalipa kipaumbele na kufuatilia kwa karibu, hoteli zilizojenga jeti ili kujiridhisha kwamba ujenzi huo unakubalika kisheria. Pia Wizara hii yenye jukumu la kuhakikisha kwamba matumizi ya ardhi yanaleta tija kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kupitia kodi mbali mbali za ardhi hiyo kwa wawekezaji, bado hadi leo haijafuatilia na kuhakikisha kwamba, kodi ya ardhi katika ujenzi wa jeti inalipwa ipasavyo.

Aidha, katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilifanya mahojiano na watendaji wa Wizara na Idara ya Ardhi na baadae iligundua kuwa, mbali na maeneo ya hoteli zilizojenga jeti kama zilivyoainishwa na Mkaguzi, kuna maeneo mengi ambayo yanahitaji muda wa ziada wa kuyafuatilia. Hivyo, kwa kuzingatia muda, Kamati iliweza ilitembelea Uroa, Kiwengwa na Wambaa kama ilivyoainishwa na Mkaguzi lakini pia ilitembelea maeneo mengine ikiwa ni pamoja na Bwejuu, Mawimbini, Nungwi na Kizimkazi Mchangamle na kushuhudia ujenzi huo ambao ni kweli Idara ya Ardhi na Usajili haikusanyi kodi yoyote na ujenzi wa jeti nyingi kati ya hizo haukufuata sheria.

Vile vile, Kamati ilibahatika kwa baadhi ya hoteli kukaa pamoja na wamiliki wake ambao wamehusika na ujenzi wa jeti na kupata maelezo yao. Aidha, mmoja kati ya wawekezaji hao ni mmiliki wa Hakuna Matata Lodge. Kamati ilimwita na ilipomhoji juu ya taratibu alizozichukua hadi kujenga jeti hiyo, alieleza kwamba, amefuatilia taratibu zake Mamlaka ya Vitega Uchumi, Zanzibar (ZIPA) huku akionesha ramani za kuthibitisha tokea awali kwamba aliomba ruhusa hiyo kutoka ZIPA. Hata hivyo, Kamati baada ya kumuita Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, aliihakikishia Kamati kwamba, ramani iliyotolewa na muekezaji huo wao kama ZIPA hawaitambui na hawajaruhusu kujengwa kwa jeti hiyo. Hivyo, pamoja na kujaribu kutoa maelezo ya kupata idhini ya ujenzi wa jeti hiyo katika mradi wake, muwekezaji huyo hatimae alikubaliana na Kamati kwamba, hakupata maelekezo hayo ya kujenga jeti kutoka Mamlaka ya Vitega Uchumi (ZIPA) wala Idara ya Mazingira wala Idara ya Ardhi na Usajili, haitambui ujenzi huo.

IDADI YA MIRADI ILIYOTEMBELEWA NA KAMATI-UNGUJA NA PEMBA NA INAYOHUSIKA NA UJENZI WA JETI:

Kamati imeona ni vyema hali halisi ya ujenzi wa jeti kwa mahoteli mbali mbali Unguja na Pemba ikafahamika na hivyo, imeorodhesha baadhi tu ya hoteli hizo, ilikuwa mifano huu, ambao ni kigezo kwa miradi mengine iliyosalia.

Namba	**Jina la Mradi**	**Mahali ulipo**	**Ukubwa wa Jeti**	**Kiwango cha Kodi Kinacholipwa.**
1.	Nungwi-Renco	Nungwi-Unguja	Sgm A=1,318,.04	Hailipiwi kodi
2.	Kizimkazi Loasis Hotel	Kizimkazi	Sgm A=47.45 & A=66.84	Hailipiwi kodi
3.	Kama Sea Clif	Kama	Sgm A=925.58	Hailipiwi kodi
4.	Kiwengwa Melia Hotel	Kiwengwa	Sgm A=1,318.04	Hailipiwi kodi
5.	The Residence Hotel	Kizimkazi Mchangamle	Sgm A=326.87	Hailipiwi kodi
6.	Kizimkazi Dolphin Paradise	Kizimkazi Mkunguni	Sgm A=459.36	Hailipiwi kodi
7.	Nungwi Sazani Hotel	Nungwi Sazani	Sgm A=1,318.04	Hailipiwi kodi
8.	Sultan Hotel	Bwejuu	-	Hailipiwi kodi
9.	Hakuna Matata Beach Lodge	Chuini	-	Haukulipiwa kodi
10.	Fundu Lagoon Resort Hotel	Wesha-Pemba	-	Hailipiwi kodi
11.	Lagema Dell’et	Nungwi	-	Hailipiwi kodi

Mapendekezo ya Kamati:

- Kamati inawataka Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais waifuatilie miradi yote iliyojenga jeti Unguja na Pemba na kuisimamia kufuata taratibu za sheria.

- Kwa kuwa bahari ni sehemu ya ardhi kwa mujibu wa Sheria namba 12 ya mwaka 1992, Kamati inamtaka Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati asimamie malipo ya kodi kwa miradi yote iliyohusika na ujenzi wa jeti ndani ya miezi mitatu baada ya kuwasilishwa ripoti hii Barazani na taarifa ya ufuatiliaji huo iwasilishwe kwa Kamati ya P.A.C.

THE MANTA RESORT (MRADI WA UJEZI WA CHUMBA CHINI YA BAHARI):

Pamoja na hoja hii kutokuwemo katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwa kuzingatia mamlaka ya Kamati iliyopewa kwa mujibu wa kanuni ya 118 (2)(c) ya kanuni za Baraza la Wawakilishi, ilifuatilia mradi huu ili kufahamu kama umefuata taratibu za uwekezaji na iwapo unalipiwa kodi ya ardhi. Aidha, kwa kuwa mradi huu unahusika na matumizi ya ardhi yanayowiyana sana na ujenzi wa jeti, Kamati imeona kuifafanua hoja hii katika eneo hili ni muafaka zaidi, hali itakayompa msomaji uelewa wa karibu baina ya hoja iliyotangulia na maudhui ya ufafanuzi wa hoja hii.

Uanzishwaji wa Mradi wa chumba cha chini ya Bahari:

Kamati imepata taarifa tofauti juu ya kampuni inayohusika na mradi huu, ambapo katika mahojiano na mmiliki wa Kampuni ya Manta Resort yaliyofanyika baina ya Katibu wa Kamati na mmiliki huyo alieleza kwamba, mradi huo umeanzishwa na kampuni ya Genberg Art Under Water Ltd, na ni kampuni tofauti na inayomiliki mradi wa The Manta Resort. Maelezo haya pia yaliungwa mkono na kuelezwa hivyo hivyo na watendaji wa ZRB Pemba, Idara ya Mazingira na hata ZIPA Ofisi ya Pemba katika kikao cha pamoja na Kamati. Hata hivyo, wakati Kamati inafanya mahojiano na Mkurugenzi wa ZIPA Unguja, alieleza kuwa mradi huo upo chini ya kampuni ya The Manta Resort na ni extension ya kampuni hiyo.

Mradi huo kwa mtazamo wa kumilikiwa na Kampuni ya Genberg, ilielezwa Kamati kuwa, wageni wanafika hapo moja kwa moja lakini wageni wengi na takriban wote hufika katika hoteli ya The Manta Resort na sehemu ya mapumziko yao ndio hufikia katika chumba hicho. Aidha, mradi huu ni wa majaribio (pilot) na unatarajiwa iwapo utafanikiwa vizuri na baada ya mwaka mmoja ukawa unaendelea vizuri, basi ruhusa kama hizo kwa wawekezaji watakaojitokeza, itatolewa kwao.

Ruhusa ya Taasisi za Serikali zilizohusika na kutoa vibali vya ujenzi wa mradi huu:

Kamati imeshuhudia majibu tofauti baina ya taasisi hizi za Serikali kuhusiana na taratibu zilizopitwa katika ujenzi wa mradi huu. Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) kwa upande wa Pemba kama vile ilivyoelezwa na Mkuugenzi mwenyewe alipofika mbele ya Kamati, kwamba mradi huo ulifuata taratibu zote za mazingira na uekezaji na taasisi zote zilishirikishwa katika utayarishaji wake na hata katika kupata vibali husika. Aidha, Kamati iliendelea kuelezwa kwamba, mradi huu unatokana na maombi ya Malta Resort, kuomba extension ya Malta Resort na ZIPA pamoja na Kamati ya kupitisha miradi walikubaliana juu ya ujenzi wake.

Aidha, Kamati ilipofika eneo la mradi husika huku ikiwa imefuatana na mtendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ameeleza kutoshiriki kwao katika mradi huo, na wakati Kamati inafanya mahojiano na Watendaji wa Wizara hii katika Ofisi ya ZAWA,Pemba, ikiwa ni pamoja na Afisa Mdhamini na Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Usajili, waliieleza Kamati kwamba, Wizara yao haikushiriki katika mradi huo na kwa ufupi sheria zao bado hazijazungumzia ujenzi wa baharini hivyo, hawakuwa na mchango wowote ama ufafanuzi wa mradi huo. Aidha, maelezo yao yaliungwa mkono na Muwakilishi wa ZIPA, Pemba kwamba, Watendaji wa Wizara ya ardhi hawana taarifa za mradi huo kwa sababu hata wao hawakuwashirikisha kutokana na mradi huo kuwa mpya na ni wa mwanzo kwa Afrika ya Mashariki.

Watendaji wa Bodi ya Mapato ya Zanzibar kwa upande wa Pemba walisema kwamba mradi huo uliombewa usajili wa VAT pekee na kuhusika kwao ni huko.

Kwa upande wa Idara ya Mazingira Pemba na Unguja walikiri na kuthibitisha mbele ya Kamati kwamba, Idara ya Mazingira haijaupitisha mradi huo na kwa hivyo, kwa upande wa Idara ya Mazingira, pamoja na mradi huo kuwa ni wa majaribio na hata kama tayari umeshafunguliwa na Makamo wa Pili wa Rais, haujapata Baraka kamili na kupitia taratibu zilizokamilika zinazohusika na Idara hii ya Mazingira kama mdau ama taasisi muhimu katika upitishwaji wa miradi ya uwekezaji. Kamati ilielezwa na Idara hii kuwa, tarehe 22/01/2010, Idara ya Mazingira imepokea barua kutoka ZIPA ya tarehe 21/01/2010 yenye kumbu kumbu namba ZIPA/HT/92/R.9/217 iliyowasilisha maelezo yakinifu (feasibility study) ya mradi huo. Aidha, barua hiyo iliyopelekwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, kama vile mbali na Idara ya Mazingira, ilipelekwa kwa Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii Zanzibar, ilieleza kama ifuatavyo:

> “Mradi wa Manta Reef Hotel ulioko Pemba umeleta ombi la kutaka kuongeza huduma zake kwa kuanzisha mradi wa boti yenye chumba chini ya maji, katika eneo la Makangale. Aidha, mradi huu una lengo la kushirikisha pwani ya karibu na mradi huo katika shughuli mbali mbali ikiwemo ya utunzaji wa mazingira ya bbaharini. Mamlaka inaleta kwako ombli hili ili kupata maoni yenu juu ya mradi huo.

> Tuanaomba maoni hayo yatufike si zaidi ya tarehe 29/01/2009 (bila ya shaka imekusudiwa 2010). Zaidi ya tarehe hiyo Mamlaka itachukulia kwamba, Taasisi yako haina pingamizi na mradi huu na itaendelea na hatua nyengine kama sheria na taratibu za uwekezaji zinavyoelekeza".

Aidha, mnamo tarehe 25/01/2010 kupitia barua ya kumbu kumbu namba IM/29/2/8 VOL.XI/120, Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira alimuandikia Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, kuelekeza kwamba, wao Idara ya Mazingira wanaelekeza kwa mujibu wa sheria ya Mazingira namba 2 ya mwaka 1996, mradi huo lazima ufanyiwe tathmini ya kimazingira kabla ya kujengwa kwake, barua hiyo ilieleza kama ifuatavyo:

> "Idara ya Mazingira baada ya kupokea na kuipitia kitaalamu 'feasibility study' ya maombi ya mradi wa boti yenye chumba chini ya bahari wenye lengo la kutoa huduma na biashara ya utalii kisiwani Pemba. Aidha Idara ya Mazingira inapendekeza maoni yafuatayo.
>
> Kwa mujibu wa sheria ya Mazingira namba 2 ya mwaka 1996 'The Environmental management for sustainable Develeopment Act, No. 2 of 1996' kifungu cha 38 cha sheria hiyo, mradi uliotajwa hapo juu unahusika na utaratibu wa mchakato wa tathmini ya athari za kimazingira. Aidha, tathmini ya athari za kimazingira kwa ajili ya mradi wake'

Pamoja na melekezo hayo ya Idara ya Mazingira, ZIPA walitoa ruhusa ya ujenzi wa mradi huo kwa Mwekezaji kupitia barua ya tarehe 26/03/2010 yenye kumbu kumbu namba ZIPA/HT/92/R.9/VOL.II/6 inayoelekeza maudhui yake kama ifuatavyo:

> 'ZIPA kimsingi haina pingamizi kwako kuendelea kuanzisha mradi wa chini ya bahari. Tafadhali wasiliana na Idara ya Mazingira na ufuate miongozo/taratibu zote zinazohusika na mradi huo.
>
> Tafadhali ufahamu kwamba, ruhusa hiyo ni kwa mradi wa majaribio wa kujenga chumba kimoja katika bahari. Kwa ajili ya kupata ruhusa na utekelezaji wa mradi kamili wa kujenga vyumba chini ya bahari, utalazimika kufuata taratibu za ZIPA kama sheria namba 11 ya mwaka 2004 inavyoelekeza'

Aidha, kufuatia barua hiyo ambayo Idara ya Mazingira walipelekewa nakla yake, Idara hii ya Mazingira ilimuandikia mwekezaji huyo Hadidu rejea za kufanywa tathmini hiyo kupitia barua yao ya tarehe 24/08/2010, yenye kumbu kumbu namba IM/29/2/8 VOL.XIII/29 na kumtaka awasilishe ripoti hiyo si zaidi ya miezi sita tokea kuandikwa kwa barua hiyo. Vile vile, tarehe 04/10/2012 kwa barua inayotoka kwa muekezaji, Idara ya Mazingira ilipokea barua ya kuwasilisha ripoti ya Tathmini ya Kimazingira ya mradi huo na baada ya kuipitia ripoti hiyo, imeona kuwa inahitaji kufanywa marekebisho hivyo, Idara ya Mazingira ilimuandikia muekezaji kwa barua ya tarehe 16/10/2012 yenye kumbu kumbu namba IM/29/2/8VOL XII, kumuelekeza kufanya marekebisho yanayohusiana na Tathmini hiyo.

Hata hivyo, hadi Kamati hii inaifanyia kazi hoja hii, Idara ya Mazingira haijapokea marekebisho hayo na ni sawa na kusema kwamba, hakuna Tathmini ya Mazingira iliyokubaliwa kwamba imefanywa kwa mujibu wa sheria, na ni sawa na kusema kwamba, muwekezaji huyo ameshakamilisha ujenzi wa mradi wake, huku akikiuka maelekezo ya ZIPA na maelekezo ya Idara ya Mazingira, na kibaya zaidi, Idara ya Mazingira na taasisi nyengine za Serikali zinafahamu hali hiyo, lakini hakuna hatua zozote za kisheria zilizochukuliwa kwa mradi huo.

Ulipaji wa kodi ya ardhi na kodi nyengine:

Kamati imethibitishiwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati chini ya Idara ya Ardhi na Usajili kwamba, mradi huu haulipiwi kodi yoyote ya ardhi, pamoja na faida kubwa inayopatikana katika kuwepo kwake. Sababu kubwa inayoelezwa kwa Kamati ni kwamba, Wizara bado haijawa na sheria inayosimamia ulipwaji wa kodi katika maendeleo ya ujenzi wa baharini. Hata hivyo, kwa kuzingatia maana halisi ya ardhi, Kamati haioni sababu hiyo kuwa ni ya msingi na inaamini Serikali pamoja na Wizara hii hazijawa tayari kukusanya kodi hizo kwa kisingizio kisicho na mashiko.

Aidha, kwa upande wa ZRB, Pemba wameeleza kwamba mradi huo bado haujaanza kulipia kodi yoyote, isipokuwa hivi karibuni mradi uliomba usajili wa VAT na wao wanatarajia kupata kodi ya VAT pekee ambayo kiwango chake ni sawa na vyumba vyengine vya hoteli ambayo ni asilimia 18, kitakachotofautisha wingi wa malipo ni bei ya chumba hicho.

Mapendekezo ya Kamati:

- Kamati inaitaka Idara ya Mazingira kusimamia sheria ya mazingira kwa mradi huo kama inavyoelekeza bila ya kujali kuwa mradi huo umefunguliwa na Makamo wa Pili wa Rais.

- Serikali iiangalie kwa karibu Mamlaka ya Vitega Uchumi, kwani ni sababu ya miradi mingi inayokiuka sheria huwa inapata ruhusa kwao tu bila ya kushirikishwa taasisi nyengine.

- Wizara ya ardhi isimamie mapato mbali mbali yanayotokana na ujenzi wa baharini, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa chumba cha chini ya bahari na aina nyengine za majenzi ya aina hiyo, ili kuiwezesha Serikali kuongeza mapato yake.

Hoja Namba 13. 6: Idara ya Ardhi na Usajili kutozifanyia mapitio bei za kodi za ardhi (land rent review) USD 244,609,910 sawa na Tsh. 50,895,206,211.

Ukaguzi umebaini kwamba, hadi sasa Idara ya Ardhi na Usajili imeshindwa kuzifanyia mapitio ya kodi ya ardhi (land rent review), zaidi ya miradi 268 iliyopatiwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji nchini tokea kuanzishwa kwake, haijafanyiwa mapitio ya bei kama ilivyoelekezwa katika sheria ya kodi ya ardhi ambapo kila baada ya miaka mitatu inalazimika kufanyiwa mapitito ya bei.

Hali hii imepelekea Serikali kukosa mapato mengi yanayotokana na miradi hiyo ambao hadi sasa haijafanyiwa mapitio ya kodi ya ardhi. Aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha 47(6) cha sheria namba 12 ya mwaka 1992 kama ilivyorekebishwa 2003 na 2010.

Majibu ya Wizara/Idara:

Wizara inakubali kwamba, ni kweli Idara ya Ardhi haijazifanyia mapitio bei za kodi za ardhi (Land Rent Review) za USD 244,609,910 ambazo ni sawa na Tsh. 50,895,206,211 kwa sababu zifuatazo:

i. Kiutalaamu inatakiwa kwanza kufanyiwa tathmini ya kila mradi husika ili kujuulikana ongezeko la thamani ya mradi (Current Market Value). Hii ni sababu inayopelekea kutofanyika mapitio ya bei za kodi za ardhi (Land Rent Review).
ii. Ukosefu wa wataalamu ambao ni wathamini (Land Valuers) na wataalamu wa kodi (Rent assessors).
iii. Hata hivyo, pamoja na changamoto walizozitaja, Idara ya Ardhi na usajili katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2013/2014 imejipanga vizuri na kutakiwa kuanza kufanya mapitio ya zoezi hilo. Hii inatokana na suala hilo kulipa kipaumbele cha mwanzo na kulisimamia ipasavyo kama ambavyo wameweza kufanya mapitio ya viwango mbali mbali vya kodi za ardhi 'Land Rate Review' katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 ambavyo vimeshaanza kutumika.

Uchunguzi wa Kamati:

Kamati ilielezwa kwamba, mabadiliko waliyoyakusudia Wizara ni kupendekeza bei mpya za kodi ambayo yalifanyika July 2013 na katika mbadiliko makubwa ni kutokuwepo kwa 'grace period' katika uwekezaji wowote kuanzia sasa. Mchakato wa mabadiliko hayo ulianzia 2011 na kuishia 2013, kazi ambayo imefanywa kwa mashirikiano na Kamisheni ya Utalii, Bodi ya Mapato Zanzibar, Mamlaka ya Vitega Uchumi, Wizara ya Fedha na Wizara ya Ardhi.

Wizara hii tokea ilipofanya marekebisho mara ya mwisho mwaka 2003 haikufanya marekebisho hayo hadi 2013, huku kukiwa na upotevu mkubwa wa mapato ya ardhi, kutokana na kuchelewa kufanywa kwa marekebisho hayo, Wizara ikishindwa kutoa sababu za msingi za kutofanywa mapema kwa marekebisho hayo. Aidha, pamoja na marekebisho waliyopatiwa Kamati, Kamati inaamini viwango hivyo havijazingatia ipasavyo uhalisia kwamba, Serikali imekosa mapato kwa muda mrefu, kwa takriban miaka 10 sasa, na kama kwamba mabadiliko hayo yangelifanywa tokea 2006.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuangalia upya viwango vipya vilivyopendekezwa na kutolewa na Wizara ya Ardhi, kwamba vipitiwe tena ili kuwe na uhalisia wa mabadiliko yake na wakati.

Hivyo, Kamati inaiagiza Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kulishughulikia suala hili ndani ya miezi sita baada ya kuiwasilisha ripoti hii katika Baraza.

Hoja Namba 13.7: Eneo lililohaulishwa kutoka Mawimbini Hotel Village Limited na kupewa Mwekezaji mwengine bila ya kufuata sheria.

Ukaguzi umebaini kwamba, Mawimbini Hotel Village Limited ni muwekezaji ambae alipewa eneo la ardhi lenye urefu wa hekta 10.9879 kisheria na Idara ya Ardhi na Usajili kwa namba DP 2/87 ya tarehe 23/8/1988 kwa ajili ya kufanya kazi za hoteli lakini eneo hilo baada ya kulitelekeza na kushindwa kulifanyia kazi kwa muda mrefu, amepatiwa muekezaji mwengine bila ya kulirejesha Serikalini kama sheria inavyoelekeza.

Aidha, ukauguzi umebaini kwamba, sehemu ya eneo hilo alilopewa mwekezaji tayari imeshajengwa nyumba (villa) na inaendelea kufanyakazi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 47(3) cha seheria namba 12 ya mwaka 1992 kama ilivyorekebishwa 2003 na 2010.

Majibu ya Wizara:

Hakuna sehemu ya eneo la mradi wa Mawimbini hotel iliyohaulishwa na kupewa Mwekezaji mwengine bila ya kufuata sheria. Kilichotokea ni kwamba, Mradi wa Mawimbini Hotel Village Ltd unamilikiwa kwa ubia baina ya wawekezaji wageni na mwenyeji. Aidha, eneo la mradi wa Mawimbini Hotel Village Ltd halikujengwa hoteli, kuna eneo lililobakishwa kwa ajili ya ujenzi wa hatua ya pili, mara baada ya kampuni hiyo kufilisika mwanzoni mwa mwaka 2009, muekezaji mwenyeji Bw. Ali Sultan Issa ambae ni mbia wa kampuni hiyo, alifanya maamuzi yake binafsi ya kumpa eneo lililojengwa kwa ujenzi wa hatua ya pili (second phase) mtu mwengine kwa lengo la kujenga nyumba yake ya mapumziko (villa). Kwa upande wa Idara ya Ardhi na Usajili haikutoa eneo hilo kwa mtu yeyote, hadi sasa Idara inatambua kuwa mpewaji rasmi wa eneo hilo ni Kampuni ya Mawimbini Hotel Village Ltd tu na sio vyenginevyo.

Uchunguzi wa Kamati:

Baada ya Kamati kuarifiwa kwamba, Ndg. Ali Sultan Issa ndie aliefanya maamuzi yake binafsi kumpa eneo hilo mtu mwengine na kujenga nyumba yake ya mapumziko, suala la msingi ni kufahamu taratibu zilizotumika kwanza katika umiliki wa eneo hilo kwa Ndg. Ali Sultan Issa na hatimae kwa mtu huyo mgeni, aliepewa ruhusa ya kujenga villa.

Kuhusiana na umiliki wa eneo hilo kwa Ndg. Ali Sultan Issa, Kamati iliarifiwa kwamba, mnamo tarehe 3/7/1986 barua yenye kumbu kumbu namba Ug.Eka,85/86/2 Ndg. Duchi A. Duchi Afisa wa Ardhi na Upimaji wa Wizara ya Kilimo na Mifugo alimjibu Ndg. Ali Sultan Issa kwa barua yake ya tarehe 9/4/86 kumkubalia ombi lake la kupewa eka 13.7 huku akitakiwa akodi eneo la eka 8.8 na kutakiwa kufanya maombi ya ‘lease’ ya eneo hilo.

Aidha, mnamo tarehe 18/2/1986, Wizara hiyo ya Kilimo na Mifugo kupitia kwa Afisa wa Ardhi na Upimaji Ndg. D.A.Duchi ilimuandikia Ndg. Ali Sultan Issa barua yenye kumbu kumbu

namba UG.EKA,85/86/2 ya kumkubalia Ndg. Ali Sultan Issa ombi lake la ardhi kwa ajili ya ujenzi wa hoteli, alilompelekea Mhe. Waziri wa Kilimo, tarehe 8/8/1985. Barua hiyo ya kumkabidhi rasmi eneo la ardhi ya eka sita (6), iliambatana na sharti la kumtaka Ndg. Ali Sultan Issa ahakikishe kuwa mali zilizomo katika eneo hilo alipe fidia kwa wamiliki wake. Aidha, jambo la msingi ambalo tunataka kulinukuu na kulisisitiza katika barua hiyo ni kwamba, mmiliki wa eneo hilo ni Wizara ya Kilimo , kama inavyohusika:

> "Kabla hujaanza shughuli za ujenzi, Wizara inakutaka uhakikishe kuwa mali zilizomo ndani ya eneo hilo uwalipe wenye kumiliki.
>
> Ilivyokuwa eneo hilo linamilikiwa na Wizara ya Kilimo pia miti ya daima iliomo kama Minazi na mengineyo ukalipe kwa mshika fedha wa Shirika la Kilimo, kabla hujakusafisha eneo hilo kwa kazi za ujenzi.
>
> Wakati wa kuhesabu miti na mimea ni vizuri wakawepo wenye konde na wawakilishi wa Tawi la C.C.M la eneo hilo pamoja na Afisa wa Kilimo ili kuepusha mizozo"

Maelezo hayo kwanza yanathibitisha wazi kwamba, eneo hilo halikuuzwa wala halikuhaulishwa kwa Ndg. Ali Sultan Issa, na alichopata ni ruhusa tu ya matumizi ya ujenzi wa hoteli na sio umiliki wake. maelezo haya aidha, yanathibitishwa na barua ya Wizara ya kilimo na Mifugo iliyoandikwa na Ndg. Duchi A. Duchi, yenye kumbu kumbu namba UG.EKA.85/86/4 ya tarehe 23/6/1986 inayohusiana na majibu kwa Ndg. Ali Sultan Issa kwa barua yake ya tarehe 20/6/1986 kwa ajili ya kuomba Waraka wa kumiliki ardhi katika eneo alilopewa kwa ujenzi wa Hoteli, Chuini.

Aidha, barua hii inaeleza kama ifuatavyo:

> "Napenda kukufahamisha kuwa kwa mujibu wa sheria ya eka, Wizara hii haina uwezo wa kutoa 'Title Deed'. Wizara imesaidia kupata eneo hilo na imekupa kienyeji tu. Sasa ni wajibu wako, kwa mujibu wa taratibu zilizopo za sheria ya Investment, kutafuta 'Title Deed'. Pia unatakiwa uelewe kuwa itabidi ukodi ardhi hiyo kwa mujibu wa sheria"

Kufuatia hali hiyo, pamoja na kwamba Kamati imekosa ushahidi wa umiliki wa eneo hilo kwa Ndg. Ali Sultan Issa kama vile ilivyoshindikana kuthibitishwa na watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Idara ya Ardhi na Usajili, Mamlaka ya Vitega Uchumi na taasisi nyengine za Serikali zilizohusika, Kamati ilithibitishiwa kwamba Ndg. Ali Sultan Issa aliingia ubia na Kampuni ya Sasa Enterprises Ltd ambapo yeye aliitoa ardhi yote aliyopewa kwa matumizi ya ujenzi wa hoteli kwa Kampuni hiyo ili awe mbia wa Kampuni.

Katika barua ya Sasa Enterprises Ltd, iliyoandikwa na Ndg. Juma Issa Noura kwenda kwa Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Upimaji mnamo tarehe 16/6/1987, barua hiyo yenye kumbu kumbu namba SE/9/98 ilitoa taarifa ifuatayo, kwa lengo la kupatiwa Lease ya eneo hilo:

"1. Resolution za Mikutano miwili ya Sasa Enterprises Ltd, ambayo uamuzi umefanywa kama ifuatavyo. Tarehe 18 February 1986 kuhusu Wakurugenzi na Shares zao:-

(a) Ali Sultan Issa
P.O Box 215
Zanzibar. 30% ya hisa.

(b) Gharib Abdulla Moh'd
P.O Box 4281
Zanzibar. 30% ya hisa.

Tarehe 18 July 1986 iliamuliwa kua Ardhi yote iliyotolewa kwa jina la Bw. Ali Sultan Issa, inakabidhiwa kwa Kampuni ya Sasa Enterprises (z) Ltd.

Resolution zote hizo zimesajiliwa katika Ofisi ya Registrar of Companies.

2. Certificate of Incorporation No. L69 ambayo inahusu Kampuni ya Sasa Enterprises (z) Ltd.

3. Napenda kukuarifu kwamba, Kampuni ya Sasa Enterprises inashikilia shughuli hizi kwa muda tu mpaka hapo baadae wakati itakapoanzishwa Kampuni ya Mawimbini Hotel Village na wakati huo Assests na Liabilities zitahamishiwa katika Kampuni hiyo iliyokusudiwa kwa mambo yote ya Hoteli inayoendelea kujengwa huko Chuini. Kwa hivyo, tunaomba lease itolewe kwa Kampuni ya Sasa Enterprises (Z) Ltd".

Juhudi hizo za kupata 'lease' ya ardhi kwa Sasa Enterprises Ltd, badala ya Ndg. Ali Sultan Issa ilizaa matunda kwa kampuni hii kuingia mkataba wa lease na Serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati na Mazingira mnamo tarehe 23/8/1988. Aidha, Kamati ilijiridhisha kwamba, mkataba wa kodi kwa ardhi hiyo ulifanyika kwa Kampuni ya Sasa Enterprises (Z) Ltd.

Aidha, Kamati ilifahamishwa kwamba, baada ya Kampuni ya Mawimbini Hotel Village Ltd kuanzishwa, 'Assets' na 'Liabilities' zote za Kampuni ya Sasa Enteprises zilihamishiwa kwa Kampuni hii mpya na hivyo, kodi ya ardhi ya eneo hilo ikawa ni baina ya Serikali kupitia Wizara inayohusika na masuala ya ardhi na Kampuni ya Mawimbini Hotel Village Ltd.

Kutelekezwa kwa eneo la ardhi lenye urefu wa hekta 10.9879 na kupatiwa Muwekezaji mwengine bila ya kufuata taratibu:

Kama tulivyoeleza awali, katika kufuatilia hoja hii, Kamati kwanza ilikaa na watendaji wa Wizara na Idara ya Ardhi na Usajili na hatimae kutembelea eneo husika. Kamati ilipokuwa inatembelea eneo hilo, ilishuhudia ujenzi wa 'Villa' katika eneo la hoteli ya Mawimbini na tayari imeshahamiwa na inatumika. Hata hivyo, Kamati ilipotaka ruhusa ya kuingia katika nyumba hiyo, haikuruhusiwa, huku mmiliki wa nyumba hiyo akiwa ndani na mlinzi aliyekuwa akilinda alitambulishwa ujio na Kamati pamoja na ujio wa Maofisa wa Afisi ya Idara ya Ardhi na Usajili.

Katika hali ya kusikitisha, Kamati ilizuilika kuingia ndani, kitendo kilichotafsiriwa kuwa ni dharau na kutoheshimu masharti na maelekezo ya uwekezaji. Aidha, Kamati ilimwita mmiliki wa hoteli ya Hakuna Matata Lodge ambae pia ni mmiliki wa villa hiyo, Bibi Rose Geuen kwa lengo la kufanya mahojiano nae, lakini kutokana na hali ya ugonjwa, alikuja mumewe ambae pia ni mbia wa Kampuni hiyo.

Kamati ilifanya mahojiano nae juu ya utaratibu alioutumia kuipata ardhi aliyojenga 'villa' hiyo, na kueleza kwamba, ameingia Mkataba wa 'Lease' na Ndg. Ali Sultan Issa, mnamo mwezi wa September 2010. Mkataba huo uliomkodisha mmiliki wa Kampuni ya Hakuna Matata heka 3, miongoni mwa masharti yake yameelezwa kama ifuatavyo:

> "AMBAPO Mkodishaji, Ali Sultan Issa, ni mmiliki kamili mwenye eneo la ardhi la hekta 27, liliopo Chuini tokea mwaka 1984.
>
> AMBAPO Mkodishaji kama ni mmiliki kamili na mwenye ardhi iliopo Chuini tokea mwaka 1989/1990 ameruhusu sehemu ya ardhi yake kutumiwa na Sasa Enterprises Limited kwa ujenzi wa hoteli ya Kitalii itakayotumiwa na Mawimbini Hotel Village Limited, bila ya kulipwa fidia, Mkodishaji na eneo lililopimwa na kukodishwa na Serikali, lilipewa kwa Mawimbini Hotel Village Limited.
>
> AMBAPO kwa manufaa ya kufurahia matumizi ya ardhi hiyo iliyokuwa haitumiki, Mkodishaji ameamua na amekubali kutoa heka tatu za ardhi iliyotelekezwa, kuunganisha na ardhi nyengine yenye mkataba wa muda mrefu na kumpa Mkodishwaji ili ajenge nyumba ya makaazi na kiwanda cha kufulia nguo na mambo mengine"

Jambo jengine la kufahamu ni kwamba, Mkodishaji amekodisha ardhi hiyo kwa USD 80,000 kwa miaka 30, huku Mkodishaji akipokea malipo ya kodi ya USD 600 kwa kila mwaka, mara baada ya kukamilika kwa ujenzi ulokusudiwa na Mkodishwaji.

Suala la msingi ni kujiuliza iwapo Ndg. Ali Sultan Issa, ana mamlaka ya kisheria ya kuikodisha ardhi ya Serikali na kodi ikamalizikia mikononi mwake. Kamati imejiridhisha kwamba, Ndg. Ali Sultan Issa amechukua mamlaka yasiyokuwa yake ya kuikodisha ardhi iliyokodishwa na Serikali kwa Mawimbini Hotel Village Limited, na Kamati imejiridhisha kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa sheria za ardhi katika hoja hii.

Aidha, Kamati baada ya kukutana na Bw. Fritz na kuomba radhi kwa kitendo cha mkewe cha kuizuia Kamati kufanya kazi zake, Kamati ilimtaka mkewe huyo aombe radhi kwa maandishi kueleza kwa nini amefanya kitendo hicho. Kufuatia kuomba radhi kwa maandishi, Kamati ilipanga siku nyengine ya ukaguzi na imefanya ukaguzi huo katika villa hiyo na kugundua mambo kadhaa ya ukiukwaji wa sheria za ardhi.

Vile vile, Kamati imeshuhudia kuwa ndani ya eneo hilo kuna nyumba (villa) mbili, ingawa moja inamilikiwa na mtu mwengine pamoja na boti kubwa inayotumiwa na wawekezaji hawa.

Katika kutekeleza kazi zake, Kamati ilihitaji kupima ukubwa wa eneo hilo pamoja na kupiga picha nje ya nyumba hiyo, lakini ilizuilika tena kufanya hivyo baada ya Bibi Rose kukataa kata kata kuiruhusu Kamati kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, baada ya majibizano makubwa baina ya Kamati na Bibi Rose, Kamati ilifanikiwa kutekeza hayo kwa nguvu. Kutokana na kitendo cha Bibi Rose kukataa kufika katika eneo hilo, Kamati ilijawa na mashaka makubwa na kuingiwa wasi wasi wa matumizi ya nyumba hiyo na ilihisi ni vyema ikawasiliana na Jeshi la Polisi Zanzibar, ili kueleza wasi wasi wake huo na hatimae Jeshi la Polisi lilichukua hatua za kufanya upekuzi. Pamoja na kwamba, hakukuwa na uhalifu wowote uliobainika kufuatia upekuzi huo, Kamati bado ina wasi wasi mkubwa wa wawekezaji hawa juu ya shughuli wanazozifanya na inaishauri Serikali kuwafuatilia kwa karibu ili kuondosha shaka iliyopo na hata kwa wananchi wa eneo hilo.

Ruhusa ya Ujenzi wa Villa, iwapo imetolewa na Taasisi yoyote ya Serikali:

Kwa mujibu wa mahojiano ya Kamati na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na watendaji wa Idara ya Ardhi na Usajili, walithibitisha kwamba, Wizara hii haifahamu lolote wala haijawahi kushiriki ama kutoa ruhusa ya ujenzi wa villa katika eneo hilo. Hata hivyo, Kamati ilipomwita mmiliki wa villa hiyo, aliieleza kwa kujiamini kwamba, Taasisi ya Serikali iliyohusika na vibali vyote vya ujenzi wa villa hiyo ni Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), hali iliyopelekea kuitwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa ZIPA, kujatoa ufafanuzi zaidi.

Kwa upande wa ZIPA, hawakuhusika na ujenzi wa villa. Ruhusa waliyoitoa wao kupitia barua ya tarehe 13 Aprili, 2011 yenye kumbu kumbu namba ZIPA/HT/2004/H.19/104 ni kuitanua hoteli yao ya Hakuna Matata.

Kamati haina pingamizi na ujenzi wa hoteli ya Hakuna Matata, kwani ilipata idhini ya ZIPA kwa barua ya tarehe 13/12/2004 yenye kumbu kumbu namba ZIPA/HT/2004/H.19/24, lakini ruhusa ya utanuzi wa hoteli hii kwa vyovyote ungelifanywa kwa kutanua hoteli na sio kujenga villa.

Kwa upande wa Kamati imeridhika kwamba, ujenzi wa villa hiyo haukufuata taratibu wala haujapewa idhini na taasisi yoyote ya Serikali. Hata hivyo, Kamati ilishtushwa na taarifa ya Mkurugenzi wa ZIPA, inayoeleza kwamba, Taasisi zote za Serikali zinazohusika na uwekezaji zimetoa idhini ya kuongezwa kwa eneo hilo kama ifuatavyo:

> “Tarehe 21/07/2009 yaliwasilishwa maombi na mwekezaji kufanya ‘extension’ ya mradi wake kwa sehemu za ‘Manager house, Supervisor house, staff house, professional laundry, water supply na storage with cooling house’
>
> Ukaguzi ulifanyika tarehe 13/08/2010 kuangalia eneo hilo kwa kushirikisha Idara zote husika. Baada ya hapo mwekezaji alitakiwa kuanza taratibu za kufanya uhaulishaji wa ardhi kupitia Idara ya Ardhi. Michoro iliwasilishwa kwa taasisi husika na Idara za Zimamoto na Uokozi na Idara ya Mazingira zilijibu kuwa hazina pingamizi.

Tarehe 4/4/2011 Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ilileta barua kueleza kuwa tayari eneo la Bw. Ali Sultan limeshakaguliwa na Wizara haina pingamizi. Ramani ya eneo hilo imeonesha kuwa eneo linaloombwa limepatikana na eneo la Mawimbini"

Maelezo hayo yanathibitisha kwamba, kulikuwa na maombi ya kuongeza ujenzi wa eneo la Hoteli ya Hakuna Matata. Lakini suala la Kamati ni wakati gani ruhusa ya ZIPA ilitolewa?

Aidha, kwa mujibu wa barua ya ZIPA ya tarehe 13/04/2011, iliyotoa ruhusa hiyo kwa nukuu ya barua ya waombaji ya tarehe 9/08/2010 wakati barua ambayo imetolewa ufafanuzi na Mkurugenzi wa ZIPA, kama tulivyoinukuu hapo juu ni ya tarehe 21/07/2009.

Kama hiyo haitoshi, barua ya muombaji ya tarehe 21/07/2009 imeambatanishwa na michoro inayoeleza ujenzi uliokusudiwa ni tofauti na ujenzi halisi ulioshuhudiwa na Kamati. kwa ujumla, barua ya tarehe 4/4/2011 haiwezi kukubaliwa na Kamati kama ushahidi kwa sababu waandishi wa barua hiyo ambayo ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na hata Idara ya Ardhi na Usajili, imekataa kufahamu suala la ujenzi wa villa hiyo, na hata Wizara hii haimtambui mmiliki wa Hakuna Matata, bali ardhi hiyo imekodishwa kwa Mawimbini Hotel Village Ltd. Kwa hali hii, Kamati imejiridhisha kwamba, Katibu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati aliehusika nabarua hii ya tarehe 4/4/2011 alitoa barua hiyo bila ya kuishirikisha Idara ya Ardhi na Usajili.

Ubadilishwaji wa Kampuni ya Hakuna Matata Beach Lodge na kuanzishwa kwa Kampuni ya Fritz & Rose Consultancy Ltd:

Kama tulivyokwishaeleza awali, Kampuni iliyopewa kibali cha kuanzisha uendeshaji wa mradi wa hoteli ni Hakuna Matata Beach Lodge ambayo ilikuwa inamilikiwa na Dr. Wilfried Geuen na Bibi Roswitha Geuen kwa 50% kwa kila mmoja. Wamiliki hawa walikubali kuuza hisa zao kwa Peter na Steffen lakini ikatokezea hitilafu baina yao na hatimae suala hilo wakalipeleka Mahakamani, ambapo Kamati ilielezwa kwamba, Mahakama iliamua kwa upande wao na kurejeshewa mali yao.

Aidha, Kamati pia ilielezwa kwamba, Bibi Rose alikuwa mgonjwa sana, hali iliyopelekea kurudi Nchini Ujerumani na hivyo waliamua na mumewe kusitisha shughuli za Kampuni ya Hakuna Matata Beach Lodge na pia kupitia barua yao ya tarehe 22/01/2013 waliomba kufutiwa ruhusa ya kuishi nchini na kufanya kazi, na taarifa hiyo kwa ilielekezwa pia kwa Kamishna Uhamiaji Zanzibar, kutoka kwa Mkurugenzi wa ZIPA. Aidha, Kamati iliarifiwa pia kwamba, wawekezaji hawa walirejea nchini na kuanzisha kampuni Kampuni nyengine ambayo sio tena Hakuna Matata Beach Lodge ambayo tayari mradi wake ulikua umeshafutwa na hivyo, kuanzisha Kampuni ya Fritz & Rose Consultancy Ltd.

Aidha, Mradi huu mpya wa Fritz & Rose Consultancy Ltd, umefanyiwa ukaguzi na Ass.Insp: Suleiman J. Suleiman, kwa niaba ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, akieleza shughuli zake ni kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya uendeshaji wa Hoteli (Hotel Management),

kutoa ushauri wa kisasa juu ya masuala ya mapokezi na kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya masuala yanayohusu malazi na makazi ya wageni (Hospitality management).

Kuhusiana na ruhusa ya kuishi kwao nchini na kufanya kazi, Kamati ilielezwa kuwa, mnamo tarehe 7/1/2013 wawekezaji hao waliomba ruhusa mpya ya kuishi na kufanya kazi nchini chini ya Kampuni yao mpya ya Ushauri kwa Mkurugenzi wa ZIPA na mnamo tarehe 28/1/2013 Mkurugenzi wa ZIPA aliwaombea bwana Fritz na bibi Rose ruhusa hiyo kwa Kamishna Uhamiaji. Aidha, mnamo tarehe 7/3/2013 Mkurugenzi wa ZIPA pia aliomba kufutwa kwa ruhusa ya kufanya kazi kwa bibi Rose kwa kua yeye mwenyewe aliamua kutojishughulisha na shughuli za kibiashara na badala yake apewe ruhusa ya utegemezi (Dependent pass) ili aweze kuishi vizuri na mkewe. Ruhusa hiyo imeombwa kwa Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar kama inavyoonekana katika**.**

Hata hivyo, Kamati ilielezwa na Taasisi hizi kwamba, Mradi wa Ushauri kwa mfano mradi huu unaohusika na masuala ya utalii, unapofanywa na wageni, kwanza hutakiwa kuwa kukodi ofisi na kutumia shughuli zao katika afisi hizo. Aidha, huwa hawatakiwi kumiliki nyumba ya makaazi.

Mapendekezo ya Kamati:

- Serikali ihakikishe kuwa inalirejesha mara moja eneo lote la iliyokuwa Mawimbini Hotel Village katika mikono ya Serikali.
- Serikali iondoshe majengo yote yaliyojengwa kinyume na utaratibu katika eneo hilo na kuliwacha wazi kama lilivyokuwa awali.
- Serikali imchukulie hatua za kisheria Bw. Ali Sultan Issa, kwa kitendo chake cha kuchukua na kukodisha mali ya Serikali kinyume na utaratibu.
- Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji wote waliohusika na kadhia hii.

Hoja 13.8 Kutokuwepo kwa Viwango Maalum vya Ulipaji wa Kodi ya Ardhi

Ukaguzi umebaini kuwa kuna viwango tofauti vya kodi ya ardhi vinavyotozwa kwa wawekezaji, hali inayopelekea kutokuwepo kwa uwiano wa bei na ukubwa wa eneo ambalo wamepatiwa wawekezaji hao.

Kutokuwepo kwa uwiano huo kunapelekea kuwepo mwanya wa upotevu wa mapato kutokana na kutojulikana vigezo na uhalali uliotumika kukusanya mapato hayo.

Majibu ya Wizara/Idara:

Sio kweli kwamba hakuna viwango maalum vya ulipaji wa kodi ya Ardhi, viwango hivyo, hufanyiwa mapitio (review) kila inapoonekana haja ya kufanya hivyo. Tangu kuasisiwa miradi ya vitega uchumi binafsi hapa Zanzibar mwaka 1986, Idara ya Ardhi na Usajili imeshafanya

mapitio ya kodi ya ardhi takriban mara nne hadi kufikia mwaka 2013. Hivi karibuni Idara ya Ardhi na Usajili ilifanya mapitio ya kodi ya ardhi ya mwaka 2003. Viwango vya ulipaji wa kodi kufanywa kwa kuzingatia;

i. Aina ya Mwekezaji (Mgeni au Mwenyeji)
ii. Eneo la uwekezaji (Location)
iii. Ukubwa wa eneo lililoekezwa (Total area)
iv. Aina ya uwekezaji
v. Mwaka wa mapitio (mwaka husika)

Aidha, walizidi kueleza kuwa wakati mwengine Mheshimiwa Waziri hutoa punguzo ya kodi ya ardhi kama Sheria ya Umiliki wa Ardhi inavyoeleza katika kifungu cha 47(5).

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilibaini kuwa viwango vya ulipaji wa kodi ya ardhi vipo ingawa watendaji wa Idara hiyo hawavifuati. Jambo hili linabashiria kuwepo kwa mwanya wa rushwa.

Aidha, Kamati imebaini kuwa Idara ya Ardhi na Usajili haikufanya mapitio ya kodi ya ardhi takriban miaka 10, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 47(6) cha Sheria ya Umiliki wa Ardhi. Hii ni kutokana na kuwa Idara hii inatakiwa kufanya mapitio ya kodi ya ardhi si zaidi ya kipindi cha miaka mitatu.

Ingawa, Mheshimiwa Waziri hutoa punguzo ya kodi ya ardhi kwa maslahi ya taifa, Kamati ilishindwa kupata jibu sahihi la neno ‘maslahi ya taifa’ hasa ikizingatia kuwa tafsiri ya neno hili linategemea na yule anayelitafsiri.

Katika kufuatilia hoja hii Kamati imebaini pia wapo baadhi ya wawekezaji ambao wamewekeza miradi yao Pemba lakini wanasema wanalipa kodi ya ardhi Unguja.

Mapendekezo ya Kamati

i. Idara ya Ardhi na Usajili itekeleze majukumu yake kwa mujibu wa sheria za nchi.
ii. Kuwepo na mawasiliano ya karibu baina ya Idara ya Ardhi na Usajili, Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Vitega Uchumi.
iii. Endapo kodi ya ardhi itapunguzwa au kumefanyika mabadiliko yoyote Kamati inapendekeza kuonekane kumbukumbu katika jalada la muwekezaji inayogusia kadhia hiyo.
iv. Wawekezaji walipe kodi zao za ardhi kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa ili kuepusha mivutano isiyo lazima ikiwa ni pamoja na kukwepa kulipa kodi hizo.

Hoja Nam. 13.9: Miradi ya Hoteli Iliyosajiliwa ambayo hailipi Kodi ya Ardhi:

Ukaguzi umebaini kuwa kuna baadhi ya miradi imesajiliwa na kupatiwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji lakini miradi hiyo imeshindwa kulipa kodi ya ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Umiliki wa Ardhi na mkataba wa ukodishwaji. Kutokulipa kodi ni kwenda kinyume na Sheria na mkataba husika.

Majibu ya Wizara/Idara:

Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imekiri kutokukushanya kodi kwa baadhi ya miradi ya hoteli iliyosajiliwa. Hata hivyo, wameanza kuchukua hatua mbali mbali zikiwemo za kuwaandikia barua za ukumbusho, kuwapelekea indhari ya kutaka kufutiwa na baadhi ya miradi tayari imeshafutwa.

Walizidi kueleza kuwa miongoni mwa sababu zinazopelekea wasikusanye kodi hizo ni pamoja na;-

- kwa upande wa Taasisi za Serikali, Taasisi hizi hazina bajeti ya kutosha.
- Taasisi za Kidini, Taasisi hizi hazifanyi biashara isipokuwa zinatoa huduma.
- Wawekezaji Wazalendo, hawana mitaji ya kujiendeleza na wanafanyakazi kwa hasara.
- kwa upande wa Kampuni ya Zantel, Kampuni hii ina hisa na Serikali kwa asilimia 18%, na kwa mujibu wa makubaliano yaliyomo kwenye 'Memorandum of Understanding' hawapaswi kulipa kodi hizo.

Uchunguzi wa Kamati

Mnamo tarehe 6 Disemba, 2013 Kamati ya PAC ilikutana na baadhi ya wawekezaji ili kupata majibu halisi ya hoja hii, isipokuwa kwamba baadhi ya miradi ilijadiliwa zaidi ya siku moja baada ya kutokea haja ya kufanywa hivyo kwa lengo la kupata ufafanuzi sahihi. Kwa kuwa hoja hii imejumuisha Wawekezaji mbali mbali bila shaka kila muwekezaji atakuwa na sababu zake na zifuatazo ni sababu hizo;-

S/NO.	JINA LA MRADI	SABABU YA KUSHINDWA KULIPA NA JUHUDI ZINAZOCHUKULIWA	USHAURI WA KAMATI
1.	Mawimbini Club Hotel	Wamefilisika. Hakuna juhudi yoyote ya kuliendelekeza eneo hilo.	Ardhi ya mradi huu irejeshwe Serikalini na Serikali itafute muekezaji mwengine.
2.	Jumuiya ya watu wenye ulemavu (Mradi wa	Uwezo wao ni mdogo wa kuliendeleza eneo hilo kutokana na Jumuiya hii haizalishi na badala	Juhudi za kudaiwa kodi ziendelee na Jumuiya ifanye juhudi ya kulipa

	Kujenga Kijiji cha Watu wenye Ulemavu, Zanzibar).	yake inatoa huduma. Nia ya Jumuiya ni kuingia ubia na na Taasisi au watu wenye uwezo, ingawa wanakabiliwa na ugumu wa kukosa mtaji au kupata watu wenye uwezo. Jumuiya kwa kushirikiana na Serikali imefanya mazungumzo na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kwa ajili ya kuliendeleza eneo hilo kwa niaba ya Jumuiya.	kodi hiyo, ili kuepuka uwezekano wa kurejeshwa eneo hilo Serikalini.
3.	Karakana Kuu (Lengo ni utengenezaji wa Magari ya Serikali).	Baadhi ya eneo lao limevamiwa na wananchi. Pia, hakuna mkataba wa ukodishwaji. Aidha, baada ya kuundwa kwa Idara ya Usafiri na Leseni, Karakana imerejeshwa Serikalini na kua chini ya Idara ya Usafiri na Leseni ambayo sio Idara inayojitegemea. Aidha, kwa mujibu wa taratibu za ukodishwaji, ruhusa ya kukodishwa na kutakiwa kulipa deni, hufanywa kwa Taasisi zinazojitegemea.	Hili ni sawa na madeni mengine baina ya Taasisi za Serikali na linawezekana likawa gumu kulipika. Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kulihakiki deni hilo na hatimae kufanywa utaratibu wa kufutwa.
4.	Baraza la Manispaa	Walipokea Invoice inayoonesha deni la USD 6,026.40 la miaka sita, ingawaje hawajawahi kupokea invoice nyengine yoyote kuhusiana na deni hilo. Hata hivyo, Baraza limekubali kulipa ingawaje kwa sasa halina uwezo wa kulilipa deni hilo kutokana na hali ngumu inayowakabili.	Hili ni sawa na madeni mengine baina ya Taasisi za Serikali na linawezekana likawa gumu kulipika. Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kulihakiki deni hilo na hatimae kufanywa utaratibu wa kufutwa.
5.	Shirika la Umeme (ZECCO)	Hawana deni lolote.	Wamelipa madeni yao na Kamati imeridhika na ushahidi uliowasilishwa. Kamati inapendekeza hoja ya deni kwa Shirika la Umeme, ifutwe.
6.	Zantel (Minara ya Kampuni)	Wameingia Mkataba na Serikali kwamba mchango wa Serikali ili kuwa na hisa 18% za Kampuni hiyo ni kuwapa Kampuni ruhusa ya kutumia ardhi katika maeneo mbali mbali Zanzibar ambayo yameainishwa katika Mkataba husika.	Kamati haipingi Mkataba huo, ila hauna uhusianao na kusamehewa kulipa kodi ya ardhi, kwani kipengele hichi hakijazungumzwa katika Mkataba huo. Serikali ikae tena na Kampuni ya Zantel,

			waweze kukubaliana vizuri juu ya suala hili la liwekwe wazi, ili lifahamike.
7.	Benki ya Watu wa Zanzibar (Peoples Bank of Zanzibar)	Eneo la Mkwajuni hawakuwahi kufanya shughuli zao na badala yake eneo hilo wamepewa Idara ya Uhamiaji na kwa upande wa Chwaka, eneo hilo wamepewa Chuo cha Uongozi wa Fedha (ZIFA). Lililokuwa tawi la Makunduchi lipo chini ya Wizara ya Fedha na hivi sasa Benki ina mpango wa kulifufua tawi hilo. Waliithibitishia Kamati kuwa taratibu zote za uhaulishwaji zilifuatwa.	Kamati inaitaka PBZ wakae pamoja na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili kuangalia deni lao ni lipi na maeneo yepi hawataweza kuyalipia kodi kama walivyoeleza, na taarifa ya vikao hivyo na makubaliano yake yawasilishwe kwa Kamati.
8.	Benki Kuu ya Tanzania (BOT)	Walipitikiwa kulipa na hivi sasa wameshapatiwa Ankara hivyo watalipa.	Kamati inawataka walipe deni hilo pamoja na adhabu ya 10%, na ZRB isimamie kulipwa deni hilo kwa ukamilifu wake (pamoja na adhabu).
9.	Amal Farm	Ardhi hiyo imechukuliwa na Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kuanzia mwaka 2011, barua ya tarehe 20/10/2011 yenye kumbukumbu namba AMMN/29/3/C.100/VOL.XXII/574 inathibitisha hilo.	Kamati inataka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia SUZA, kuharakisha malipo kwa mmiliki wa zamani wa Amal Farm ili haki itendeke, na inapendekeza deni hilo lifutwe.
10	Wakfu Almazrui Charitable Islamic Society School (Kuwasaidia watoto yatima wa Zanzibar kwa na kuwaendeleza kuelimu).	Hawana deni hadi 2011. Hata hivyo, wamewasilisha malalamiko yao kwa Kamati hii kuwa wanalipia eneo lote walilopewa ingawa sehemu ya eneo hilo limechukuliwa na Serikali na kujengwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Afisi ya Bodi ya Mapato – Zanzibar (ZRB). Aidha, wameiomba Serikali kutowalipisha kodi kwa kuwa shughuli inayofanywa hapo ni ya kutoa huduma (wanalea watoto yatima) hivyo, hawana faida yoyote inayoingia.	Kwa kuwa baadhi ya eneo limechukuliwa na Serikali, Kamati imewataka Wawekezaji hawa waiandikie barua Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili wapimiwe upya eneo ambalo wanalitumia. Aidha, Kamati inaitaka Wizara ya ardhi iwalipishe kodi kwa kuzingatia ukubwa wa eneo wanalomiliki sasa baada ya kuwapimia.

11	Ifa Hotels And Resort	Wameirejesha ardhi Serikalini ingawa barua yao haijajibiwa na Wizara husika na Ankara za malipo zinapelekwa kama kawaida	Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Taasisi zote zinazohusika kushughulikia suala hili, ili kusiwe na gharama zozote dhidi ya mmiliki wa Kampuni hii.
11	Catholic Diocess	Wameitwa na Kamati na taarifa ziliwafika, isipokuwa kwa wahusika wa kanisa la Machui, hawajahudhuria.	Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, kusimamia kulipwa kwa deni hilo na lisipolipwa ndani ya miezi sita (tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii), hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.
12	Zanzibar Sugar Factory Limited	Katika ukubwa wa ekari 6644 za ardhi walizoahidiwa kukabidhiwa, mpaka sasa wamekabidhiwa ekari 1000 tu na zilizobaki zainatumiwa na walimaji wazawa kwa kilimo cha mpunga. Aidha, kati ya nyumba 172 walizoahidiwa kwa wafanyakazi wao, ni nyumba chache tu zimekabidhiwa kwao. Pia muda wa matayarisho (grace period) waliopewa ni mdogo kwa sababu kiwanda kilikuwa katika hali mbaya kwa uwekezaji na uzalishaji mpya wa sukari. Vile vile wamewasilisha maelezo yao kwa Wizara ya Fedha, lakini hawakujibiwa. Wametoa malalamiko yao kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na kumuandikia, na amezingatia hoja zao.	Kamati imependekeza ifuatavyo: 1. Idara ya Ardhi kupitia wakala wake ZRB, ipige hesabu ya malipo ya kodi kwa sehemu walizokabidhiwa ili waweze kulipa baada ya kukamilika kwa kipindi cha ‘grace period’. 2. Serikali ikae pamoja na Kampuni kutatua tatizo hili na majibu yawasilishwe mbele ya Kamati. 3. Baada ya Idara ya Ardhi na Usajili kutoa malalamiko yake ya kutokushirikishwa katika kadhia hii, Kamati imeitaka Wizara ya Fedha kuishirikisha Idara ya Ardhi na Usajili kwa kuwa ndio mhusika mkuu wa masuala ya ardhi Zanzibar.

13	Mitras International Trading LLC	Wameiomba Idara ya Ardhi na Usajili waongezewe grace period. Aidha, wameeleza kuwa hawana deni lolote na risiti namba D385358 inathibitisha hilo.	Kamati iliwataka wawasilishe supporting documents za kuthibitisha kuomba grace period, jambo ambalo bado hawajafanya. Hivyo, Kamati imeshindwa kutoa maoni ya hoja hii. Hata hivyo, Kamati inaitaka ZRB kufuatilia ulipwaji wa deni linalowakabili, baada ya kujiridhisha kuwa mwekezaji huyu ana deni.
14	Tb Investment Limited	Alofika sio mhusika	Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, kusimamia kulipwa kwa deni hilo pamoja na adhabu, na lisipolipwa ndani ya miezi mitatu (tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii), hatua za kuirejesha ardhi hiyo Serikali kwa kukiuka masharti ya Mkataba zichukuliwe dhidi yao.
15	Vuai Ali Vuai	Hajalipa kodi ya ardhi tokea mwaka 2010 kutokana na sababu za kifamilia. Aidha, ameshindwa kuliendeleza eneo hilo kwa kukosa mbia wa dhati na hivi sasa ameamua kuwasiliana na vyombo vya fedha ili aweze kupata mkopo na alitumie eneo hilo kama alivyodhamiria kwa ujenzi wa hoteli.	Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi kusimamia kulipwa kwa deni la ardhi hiyo na iwapo haitalipwa baada ya miezi sita kutoka tarehe ya kuwasilishwa ripoti hii, Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi kulishughulikia suala hilo kisheria.
16	Shirika la Bandari (Mradi wa Wtel/Tower; Workshop).	Kwa mujibu wa kumbu kumbu za Shirika, hawana mradi huo na Shirika halijawali kupokea hati ya madai (invoice) kwa kipindi kilichotajwa cha miaka 10.	Kamati haikupatiwa ufafanuzi wa kutosha kuhusiana na sababu za kuwepo kwa mradi huu. Aidha, inashauri ufanyiwe kazi tena na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na akiridhika kuwa haupo, basi aijuulishe Kamati.
17	Mamlaka ya Uwanja wa Ndege (Airport)	Mamlaka haikuwa na taarifa na kuwepo kwa deni ama mradi huo na baada ya kuitwa mbele ya	Kamati inaitaka Mamlaka kuharakisha kutekeleza ahadi ya kulifuatilia deni

		Kamati na kuelezwa ndipo imepanga kuonana na uongozi wa Idara ya Ardhi na Usajili, kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa sababu deni hilo limerithiwa kutoka iliyokuwa Idara ya Anga. Aidha, utaratibu wa malipo utafuata baada ya kupata maelekezo kutoka Serikalini pamoja na mchanganuo wa deni husika	hilo ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii na iiarifu Kamati kila hatua itakayoichukua.

13.10 MAENEO YA ARDHI YALIYOTOLEWA NA IDARA YA ARDHI NA USAJILI AMBAYO HAYAJAENDELEZWA HADI SASA:

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya maeneo yaliyotolewa na Idara ya Ardhi na Usajili kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya hoteli hadi sasa hayajaendelezwa. Kutokuyaendeleza maeneo hayo ni kwenda kinyume na Sheria ya Umiliki wa Ardhi na mkataba wa ukodishwaji.

Majibu ya Wizara/Idara:

Ni kweli kwamba yapo maeneo kadhaa ya ardhi ambayo yametolewa na Idara ya Ardhi na Usajili na hayajaendelezwa ingawa yanalipiwa kodi ya ardhi. Hata hivyo, Idara ya Ardhi na Usajili imeanza hatua ya kuyaorodhesha maeneo hayo ili taratibu za kisheria ziweze kuchukuliwa. Kwa kuwa maeneo hayo ni mengi ukiacha yale yaliyoorodheshwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ukurasa wa 53 wa Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Ardhi na Usajili iliiomba Kamati ya PAC kuyafanyia kazi pia maeneo hayo.

Uchunguzi wa Kamati

Ingawa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeonesha maeneo saba tu ya ardhi ambayo hayajaendelezwa, Kamati ya PAC kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi na Usajili ilibahatika kupata maeneo 119 ya ardhi ambayo hayajaendelezwa ijapokuwa baadhi ya watumiaji wa ardhi hizo wana hati ya kawaida ya matumizi ya ardhi ‘Right of Occupancy’ na wengine wana mikataba ya kodi ‘Lease Agreement’.

Kwa msingi huo, Kamati ilikutana na baadhi ya wawekezaji na kwa kuwa maeneo ambayo hayajaendelezwa ni mengi na muda uliopangwa wa Kamati kutekeleza majukumu yake ni mdogo, Kamati haikuweza kuwafikia wote walioorodheshwa. Sambamba na hilo, wapo baadhi ya wawekezaji hawakufika kutoa maelezo yao mbele ya Kamati ingawa barua za wito ziliwafika kutoka na sababu mbali mbali ikiwemo, wahusika kuwa nje ya nchi, wengine ni kudharau

Kamati na kutolipa suala la wito uzito wake na wengine ni kuchelewa kupata barua za wito. Vile vile, baadhi yao waliwasilisha majibu yao kwa maandishi baada ya kutoa dharura zilizokubaliwa na Kamati.

Katika kufuatilia hoja hii Kamati imebaini kuwa, baadhi ya wananchi hawaijui Sheria ya Umiliki wa Ardhi hasa wale waliopewa haki ya kawaida ya matumizi ya ardhi (Right of Occupancy). Suala hili limebainika baada ya baadhi ya wananchi hao kushangazwa na kitendo cha Kamati hii kuwahoji kuhusiana na kutoyaendeleza maeneo hayo wakati wao wana haki ya kawaida ya matumizi ya ardhi.

Aidha, tumebaini kwamba Idara ya Ardhi na Usajili inatoa nambari ya usajili ya ukodishwaji wa ardhi kwa Muwekezaji kinyume na mwaka ambao amekodi ardhi hiyo. Kwa mfano;- Island United Petroleum imeripotiwa kuwa amekodishwa ardhi mwaka 2008 wakati amekodishwa mwaka 2010, Marasa Beach Resort Ltd imeripotiwa kuwa amekodishwa ardhi mwaka 2003 wakati amekodishwa mwaka 2007 nakadhalika.

Vile vile Kamati imefahamu kwamba, orodha hiyo imehusisha maeneo ambayo hayajaendelezwa katika ukanda wa pwani pekee kwa miradi zaidi ya mahoteli na ujenzi unaofanana, lakini hayajahusishwa maeneo ya yaliyotolewa kwa ujenzi wa viwanda na maeneo mengine ambayo hayapatikani katika ukanda wa pwani. Aidha, ufuatiliaji huo haujahusisha maeneo ya Pemba, na Kamati imeelezwa kwamba, baada ya kufanyika kazi hiyo Unguja, Wizara imejipanga kufuatilia Pemba na kikwazo kikawa kazi za Kamati na shughuli za Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Zifuatazo ni sababu za baadhi ya Wawekezaji waliokuwa hawajaendeleza ardhi walizopewa;-

S/NO.	ALIYEPEWA ARDHI	SABABU YA KUTOENDELEZA	USHAURI WA KAMATI
1.	ASB Properties	Wanamiliki zaidi ya eneo moja hivyo, wameupa kipaumbele ujenzi wa hoteli ya Mambo Msige.	Kamati haikuridhishwa na sababu hizi na inashauri Serikali ichukue hatua za kuirejesha ardhi hiyo Serikalini mara moja kwa ajili ya matumizi mengine ya Serikali, kwani Kampuni hii imekiuka masharti ya Mkataba wa Ukodishwaji wa ardhi.
2.	Blue Lodge	Walibaini kuwa eneo waliloomba ni dogo hivyo, halitoshi kwa shughuli zao wazizozikusudia.	Kamati inapendekeza Kampuni hii iachiwe kwa miezi sita, iwapo ikifika

		Kutokana na hilo wameomba eneo la ziada Idara ya Ardhi na Usajili pamoja na kuambatanisha ramani mpya ya ujenzi huo. Vile vile, wameomba eneo hilo litambulike kuwa ni eneo moja. Aidha, waliomba kuongezewa muda wa kujiandaa (grace period) lakini Idara hii haikuwajibu, hata hivyo, wamachukulia kuwa Idara imelikubali ombi lao hilo kwa kuwa ukimya unaashiria kuwa umekubali 'silence means yes'. Pia, wameomba kuongezewa muda huo kutokana na kushuka kwa uchumi katika nchi za Ulaya jambo ambalo limeathiri dunia kwa ujumla. Sambamba na hayo, wameendeleza ujenzi katika Hoteli yao ya Karafuu na Spa kitendo ambacho kimewagharimu pesa nyingi sana. Wameiomba Kamati hii iwavumilie na hasa ikizingatiwa kuwa tayari wameshapata fedha kutoka Italia, hivyo, wanatarajia kuanza ujenzi mwishoni mwa Januari, 2014.	August 2014, ikawa haijaanza ujenzi, Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi kuchukua hatua za kuirejesha Serikalini ardhi hiyo ili iweze kutumiwa kwa matumizi mengine ya Serikali.
3.	Mswakini Limited	Pamoja na muda mrefu wa kutoendeleza kwake, hivi sasa tayari ameshaanza ujenzi wa hoteli hiyo iliyopo Michamvi.	Ujenzi unaoendelea uharakishwe ili uweze kukamilika na kuleta tija iliyokusudiwa.
4.	Raja Real Estate Dev. Co. Ltd	Kukosekana na kwa huduma muhimu kama vile umeme wa uhakika, barabara n.k. Hivyo, wanaiomba Serikali kuyatatua matatizo hayo ili waendelee na shughuli walizotarajia kuzianzisha.	Kamati inaishauri Serikali kumvumilia mwekezaji huyu kwa muda wa miezi sita na kama hakutakua na maendeleo yoyote, Kamati inaitaka Serikali

		Aidha, wanaomba kuongezewa muda zaidi na wanaahidi kuwa ndani ya miezi 24 watakamilisha ujenzi huo	iirejeshe ardhi hiyo Serikalini kwa matumizi mengine ya Serikali.
5.	Opulent Zanzibar Ltd	Wanamiliki miradi mingi, hivyo, wameipa kipaumbele miradi hiyo kwanza na baada ya kumaliza ujenzi huo wataanza kujenga katika eneo hilo la Pongwe. Kwa kuwa wao ni wawekezaji makini, na kwa kuwa wanashirikiana na wananchi wa Zanzibar katika shughuli mbali mbali za kijamii kama vile kujenga misikiti, kusambaza umeme wa jua n.k na kwa kuwa hawana deni katika ardhi hiyo, hivyo, wanaiomba Kamati kuwapa miezi 24 zaidi.	Kamati inaishauri Serikali kumvumilia mwekezaji huyu kwa muda wa miezi sita. Iwapo hakutakua na maendeleo yoyote, Kamati inaitaka Serikali kuichukulia hatua ardhi hiyo kwa kuirudisha Serikalini kwa matumizi mengine.
6.	Island Petroleum Group	Kutokuwepo kwa miundo mbinu muhimu katika eneo hilo kama barabara ya uhakika, umeme wa kutosha pamoja na huduma nyengine muhimu mbazo wanategemea Serikali itawasaidia. Hivyo, wanaomba kupatiwa muda zaidi kwani mikakati ya kuendeleza eneo hilo inaendelea vyema na wanatarajia kukamilisha mradi huo.	Kamati inaishauri Serikali kumvumilia mwekezaji huyu kwa muda wa miezi sita. Iwapo hakutakua na maendeleo yoyote, Kamati inaitaka Serikali kuichukulia hatua ardhi hiyo kwa kuirudisha Serikalini na kumtafuta mwekezaji mwengine kwa kufuata misingi ya sheria.
7.	Said Salim Bakhresa	Wanaomba kupatiwa muda zaidi kwani mikakati ya kuendeleza eneo hilo inaendelea vyema na wanatarajia kuanza ujenzi mwaka 2014.	Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi kumvumilia mwekezaji huyu kwa muda wa miezi sita tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii, ili aanze kuiendeleza ardhi hiyo. Na kama hakutakua na maendeleo yoyote, Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi kuichukulia hatua ardhi hiyo kwa kuirudisha

			Serikalini na kumtafuta mwekezaji mwengine kwa kufuata misingi ya sheria.
8.	ZAS VILLA INVESTMENTS	Wameendeleza eneo hilo kwa kujenga ukuta, misingi ya vyumba saba na kazi zinaendelea na wanatarajia kufungua mradi huu katika awamu ya kwanza katika mwezi wa Disemba, 2014. Hivyo, wanaomba kupatiwa muda zaidi ili kukamilisha mradi huo.	Kamati inaishauri Serikali kumvumilia mwekezaji huyu na itakapofika Julai, 2014, Wizara ya Ardhi ifike katika eneo linalohusika na ijiridhishe maendeleo yaliyofikiwa. Na kama hakutakuwa na maendeleo yoyote, Kamati inaitaka Wizara ichukue hatua za kuifuta ardhi hiyo ili irudi Serikalini kwa matumizi mengine.
9.	Ramadhan Nyonje Pandu	Ameshaendeleza kwa kujenga hoteli ijulikanayo kuwa ni Ras Shungi	Kamati inaitaka Serikali kutolifuta eneo hilo kwa sababu tayari limeshaendelezwa.
10.	Salum Taufiq	Alipewa mwekezaji mwengine (Kwetu Matemwe Ltd) mwaka 2012, hata hivyo, hati hiyo imeshafutwa kutokana na mzozo uliojitokeza. Mwanzoni mwa mwaka 2013 aliomba ruhusa ya kujenga kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kati, isipokuwa, kwamba tarehe 18 Machi, 2013 alipokea barua kutoka kwa Sheha wa Shehia ya Pongwe inayomjulisha kuwa ardhi hiyo imerejeshwa kwenye shehia yake. Kutokana na kauli hiyo ya Sheha tarehe 27 Novemba, 2013 Ndg. Salum aliwasilisha malalamiko yake kwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na hivi sasa anasubiri maamuzi ya Wizara.	Kwa kuwa ardhi hii alipewa tokea mwaka 2004, Kamati hii inahisi bado majibu yaliyotolewa hayaridhishi. Hii ni kutokana na kuwa kifungu cha 60 cha Sheria Namba 12/1992 kinaeleza kwamba ardhi hiyo ilitakiwa iendelezwe ndani ya miaka miwili na kinyume na hapo ardhi hiyo itakuwa imetelekezwa na Mhe. Waziri ana mamlaka ya kuchukua hatua nyengine. Hivyo, Kamati inamshauri Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kumpa muda wa

			miezi sita mhusika wa ardhi hii na utakapomalizika, huku Ndg. Salum akishindwa kuiendeleza, hatua ya kuirejesha Serikalini zichukuliwe.
11.	Neptune Hotel (Zanzibar) Ltd	Muwekezaji pamoja na Ndg. Mahmoud Idd Juma katika mwaka 2007 wamefunguliwa kesi ya madai mahkamani na Ndg. Amour Ali Makame na wenzake watano kuhusu ulipwaji wa fidia. Kutokana na mazingira hayo wameshindwa kuendeleza ardhi hiyo ingawa hakuna amri ya zuio (Injuction Order) kutoka Mahkamani.	Kwa kuwa mwekezaji huyu anaendelea kulipa kodi huku akishindwa kujua hatma ya kesi hiyo na kupelekea kushindwa kuiendeleza, Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kuangalia uwezekano wa kumpunguzia kwa kiasi kikubwa mzigo wa kodi, huku Kamati ikishauri Mahakama iharakishe kumalizika kwa kesi hiyo.
12.	Marasa Holdings Zanzibar Ltd	Kushuka kwa uchumi, hata hivyo, mnamo mwezi wa Juni 2013 wameanza ujenzi na wanatarajia kumaliza baada ya miezi 24. Kwa msingi huo, wanaomba waongezewe huo.	Kamati haikukubaliana na sababu hiyo hasa ikizingatiwa kuwa uchumi uliimarika duniani mnamo mwaka 2010. Hivyo, inawataka wakamilishe ujenzi huo ndani ya miezi sita ili ipatikane tija iliyokusudiwa.
13.	Reef View/Sea Sport Centre	Wawekezaji ni wenyeji ambao walishindwa kuendeleza ardhi hiyo na hatimae walitafuta mshirika ‘partner’ ingawa baadae walishindwa kuelewana na kuwafungulia kesi mahkamani ili warejeshewe wenyewe ardhi yao.	Kamati iliwasisitiza kuchukua juhudi zozote ili kuliendeleza eneo hilo kabla hatua za ufutwaji hazijachuliwa dhidi yao. Aidha, Kamati inaishauri mahakama kuharakisha umalizaji wa kesi inayowakabili wawekezaji hawa, ili wajue hatima ya matumizi ya ardhi

			waliyopewa.
14.	Milele Limited	Kutokana na kushuka kwa uchumi duniani Kampuni hii ilishindwa kuendeleza ardhi hiyo. Hii ni kutokana na kuwa mradi unaotarajiwa kutekelezwa hapo ni mkubwa hivyo, Kamapuni pekee haitoweza kuendeleza eneo hilo, na ni lazima ipate mkopo kutoka taasisi za fedha. Pamoja na hayo, mnamo mwaka 2007 waliaza kujenga ukuta na kuchimba kisima. Aidha, waliihakikishia Kamati kuwa Kampuni hii haidaiwi deni lolote. Kwa sababu hizo wanaomba kuongezewa muda zaidi na wanatarajia kukamilisha ujenzi wao ndani miezi 36.	Pamoja na majibu na sababu zao, Kamati inawapa miezi sita kukamilisha ujenzi huo. Vyenginevyo Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati isimamie hatua za kuirudisha Serikalini ardhi hiyo kwa matumizi mengine.
15.	UNICOM RESORT LTD	Wamejenga takriban asilimia themanini (80%) na waliwasilisha picha ikiwa ni ushahidi wa kauli yake hiyo. Isipokuwa kwamba Mhandisi wa mradi huo amefilisika wakati ameshalipwa fedha zote na muwekezaji ujenzi huo umesita tangu mwezi wa Juni, 2013.	Kamati inahitaji kufanya ziara katika eneo hili na imewataka wamalizie ujenzi huo ndani ya mwaka mmoja. Aidha, kushindwa kumalizika kwa ujenzi kwa muda huo, Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi kuchukua hatua za kuirudisha ardhi hiyo Serikalini.
16.	Samira, Thauria na Zeinab Hassan Diria	Wameshaendeleza kwa kujenga nyumba/mabanda, kwa bahati walivamiwa na wezi na kupelekea zoezi hilo kusimama.	Kamati inaishauri Wizara kuwavumilia kwa muda wa miezi sita tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii kwa lengo la kuiendeleza ardhi hiyo. Iwapo muda huo utamalizika bila ya kuendelezwa, Kamati inaitaka Wizara

			kuchukua hatua za kuirudisha ardhi hiyo Serikalini.
17.	Vuai Ali Vuai	Ni mzaliwa wa eneo hilo (Pongwe) na alikuwa anamiliki shamba la mivinje kwenye miaka ya 1980. Mnamo mwaka 2004/2005 aliimngia ubia na mwekezaji kwa ajili ya kujenga hoteli na ndipo alipolazimika kutafuta lease. Alibaini kuwa mwekezaji huyo kumbe alikuwa anataka apewe ardhi ile na yeye hakuwa tayari. Kwa kuwa wawekezaji wengi hawataki kuingia ubia na kwa kuwa Ndg. Vuai hana uwezo wa kujenga hoteli ameamua kupokea fidia endapo atatokea mwekezaji ili amwachie ardhi ile. Isipokuwa kwamba baada ya kupata ushauri kwa watu mbali mbali ameamua kuomba haki ya kawaida ya matumizi kwa kuwa yeye ni mzalendo. Aidha, amekiri kuwa hajalipa kodi ya ardhi tokea mwaka 2010 kutokana na sababu za kifamilia.	Kamati inaishauri Serikali kumvumilia mwekezaji huyu kwa muda wa mwaka mmoja. Iwapo hakutakua na maendeleo yoyote, Kamati inaitaka Serikali kuichukulia hatua ardhi hiyo kwa kuirudisha Serikalini na kumtafuta mwekezaji mwengine kwa kufuata misingi ya sheria.
18.	Hamad Masoud Hamad	Ameshaliendeleza eneo hilo kwa kufanya yafuatayo;- i. Kujenga uzio (ukuta wa mawe wenye urefu wa mita 2 na mzunguko wa mita 287). ii. Kupeleka maji safi. iii. Kupeleka umeme (3 phase). iv. Kujenga villa moja v. Kujenga uzio wa magogo ya miti. Yupo kwenye mpango wa kuendeleza eneo hilo	Pamoja na majibu hayo, Kamati inapendekeza kupewa muda wa mwaka mmoja kumaliza maendeleo ya eneo hilo na kushindwa kufanya hivyo, ardhi hiyo ichukuliwe hatua za kurudishwa Serikalini.
19	Nungwi Dreams Resort Ltd	Wameeleza kuwa ardhi hiyo hawajaitelekeza kwa sababu wameshajenga jengo la walinzi ambao wanalinda na wenyewe wanafuatilia kwa karibu kuona	Kamati haijakubaliana na hoja zilizowasilishwa na mwekezaji. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi kumvumilia

		usalama na ardhi hiyo. Hata hivyo, kutoiendeleza ardhi hiyo kwa muda mrefu kumetokana na kushuka kwa uchumi ulimwenguni, isipokuwa kwamba wanataraji kujenga hoteli hiyo miezi ya karibuni.	mwekezaji huyo kwa muda wa miezi sita tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii, na iwapo itamaliza muda huo bila ya kuendelezwa, Wizara hii ichukue hatua ya kuirejesha ardhi hiyo Serikalini.
20	Aman I. Makungu na Mahmoud Th. Kombo	Ardhi hiyo wamerithi na baadae walikwenda kuisajili na tayari wameshapata hati ya umiliki wa ardhi. Sababu kubwa ya kutoiendeleza ni uwezo mdogo wa wamiliki hawa.	Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi kuwavumilia wamiliki hawa kwa muda wa miezi sita tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii. Iwapo muda huo utamalizika bila ya kuendelezwa, Kamati inaitaka Wizara kuchukua hatua za kisheria za kuirudisha ardhi hiyo Serikalini.
21	Zanzibar Investment Group	Muwakilishi alieyefika mbele ya Kamati hakua msemaji wa Kampuni hii na Kamati imehitaji kukutana na mmiliki mwenyewe aua majibu yake mwenyewe ya maandishi. Hata hivyo, majibu hayo hayajapatikana.	Kamati inashauri Wizara kuwavumilia kwa miezi sita tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii na iwapo mwekezaji huyo hatoanza maendeleo ya mradi huo, Kamati inaitaka Wizara kuichukulia hatua za kuirudisha ardhi hiyo Serikalini.

Maeneo ambayo hayajaendelezwa hadi sasa na wamiliki/ wakodishwaji wake wameitwa na Kamati lakini hawakuhudhuria na wala hawajajibu kwa maandishi kueleza sababu zao za kutoiendeleza ardhi waliyopewa:

SN	**JINA LA MRADI/MMILIKI**	**AINA YA HATI MILIKI NA MWAKA ILIYOTOLEWA**
1.	Ahmed Aman Karume	R/O NO. Z.98/2007
2.	Mohammed Salum Juma	D P NO. 690/2005

3.	Nakupenda Resort	D P NO. 808/2007
4.	SK Investment Ltd	DP NO. 900/2005
5.	Mhe. Dr. Hussein Mwinyi (Dharura)	R/O NO. Z.94/2007
6.	Aficano Beach Resorts	D P NO. 938/2008
7.	Zanzi Investment Ltd	D P NO. 920/2008
8.	Spice Beach Resort	D P NO. 861/2007
9.	Abeid Amani Abeid Karume	R/ O NO./Z.628/2007
10.	Abdalla Mohammed Ali	R/O NO/Z.151/2008
11.	Fatma Aman Karume	R/O NO/Z.636/2008 na R/O NO./Z.09/2012
12.	Shumbana Amani Karume	R/O NO/Z.827/2006
13.	Hasnain Fida Hussein Remtulla	D P NO. 896/2008
14.	Abdalla Salum Hassan and Tawfiq Salum Hassan	D P NO. 225/2000
15.	Hafidh Seif Magid	D P NO. 496/2002
16.	Landmark Hotel	D P NO. 866/2007
17.	Zanzibar Masai Resorts	D P NO. 832/2007
18.	Sunset Resident Hotel (SPA)	D P NO. 892/2008
19.	Sobha Group	D P NO. 828/2007
20.	Zanzibar Resorts and Hotel Ltd.	D P. NO. 931/2008
21.	Reliance Resort and SPA ltd	D P NO. 858/2007
22.	Hassan Haji Ame	R/O NO/Z.224/2007
23.	Mayur Madhvani	D P NO. 220/1995
24.	Mr. Abdalla Saleh Mohammed A-Mutawaa	D P NO.935/2008
25.	Omar Khamis Haji	R/O NO/Z.114/2009

26.	Shungi Bangallows C. Ltd	D P NO. 1096/2011
27.	Mwita Abdu Mwita	R/O NO/AG./Z.92/2010
28.	Abeid Aman Karume	R/O NO/Z.40/2007 na R/O NO/Z.336/2007
29.	Balladin Ltd	D P NO.1161/2012

Maeneo ambayo hayajaendelezwa hadi sasa, lakini kutokana na ukosefu wa wakati, Kamati imeshindwa kuwaita na kufanya mahojiano nao.

SN	**JINA LA MRADI/MMILIKI**	**AINA YA HATI MILIKI NA MWAKA ILIYOTOLEWA**
1.	Hassnein Hussein Virjee	R/O NO. Z.749/2004
2.	Karume Family	R/O NO. Z.625/2005
3.	Abdullsawad Said Ahmed	R/O NO. Z.196/2010
4.	Salum M. Mbarak and Nahaat M. Mahfoudh	R/O NO. Z.132/2010
5.	Salum Mohammed Mbarak	R/O NO. Z.194/2010
6.	Aden Patners Ltd	R/O NO. Z.135/2010
7.	Ahaad Abeid Miskry	R/O NO. Z.722/2008
8.	Ali Salum Ali	R/O NO. Z.428/2005 na R/O NO.Z.429/2009 na eneo la Muyuni Kigomani ambalo halina hati ya Ardhi.
9.	Omar Mohammad Ali na Fatma Aman Karume	R/O NO. Z.150/2008
10.	Salma Ibrahim Mohammed	R/O NO. Z.294/2010
11.	Hemed Nassor Mohammed	Eneo lipo Kigomani ambalo Hakuna Hati ya Ardhi
12.	Beach Hotel Holiday	D P NO. 1164/2012
13.	Kisiwa Developers	D P NO. 855/2007

14.	Mohammed Hashim Ismail	Eneo lipo Pwani Mchangani Ndogo ambalo hakuna hati ya ardhi na eneo lina mgogoro.
15.	Pandu Kheir Makame	R/O NO. Z.204/2004
16.	Wanakijiji	Eneo lipo Kumbaurembo ambalo kalina hati ya ardhi (Public Beach)
17.	Mama Siti Abdalla Ali	R/O NO. Z.1191/2003
18.	Haroub Shaib Mussa	R/O NO. Z.1005/2009
19.	Saad Abubakar Abdi	R/O NO. Z.1671/2003
20.	Bumbwini Sea View	D P NO.736/2005
21	Eneo la Wazi Agakhan (Mangapwani)	Lease imefutwa na imerejeshwa Serikalini
22.	Ronit Heskovitz	Eneo lipo Mangapwani, limefutwa na kurejeshwa Serikalini
23.	Mohammed Omar	Eneo lipo Pongwe, hakuna hati ya ardhi.
24.	Ilham Mohammed Said	D P NO. 954/2008
25.	Eneo la Kanisa	Eneo lipo Pongwe, hakuna hati ya ardhi
26.	Maeneo mawili yapo Pongwe, wamiliki hawajapatikana	Hakuna hati za ardhi.
27.	Michamvi Rahisi Village	D P NO. 898/2008
28	Hassan Ahmed Hamid	D P NO. 897/2008
29.	Ali Salum Said	R/O NO. Z.1015/2008
30.	Ali Miraji Suleiman	R/O NO. Z.81/2007
31.	Rashid Omar Ghassany	R/O NO. Z.329/2005
32.	Haji Ameir Haji	R/O NO. Z.374/2005
33.	Lilian	Sale Deed

34.	Majina ya hati ya umiliki wa ardhi hayakupatikana	Eneo liko Michamvi, na hakuna hati ya ardhi.
35.	Gulam Hussein Somji	Sale Deed
36.	Bwejuu Beach Resorts	D P NO.877/2007
37.	Palm Beach Inn	D P NO. 424/2000
38.	Jina la Mmiliki halijapatikana	Eneo lipo Paje, halina hati ya ardhi.
39.	Kivinjeni Bangallow	D P NO.995/2009
40.	Simai Haji Simai na Vuai Makame Vuai	R/O NO. Z.89/2012
41.	Muzdalifat Mohammed Ali	R/O NO. Z.263/2007
42.	Majina ya wamiliki hayakupatikana	Eneo lipo Jambiani, hakuna hati ya ardhi.
43.	The Adress Ltd	D P NO. 1171/2012 kuna kesi Mahakamani
44.	Coconut Resots and Villas Ltd	D P NO. 1172//2012 kuna kesi Mahakamani
45.	Diko (Eneo la Wazi)	Lipo Nungwi kwa kujengwa Diko
46.	Aman Abeid Karume	D P NO. 806/2007

Mapendekezo ya Kamati

- Kwa maeneo yote ambayo yameorodheshwa katika orodha ya maeneo ambayo hayajaendelezwa, huku yakiwa hayajaitwa na Kamati, kwamba Kamati ipate muda wa zaidi ili kuwasiliana na wamiliki wa maeneo haya, ili kufahamu sababu zilizowapelekea kushindwa kuyaendeleza.
- Kuhusiana na orodha hiyo ya maeneo 119, Kamati inaitaka Serikali kufanya uhakiki upya na kufahamu kwa kina sababu zinazowapeleka wamiliki wa maeneo hayo kushindwa kuyaendelea, kabla ya kuchukua hatua za kuyafuta (termination).
- Idara ya Ardhi na Usajili iendelee kutoa taaluma kwa wananchi kuhusiana na masuala ya ardhi.

- Nambari za usajili wa ardhi zitolewe mwaka ambao kodi ya ardhi imetolewa na sio kabla ya hapo ili kuwe na uwiano wa taarifa hata kama eneo hilo lilifanyiwa utafiti siku nyingi zilizopita au hata kama eneo hilo alipewa muwekezaji hapo kabla na kufutiwa.

MPAPINDI HOLIDAY AND DIVING COMPANY:

Kampuni hii haikuwemo katika orodha ya wawekezaji 119 ambao hawajaendeleza kwani Kampuni hii inahusika na ardhi iliyopo Pemba, ambako kama tulivyoeleza awali, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia Idara ya Nyumba na Usajili, bado haijafuatilia ardhi ya Pemba. Hata hivyo, Kamati ilipokea taarifa ya uwepo wa kampuni hii Pemba, inayohitaji kufuatiliwa na Kamati na ikishauriwa kuwa ni vyema ikatembelea eneo hilo na kuweza kushuhudia maendeleo yaliyokusudiwa namna yalivyokuwa hayajafikiwa hadi leo.

Wakati Kamati ilipokuwa inafuatilia hoja za ardhi-Pemba, ilipata nafasi ya kuitembelea Kampuni hiyo na kugundua mambo yafuatayo:

Ukodishwaji wa ardhi kwa Kampuni ya Mpapindi:

Kamati imegundua kuwa, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati iliikodisha Kampuni hii ardhi tokea mwaka 2004 kwa lengo la ujenzi wa hoteli ya kitalii. Hata hivyo, hadi hii leo, hakuna maendeleo ya ujenzi huo. Jumla ya sq mitres 46158, hekta 4.6 za ukubwa wa ardhi imetolewa kwa Kampuni hii lakini miaka 10 sasa, hakuna maendeleo yaliyokusudiwa.

Kamati ilielezwa na wamiliki wa kampuni hiyo kwamba, wao walikusudia kuendeleza ardhi hiyo kwa ujenzi wa eco lodge, yaani ni aina ya mradi utakaotoa huduma ya kitalii lakini kwa kuendana na mazingira halisi ya msitu uliopo hapo. Wao walikuwa na udhati wa kuiendeleza ardhi hiyo kama walivyokusudia, lakini walitatizwa na ukosefu wa fedha na hatimae wakawa karibu kuwasiliana na Mamlaka ya Vitega Uchumi, Zanzibar (ZIPA) ili iwashauri nini cha kufanya. Walikuwa wanapeleka ripoti zao za kila robo mwaka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo na hatimae ZIPA waliwashauri kutafuta mshirika (patner) na wao walifanya hivyo kwa kutoa hisa ya asilimia sitini (60%), lakini wamepata tatizo la patner huyo kuwa tapeli, hali iliyowalazimisha kufungua kesi Mahakamani kwa ajili ya kutatua tatizo hilo kwanza kabla ya kuliendeleza. Hivi sasa kesi yao iko Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, ambapo itasikilizwa ama Aprili, 2014 (Dar es Salaam) au Disemba, 2014 hapa Zanzibar.

Kwa ufupi, wao wana nia ya kuiendeleza ardhi hiyo na hivi sasa wanaomba uraia wa Tanzania, kwani wameshakaa kwa miaka zaidi ya 10 na iwapo kesi hiyo itamalizika kwa maslahi yao, basi wamekusudia kubadilisha mradi kama vile ambavyo tayari wameshaanzisha taratibu za kufungua kampuni nyengine itakayojishughulisha na uvuvi wa bahari kuu.

Uchunguzi zaidi wa Kamati:

Kampuni hii inaitwa Mpapindi Holiday & Diving Company huku jina la biashara ni Mpapindi Beach Resort. Aidha, Kamati imegundua kuwa, wamiliki wa kampuni hii ambao ni Ndg. Marek

Antony Kroyga na Ndg. Iwona Anna Klorgya, wenye kutumia anuani S.L.P 211, Chake Chake - Pemba, ni raia wa Afrika ya Kusini wenye asili ya Poland. Wamiliki hawa walianza na Kampuni ya BESKID International Import and Export, mnamo mwaka 2001 huko Afrika ya Kusini, huku Ndg. Marek akiwa ni Veteran na mkewe Ndg. Iwona ni Mhasibu 'Accountant', kazi yao kubwa ni kusambaza vifaa vya ofisi na mtaji wa kampuni yao ilikuwa ni Rand milioni 1.03 na mtaji wa biashara ni Rand milioni 3.125.

Kampuni hii ilipoanzishwa hapa Zanzibar kwa jina hilo la Mpapindi Holiday & Diving Company, ilikusudia kuanzisha ujenzi wa vyumba vya tents (nyumba za kutumia maturubali) 70, lakini waliruhusiwa na Serikali kujenga vyumba 50, tokea kupewa idhini hiyo mwaka 2004 hadi leo hawajajenga isipokuwa tents mbili ambazo ndizo wanazozitumia wao kuishi katika eneo hilo liliopo Makangale - Pemba.

Kampuni hii ambayo kwa mujibu wa usajili wao katika Afisi ya Mrajis ilikuwa inamilikiwa na watu hao wawili Ndg. Marek na mkewe Ndg. Iwona, baadae waliuza hisa zao za asilimia sitini (60%) kwa Ndg. Raymond Campion Vincent, uhaulishaji huo ni wa kienyeji ambao unafahamika na Mamlaka ya Vitega Uchumi (ZIPA) pekee chini ya usimamizi wa Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo Ndg. Salum Nassor, huku Ndg. Marek na mkewe wakibaki na asilimia ishirini (20%) kwa kila mmoja.

Aidha, Kamati imegundua kuwa, Kampuni hiyo haijasajiliwa katika Kamisheni ya Utalii na haina hata cheti cha kufanyia biashara tokea mwaka 2004 hadi leo, na kwa upande wa ZIPA, imepewa Cheti cha Muda (Interim Certificate), tokea mwaka 2004 na kamwe Kampuni hiyo haijapewa utambulisho mwengine zaidi ya huo.

Vile vile, kwa upande wa Mrajis wa Makampuni, Kampuni hii haijawahi kufanya marejesho ya taarifa zake za mwaka (annual returns) tokea kuanzishwa kwake 2004 na Afisi ya Mrajis wa Makampuni haina taarifa zozote za uhai wa Kampuni hii.

Sambamba na hilo, Kamati imegundua kutokana na maelezo aliyoyatoa Ndg. Iwona Anna Kloryga, kwamba wao wanatoa ripoti kwa kila robo mwaka na Mkurugenzi wa ZIPA (Ndg. Salum Nassor) huwa anafika kwao tena kibinafsi mara kwa mara na wanamueleza matatizo yao. Kitendo hiki kimeipa mashaka makubwa Kamati juu ya kuwepo kwa dalili za rushwa na hatimae Mkurugenzi huyu anashiriki kuficha maovu ya wawekezaji hawa.

Aidha, Kamati imegundua kutokana na kushindwa kuridhika na hali halisi ya mradi huu, kwamba, Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA aliithibitishia Kamati kwamba, miradi ya aina hii iko mingi na inafika 100 katika kumbu kumbu za Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar. Hali hii kwa vyovyote vile inatoa picha mbaya na kuna haja kubwa ya kufuatiliwa kwa kina miradi ya aina hiyo ambayo haitekelezwi kama ilivyokusudiwa.

Ulipaji wa Kodi ya ardhi:

Pamoja na kupewa ardhi hiyo tokea mwaka 2004, Kamati imegundua kuwa, hakuna hata mwaka mmoja kampuni hii iliwahi kulipa kodi. Kamati imefanya mahojiano na watendaji wa taasisi ya ukusanyi wa kodi (ZRB) kwa upande wa Pemba, ambao nao walikuwa pamoja na Kamati na kuthibitisha kwamba, hakuna hata mwaka mmoja ambapo Kampuni ya Mpapindi imelipia kodi ya ardhi. Kamati imethibitishiwa na watendaji wakuu wa ZRB Pemba, kwamba, walifuatilia kulipwa kwa kodi hiyo na walikaa na mwekezaji kwa muda mrefu lakini hakuna kodi yoyote iliyolipwa zaidi ya kuelezwa kuwa wana kesi Mahakamani na wasubiri imalize ndipo waweze kulipa kodi hiyo.

Kamati imeitaka ZRB kutayarisha orodha ya kodi inayodaiwa kwa mwekezaji huyu kutoka mwaka 2004 pamoja na adhabu ya faini ya asilimia kumi (10%). Orodha hiyo ni hii ifuatayo:

MWAKA	**KODI YA MWAKA (USD)**	**ADHABU (USD)**	**JUMLA (USD)**	**KODI ILIYOLIPWA (USD)**	**BAKAA (BALANCE)(USD)**
2006	9,230.00	78,455.00	87,685.00	NIL	87,685.00
2007	9,230.00	67,379.00	76,609.00	NIL	76,609.00
2008	9,230.00	56,303.00	65,533.00	NIL	65,533.00
2009	9,230.00	45,227.00	54,457.00	NIL	54,457.00
2010	9,230.00	34,151.00	43,381.00	NIL	43,381.00
2011	9,230.00	23,075.00	32,305.00	NIL	32,305.00
2012	9,230.00	11,999.00	21,229.00	NIL	21,229.00
2013	9,230.00	923.00	10,153.00	NIL	10,153.00
JUMLA	**73,840.00**	**317,512.00**	**391,352.00**	**NIL**	**391,352.00**

Kwa ujumla deni la kodi ya ardhi kwa Kampuni ya Mpapindi ni USD 391,352.00 ambapo Kamati inasisitiza ni deni halali na linapaswa kulipwa. Aidha, msimamo huu ni sawa na wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati uliofanywa na Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Usajili Ndg. Salum O. Simba kupitia barua yake ya tarehe 21/06/2010 yenye kumbu kumbu namba AU/UMM/MUN/K.70/30 VOL.XX/8 ambapo katika barua hii aliyomuandikia mmiliki wa Kampuni hii kumjibu kuwa anawajibu wa kulipia kodi ya ardhi kupitia ZRB ambae ni wakala wa Wizara hii, bila ya kujali kuwa wana kesi Mahakamani, maelezo hayo tuliyoyatafsiri kwa lugha ya Kiswahili, tunayanukuu kwa ufupi wake kama ifuatavyo:

"Afisi hii inakupa taarifa kwamba, Bodi ya Mapato ya Zanzibar imepewa jukumu rasmi la kukusanya kodi ya ardhi hapa Zanzibar. Kwa hali hiyo, wakodishwaji wote wa ardhi, ikiwa ni pamoja na kampuni yako (ya Mpapindi Holiday and Diving Company), lazima mheshimu mahitaji yote ya ZRB. Katika taratibu za kukusanya kodi, ZRB itatumia taratibu kisheria za kukusanya kodi ikiwa ni pamoja na kutoza adhabu ya faini, itakayopelekea kodi hiyo kuongezeka.

Kuhusiana na Kampuni kuwa na kesi Mahakamani, kwa mujibu wa Mkataba wa Kodi uliousaini (baina ya Kampuni yako ya Mpapindi na Serikali), tatizo hili halihusiani na wajibu wako wa kulipa kodi ya ardhi, na kwa hivyo, hiyo isiwe sababu ya kusameheka kulipa kodi ama kucheleweshe kodi hiyo".

Kuongezwa kwa kipindi cha ujenzi (Grace period) na kusamehewa kulipa kodi:

Kamati ilielezwa na wamiliki wa Kampuni ya Mpapindi na kama vile ilivyoelezwa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar, kwamba wamiliki hao walisamehewa kulipa kodi ya ardhi, kwani ilipofika mwaka 2008, waliomba grace period kwa Mhe. Waziri wa Ardhi ambae aliwakubalia na hivyo wamesamehewa kulipa kodi kabisa.

Kamati ilihitaji kupewa ushahidi wa maelezo ya kuombwa na kupewa grace period. Hata hivyo, mpaka tunaandika ripoti hii hakuna ushahidi wowote uliowasilishwa kwa Kamati na ni sawa na kusema kwamba, Kamati haikubaliani na maelezo hayo. Aidha, Kamati imeshitushwa na kauli kwamba, Waziri amemsamehe kodi mwekezaji huyu kupitia grace period, ambapo kwa mujibu wa sheria ya Ardhi namba 12 ya mwaka 1992, mamlaka hayo hajapewa kisheria isipokuwa kwa kutumia kifungu cha 47(5) cha sheria hiyo, Waziri amepewa mamlaka ya kupunguza kiwango cha kodi iwapo kufanya hivyo kuna maslahi ya taifa na kuna ushahidi wa wazi na unaohitaji kuangaliwa.

Maendeleo ya mradi na baadhi ya shughuli zinazofanyika:

Kamati ilipomhoji mmiliki wa mradi huyo kuhusiana na maendeleo waliyoyafanya na malengo ya mradi alieleza kuwa wamejenga vibanda viwili vitatu, ujenzi wa tent ambamo ndimo wanamoishi wao, sehemu ya mbwa kwa ulinzi wao na sehemu nyengine ndogo ndogo. Kiujumla, ujenzi huo hauashirii maendeleo yoyote ya ujenzi wa ardhi hiyo kwa mnasaba wa malengo ya kodi husika.

Aidha, Kamati imeshudia kumilikiwa kwa boti kubwa, ulinzi mkubwa wa mbwa na maisha ya msituni kutokana na misitu asili ya eneo hilo, hali ambayo kwa mwananchi wa kawaida, hasa kwa wamiliki wa kampuni hii wasio na vibali vya kazi na walioshindwa kuendeleza mradi huo, huku kwa mujibu wa maelezo yao wakibaki omba omba na wanaohitaji msaada wa wasamaria wema, kama Kamati ilivyoelezwa na wawekezaji hao, Hali hii inaifanya Kamati kuwa na masuala mengi na maisha halisi ya wamiliki hawa.

Ruhusa ya Kuishi nchini na kibali cha kufanya kazi:

Tarehe 09/01/2014, Kamati iliwaita pamoja Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar aliewakilishwa na Ndg. Nassra J. Mohammed na Kamishna wa Kazi, Ndg. Kubingwa Simba kupata ufafanuzi wa ruhusa ya kuishi nchini na ridhaa ya kufanya kazi kwa wamiliki wa kampuni ya Mpapindi.

Kuhusiana na ruhusa ya kuishi nchini, mwakilishi wa Uhamiaji aliieleza Kamati kwamba, wawekezaji hawa tokea mwaka 2000 walifika nchini, wapo kihalali na wamekuwa wakifanya mapitio 'review' kila mwaka unapofika na kuomba ruhusa mpya 'permit' ya miaka mitatu mitatu, na mwaka wa mwisho walioomba permit hiyo tarehe 6/6/2012 na mwaka wa mwisho wa kumalizika kwa ruhusa hiyo ni mwaka 2015 na wanaruhusa ya Daraja 'A'.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati imeshangazwa na kitendo cha Afisi ya Uhamiaji kutoa ruhusa ya kuishi (permit), Daraja 'A', wakati wawekezaji hao hawana kazi yoyote wanayoifanya na wameieleza Kamati kwamba, wanategemea misaada kutoka kwa wahisani mbali mbali tena waliopo nchini.

Ama kwa upande wa Kamisheni ya Kazi, Kamishna wa kazi aliieleza Kamati kwamba, wao wamewanyima kibali cha kazi wawekezaji hawa tokea mwaka 2007 kutokana na kutokuwa na mradi wowote wanaouendeleza, kwa mnasaba huo, wawekezaji hawa hawana kibali cha kufanya kazi nchini.

Mapendekezo ya Kamati:

- Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuirejesha ardhi hiyo Serikalini kwa vile imeshindwa kuendelezwa kwa miaka 10 sasa na hailipiwi kodi kinyume na masharti ya Sheria ya Umiliki wa Ardhi na Mkataba wa ukodishwaji.

- Kamati inaitaka ZIPA na Taasisi nyengine zinazohusika kuwachukulia hatua za kuwaondosha nchini Ndg. Marek Antoni Kloryga na Ndg. Iwona Anna Kloryga kwa kuwepo nchini bila ya kufanya kazi. Kwa msingi huo wawekezaji hawa wanaonekana kama ni wazururaji wa kigeni tu.

- Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, kupitia wakala wake ZRB kufuatilia deni wanalodaiwa wamiliki wa kampuni hii kutoka mwaka waliopewa mkataba wa kodi hadi sasa pamoja na adhabu na wahakikishe kuwa deni hilo linalipwa kabla ya kurejeshwa kwao na ikishindikana hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

- Kamati inaitaka ZIPA kukifuta mara moja Cheti cha Muda 'Interim Certificate' walichotoa kwa Kampuni hiyo, kwani ni takriban miaka kumi (10) sasa Kampuni hii haijaweza kuendeleza mradi huo.

- Kamati inamuagiza Mkurugenzi wa Uhamiaji kufuta kibali cha ukaazi kwa Wakurugenzi wa Kampuni hii mara moja kwani ukaazi wao hapa Zanzibar unaonekana ni wa ubabaishaji na sio ule walioumbea wa uwekezaji na kuwachukulia hatua za kisheria.

- Kamati inamshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Zanzibar kuifuatilia miradi 547 iliyoelezwa kuwepo kwenye kumbu kumbu za ZIPA, kuona namna inavyoendeshwa na kama kuna faida kwa Taifa.

- Kamati inazishauri Taasisi za ulinzi na usalama kuchunguza kazi halisi zinazofanywa na wawekezaji hawa wa Mpapindi Holiday and Diving Company na wawekezaji wengine wanaofanana kazi zao na mwekezaji huyu.

KIGOMASHA ECO BEACH:

Kamati katika ziara yake ya tarehe 06 Januari, 2014 alibahatika kufika katika Kampuni ya Kigomasha Eco Beach na kukutana na Mhusika aliachiwa hoteli hiyo ambaye anafanya kazi kwa niaba ya mmiliki wa hoteli. Kwa kuwa mazingira ya hoteli ile yanaonesha kama hoteli hiyo haifanyi kazi zake ipasavyo, Kamati ilitaka kujua baadhi ya mambo ikiwemo historia ya upatikanaji wa ardhi ile, ulipaji wa kodi ya ardhi n.k. Hata hivyo, Kamati ilishindwa kupata majibu ya maswali yake kwa kina kwa kuwa kijana huyo, hafahamu kwa undani masuala hayo. Kutokana na majibu yake hayo Kamati ilimtaka awasiliane na wahusika wa hapo ile apatiwe taarifa hizo pamoja na kuwasilisha nyaraka zinazohusiana na ardhi hiyo siku ya tarehe 07 Januari, 2014 katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Pemba.

Kijana huyo alishindwa kuhudhuria mbele ya Kamati tarehe hiyo na baada ya kuwasiliana naye kwa njia ya simu aliieleza Kamati kuwa alishindwa kupata taarifa alizotakiwa aje nazo mbele ya Kamati kwa kukosa mawasiliano na wamiliki wa hoteli hiyo. Lakini pia, kwa kutokuwa na majibu ya ziada zaidi ya yale aliyoyaeleza kwa Kamati, kwamba, yeye hana vielelezo vyovyote vya uhalali wa ardhi ama ujenzi na hoteli ya Kigomasha Eco Beach.

Hata hivyo, Watendaji wa Idara ya Ardhi na Usajili aliieleza Kamati kuwa ardhi hiyo ilikuwa inamilikiwa na Ndg. Said Abdalla (maarufu Said Mbuzi) na hivi sasa ipo chini ya mwekezaji mwengine. Wakati Hoteli hii ipo chini ya Ndg. Said ilikuwa inajulikana kuwa ni Matango Beach na alikuwa analipa ‘Hoteli levy’ ingawa alikuwa hana mtakaba wa ukodishwaji wa ardhi hiyo. Walizidi kueleza kuwa Muwekeza aliyekuwepo hivi sasa ameanza kulipa mwaka 2011 wakati Hoteli hiyo imeanza kufanya kazi mwaka 2010.

Kamati haikuridhika na majibu hayo hasa ikizingatiwa kuwa Muwekezaji huyu anatumia ardhi ile bila ya mkataba wowote na anamiliki hoteli kubwa yenye uwezo wa kupokea wageni wengi, kitendo ambacho kinaipelekea Serikali kukosa mapato. Kutokana na hilo Kamati ilitaka kufanya mahojiano na Ndg. Said tarehe 10 Januari, 2014 ambaye aliieleza Kamati kama ifuatavyo;-

Maelezo ya Ndg. Said Abdalla (Said Mbuzi)

Ni kweli kwamba yeye ni mmiliki wa eneo hilo la Kigombasha Eco Beach na alifanya maombi ya kukodishwa ardhi ile Idara ya Ardhi na Usajili. Hata hivyo, Idara hiyo haikumpatia mkataba huo wa ukodishwaji. Aidha, alizidi kueleza kwamba katika ardhi ile kuna mgogoro na wanakijiji wa eneo lile, isikupokuwa kwamba, mgogoro huo unachochewa na Muwekezaji mwengine aliyepo pembezoni kwake na kupelekea wanakijiji hao kuziba njia kwa madai kwamba Ndg. Said asiitumie njia ile hadi hapo atakapowalipa fidia wanakijiji hao, jambo ambalo anahisi haliingii akilini kwa kuwa huyo muwekezaji mwengine ndie anayepaswa kulipa fidia ile.

Maelezo ya Idara ya Ardhi na Usajili kuhusiana na hili:

Idara ya Ardhi na Usajili ilikiri kutokumkodisha muwekezaji huyo baada ya Idara hii kugundua kuwa kuna mapungufu katika maombi yake hayo na kumtaka ayachukulie hatua ili akamilishiwe maombi yake hayo. Baadhi ya mambo yaliyokosekana ni pamoja na ‘site plan’. Hadi Idara hii inawasilisha taarifa hii mbele ya Kamati, Muwekezaji huyo hajachukua hatua yoyote.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imegundua kwamba Ndg. Said anatumia ardhi ile kinyume na Sheria za Ardhi zinavyoelekeza. Aidha, Kamati iligundua kuwa Ndg. Said alifanya uhauhaulishaji wa kuikodisha hoteli hiyo kwa mwekezaji mwengine kutoka Afrika ya Kusini, lakini suala hili halifahamiki katika Idara ya Ardhi na Usajili, kama vile lililvyokuwa halitambuliki katika Wizara hii ya Ardhi. Hata hivyo, maelezo yote hayo kwa Kamati yanaashiria zaidi kwamba, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati haifahamu kinachoendelea katika hoteli hiyo, na imeshindwa kufuatilia kwa undani ikafahamu kasoro zilivyo na kuzichukulia hatua.

Mapendekezo ya Kamati

- Kamati inamtaka Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kushirikiana na wakala wake ZRB kwa kukusanya kodi yote inayodaiwa kwa Kampuni hii tokea kuanza kutumia eneo hilo hadi sasa pamoja na adhabu ya asilimia 10 (10%), ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii Barazani, na iwapo kodi hiyo haitolipwa, Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi kuichukulia hatua ardhi ya eneo hilo kwa kuirejesha Serikalini.

- Kamati imemtaka Ndg. Said amalizie hatua alizotakiwa kuchukua na Idara husika ili atumie ardhi ile kama Sheria za Ardhi zinavyoelekeza.

- Kamati inaitaka Idara ya Ardhi na Usajili kufuatilia mgogoro huo kwa karibu zaidi ikiwa ni pamoja na kulipima eneo hilo ili haki itendeke.

MISALI MATUMBAWE

Katika ziara yake ya eneo la Wambaa – Pemba, Kamati hii iligundua pia Ndg. Saidi anamili ardhi katika eneo hilo, ardhi ambayo ameitekeleza kwa muda mrefu bila ya kuchukuliwa hatua za kisheria ingawa Kamati ilipofika iligundua kuwa Ndg. Said ameanza ujenzi hivi karibuni. Kamati ilitaka kujua sababu zilizompeleka Muwekezaji huyo kushindwa kuliendeleza eneo hilo.

Maelezo ya Ndg. Said Abdalla

Ndg. Said alikiri kukodishwa ardhi hiyo ijulikanayo kwa jina la Misali Matumbawe. Kutokana na matatizo yaliyokuwa yanamkabili binafsi pamoja na kutokuwepo miundombinu bora katika eneo lile alishindwa kuiendeleza ardhi hiyo, isipokuwa kwamba alieleza kuwa ardhi ile anailipia kodi kama sheria inavyoelekeza.

Maelezo ya Idara ya Ardhi na Usajili

Idara hii haikukubaliana na maelezo ya Ndg. Said kwa kuwa baada ya Serikali kuona kuwa haikuweka miundo mbinu bora katika eneo lile iliamua kupunguza kodi ya ardhi ili kuwavutia wawekezaji na hatimae kukuza uchumi wa nchi.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kujiridhisha na kauli iliyotolewa na Ndg. Saidi juu ya ulipaji wa kodi, Kamati ilimtaka awasilishe stakabadhi ya malipo yake hayo saa 8:00 mchana kwa kuwa kwa wakati ule hakuwa nayo. Ndg. Said alishindwa kuwasilisha stakabadhi hiyo kama alivyotakiwa na kuomba muda zaidi kwa Kamati, ambapo Kamti ilikubaliana na maombi yake hayo na ilimtaka awasilishe Jumatatu ya tarehe 13 Januari, 2014. Hata hivyo, Ndg. Said alishindwa kuwasilisha stakabadhi hiyo. Kutokana na kitendo hicho Kamati ya PAC imeamini kuwa Ndg. Said hajafanya malipo yoyote.

Mapendekezo ya Kamati

Kwa kuwa Ndg. Said alishindwa kuwasilisha stakabadhi ya malipo inayothibitisha ulipaji wake wa kodi, Kamati inaitaka Bodi ya Mapato Zanzibar kufuatilia hili ili ijue na imtake Ndg. Said kulipa deni lake kama lipo sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kuwasilishwa ripoti hii mbele ya Baraza la Wawakilishi pamoja na adhabu ya asilimia kumi (10%). Na kama deni hilo halitolipwa, Kamati inapendekeza hatua za kisheria zichukuliwe kwa ardhi hiyo kurejeshwa Serikalini.

N.B:

- ***Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi na Usajili, kuyafuatilia maeneo yote ambayo hayajaendelezwa katika ukanda wa pwani, Pemba ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii na nakla ya ripoti hiyo iwasilishwe kwa Kamati.***

- ***Kamati imegundua kuwa, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Pemba haina kumbu kumbu na maeneo ya uwekezaji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuhakikisha kumbu kumbu halisi ya maeneo ya wawekezaji kwa upande wa Pemba zinapatikana.***

Hoja Nam. 13.11: Mapungufu yaliyojitokeza katika ufutaji wa Hati ya umiliki wa Ardhi:

Ukaguzi umebaini kuwa kuba baadhi ya wamiliki wa ardhi wamefutiwa hati za umiliki wa ardhi lakini bado wanaendelea kulipa malipo ya kodi ya ardhi hizo hadi Ofisi hii inafanya ukaguzi huu. Kuendelea kupokelewa mapato ya maeneo hayo kunaweza kusababisha migogoro na kwenda kinyume na sheria na kanuni zilizopo. Maeneo yaliyobainika ambayo yanamapungufu ni Mradi wa Sago Palm Resort, Mradi wa Sovereign Sands Resort na Mradi wa Pemba Tours & Hoteli Company Ltd.

Majibu ya Wizara/Idara:

Mradi wa Sago Palm Resort na Sovereign Sands Resort inamilikiwa na Mwekezaji mmoja, miradi hii ilifutwa kwa kufuata taratibu za Sheria ya Ardhi No. 12 ya 1992, ambapo Mwekezaji alipewa indhari tarehe 31 Oktoba, 2011 kwa barua yenye kumbukumbu Namba MUNA/29/3/C.100/VOL.XXII/47 na hatimae tarehe 01 Februari, 2012 hati ya ufutwaji ilitolewa.

Walizidi kueleza kuwa, Idara ya Ardhi na Usajili tayari imetoa ardhi hizo kwa Wawekezaji wengine ambapo, ardhi iliyokuwa ya Mradi wa Sago Palm Resort umepatiwa Mradi wa Coconut Resort and Villas Ltd na Mradi wa Sovereign Sands Resort umepatiwa Mradi wa The Address Ltd tarehe 28 Februari, 2012. Hivyo, Wakaguzi wa Hesabu hawakuweza kufahamu kilichotokea na kuiweka hoja hii.

Uchunguzi wa Kamati

Ingawa Idara ya Ardhi na Usajili ilieleza suala hili kwa kina na kuwasilisha nyaraka mbali mbali zinazothibitisha kauli zao, Kamati ya PAC haikuridhika na hilo na ilikutana na Mwekezaji wa ardhi hizo siku ya Jumapili ya tarehe 1 Disemba, 2013 ili kujiridhisha na kile kilichoelezwa mbele ya Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Usajili na baadhi ya Watendaji wake.

Ndugu Yussuf Idrissa aliieleza Kamati kuwa wanamiliki miradi hiyo miwili, walizipata ardhi hizo baada ya kulipia vipando vya wananchi na baadae walianza kazi ya ujenzi. Wakati wanaendelea na kazi ya ujenzi alipata ajali hapo Bungi na ilimfanya apoteze kumbukumbu kwa baadhi ya mambo. Alipokea simu kutoka kwa Afisa wa Idara ya Ardhi na Usajili Ndugu Haji Juma kuhusiana na masuala ya ufutaji wa ardhi hizo. Hata hivyo, alimjibu kuwa eneo wameshaendeleza na wameshalipa kodi ya ardhi pamoja na fidia waliyotakiwa kulipa kama

sheria inavyoelekeza. Ingawa kulikuwa hakuna tatizo lolote kwa upande wa Muwekezaji, Ndugu Haji alimtaka Muwekezaji huyo kumpatia milioni moja (1,000,000/-) nae alifanya hivyo.

Alieleza kuwa siku chache baadae alipata taarifa kuwa ardhi zile zimeshapewa watu wengine na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Mheshimiwa Ali Juma Shamhuna na aliyesimamia zoezi lile ni Ndugu Saleh Moh'd Said ingawa Idara ya Ardhi na Usajili haikumpatia taarifa rasmi ya indhari na ufutwaji wenyewe.

Muwekezaji huyo alifatwa na Maafisa wa Polisi kutoka Kituo cha Polisi Makunduchi wakimtaka kwa nguvu aingie kwenye gari lao ili afikishwe Kituoni huko pamoja na vifaa vyake vya ujenzi. Kwa kuwa Maafisa hao walikiuka maadili ya kazi yao muwekezaji huyo aligoma kuingia kwenye gari hiyo na alikwenda Kituoni kwa khiyari na nguvu zake mwenyewe. Baada ya mvutano mrefu baina ya Maafisa wa Polisi na Muwekezaji wa ardhi hizo, na Muwekezaji huyo kuhisi kuwa anapoteza muda na fedha zake, alifungua kesi hapo Mahkama ya Ardhi na hatima kesi hiyo aliifuta baada ya kulipwa baadhi ya hasara alizopata na Ndugu Saleh kwa kupitia Ndugu Chande.

Alizidi kueleza kuwa, katika kufuatilia suala hili alibaini kuwa hakuna kumbukumbu zozote za usajili kwa Kampuni ya Coconut Resort and Villas Ltd na The Address Ltd.

Ingawa malumbano ya kuhodhi ardhi hizi yalikuwa yanaendelea, bado mwekezaji huyu alikuwa analipa kodi kama kawaida. Kwa kuwa Bodi ya Mapato ni wakala wa Idara ya Ardhi na Usajili, na kwa kuwa Idara hii ilikuwa imeshampatia ardhi zile Kampuni nyengine, kuanzia mwaka 2013 Afisa wa Bodi ya Mapato Ndugu Saadie alikataa kupokea fedha kutoka kwa Mradi wa Sago ikiwa ni malipo ya kodi ya ardhi.

Wakati Kamati ya PAC inaendelea na mahojiano na Muwekezaji - Ndugu Yussuf Idriss, Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Usajili aliunga mkono maelezo yote yaliyotolewa na Muwekezaji huyo na kueleza kuwa katika kutekeleza majukumu yake Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Ramadhan Abdalla Shaaban alibaini kuwa ufutwaji uliofanyika haukufuata Sheria husika, hivyo, Idara yao ina nia ya kuirejesha tena ardhi hiyo kwa Muwekezaji huyo.

Wajumbe wa Kamati ya PAC walipatwa na mshituko na kauli ya Mkurugenzi huyo aliyoitoa siku hiyo, kwa kuwa ilikuwa inapingana na maelezo yake aliyoyatoa tarehe 27 Novemba, 2013 mbele ya Kamati hiyo hiyo huko Afisini kwake Shangani. Kitendo hiki kimeifanya Kamati hii iamini kuwa baadhi ya taarifa zilizokuwa zinawasilishwa mbele yake hazikuwa na usahihi, jambo ambalo ni kosa chini ya Sheria ya Kinga, Fursa na Uwezo wa Wajumbe - Namba 4 ya 2007, kifungu cha 22 na 24.

Mapendekezo ya Kamati:

- Watendaji wa juu wa Serikali (i.e Mawaziri) wasiridhike na kile wanachoambiwa na wasaidizi wao kwa yale mambo yatakayoitia hasara Serikali kutokana na hatua

inazoichukua na badala yake wafuatilie kwa karibu masuala hayo ikiwa ni pamoja na kutembelea maeneo husika na kufanya mahojiano na wahusika.

- Watendaji wa Serikali watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Maadili ya kazi zao na maslahi ya nchi, na waache tabia ya kufanya kazi kwa kuweka mbele maslahi yao binafsi.

- Waziri anayehusika na masuala ya Ardhi – Zanzibar, afuatilie kwa kina hati zote zilizotolewa za ufutaji wa umiliki wa ardhi ili haki itendeke.

- Kutokana na tukio la kusikitisha la Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Usajili la kuidanganya Kamati tarehe tarehe 27 Novemba, 2013Kamati inamtaka Mkurugenzi huyo kuiomba radhi Kamati hii ndani ya wiki moja tokea siku ya kuwasilishwa taarifa hii mbele ya Baraza hili Tukufu, kushindwa kufanya hivyo, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Maelezo ya Idara ya Ardhi na Usajili kuhusiana na Mradi wa Pemba Tours & Hotel Company Limited

Kwa upande wa muwekezaji wa Mradi wa Pemba Tours & Hotel Company Limited, muwekezaji huyu alikuwa anamiliki maeneo mawili ya ukodishwaji. Hata hivyo, alimuomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kutaka kuunganishiwa mikataba yake ili apatiwe mkataba mmoja tu. Ombi hilo lilikubaliwa na kutayarishiwa mkataba mmoja wa maeneo mawili. Kutokana na hilo mikataba ya ukodishaji ya awali imefutwa kama taratibu zinavyoelekeza na taratibu za kodi na masharti ya ukodishaji bado yanaendelea kama kawaida.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imeridhika na maelezo yaliyotolewa, hivyo kwa kutumia kifungu cha 52(5)(c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, inapendekeza hoja hii ifutwe.

Hoja Nam. 13.12: Madeni ya muda mrefu ya umiliki wa Ardhi:

Ukaguzi umebaini kuwa Idara ya Arshi na Usajili imewakodisha ardhi wawekezaji mbali mbali kwa ajili ya maendeleo lakini wamiliki wa maeneo hayo wameshindwa kulipa kodi zao za ardhi kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za nchi.

Majibu ya Wizara/Idara:

Idara ya Ardhi na Usajili imekiri kuwepo kwa madeni ya muda mrefu na imeanza kuchukua hatua mbali mbali zikiwemo;-

- Kufutwa kwa miradi yote ambayo inamilikiwa na Wawekezaji wageni ambayo hailipiwi.

- Kuendelea kutoa elimu kwa wawekezaji wazalendo juu ya wajibu wao wa kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria.
- Kutoa hati za matumizi ya kawaida kwa Taasisi za Serikali na Taasisi za dini.

Uchunguzi wa Kamati

Ingawa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alijaribu kutenganisha wawekezaji binafsi na Taasisi za Serikali, Kamati imebaini kuwa zoezi hili halikutekelezwa kwa asilimia mia moja (100%). Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya Taasisi za watu binafsi zimeorodheshwa kwenye Taasisi za Serikali, kitendo ambacho kimeichanganya Kamati wakati wa kuziita Taasisi hizo. Hata hivyo, Kamati ilifuatilia hoja hii, na kukutana na kufanya mahojiano na baadhi ya Wawekezaji hao kutokana na uchache wa muda uliokuwa nao kama ifuatavyo;-

TAASISI ZA SERIKALI

S/NO.	JINA LA MRADI	MUDA WA DENI	SABABU YA KUTOKULIPA	USHAURI WA KAMATI
1.	Karakana Kuu ya Serikali	11	Baadhi ya eneo lao limevamiwa na wananchi. Aidha, mwaka 1994 walipatiwa hati ya ukodishwaji pale ilipotakiwa kugeuzwa Kampuni, jambo ambalo limeshindikana na kubakia Kitengo cha Wizara na mwaka 2003 baada ya kuundwa kwa Idara ya Usafiri na Leseni, Karakana imerejeshwa Serikalini na kua chini ya Idara ya Usafiri na Leseni ambayo sio Idara inayojitegemea. Aidha, kwa mujibu wa taratibu za ukodishwaji, ruhusa ya kukodishwa na kutakiwa kulipa deni, hufanywa kwa Taasisi zinazojitegemea.	Kamati inashauri ardhi hiyo ipimwe tena na Idara ya Ardhi na Usajili ili lijuulikane deni halisi linalowakabilia Karakana Kuu. Aidha, kuhusiana na deni hilo, Kamati inaliona ni sawa na madeni mengine baina ya Taasisi za Serikali na linawezekana likawa gumu kulipika. Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kulihakiki deni hilo na hatimae kufanywa

				utaratibu wa kufutwa.
2.	Zanzibar Municipal Council (Baraza la Manispaa)	8	Walipokea Invoice inayoonesha deni la USD 6,026.40 la miaka sita, ingawaje hawajawahi kupokea invoice nyengine yoyote kuhusiana na deni hilo. Hata hivyo, Baraza limekubali kulipa ingawaje kwa sasa halina uwezo wa kulilipa deni hilo kutokana na hali ngumu inayowakabili.	Hili ni sawa na madeni mengine baina ya Taasisi za Serikali na linawezekana likawa gumu kulipika. Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kulihakiki deni hilo na hatimae kufanywa utaratibu wa kufutwa.
3.	Zanzibar Port Corporation (Shirika la Bandari)	10	Kwa mujibu wa kumbu kumbu za Shirika, hawana mradi huo na Shirika halijawali kupokea hati ya madai (invoice) kwa kipindi kilichotajwa cha miaka 10.	Kamati haikupatiwa ufafanuzi wa kutosha kuhusiana na sababu za kuwepo kwa mradi huu. Aidha, inashauri ufanyiwe kazi tena na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na akiridhika kuwa haupo, basi aijuulishe Kamati.
4.	Zanzibar Electricity Co. Ltd (Shirika la Umeme)	7	Hawana deni.	Wamelipa madeni yao na Kamati imeridhika na ushahidi uliowasilishwa. Kamati inapendekeza

				hoja ya deni kwa Shirika la Umeme, ifutwe.
5.	Zanzibar State Trading Corporation (ZSTC)	6	Hawana deni kwa mujibu wa Ankara za malipo walizopewa na Bodi ya Mapato na wamekamilisha malipo ya miaka sita kama walivyopewa ankara hizo.	Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.
6.	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	2	Sio eneo la Wizara hii, ni eneo lililopewa Islamic Azaq University ya Iran kwa ajili ya ujenzi wa Chuo.	Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kukaa pamoja na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kumpada mdaiwa anaehusika na malipo.

TAASISI ZA WATU BINAFSI

S/NO.	**MMILIKI**	**MUDA WA DENI (MIAKA) NA JUMLA YA DENI**	**SABABU YA KUTOKULIPA**	**USHAURI WA KAMATI**
1.	Bombay Bazar	5 sawa na US$ 2,332	Hawakueleza sababu ya kutokulipa, isipokuwa kwamba wamesema wapo yatari kulipa.	Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi kupitia ZRB, kufuatilia malipo ya deni pamoja asilimia 10 ya adhabu, kwa mmiliki huyo ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii. Aidha, deni hilo likishindwa kulipwa

				kwa wakati, Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi kuchukua hatua za kisheria kwa ardhi husika.
2.	CCM Mkoa wa Kaskazini	3 sawa na US$ 2,943.00	Hawajapata mradi wa kuwekeza	Kamati inakitaka Chama Cha Mapinduzi, ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii, kulipa kodi ili kuepuka eneo lao kufutwa na Serikali. Aidha, kama hawana uwezo wa kuwekeza watafute Muwekezaji. Iwapo chama kitashindwa, Kamati inashauri Wizara ichukue hatua ya kuirejesha ardhi hiyo Serikalini.
3.	Anglican Church	9 sawa na US$ 9,625.00	Waliandika barua kwa aliyekuwa Waziri wa Fedha na Uchumi Mhe. Othman Nyanga ya kuomba kufutiwa deni na kupatiwa haki ya matumizi 'Right of Occupancy', ambapo Mhe. Waziri alimuandikia aliyekuwa Waziri anayehusika na mambo ya ardhi Mhe. Burhani kwa barua yenye kumbukumbu Namba IKL/TS/MNV – 86/VOL.4/37ya tarehe 04 Novemba, 2003 na hatimae ombi lao lilikubaliwa na tokea mwaka 2003,	Ingawa wahusika wana haki ya matumizi ya ardhi tokea mwaka 2007, Kamati imewataka walipe deni hilo kwa kile kipindi ambacho wanadaiwa hasa ikizingatiwa kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi hana mamlaka ya masuala ya ardhi. Aidha, Wizara ya Ardhi kupitia wakala wake ZRB wafuatilie ulipwaji wa madeni hayo pamoja na faini, na kuhakikisha deni

			hawajapokea Ankara yoyote ya malipo. Isipokuwa kwamba mnamo mwaka 2010 walipokea Ankara ya malipo kutoka Bodi ya Mapato Zanzibar kwa Ankara Namba 224/2010.	hilo linalipwa ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii.
4.	Petrol Station – Chwaka	9 sawa na US$ 3,366	Mradi ulioripotiwa na Mdhibiti umefutwa tokea mwaka 2006. Isipokuwa, kwamba wito uliotolewa na Kamati uliitikiwa na Kampuni ya GAPCO. Kampuni hii imeeleza kuwa imelipa US$ 3000 (sawa na USD 1,000 kwa kila mwaka) kwa risiti namba 125598 ya mwaka 2010, risiti namba 01026 ya mwaka 2011 na risiti namba 362716 ya mwaka 2012. Aidha, wamiliki wa mradi huu wameeleza kuwa hawajaendeleza maeneo ya ardhi ya Makunduchi, Paje, Pwani Mchangani, Mangapwani na Kombeni kwa kuwa maeneo hayo yana mgogoro.	Kamati imekubaliana na malipo hayo ya GAPCO, isipokuwa inaitaka ZRB iangalie adhabu ya 10% kama ilivyo katika sheria, kwa kua muekezaji huyu alichelewa kulipa kodi yake ya ardhi. Aidha, kuhusiana na kutoyaendeleza maeneo ya ardhi waliyopewa, Kamati imewataka GAPCO waendeleze maeneo hayo haraka iwezekanavyo kabla Sheria ya Umiliki wa Ardhi haijatekelezwa chini ya kifungu cha 48.
5.	Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu imeandika aina ya mradi pekee (Diving), hata hivyo, kwa mujibu wa Maafisa wa Idara ya Ardhi na Usajili – Pemba Mmiliki wa mradi huu ni Pemba Tours & Hotel Company Ltd - Vumawimbi	4 sawa na US$ 36,960.00	Muwekezaji hajapatikana (hawana Ofisi Zanzibar) na kwa mujibu wa Hoja Namba 13.11 ya Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu Muwekezaji huyu amelipa kodi hadi tarehe 30/1/2012, ingawa mkataba wa	Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ifuatilie kwa kina pahala ambapo Kampuni zitafanya shughuli zake wakati wa usajili ili kuepuka kuwa na kampuni za mikobani (briefcase)

			ukodishwaji umefutwa mwaka 2011.	
6.	Petrol Station – Jumbi	7 sawa na USD I,540	Mradi ulioripotiwa na Mdhibiti umefutwa tarehe 11 Mei, 2006 kwa kuvunja ibara ya 2(ii), 3(iv) na (vii) ya mkataba wa ukodishwaji. Isipokuwa kwamba wito wa Kamati uliitikiwa na Petrol Station – Jumbi ambayo sio iliyoandikwa kwenye Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu uk. 87) na wameeleza kwamba hawajalipa kodi ya ardhi kwa kuwa walivamiwa na majambazi zaidi ya mara moja.	Kamati imeitaka Petrol Station-Jumbi (iliyopo sasa) kulipa deni hilo ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii.
7.	The Cristal Resort Ltd	USD 5,104	Mpaka Mwezi March 2013 tayari walikwishalipa kupitia Risiti namba D:418594, na risiti namba D:423073 zote za tarehe 11/03/2013 zenye uthibitisho wa malipo ya USD 600.	Kamati imejiridhisha kwamba, muwekezaji huyu analipa kama kawaida. Aidha, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

Sambamba na hayo, katika kufuatilia hoja hii, Kamati imebaini kuwa baadhi ya wawekezaji wanapeana maeneo ya ardhi (Land transfer) bila ya kuishirikisha Idara ya Ardhi na Usajili.

Aidha, kila muwekezaji alikuwa anapewa kipindi cha kujitayarisha au kujiandaa (grace period) ingawa wengine walikuwa hawana haki ya kupewa kwa kuwa tayari maeneo hayo kipindi cha kujitayarisha kimeshatolewa, kitendo hiki kilikuwa kinainyima mapato Serikali.

Hoja Nam. 13.13: Miradi ya wawekezaji ambayo imefutwa baada ya kushindwa masharti ya uwekezeji

Ukaguzi umebaini kuwa maeneo mbali mbali ya ardhi yametolewa na Idara ya Ardhi na Usajili kwa ajili ya uwekezaji ili kutoa fursa mbali mbali za ajira kwa wananchi lakini baada ya

kushindwa masharti ya uwekezaji Serikali imeamua kuifuta miradi hiyo na maeneo hayo ya ardhi kurudi katika mamlaka ya Serikali ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Kiambatanisho Namba 4 cha Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaonesha Miradi ambayo haiyalipa kodi ya ardhi kwa muda mrefu.

Vile vile, Kiambatanisho Namba 5 cha Ripoti hiyo kinaonesha Miradi ambayo maelezo ya ukodishwaji pamoja na malipo ya kodi ya ardhi hayakupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Wizara/Idara:

Baadhi ya miradi ya uwekezaji imefutwa na Idara hii baada ya wawekezaji hao kushindwa masharti mbalimbali ya uwekezaji kwa mujibu wa Sheria ya Umiliki wa ardhi pamoja na mkataba wa ukodishwaji, miongoni mwa maeneo hayo yameshapatiwa wawekezaji wengine. Hata hivyo, kuchelewa kwa kuwepo kwa mfumo wa 'Data base' kumepelekea kuonekana kuwa maeneo hayo hayajapewa wawekezaji wengine hadi baada ya kufuatilia kumbu kumbu zote zilizopo za umiliki wa miradi hiyo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati katika kujiridhisha na hoja hii ilibahatika kuyapitia baadhi ya majalada ili kuona sababu za ufutwaji wa mkataba huo. Miongoni mwa majalada hayo kwa mujibu wa kiambatanisho namba 4 cha Ripoti ya Ukaguzi Yakini kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2011/2012 ni kama yafuatayo;-

JINA LA MRADI	DP/NO	SABABU YA KUFUTWA
A Rosso Reef	430/2000	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Shakaza Beach Resort	530/2002	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1) na (3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
William Du Tpit	719/2005	Maslahi ya Taifa
Maweni Resort	600/2004	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Extension Of Zanisun	569/2003	Alifunga njia baharini kinyume na ibara ya 2(2) na 3(3) ya mkataba. Hata hivyo, mwaka 2005 alipewa tena eneo hilo na kuongezewa hekta 0.2403 ingawa kwenye jalada hakuna barua ya maombi hayo wala barua ya kuomba radhi.

Magellan Zanzibar Ltd	445/2000	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Wambaa Zanzibar Ltd	450/2000	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Anex Of Magellan	513/2002	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Two Tribes International	262/1996	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Sun Rise Resort	86/1992	Amehaulisha kwa Reem Resort na sio kama imeshindwa masharti.
Orient Hotel	202/1995	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa
Mohammed Abubakary Abdalla	310/1998	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Roger Sarda	400/2000	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Wally N Do	286/1997	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Daffodills Private School	268/1997	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Dr. H.H Ahmed Bin Saif Al-Nahyan	376/1999	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Coral Beach Resort	163/1994	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Mr Keith Philip	273/1997	Hakuna kumbukumbu yoyote ya kufutiwa, ingawa, imeripotiwa na Ofisi ya Mdhibiti

		kuwa umefutwa.
Ms. Josephine Noel	282/1997	Katika jalada hakuna barua ya kufutiwa matumizi ya ardhi, isipokuwa kwamba amelipa kodi hadi mwaka 2006
Hass House Ltd	84/1992	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Mr. Dhiren G. Kotak	444/2000	Alifutiwa mara ya kwanza mwaka 2006 baada ya kukiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) cha Sheria ya Ardhi. Alifutiwa mara ya pili mwaka 2007 baada ya Mradi kuuzwa kwa Nungwi Co. Ltd.
Dorada Ltd	37/1991	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Blue Harizon Investment	634/2004	Ni eneo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusiana na mambo ya Historia – Maruhubi chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya An Ancient Monument Preservation Sura ya 102
Al-Youseif Charitable	502/2002	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Ifa Hotel And Resort	702/2005	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Spice Island Ltd	747/2005	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo. Eneo hili liligawiwa kwa wawekezaji wengine wanne ambao ni Sun Shine, F&K Enterprise, Mauritius na Shiva Hotel. Hata hivyo, Wawekezaji hawa wamefutiwa chini ya kifungu cha 48(1-3) cha Sheria ya Ardhi. Aidha, Idara ya Ardhi ina mpango wa kumrejeshea Spice Island Ltd baada ya kugundua mapungufu yaliyojitokeza.
Mada Hotel	770/2006	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya

		Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo. Hata hivyo, mnamo mwaka 2011 alirejeshewa ardhi hiyo kwa kuwa aliwahi kuliendeleza eneo hilo.
Global Trading Enterprise	692/2005	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1-3) ya Sheria ya Ardhi. Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Hotel & Property Development	775/2006	Wamebadilishiwa eneo kutokana na kubadilika kwa Master Plan, isipokuwa kwamba hakukuwa na barua inayoonesha kuwa wamepatiwa eneo jengine.
J. V Properties	792/2006	Kuna mauziano ya ardhi baina ya Co. hii ambayo mwekezaji wake ni Mgeni na Parachichi Ltd
Kendwa Beach	795/2006	Kuna mauziano baada ya ardhi kuendelezwa baina ya Kendwa Beach na Parachichi Ltd
Zanzibar Masai	832/2007	Amekiuka masharti ya kifungu cha 3(4) cha mkataba
Zenji Lodge	912/2008	Kwa mujibu wa taarifa kutoka Bodi ya Mapato - Zanzibar Mwekezaji huyu bado hajafutiwa ingawa hakuna mawasiliano nae. Aidha, hakuna barua inayothibitisha ufutwaji huo.
F&K Enterprise	989/2009	Alikuwa ana haki ya kuhodhi ardhi hiyo na alifutiwa kwa kuwa eneo hilo limetengwa kwa ajili ya uekezaji
Sun Shine	1147/2011	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1)(b) cha Sheria ya Ardhi, ibara ya 3(3)(4) ya mkataba na walipewa watumiaji wawili (Double allocation). Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Mauritius Hotel	1148/2011	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1)(b) cha Sheria ya Ardhi, ibara ya 3(3)(4) ya mkataba na walipewa watumiaji wawili (Double allocation). Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Shiva Hotel	1150/2011	Amekiuka masharti ya kifungu cha 48(1)(b) cha Sheria ya Ardhi, ibara ya 3(3)(4) ya mkataba na walipewa watumiaji wawili

		(Double allocation). Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Pennyroyal Ltd	1156/2011	Amekiuka masharti ya vifungu vya 48(1)(b), 3, 46(3) vya Sheria ya Ardhi, na walipewa watumiaji wawili (Double allocation). Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Chrysogonus	1174/2012	Amekiuka masharti ya vifungu vya 48(1)(b), 3, 46(3) vya Sheria ya Ardhi, na walipewa watumiaji wawili (Double allocation). Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Chrysogonus	1175/2012	Amekiuka masharti ya vifungu vya 48(1)(b), 3, 46(3) vya Sheria ya Ardhi, na walipewa watumiaji wawili (Double allocation). Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Abacus Ltd	1107/2011	Amekiuka masharti ya vifungu vya 48(1)(b), 3, 46(3) vya Sheria ya Ardhi, na walipewa watumiaji wawili (Double allocation). Hakuna indhari ilotolewa ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo.
Aeacus Ltd	1118/2012	Amekiuka masharti ya vifungu vya 48(1)(b), 3, 46(3) vya Sheria ya Ardhi, na walipewa watumiaji wawili (Double allocation). Hakuna indhari ilotolewa. ingawa sheria ilikuwa hailazimishi kufanya hivyo
Sargo Palm Resort	781/2006	Alipewa indhari ya kufutiwa kwa barua ya tarehe 31 Oktoba, 2011 yenye kumbu kumbu namba MUNA/29/3/C.100/VOL.XX11/47 baada ya kwende kinyume na kifungu cha 48 (1-3) cha Sheria ya Umiliki wa Ardhi na kufutwa tarehe 01 Februari, 2012 kwa barua yenye kumbu kumbu namba MUNA/29/3/C.100/VOL.XX11/84. Eneo hilo alipewa Kampuni ya Coconut Resort and Villas Ltd tarehe 28 Februari, 2012.
Sovereign Sands Resort	780/2006	Alipewa indhari ya kufutiwa tarehe 31 Oktoba, 2011 na alifutiwa tarehe 01 Februari, 2012 chini ya kifungu cha 48 (1-3) cha Sheria ya Umiliki wa Ardhi. Eneo hilo alipewa Kampuni ya Address Ltd tarehe 28 Februari, 2012.

Sanjari na hayo, Kamati ya PAC ilipitia jalada moja baada moja kwa upande wa Kiambatanisho namba 5 cha Ripoti ya Ukaguzi Yakini kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2011/2012 kinachohusiana na Maeneo ya ardhi ambayo taarifa zake zimekosekana.

Kamati hii ilibahatika kupata taarifa hizo ingawa zinamapungufu na kubaini kuwa takriban miradi yote ilikuwa imefutwa na baadhi ya maeneo ya ardhi wameshapewa wawekezaji wengine.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilishindwa kupata taarifa hizo kwa kuwa haikuzifuatilia huko Idara ya Ardhi na Usajili ambayo ndio taasisi yenye dhamana na mambo ya ardhi kwa Zanzibar.

Baadhi ya taarifa ambazo Kamati imezipata ni kama ifuatavyo;-

S/NO.	**JINA LA MRADI NA PAHALA ULIPO**	**DP NO.**	**SABABU YA KUKOSEKANA TAARIFA ZAKE**
1.	Coastal Steel Z'bar Ltd - Nungwi	6/88	Imefutwa, ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Kampuni ya Mtoni Marine.
2.	White Sand Group Ltd – Nungwi	7/89 badala ya 7/88 iliyoandikwa na Mdhibiti	Imefutwa mwaka 1992 kwa barua Namba KAM/MUN/K.70/20/8/3 baada ya kushindwa kuiendeleza.
3.	White Sand Group Ltd – Pwani Mchangani	8/89 badala ya 8/88 iliyoandikwa na Mdhibiti	Imefutwa, ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo
4.	Bulk Oil – Mtoni	11/89	Imefutwa mwaka 1994 baada ya kushindwa kulilinda eneo la hifadhi 'buffer zone'. Aidha, cheti cha muda cha matumizi 'interim certificate' kilifutwa kwa barua yenye kumbu kumbu Namba ZIPA/TS/92/S.5/33
5.	Tiawi International Ltd - Bwejuu	15/90	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Palm Hotel.
6.	Dr. H.C.M Kairuki – Mbweni	18/90	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Zanzibar Beach Resort.
7.	Zenj Hotel Z'bar Ltd – Mbweni	19/90	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Bregedia Suleiman Moh'd Yahya Al-Alawy.
8.	El – Haj Investment Ltd - Bawe	22/91 badala ya 22/90	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa

		iliyoandikwa na Mdhibiti	Kampuni ya GAPCO.
9.	Mbweni Palace Hotel	23/90	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Mbweni Wings
10.	Village Resort Hotel – Mbweni	24/90	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Mbweni Wings.
11.	African Charitable Society – Mombasa	27/90	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo katika jalada na kupatiwa wananchi mbali mbali kwa kuwa eneo hili lilikuwa kubwa.
12.	Abdul – Rahman & Son – Mombasa	32/90	Alishindwa kuendeleza na baadae alipatiwa haki ya matumizi 'Right of Occupancy'.
13.	Dr. H.C Kairuki – Mwanakwerekwe	36/91 badala ya 36/90 iliyoandikwa na Mdhibiti	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Skuli ya SHAA
14.	Zekon – Uroa badala ya Zekozi iliyoandikwa na Mdhibiti	38/91	Alishindwa kuendeleza na baadae alipatiwa haki ya matumizi 'Right of Occupancy'.
15.	Ital Food C. – Bwejuu	39/91	Imefutwa mwaka 2004 baada ya kushindwa kutekeleza matakwa ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Umiliki wa Ardhi na Ibara ya 2(ii) ya Mkataba wa Ukodishwaji, kwa barua yenye kumbu kumbu MUNA/29/3/2/C.100/VOL.IX/334. Eneo hili amapewa Mango Hotel
16.	Shrbaji Enterprise – Mombasa na sio Bwejuu kama ilivyoripotiwa na Mdhibiti	46/91	Ni Soko la Mboga mboga la Mchina
17.	Bot – Mwanakwerekwe	52/91	Imefutwa mwaka 2001 ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Kikosi cha Zima Moto na Uokozi.
18.	Silkh Saw Millsltd Mombasa	54/91 badala ya 544/91 iliyoripotiwa na Mdhibiti	Imefutwa baada ya kutangazwa kuwa amefilisiwa 'Bankcrupt' ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na amelipa kodi ya ardhi hadi mwaka 98 kwa risiti namba 438421.
19.	International Motors Ltd –	57/91	Imefutwa ingawa hakuna barua

	Amani		inayothibitisha hilo katika jalada na kupatiwa wananchi mbali mbali kwa kuwa eneo hili lilikuwa kubwa.
20.	Buyuti Baraka – Chuini	59/91 badala ya 89/91 iliyoripotiwa na Mdhibiti	Imefutwa mwaka 2000 kwa barua yenye kumbu kumbu namba MUNAM/29/3/2 C.100 VOLII/570 baada ya kukiuka masharti ya mkataba ya ukodishwaji Ibara ya 3(iii) na (xiv). Eneo hili amepewa Mangroove Hotel.
21.	Holiday Village Estate – Pwani Mchangani	64/91	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Zanzibar Leisure.
22.	Coral Cove – Kama	67/92	Imefutwa baada ya kukiuka Ibara ya 2(ii), 3(iii) na (iv) za mkataba wa ukodishwaji. Mnamo mwaka 2008 ardhi hii alipatiwa Sea Rock Resort.
23.	Makunduchi Beach – Makunduchi	87/92	Alishindwa kuendeleza na baadae alipatiwa haki ya matumizi 'Right of Occupancy'.
24.	Vumawimbi Tourist Hotel – Vumawimbi	85/92	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kufanywa kuwa ni eneo la ziada la Msitu wa Ngezi 'Extension of Ngezi Forest'.
25.	F.J.W Sjansen – Fundo	95/92	Mradi haustahiki kuwepo katika eneo hilo
26.	Rijaals Tourist Lodge – Paje	101/92	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Hakuna Majiwe.
27.	Zanzibar Bottlers – Mwanakwerekwe	109/92	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Kikosi cha Zima Moto na Uokozi.
28.	Gogefar Investment – Mtoni	110/92	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Mtoni Marine.
29.	Robio Limited – Kiuyu	112/92	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo ni eneo la Msitu.
30.	Ams Investment – Mombasa	127/93	Taarifa zake zimekosekana katika Idara ya Ardhi na Usajili (ingawa

			inaaminika kwamba, taarifa hizo zipo).
31.	Maruhubi Palace – Maruhubi	130/93	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo ni eneo la historia.
32.	Tptc – Mwanakwerekwe	153/93	Imefutwa mwaka 2001 kwa barua yenye kumbu kumbu namba MUNA/29/3/2/C.100 VOL.II/663 baada ya kukiuka masharti ya Ibara ya 3(iii). Eneo hilo umepewa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar 'ZSSF'.
33.	Chukwani Resort	159/94	Imefutwa kwa kuwa ni eneo la hifadhi 'baffer zone' ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo. Hata hivyo, eneo hilo amepatiwa Mark Antony.
34.	Door Company – Kiwengwa	170/94	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Bravo. Muwekezaji wa awali amelipa hadi mwaka 1999.
35.	Asya Village – Paje	173/95 badala ya 173/94 iliyoandikwa na Mdhibiti	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupewa Kampuni ya UNICOM, hata hivyo, Kampuni hii nayo haijaendeleza ardhi hii.
36.	Rock Resort – Bwejuu	176/94	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo katika jalada. Eneo hilo alipatiwa Sultan Palace. Muwekezaji wa awali amelipa hadi mwaka 1995.
37.	Z'bar State Engineering – Mwanakwerekwe	182/95	Imefutwa mwaka 2002 kwa barua yenye kumbukumbu namba AU/UMM/MUN/K.70/30 VOL.VIII baada ya kushindwa masharti ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Umiliki wa Ardhi. Eneo hili limepatiwa Skuli ya SHAA.
38.	British Petroleum – Darajani	188/95	Eneo la wazi
39.	Z'bar Dairy – Maruhubi	195/95	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Zanzibar Dairy Products Co. Ltd (Bakhresa).
40.	Platium Holding – Pwani Mchangani	203/95	Cheti cha muda 'interim certificate' imefutwa mwaka 2000 kwa barua yenye kumbu kumbu namba

			KAM/MUN/K.10/4 FK1/40 kupatiwa Dodsal.
41.	M.S Ltd – Bwejuu	209/95	Cheti cha muda 'interim certificate' imefutwa mwaka 2004 kwa barua yenye kumbu kumbu namba ZIPA/HT/94/M.20/31 na kupatiwa Kampuni ya UNICOM ambayo haijaendeleza eneo hili.
42.	Tegezi Diving - Kizimkazi	212/95	Imefutwa mwaka 2003 kwa barua yenye kumbu kumbu namba AU/UMM/MUNA/K/70/30 VOL X, baada ya kushindwa masharti ya Ibara ya 2(ii) na kupatiwa Hotel & Lodges.
43.	Ttcl – Kikwajuni	213/95	Imefutwa mwaka 2003 kwa barua yenye kumbu kumbu namba MUNA/2/9/144 na upatiwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar
44.	Grand Hotel – Nungwi	215/95	Imefutwa baada ya kushindwa kuendeleza ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa kampuni ya RENCO. Muwekezaji wa awali amelipa kodi ya ardhi hadi mwaka 1996.
45.	Holiday Inn – Maisara	216/95	Imefutwa kwa kuwa ni eneo la hifadhi ya maji ya bahari.
46.	Safari Pemba Hotel – Panga watoro	227/95	Imefutwa mwaka 1998 kwa barua yenye kumbu kumbu namba ZIPA/HT/94/S.29/17 na kupatiwa Manta Resort.
47.	One Earth Ag Matemwe	229/95	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Zanzibar Leisure Hotel.
48.	Al-Imran Investment – Paje	246/96	Imefutwa baada ya kushindwa masharti ya Ibara ya 2(ii) na 3(iv) na (v) za mkataba wa ukodishwaji na kupatiwa Kampuni ya Hakuna Majiwe.
49.	Al-Imran Investment – Paje	247/96	Imefutwa baada ya kushindwa masharti ya Ibara ya 2(ii) na 3(iv) na (v) za mkataba wa ukodishwaji na kupatiwa Kampuni ya Hakuna Majiwe.
50.	Zayn Zal Z'bar – Matemwe badala ya Zamu Zanzibr	252/96	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kupatiwa Kampuni ya Protea.

51.	Amal Farm Tunguu	258/96	Imefutwa kwa barua yenye kumbukumbu namba AMMN/29/3/C.100/VOL.XXII/574 ya tarehe 20 Oktoba, 2011na kupatiwa Chuo Kikuu cha Taifa 'SUZA'.
52.	Z'bar State Engneering – Buyu	261/96	Imefutwa ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo kwa kuwa ni eneo linalotarajiwa kujengwa Uwanja wa Ndege.
53.	Bin Ameir Establishment – Mwanakwerekwe	270/97	Imefutwa kwa maslahi ya umma, ingawa hakuna barua inayothibitisha hilo na kujengwa Skuli ya Mwanakwerekwe 'C'.

Maoni ya Kamati

- Kwa kuwa miradi hii imefutwa kutokana na sababu mbali mbali, ingawa wawekezaji hawakupewa indhari ijapokuwa Sheria zilikuwa hazijatilia nguvu suala hilo, hata hivyo, Watendaji wa Taasisi hii walipaswa kuwa na busara ili kutekeleza misingi ya utawala bora.

- Kamati ya PAC imebaini kuwa ufutwaji huu umeleta tija kwani miradi mingi iliyofutwa imeshapatiwa wawekezaji wengine ambao wameshachukua hatua za uendelezaji.

- Kwa kuwa asilimia kubwa ya miradi hii imefutwa baada ya wawekezaji hao kushindwa masharti ya uwekezaji ambapo sharti kubwa lililobainika na Kamati hii ni wawekezaji kushindwa kuiendeleza ardhi hiyo. Hii ni kutokana na kuwa muwekezaji anaamua kukodi ardhi wakati hana mtaji wa kutosha wa kuendeshea shughuli hiyo. Kutokana na kitendo hicho Kamati hii inaishauri Serikali kuchukua jitihada za kutosha ikiwa ni pamoja na kujua mtaji halisi wa muwekezaji husika kwani kuendelea kutegemea taarifa za benki 'bank statement' kunaipotosha Serikali.

- Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ishirikiane kwa karibu zaidi na taasisi zinazohusika na hoja husika ili kupata taarifa kamili na sahihi.

Hoja Nam. 13.14: Maeneo ya wawekezaji ambayo hayajaingizwa katika Mtandao wa ulipaji Kodi ya ardhi:

Ukaguzi umebaini kwamba, kuna baadhi ya wawekezaji ambao wanafanya biashara katika maeneo mbali mbali, biashara hizo zikiwemo za hoteli za kitalii lakini maeneo hayo ya ardhi bado hayajasajiliwa katika mtandao wa ulipaji kodi ya ardhi katika Idara ya Ardhi na Usajili, Zanzibar.

Kwa vile maeneo hayo ni muhimu katika ukusanyaji wa mapato, Idara ya Ardhi na Usajili ikishirikiana na Serikali kuu inapaswa kuhakikisha kwamba, utaratibu mzuri unaandaliwa ili kuiwezesha taasisi hizi kulipia kodi ya ardhi.

Majibu ya Wizara/Idara:

Ni kweli maelezo ya mdhibiti na hali hiyo imesababishwa na ukweli kwamba, miradi hii katika kuanzishwa kwake huwa haitafuti ardhi bali huanzishwa katika maeneo ambayo tayari kuna majengo ambayo yanamilikiwa na wazalendo na wanapobadilisha mawazo ya kuanzisha miradi ya vitega uchumi, huanzia ZIPA pamoja na Kamisheni ya Utalii kwa ajili ya kupata vibali husika.

Pia, baadhi ya wananchi kupitia Masheha na Wilaya huidhinisha mauzo ya viwanja na nyumba katika maeneo yao bila ya kufuata sheria za ardhi.

Uchunguzi wa Kamati:

Pamoja na hoja zilizoelezwa na Idara, Kamati haijakubaliana nazo kiasi ya kuwepo utaratibu wa kuingizwa taarifa hizo katika mtandao wa kodi. Kwa kua wamiliki wa maeneo hayo wanafanya biashara, ni vyema wakalipia kodi na hivyo ni wajibu wa Wizara hii ya Ardhi chini ya Idara ya Ardhi na Usajili, kuhakikisha kwamba, wawekezaji hao wanaingizwa katika mtandao wa kodi.

Mapendekezo ya Kamati:

Kamati inaitaka ZRB kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi na Usajili ndani ya miezi sita baada ya kuwasilishwa kwa ripoti hii, ihakikishe wawekezaji hao wanaanza kupelekewa Ankara za kodi na utekelezaji huo uarifiwe kwa Kamati.

SEHEMU YA TATU :

HITIMISHO :

Kamati inapenda kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zote za Serikali walioshiki moja kwa moja ama namna nyengine katika kusaidia kufanikisha kazi za Kamati. Kamati haingeweza kutekeleza kazi zake bila ya mashirikiano yao. Aidha, ufanisi na ubora wa kazi za Kamati sambamba na uwasilishaji wa ripoti ya Kamati, ni matokeo ya msaada mkubwa wa mashirikiano ya pamoja baina ya Kamati na Wizara na Taasisi mbali mbali zilizohusika na

kazi. Kamati inaendelea kuwashukuru wananchi mbali mbali walioitwa mbele ya Kamati na kuhudhuria ama kuheshimu wito wa Kamati, hata ikiwa ni kujibu kwa maandishi kuonesha heshima na kutoa ufafanuzi uliotakiwa na Kamati.

Aidha, kifungu cha 122(5) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi kinachotoa muongozo na utaratibu wa uandishi wa ripoti za Kamati, katika sehemu hii ya tatu ya Hitimisho, kinaelekeza wajibu wa kila Kamati kutoa maoni na mapendekezo yake kwa Baraza. Hata hivyo, pamoja na muongozo huo, kwa Kamati ya P.A.C inayofanyia kazi ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na hufuatilia hoja moja baada ya nyengine kama ilivyo katika ripoti ya Mdhibiti na kutakiwa kutoa maoni na mapendekezo ya kila hoja kwa namna ilivyoripotiwa na Mdhibiti na kufanyiwa kazi na Kamati na kwa kutimiza maelekezo ya kanuni hii, Kamati huungana kwa kueleza na kusisitiza kwamba, mapendekezo ya Kamati hii ni yote yanayopatikana katika ‘Mapendekezo ya Kamati’ baada ya uchunguzi wa Kamati kwa kila hoja ya Mdhibiti, na Kamati inaliomba Baraza la Wawakilishi kuyakubali na kuyapitisha mapendekezo yote ya Kamati.